# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Tano – Tarehe 8 Aprili, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, Asalaam Aleykum! Bwana Yesu asifiwe! Baada ya msimu wa Pasaka na sikukuu zake na jana tulikuwa na Kumbukumbu ya Mashujaa na kipekee kumkumbuka Mwanzilishi wa Taifa letu, Mzee Karume, sasa leo tunaendelea na kazi. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

**WABUNGE FULANI:** Kazi iendelee.

**SPIKA:** Aah, kumbe mnajua! Jipigieni makofi basi, kazi iendelee. *(Kicheko/Makofi)*

Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

(a) Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano kuanzia 2021/2022 – 2025/2026 *(The 3rd National Five Years Development Plan, 2021/22 – 2025/26);*

(b) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Central Government for the Financial Year Ended 30th June, 2020);*

(c) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Development Projects for the Financial Year Ended 30th June, 2020);*

(d) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Public Authorities and Other Bodies for the Financial Year Ended 30th June, 2020);*

(e) Ripoti ya jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa kipindi kinachoishia Tarehe 31 Machi, 2021 *(The Annual General Report on the Performance and Specialised Audits for the Period Ending 31st March, 2021);*

(f) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Mali zilizotelekezwa *(Performance Audit on the Management of Unclaimed Assets);*

(g) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Utekelezaji wa Udhibiti wa Uhamishaji wa Bei ya Mauziano ya Bidhaa au Huduma Baina ya Makampuni yenye Mahusiano

*(Performance Audit on the Implementation of Controls over Transfer Pricing);*

(h) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Ununuzi wa Pamoja wa Magari ya Serikali na Usambazaji wa Mafuta *(Performance Audit on the Management of Procurement of Government Vehicles and Distribution of Fuel);*

(i) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Misamaha ya Kodi kwenye Miradi ya Uwekezaji *(Performance Audit on the Management of Tax Exemption on Investment Projects);* na

(j) Majumuisho ya Majibu ya Hoja na Mpango wa Kutekeleza Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha, umeanza vyema, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, bado ripoti zinaendelea kuja. Sasa ni ripoti kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, karibu sana Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, AJIRA, VIJANA, NA WATU WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):**

(a) Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi zilizofanyika na kuwasilishwa Bungeni mwezi Aprili, 2016 *(Follow-Up on Implementation of the Controller and Auditor General's Recommendations for Performance Audit Reports Issued and Tabled to Parliament in April, 2016);*

(b) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Utekelezaji wa Mradi wa Uzalishaji Sukari wa Mbigiri *(Performance Audit*

*on the Implementation of Mbigiri Sugar Production Project);* na

(c) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Udhibiti wa Mafuriko *(Performance Audit on Flood Control Measures);*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tuelekee TAMISEMI. Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):**

(a) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Local Government Authorities for the Financial Year Ended 30$^{th}$ June, 2020);*

(b) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Usafi wa Masoko ya Vyakula *(Performance Audit on Hygiene Control in Food Markets);*

(c) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo ya Vituo vya Huduma za Afya Nchini *(Performance Audit on the Management of Construction of Healthcare Facilities);*

(d) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Miradi ya Ujenzi kwenye Sekta ya Elimu inayotekelezwa kwa njia ya *"Force Account" (Performance Audit on Monitoring and Supervision of Construction Projects Implemented through Force Account in Education Sector);* na

(e) Taarifa ya Majibu ya Serikali na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu. Nakushukuru sana Mheshimiwa Silinde.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona ripoti zipo nyingi, ndiyo maana tunasema ukiwa Mbunge lazima uwe na juhudi ya kusoma na kupitia vitu, utaona *volume* na *volumes*.

Waheshimiwa Wabunge, sasa baada ya TAMISEMI kutupatia ripoti zao, niseme kwamba hatutakuwa na kipindi cha maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa udhuru kidogo asubuhi hii. Kwa hiyo, tutaendelea na maswali ya kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya hapo, niendelee kuwakumbusha kuendelea kujaza kipaumbele cha uchangiaji wetu katika kupitia mfumo wa Bunge mtandao unaopatikana katika dirisha la shughuli za Bunge. Wataalamu wa TEHAMA wapo katika maeneo ya ukumbi wetu, watakuwa wanapita humo. Kama unahitaji msaada wao, tafadhali unaweza ukawaambia, *ushers* hao wakakuitia ili uweze kuchagua ni Wizara gani ambazo ungependa upate nafasi ya uchangiaji. Kwa sababu ukisubiri siku hiyo, inawezekana katika maombi ambayo yako siku hiyo usipate nafasi. Nawe labda kama Mbunge ungependa sana Wizara fulani na Wizara fulani usikose kupata nafasi ya kuchangia kwa kusema.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tunaelewana katika hilo, ili tusilaumiane mbele ya safari, bora uonyeshe vipaumbele vyako mapema ili tuwe navyo.

Baada ya hilo, tunaendelea sasa. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Bado kuna hati hazijawasilishwa.

**SPIKA:** Aah, kuna hati! Ooh, bado, bado. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora). Samahani.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya *TEHAMA* kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Information Systems for the Financial Year Ended 30th June, 2020).*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deogratius Deo Ndejembi kwa uwasilishaji huo.

Sasa twende na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge wa Kojani, karibu sana Bungeni.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara ya mwanzo kusimama hapa naomba kwa idhini yako nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhna-huwataala. Pili nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini nami naahidi kujiaminisha. Kama mwana Falsafa alivyosema, wasia tatu ni vyema kuzingatiwa. Moja, unapoaminiwa ujiaminishe; pili, anapotajwa Mungu, basi usipite, mtangulize Mungu; na jambo la tatu subiri kichache upate kingi. Maana yake tutangulize subira.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Udhibiti wa Uchafuzi unaotokana na Taka za Plastiki kwenye Bahari na Maziwa *(Performance Audit on the Control of Plastic Wastes Pollution in Lakes and Ocean).*

**SPIKA:** Ahsante sana. Huyo ni Mbunge wa Kojani anaitwa Mheshimiwa Chande.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Karibu sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Uandikishaji na Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa *(Performance Audit on the Registration and Issuance of National Identification Cards).*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, Mbunge wa Uzini.

Waheshimiwa Wabunge, Watanzania wanataka kuwafahamu, ndiyo maana inanibidi niweke msisitizo. Ahsante sana.

Mheshimiwa Khamis, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi sasa, karibu sana *Engineer*.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

(a) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa Awamu ya Pili ya Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam *(Performance Audit on the Implementation of the Construction of Dar es Salaam Bus Rapid Transit (BRT) Infrastructure – Phase 2);* na

**SPIKA:** Ahsante sana. Huyo ni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe, yeye ni Mbunge wa Ileje.

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Mifumo ya Kudhibiti Ubora wa Vyakula Vinavyosindikwa Nchini *(Performance Audit on the Management of System for Quality Control of Processed Food).*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, tunaendelea.

Leo ripoti ziko nyingi! Kabla sijamwita Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi umewasilisha ripoti moja, ile ya pili bado. Ripoti ya ufanisi; ile ya matengenezo ya magari umewasilisha pia?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** *(Aliongea nje ya microphone)*

**SPIKA:** Zote mbili? Rekodi zangu zinaonyesha umewasilisha moja.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

(b) Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Matengenezo ya Magari ya Serikali *(Performance Audit on the Provision of Maintenance Services to Government Vehicles).*

**SPIKA:** Ahsante sana Eng. Kasekenya Msongwe. Kwa hiyo, zote mbili sasa zimewasilishwa.

Baada ya hapo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Tafadhali. kwa niaba yake, anakuja Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL B. SILLO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano kuanzia 2021/2022 – 2025/2026 *(The 3rd National Five Years Development Plan 2021/2022 - 2025/ 2026)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Hayo ni maoni ya Kamati ya Bajeti mtapata kwenye *Tablets* zenu muda mfupi ujao. Kwa kuwa tutakuwa na uchangiaji siku mbili tatu hizi, ni vizuri basi ukapitia na maoni ya Kamati ya Bajeti ili kujenga msingi wa uchangiaji wako pia katika eneo hili.

Katibu wa Bunge.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA**: Maswali ya Kawaida. leo tunaanza na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungaono na Mazingira), Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, uliza swali lako tafadhali.

Na. 32

**Mashimo Yaliyosababishwa na Ulimaji na Uchimbaji Madini**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufukia mashimo makubwa yaliyosababishwa na ulimaji wa barabara na uchimbaji wa madini hasa katika Mikoa ya Mara, Geita na Shinyanga?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Hamad Hassan Chande. Leo tunaanza na wewe moja kwa moja. Pole sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande. Leo tunaanza na wewe moja kwa moja, pole sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 inaelekeza maeneo yaliyoharibiwa kutokana

na shughuli za uchimbaji wa madini kurejeshwa katika hali yake awali ikiwemo kufukia mashimo, kupanda miti na kudhibiti taka. Aidha, wamiliki wa migodi yote wanatakiwa kuweka Hati Fungani *(Environmental Performance Bonds)* kama dhamana ya Usimamizi wa Mazingira katika migodi husika.

Aidha, Sheria ya Madini, Sura ya 123 inawataka wamiliki wote wa leseni za uchimbaji madini kuhakikisha uzingatiaji wa utunzaji wa mazingira katika maeneo ya uchimbaji wa madini ikiwemo ufukiaji wa mashimo yatokanayo na shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, Mikakati mbalimbali imewekwa ili kuzingatia utekelezwaji wa Sheria hizi ikiwemo:-

(i) Serikali kupitia Kamati ya Kitaifa ya Kufuatilia Utekelezaji wa Mipango ya Ufungaji Migodi inahakikisha hatua zote za urejeshwaji wa maeneo ya uchimbaji ikiwemo kufukia mashimo yaliyotokana na shughuli za uchimbaji zinazingatiwa ipasavyo; na

(ii) Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika migodi husika mara kwa mara imekuwa ikifanya ufuatiliaji na ukaguzi wa uzingatiaji wa matakwa haya ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, mashimo makubwa yote yaliyotokana na uchimbaji wa madini katika Mikoa ya Mara, Geita na Shinyanga yanapaswa kufukiwa. Serikali inaendelea kufuatilia na kuhakikisha kuwa matakwa haya ya kisheria yanazingatiwa. Aidha, kwa upande wa mashimo makubwa yanayotokana na ulimaji wa barabara, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kuhimiza uzingatiaji wa masuala ya hifadhi ya mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushuru Mheshimwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa chande kwa kuteuliwa kupata nafasi hiyo, tunakuombea kwa Mungu akusaidie ili uweze kuona mbele zaidi, kwake nina swali moja tu. Kwa kuwa humu ndani ameandika sheria nyingi za mazingira, sasa swali ni lini atafika kwenye Jimbo la Bunda kwenye Vijiji vya Nyabuzume, Jabulundu na maeneo yaliyoharibiwa na barabara inayojengwa ya lami kutoka Butiama -Nyamswa na Sanzati ili kuangalia athari za mazingira katika maeneo hayo? (*makofi*)

**SPIKA:** Swali zuri sana hilo, Mheshimiwa Chande majibu tafadhali, ni lini tu utatembelea huko na maeneo mengine Tanzania nzima.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, siku za karibuni mara tu baada ya Bunge kumalizika tutafuatana mguu kwa mguu mimi na yeye twende kuangalia hali hiyo na *insha Allah* tutekeleza. (*Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri chande. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo tulikuwa Bunda sasa tunakwenda Musoma Mjini, Mheshimwa Manyinyi uliza swali lako tafadhali.

Na. 33

**Bodaboda Zinazoshikiliwa – Vituo Vya Polisi kwa Muda Mrefu**

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO** aliuliza:-

Jeshi la Polisi linashikilia pikipiki nyingi katika Vituo vya Polisi kwa muda mrefu.

(a) Je, Serikali haioni fedha nyingi zinapotea kwa pikipiki nyingi kuchakaa zikiwa katika Vituo vya Polisi na hivyo kuleta hasara kwa Taifa?

(b) Je, kwa nini Serikali isiunde Kamati Maalum kila baada ya miaka mitatu kupitia sababu zilizosababisha pikipiki hizo zishikiliwe kwa muda mrefu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, Mbunge wa Uzini, Mheshimiwa Hamza Khamisi Khamisi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, pikipiki ni mojawapo ya chombo cha moto kinachotumika kufanya biashara ikiwemo kusafirisha watu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Kuna sababu tatu zinazopelekea kushikiliwa kwa pikipiki hizo kwenye Vituo vya Polisi:-

(i) Kundi la kwanza, ni zile pikipiki zilizokamatwa kwenye makosa ya jinai ambazo zimetumika kwenye kutenda makosa au zilizoibiwa toka kwa watu;

(ii) Kundi la pili ni zile pikipiki zilizokamatwa baada ya kutenda makosa ya usalama barabarani; na

(iii) Kundi la tatu ni zile pikipiki zilizookotwa na hazina wenyewe na kuhifadhiwa vituoni. Hivyo pikipiki hizi zipo vituoni kama vielelezo vya kesi na vielelezo ambavyo havina mwenyewe na kuwepo kwake kituoni ni kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufuatilia kwa ukaribu mashauri yote yaliyopo Mahakamani yanayohusu

vielelezo vilivyopo Vituo vya Polisi yamalizike kwa wakati ili mashauri hayo yasikae muda mrefu. Aidha, Pikipiki na vyombo vingine vya moto kuondolewa kwake vituoni kunategemea na amri ya Mahakama na maamuzi ya kesi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa tatizo hili si kubwa linahimilika, lakini iwapo tathmini itaonyesha kuongezeka ukubwa wa tatizo hili, basi Serikali ipo tayari kuunda Kamati Maalum kama ilivyoshauriwa na Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Spika asante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, tatizo sio kubwa.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimwa Spika, ahsante. Naomba kumuuliza Mheshimwa Naibu Waziri maswalli mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa. Swali la kwanza; ni ukweli usiopingika kwamba kama alivyosema ziko pikipiki ambazo labda wakati mwingine zinaokotwa na zinapelekwa pale. Kwa maana yake ni kwamba hakuna jalada lolote llinalofunguliwa kwenda mahakamani na matokeo yake pikipiki na magari kama hayo yanaweza kukaa zaidi ya miaka kumi.

Je, tunakubaliana kwamba sasa viendelee kukaa hapo na kuozea hapo au ni vizuri vikafanyiwa utaratibu mwingine ili hiyo fedha ikapatikana kwa ajili ya maendeleo ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wakati tunaunda Sheria ya kuruhusu bodaboda ili waweze kufanya kazi na kupata ajira kilichotokea ni kwamba zilezile faini zilizokuwa zinatumika kwenye vyombo vya usafiri ndio zilizochukuliwa na wakaanza kubandikwa bodaboda, lakini ikumbukwe kwamba bodaboda anabeba abiria mmoja, akikutwa na kosa analipa Shilingi elfu thelathini basi lenye abiria 60 akikutwa na kosa hilo hilo analipa elfu thelathini. Sasa napenda kujua ni lini Serikali itabadili hizi adhabu inayolingana na bodaboda ambayo ni ya chini ukilinganisha na adhabu iliyopo ambayo pia inatozwa kwa magari?

**SPIKA:** Umeeleweka Mheshimiwa Mbunge wa Musoma Mjini, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

Majibu ya maswali haya, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ameulizia, je, Serikali haioni haja ya bodaboda hizi ambazo zimelundikana katika vituo hivyo vya polisi basi ziuzwe au zipigwe mnada ili sasa Serikali iweze kujipatia mapato? Jibu ni kwamba, uwepo wa pikipiki hizi kwenye vituo hivi kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kutokana na sababu tofauti. Ukiziona pikipiki zimekaa kwenye Kituo cha Polisi usifikirie kwamba zimekaa kwa muda mrefu kwa sababu, utaratibu ni kwamba baada ya miezi sita endapo mwenye pikipiki yake asipokwenda kwenda kuikomboa pikipiki ama kulipa faini au taratibu nyingine akaziruhusu zikaendelea, maana pikipiki ile itaendelea kubakia pale.

Mheshimiwa Spika, baada ya miezi sita itaenda kupigwa mnada. Kwa hiyo inawezekana pikipiki hizo ambazo mnaziona kwenye Vituo vya Polisi ni kutokana na kwamba muda wake haujafika. Kwa mujibu wa taratibu hatutaweza kuipiga mnada ama kuiuza pikipiki ya mtu bila ya muda uliokusudiwa ama uliowekwa katika utaratibu kuwa haujafika.

Mheshimiwa Spika, utaratibu upo na kanuni na sheria zipo; ukiangalia kwenye *PGO,* ile 304 ukiangalia kwenye kifungu cha (1), (2), (3), (4), (5) na kuendelea imeelezwa Jeshi la Polisi limepewa *mandate* au limepewa mamlaka ya kuuza na kupiga mnada endapo itazidi zaidi ya miezi sita. Kwa hiyo hizo pikipiki zilizopo huko ni kwa sababu muda wake wa

kufanyiwa hivyo haujafika, utakapofika hazitaonekana hizo. Aidha, nipende kusema kwamba tuendelee kushirikiana kutoa elimu huko kwa vijana wetu ili wasiendelee kuzifikisha huko.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa swali la pili, anasema, basi litapakia watu zaidi ya 30 faini yake ni Shilingi elfu thelathini, bodoboda ambayo inapakia mtu moja faini yake ni Shilingi elfu thelathini; sasa Serikali haioni haja hapa sasa ya kufanya marekebisho? Serikali katika hili bado haijaona haya ya kufanya marekebisho ya hili. *The way* itakavyofanya marekebisho kwa sababu nilivyomfahamu Mheshimiwa tushushe, maana kama basi watatoa shilingi 80,000, maana yake bodaboda watoe shilingi 10,000.

Mheshimiwa Spika, hizi Shilingi elfu thelathini ambazo zimewekwa bado matukio yanaongozeka na lengo letu sio kuwakomoa wananchi ama kuwakomoa vijana watumiaji wa bodaboda na pikipiki, lengo ni watu kufuata sheria kuepuka na kupunguza idadi ya ajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka kufika Disemba, 2020 ajali za bodaboda ni 164; waliokufa ni 134 ambao wamekuwa *injured* 129 tu, tukizipunguza hizi tukisema sasa tuweke shilingi elfu kumi, vijana watazidi kufanya zaidi na hapo lengo na madhumuni ana uwezo wa kulipa Shilingi elfu kumi. Kwa hiyo tu niseme hatufanyi hayo kwa ajili ya kuwakomoa, tunafanya ili watu wafuate.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa kuna utaratibu, nimekuwa nauona sana kule Zanzibar, vijana wanajazana kwenye magari makubwa yanaitwa mafuso, wanakwenda ufukweni huko muda wanaorudi huko wanarudi na bodaboda pikipiki hazipungui 30 au 40 njiani, lazima ajali inatokea, sasa kwa sababu analipa shilingi elfu kumi watafanya vyovyote kwa hiyo.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba tunayachukua mawazo tutakapo ona haja ya kufanya mabadiliko ya hii sheria tutafanya lakini kwa sasa naomba tuwe na hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi)*

**SPIKA:** Nilidhani Naibu Waziri ameeleweka na makofi haya, Mheshimiwa Sanga bado umesimama tu, haya uliza swali lako.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, swali langu lilikuwa linaendana na haya mahusiano kati ya bodaboda na Trafiki na kule Makete mahusiano ya bodaboda na *traffic* ni kama Refa ambaye yuko uwanjani ana kadi nyekundu tu, mahusiano yao ni mabaya sana kwa kiwango ambacho *Traffic* wanatoza faini ya shilingi laki mbili, tofauti na utaratibu wa kawaida. Tumejaribu kufanya vikao vya *negotiation* kati ya sisi na watu wa Trafiki lakini imeshindikana. Pili, *Traffic* wanafuata bodaboda wangu mashambani kule Matamba, kule Makete, kitu ambacho ni kunyume na utaratibu. Sasa je, Mheshimiwa Naibu Waziri anatupa kauli gani na maelekezo yapi kwa Trafiki Mkoa wa Njombe hususani Wilaya ya Makete dhidi ya vitendo viovu ambavyo vinafanywa na wao dhidi ya bodaboda wa Makete? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Hamza Khamisi Khamisi, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wetu kwenye *PGO* na utaratibu uliowekwa kwenye ile sheria au kanuni ya 168 ambayo imefanyiwa mabadiliko mwaka 2002, umesema ni Shilingi elfu thelathini, sasa kama kutatokezea askari au yoyote ambaye anayehusika na hili akawatoza watu zaidi ya kiwango kilichowekwa maana huyo anafanya kosa kwa mujibu wa taratibu kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, watu kuwafuata huko, unajua mtu anapokuwa mhalifu kwa mujibu wa utaratibu vyombo vinavyohusika kumkamata vina uwezo wa kumfuta popote alipo endapo amefanya makosa, lakini sasa hiyo namna ya

kumfuata nayo ina utaratibu wake. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, kama kutakuwa kuna askari amechukua zaidi ya hizo, maana huyo anavunja sheria, nadhani Mheshimiwa tushirikiane katika hili kuweza kuwakamata na kama tunawajua tuwalete katika ofisi yetu, tujue namna ya kuwashughulikia kwa mujibu wa taratibu. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rita Kabati na Mheshimiwa Mbunge wa Arusha Mjini nimewaona tuanze na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati**.**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa ili tatizo la mlundikano wa pikipiki kwenye Vituo vya Polisi liko katika mikoa mingi, lakini utaona vijana wengi ambao wanakamatwa kuna wengine ambao hawana makosa yale ya kusema kwamba pikipiki ziwekwe kituoni. Hata hivyo, kuna wengine wameenda kukopa benki ili kama ni ajira kwa vijana, sasa wasema kwamba lazima miezi sita. Sasa ni kwa nini kusiwepo na kitengo maalum kwa sababu limeonekana hili ni tatizo karibu nchi nzima, cha kushughulikia hili tatizo la ukamataji wa bodaboda ili pengine kipindi kiwe kifupi miezi miwili au mitatu kwa sababu mengine ni makosa ambayo sio makubwa sana ya kuweka mpaka miezi sita na wengine wamepata ajali wamekufa na wengine wako hospitali? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu tafadhali;-

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa almaarufu Chilo, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na matukio ya mengi yanayotakana na namna ya uendeshaji wa biashara yenyewe ya bodaboda lakini pia *industry* nzima

hiyo ukilinganisha na hatua zinazochukuliwa katika kupambana katika kuweka utaratibu wa kufuata sheria katika kufanya biashara yenyewe ifanyike lakini pia usalama wa watu.

Mheshimiwa Spika, moja kati ya vyombo vinavyotumika sana kwa sasa kufanya uhalifu ni pikipiki kuliko hata magari na kwa hivyo kumekuwa na sababu tofauti tofauti ambazo zinapelekea ukamataji na wenyewe kuwa mkubwa. Wengine wengi ni rahisi akienda kufanya tukio lenye thamani kubwa au akapora au akafanya nini kuitelekeza pikipiki ni jambo jepesi, kwa hiyo tunajikuta tuna pikipiki nyingi ziko mikononi mwa polisi, lakini wahusika ama hawajulikani walipo wamezitelekeza na ndio maana zinaitwa mali zilizookotwa.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, kwa sababu *concern* ya Waheshimiwa Wabunge ni kubwa kwenye jambo hili na kwa sababu pengine sababu hizi tatu zilizotolewa katika jibu letu la msingi zinaonekana hazikuwatosheleza Waheshimiwa Wabunge, acha tukafanye tathmini ya kina na tutakuja na matokeo haya tueleze kwa kina katika pikipiki zilizokamatwa nchi nzima zilizopo kwenye Vituo vya Polisi ni ngapi; na ngapi zina tatizo gani na ngapi zina tatizo gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua ya muuliza swali la msingi kwamba tuone utaratibu wa kuzi-*dispose* kwa sababu tumesimamisha uchumi na yenyewe ni hoja ambayo ni *valid.* Tutakachokifanya katika tathmini hiyo tutaona kama tutapata wale waliopo husika, ili tuweze kuzipiga mnada. Kwa hiyo, nadhani tupewe muda, twende tukafanye tathmini ya jambo hili na baadaye tutoe matokeo yake hadharani.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri hayo. Mkijitahidi mpaka wakati wa bajeti yenu itasadia sana, maana uchangiaji mwingi inaelekea utakuwa ni bodaboda.

Mheshimiwa Mrisho Gambo, nilishakutaja, swali fupi.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri na Waziri lakini tumeona kwamba pamoja na faini ya bodaboda kuwa kubwa, lakini bado matukio ya uhalifu yameongezeka kwa hiyo ni ishara kwamba faini haiwezi kuzuia uhalifu, lakini ukiangalia pia katika utaratibu wa kawaida sasa hivi tuna changamoto kubwa ya ajira katika nchi yetu na Serikali yetu imeahidi kutoa ajira milioni nane na miongoni mwa watu ambao wanajiajiri sehemu yao ni bodaboda.

Mheshimiwa Spika, nadhani ni vizuri sasa Wizara ya Mambo ya Ndani ikaleta utaratibu hapa ili tuweze kupitia upya mchakato wa faini hizi kwa sababu tunafahamu mtu leo ukiua una adhabu yake, lakini pia leo mtu ukiiba kuku una adhabu yake, haiwezekani gari ambalo ni milioni mia tatu faini yake elfu thelathini na pikipiki ya milioni mbili faini yake elfu thelathini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa tunasema elfu thelathini kama ni kosa ni moja, bodaboda anaweza kupigwa makosa manne kwa siku akalipa laki na ishirini na pikipiki ile sio ya kwake, inabidi pia apekeleke hela kwa mwenye pikipiki na yeye pia aweze ku-*survive.* Nadhani Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma watu hawa wa bodaboda ili changamoto iweze kuondoka.

Mheshimiwa Spika, swali langu katika eneo hili tumeona watu wa *traffic* wamekuwa kwa kiwango kikubwa wanawakamata sana bodaboda pamoja na watu wa bajaji. Je, Wizara ya Mambo ya Ndani ina mpango gani wa kutoa maelekezo mahususi kwa watu wa *traffic* ili sio kila kosa analokamatwa nalo mtu lazima apigwe faini waweze kutoa onyo pamoja na utaratibu mwingine?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mrisho Gambo. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika naomba kujibu maswali mawili nadhani...

**SPIKA:** Hapana, hili la pili ndio swali lile lingine ulikuwa ni ushauri tu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa kukijitokeza baadhi ya askari wetu kutokuwa waungwana. Unajua shughuli hizi huwezi ukazi-*control* kwa sheria *per se a hundred percent.* Kwa hiyo, hekima, busara na hasa unapokuwa mtumishi wa Umma unayewatumikia watu lazima utumie hekima na busara. *Enforcement a hundred percent* na yenyewe huwa kidogo ina shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, lakini pia na Waheshimiwa Wabunge mtusaidie, baadhi ya vijana wetu wanafanya kusudi na ninyi wenyewe mashuhuda, mnaendeshewa vibaya sana bodaboda hata hapa mjini, tukiacha hii hali na yenyewe ni shida pia. Mimi niseme tu, sote tutekeleze wajibu wetu na kwa upande wa askari polisi, hasa wa usalama barabarani wajitahidi kuwa wanatumia busara katika kuhakikisha kwamba wanasimamia sheria siyo kukomoa.

**SPIKA:** Kwa kweli maswali kwenye eneo hili muda wake sasa umepita, inabidi tuendelee na maswali mengine, nawaomba radhi sana Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo, mtakubaliana nami kwamba Pasaka ya mwaka huu ilikuwa nzuri sana, hasa baada ya mtu kupigwa bao 4 – 1, kwa hiyo, nashindwa kujizuia kumpa nafasi Mbunge wa Kinondoni aulize swali. Mheshimiwa uliza swali lako tafadhali. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naona kijembe kimeingia sawasawa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nami niwapongeze kwa sababu *Simba Sports Club* wameisadia Tanzania kuonekana vizuri. Pia ule utaratibu wa kuitangaza Tanzania, "*Visit Tanzania",* kusema kweli ni jambo ambalo linafaa kuigwa hata na

wenzetu wa *Young Africans* pindi watakapopata nafasi ya kuingia katika mashindano haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu ni jepesi sana kuhusiana na bodaboda. Ni dhahiri kabisa biashara...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, umesikia maoni ya Mheshimiwa; muige mambo mazuri tunayofanya. Mheshimiwa endelea. *(Kicheko)*

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, biashara ya bodaboda ni nzuri sana kwa vijana wetu. Pale Dar es Salaam bodaboda wanafanya vitu ambavyo vinasababisha abiria ambao ni raia wa Tanzania, ni *very innocent,* wapate ajali, kupoteza miguu, mikono na wengine maisha yao kwa kupita kwenye alama za taa nyekundu bila kujali, kupita *no entry* bila kujali, kupita katika barabara za mwendokasi bila kujali na mambo haya yanafanyika mbele ya askari wa usalama wa barabarani. Je, ni lini Serikali itasimamia kidete kuhakikisha kwamba biashara hii inaendeshwa kwa utaratibu wa kisheria ili kupunguza na kuondoa ajali ambazo zinawafika watu wetu?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kweli hili tatizo ni kubwa sana. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hawa madereva wa bodaboda kwa kweli ni shughuli kubwa kuwasimamia. Sheria hairuhusu ku-*overtake* kushoto lakini ukiangalia wote utadhani wana chuo walichojifunza ambapo wamefundishwa ku-*overtake* kushoto. Nafahamu kwa nini wanafanya hivyo; wanafanya hivyo kwa sababu ku-*overtake* kulia wanakuwa kati ya gari moja na nyingine, si salama zaidi kwao. Madereva wa magari mtu aki-*overtake* kushoto jicho

lako linakuwa kulia zaidi, ni rahisi kama unakwenda kushoto ukaingia bila kutazama, ndiyo ajali nyingi zinatokea kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Spika, niseme tu, bado tuna kazi kubwa. Nami niwaagize tu Jeshi la Polisi Kitengo cha *Traffic* kuhakikisha kwamba madarasa yanafanyika ili kutoa elimu kwa sababu watu hawa tunawahitaji. Kuna *graduates* wanaendesha bodaboda, kuna watu wa *masters* wanaendesha bodaboda, kwa hiyo, siyo *industry* ya kuidharau, ni *industry* inayofanywa na watu wanapata riziki yao, lakini tuwaombe sana kwamba wazingatie sheria kwa sababu wanazifahamu lakini wanafanya kusudi. Jeshi la Polisi upande wa *traffic* wahakikishe wanatoa elimu kama tunavyofanya katika utoaji wa elimu ya usalama barabarani kwenye vituo vya bodaboda, wafundishwe namna ya kutumia chombo cha moto.

Mheshimiwa Spika, jambo hili nadhani liwe *concern* ya sisi sote kwa sababu kundi hili ni kubwa, askari wetu ni wachache, hawawezi wakafanya kwa kila mahali. Matajiri wa hizi bodaboda wako na humu ndani, kila mmoja akitekeleza wajibu wake tunaweza angalau kupunguza vifo vya hawa vijana, nguvu kazi kubwa ya Taifa inapotea. Ahsante sana.

**SPIKA:** Yaani Mbunge unamiliki bodaboda? Napiga marufuku kabisa, tuwaachie vijana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri niliwahi kusafiri miaka ya nyuma nikaenda Singapore. Nchi za Asia wanatumia pikipiki zaidi kuliko hata sisi, kwa kiwango kikubwa sana, lakini hawana hizi fujo tulizonazo. Sasa pale Singapore nikauliza hapa vipi? Nikagundua kitu kimoja, kule haya makosa madogomadogo ya bodaboda ame-*cross* au amefanya nini, askari wale wana viboko, wanachapa palepale halafu kesi imeisha, hakuna haja ya kukusanya mapikipiki vituoni, tandikwa palepale kesi imeisha anaendelea na safari na shughuli zake palepale. *(Makofi)*

Vitu vinginena ni ujana, yaani vinataka hatua palepale halafu mmemalizana palepale. Mzidi kuangalia haya mambo. Ni kweli kabisa ni *practical* na wanafanya. Wenzetu ni nchi iliyoendelea na imemaliza kabisa haya matatizo kwa kiasi kikubwa sana. Sasa hii ya kukusanya pikipiki kurundika kituoni miezi sita, mingapi, tuliangalie.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Fedha na Mipango; Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba aulize swali lake.

Na. 34

**Muundo wa Kada ya Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza kikamilifu Waraka Na. 3 wa mwaka 2015 kuhusu Muundo wa Kada ya Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani?

(b) Je, ni lini Kitengo cha Uhasibu na Fedha katika Wizara na Sekretarieti za Mikoa zitapewa hadhi ya kuwa Idara?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, *Engineer* Hamad Masauni Yussuf, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima pamoja na afya njema. Pia nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa imani yake aliyokuwa nayo kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo, naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, nijibu swali

la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Waraka Na. 3 wa mwaka 2015 kuhusu Muundo wa Kada ya Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani ulianza kutekelezwa mwezi Julai, 2018 kwa kutenganisha Kada ya Maafisa Hesabu na Wahasibu. Kwa mujibu wa muundo huo mpya Wahasibu na Wakaguzi ni wale ambao wana *CPA* na wale wasio na *CPA* wanatambulika kama Maafisa Hesabu na Maafisa Ukaguzi.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu kupandisha hadhi vitengo vya uhasibu na fedha katika Wizara na Sekretarieti za Mikoa kuwa idara, katika kuandaa miundo ya taasisi, vigezo kadhaa hutumika ili kufikia maamuzi ya kuwa Idara, Vitengo na Sehemu. Kwa kuwa miundo hii hufanyiwa marekebisho mara kwa mara kwa kushirikiana na wataalamu wa miundo kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kujadiliwa katika ngazi ya maamuzi, ni mategemeo yetu kwamba Serikali itakapoona kuwa Kitengo cha Uhasibu na Fedha kinakidhi vigezo vya kuwa idara, kitapewa hadhi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali ya kuridhisha kwa kiasi, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, pamekuwa na watumishi wengi ambao wamekaa muda mrefu, zaidi ya miaka kumi hadi ishirini wakiwa wanalilia suala la muundo huu ambapo umetoka Waraka Na.3 wa Mwaka 2015 bila kutekelezwa kwa wakati. Serikali ina mpango gani wa kupandisha vyeo vyao kwa mserereko ili kuzingatia muda waliotumia kazini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, suala la hadhi ya Kitengo cha Uhasibu, ni kweli Serikali inajibu juu ya vigezo ambavyo vinafanyiwa tathmini mara kwa mara na Ofisi ya

Rais, Utumishi. Natambua vigezo vyenyewe vinazingatia *job analysis* na *job design.* Kwa msingi huo, ni ukweli kada hii imeacha kutumia *local standards* kwa muda mrefu sana na sasa wanatumia *international standards* katika kutengeneza mizania mbalimbali ya taasisi. Vilevile hata ripoti za *CAG* tunaziona jinsi gani zinavyotoka tayari kila mmoja anahamaki juu ya kuiona hadhi ya taasisi inabebwa na sehemu au kitengo hiki. Tunao mfano, juzi tu taarifa ya *CAG* baada ya kuitoa tayari viongozi wa Serikali wametoa maelekezo magumu kwa *section* hii, yaani Wakuu wa Idara au Vitengo hivi.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho hadhi hii inategemea kazi kubwa wanayoifanya. Tayari uchumi na mipango wana hadhi ya Kurugenzi...

**SPIKA:** Mimi nilifikiri swali huwa linakuwa ni swali.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, ni swali, natengeneza hoja ya kuuliza swali la mwisho hili.

**SPIKA:** Hapana, unahutubia Mheshimiwa.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, basi kwa misingi hiyo miwili sasa Serikali haioni ni muda mwafaka wakifanya *analysis* yao wa kukipa hadhi Kitengo hiki cha Uhasibu na Idara ya Ukaguzi?

**SPIKA:** Umeeleweka; majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Watu wa Pwani hao maneno mengi. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza; kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mtemvu kwa kuwatetea watumishi hawa, lakini nimjulishe kwamba ni dhamira ya Serkali na Serikali imekuwa ikifanya hivyo kila mwaka kuhakikisha

kwamba inapandisha vyeo na hadhi za wafanyakazi na watumishi wake ambao wanafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba hao Wakaguzi wa Hesabu, Wahasibu pamoja na Wasaidizi wao watapandishwa vyeo pale ambapo hali ya bajeti itaruhusu lakini kwa kuzingatia vigezo ambavyo vimewekwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusiana na vigezo hivyo, kama ambavyo nimejibu katika swali lake la msingi ni kwamba utaratibu huu ambao umewekwa upo kwa mujibu wa Sheria ile ya Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi ambayo ndiyo imesababisha kutayarishwa Waraka huu Na.3. Kwa kuzingatia sheria hiyo na Waraka ule, ndiyo utaratibu huohuo ambao utaendelea kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi.

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Leo tumepokea taarifa ya *CAG,* tunashukuru. Nitawaletea *LAAC, PAC* na wengine wote wanaohusika na taarifa hizo. Ukizingalia tu kwenye *surface* unaona baadhi ya mambo yanayoendana na swali la Mheshimiwa Mtemvu. Baadhi ya Halmashauri zinakuwa na matatizo hayo kwa sababu tu ya aina ya Mhasibu. *Purely* Mhasibu anasababisha Halmashauri inatajwa hapa kwamba ina hati chafu, sijui hati nini, kwa sababu ya uhasibu wa aina ambayo ni mbovu kabisa. Wengine walifanya hivyo kwenye halmashauri moja wakahamishiwa kwenye nyingine na nyingine na kila wanapohamishiwa wanasababisha hizo hati za mashaka, chafu, oh, vocha hazionekani. Vocha hazionekani kwa nini? Sasa vocha anatunza nani kama siyo Mhasibu, anaipa jina baya halmashauri au chombo fulani cha Serikali. Kwa hiyo, muangalie sana na kwa sababu wahasibu hawa ni watu wa Wizara ya Fedha, ni vizuri kuwaangalia sana.

Pia la jumla, utakuta hati zenye mashaka, sehemu kubwa ya halmashauri ni Kanda ya Kati kiukaguzi. Kanda ya Kati halmashauri karibu zote za Tabora ziko kwenye kundi hilo, halmashauri zote za Singida, labda kasoro moja au mbili, halmashauri zote za Dodoma ziko kwenye kundi hilo. Kwa hiyo, ukitazama tu kwa ujumla wake unaona Mkaguzi wa

Kanda na yeye ana matatizo. Haiwezekani halmashauri zote za Dodoma, Singida, Tabora ziwe na shida. Kwa nini kanda nyingine haiko hivyo, ina maana hawa wa kanda hii tu ndiyo wabaya kiasi hicho?

Kwa hiyo, haya mambo yanataka muyaangalie kwa undani kidogo na kama kuna haja ya usaidizi basi kanda hii waondolewe hawa Wahasibu waletwe Wahasibu ambao wanafaa zaidi. Hata hivyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Mtemvu, swali lake ni zuri, linatusaidia. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa aulize swali lake.

Na. 35

**Kuweka Miundombinu ya Barabara Mbuga ya Ibanda na Rumanyika**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka miundombinu mizuri ya barabara katika Mbuga ya Ibanda na Rumanyika ili kuvutia watalii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii, Mary Francis Masanja, karibu sana kwa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu kwa kuendelea kuniamini kuhudumia Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe zilianzishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 509 na 510 la tarehe 05/07/2019. Hifadhi hizo zilitokana na kupandishwa hadhi kwa yaliyokuwa Mapori ya Akiba Ibanda na Rumanyika Orugundu.

Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha kufikika kwa hifadhi hizo, Serikali kupitia Taasisi za *TANROADS* na *TARURA* imekuwa ikitengeneza barabara mbalimbali zinazorahisisha kufika kwa watalii katika hifadhi hizo. Barabara hizo ni pamoja na Mgakorongo (Karagwe) hadi Murongo (Kyerwa) yenye urefu wa kilometa 112, ambayo inafanyiwa matengezo na *TANROADS* kila mwaka na imewekwa katika mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Vilevile barabara ya Omushaka – Kaisho – Murongo yenye urefu wa kilometa 120 imekuwa ikifanyiwa matengenezo kila mwaka na *TANROADS.*

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha uwepo wa miundombinu mizuri ya barabara ndani ya hifadhi, Serikali imetenga shilingi milioni 311.9 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kuchonga barabara yenye urefu wa kilometa 20 katika Hifadhi ya Taifa Rumanyika-Karagwe.

Vilevile, kwa mwaka 2021/2022, Serikali ina mpango wa kutengeneza barabara yenye urefu wa kilometa 51 katika Hifadhi ya Taifa Ibanda-Kyerwa; na barabara ya kilometa 20 katika Hifadhi ya Taifa Rumanyika-Karagwe.

Mheshimiwa Spika, ni imani yetu kwamba jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali za kuboresha miundombinu ya barabara katika Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe na maeneo mengine yote ya hifadhi zitasaidia kuweka mazingira mazuri ambayo yataziwezesha hifadhi hizo kutembelewa na watalii wengi waliopo katika maeneo ya karibu pamoja na wageni kutoka nchi jirani. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Mchungaji Innocent Sebba Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kinipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza niipongeze Serikali kwa juhudi zinazoendelea kuboresha miundombinu katika Hifadhi ya Ibanda na Rumayika.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwenye awamu iliyopita ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, alitoa maelekezo kuwekwa mipaka maeneo ambayo yalikuwa yamevamiwa na wananchi na akaelekeza maeneo haya yawekewe mipaka ili wananchi wasiendelee kuvamia yale maeneo, na Serikali ilileta wataalam wakaja kupitia maeneo yale. Baada ya kupitia, Serikali bado haijaweka mipaka kwenye maeneo hayo ya hifadhi na wananchi wameendelea kubugudhiwa. Je, ni lini Serikali itaweka mipaka inayotambulika ili wananchi hawa wasiendelee kusumbuliwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwenye hifadhi hizi pamoja na kutengwa sisi tunashukuru sana Serikali, lakini bado hatujaona juhudi za Serikali za kuweka vivutio ambavyo vitawavutia watalii. Ni lini Serikali italeta vivutio katika Hifadhi ya Ibanda na Rumanyika ili kuvutia watalii waje katika maeneo hayo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali lako la pili halijaeleweka Mheshimiwa Bilakwate; Serikali ilete vivutio tena wakati hifadhi zenyewe ndiyo vivutio?

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, samahani, kwenye hizo hifadhi hakuna wanyama, yaani hakuna vile vivutio ambavyo vinaweza kuwavutia watalii kuja kuangalia.

**SPIKA:** Sasa umeeleweka, wa-*translocate* wanyama. Naibu Waziri, tafadhali majibu, Mheshimiwa Mary Masanja.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa

Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, lenye kipengele (a) na (b), kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nianze na mipaka. Ni kweli Wizara ya Maliasili na Utalii imekuwa ikiainisha maeneo mbalimbali yanayohusiana na hifadhi kwa kuweka mipaka katika maeneo ambayo yanahusiana na uhifadhi. Katika Hifadhi ya Ibanda – Kyerwa na Rumanyika tulifanya tathmini baada ya wataalam wetu kwenda kuainisha mipaka na utekelezaji wake tunaendelea kuandaa mazingira ya kupeleka wataalam kwa ajili ya gharama za uthamini ikiwemo kuainisha maeneo yenye changamoto hizi za uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, lakini tunatoa maelekezo kwenye upande wa maeneo haya ambayo tayari yamesha ainishwa, kwamba wananchi ambao wanazunguka maeneo haya wasiendelee kubugudhiwa mpaka pale ambapo wataonyeshwa eneo ambalo linahitajika kwa ajili ya uhifadhi na maeneo ambayo wataachiwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upande wa vivutio. Serikali inatambua kwenye hifadhi hizi ambazo ni mpya ambazo tayari zimeshatangazwa, zina wanyama lakini baadhi hawapo, hasa vivutio vya wanyama wakali kama simba na tembo. Serikali ina mpango wa kupeleka mbegu za wanyama hawa ili kuimarisha maeneo yenye uhifadhi katika maeneo hayo ili kuendelea kuongeza idadi ya Wanyama katika hifadhi hizi, lakini pia vivutio mbalimbali vinavyohusiana na mambo ya mali kale na mambo mengine ambayo yanahusiana na vivutio. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tuendelee na Wizara ya Maji Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda.

Na. 36

**Mradi wa Maji wa Masukulu – Rungwe**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka wakaguzi ili kuhakiki thamani ya fedha ya Shilingi bilioni 15 zilizotolewa na Serikali kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa ajili ya mradi wa maji wa Masukulu ambao unaonekana kujengwa chini ya kiwango?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji (Mhe. Eng. Maryprisca Wilfred Mahundi, tafadhali majibu.

**NAIBU WAZIRI MAJI:** Mheshimiwa Spika; kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda Mbunge wa Rungwe Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika; ni kweli Serikali kupitia Wizara ya Maji ilitekeleza mradi wa Maji wa Masukulu katika Wilaya ya Rungwe ambao ulitenga kuhudumia vijiji viwili vya Ijigha na Masukulu kwa gharama ya Shilingi milioni 335.6 na si shilingi bilioni 15 kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Mbunge. Mradi huo ulihusisha ujenzi wa chanzo, tanki lenye ujazo wa lita 90,000 na vituo 13 vya kuchotea maji vimekamilika na vinatoa huduma kwa wananchi wapatao 3,706.

Mheshimiwa Spika; katika kuhakikisha vijiji vya Ijigha na Masukulu vinapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza; *RUWASA* Wilaya ya Rungwe inatumia chanzo cha maji cha Mto Mbaka ambacho kina cha maji kinatoa maji ya uhakika na tayari mradi huo umewekwa kwenye mpango wa bajeti ya *RUWASA* ya mwaka 2021/2022.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia nimekuona, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA,** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa majibu yaliyotolewa na Serikali, nilikuwa ninamuomba Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na mimi pamoja na Madiwani wa Wilaya ya Rungwe aweze kufuatilia uhalali wa majibu waliyompatia, hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kijiji cha Mpuguso Itula, Lukoba kinapata maji kutoka chanzo cha Kasyeto lakini, Kasyeto yenyewe ambayo inatoa chanzo cha maji wanakijiji wake hawapati maji. Je, ni lini Serikali itahakikisha watu hawa wa Kasyeto pamoja na Mpumbuli wanapata maji, maana wao ndiyo wanaotoa chanzo cha maji nao si wanufaika wa maji? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa majibu ambayo Serikali imeweza kutoa hapa ni majibu yenye uhakika. Hata hivyo tutatuma timu yetu kwenda kufanya uhakiki wa kuona uhalali wa maelezo ya Mheshimiwa Mbunge. Vilevile kwa vijiji vya Mpuguso na vijiji jirani, na vile vijiji ambavyo chanzo cha maji kinatokea kama ilivyo ada ya Wizara ya Maji vijiji ambavyo vinatoa chanzo cha maji huwa ndio wanufaika namba moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili ninaendelea kutoa maelekezo kwa watendaji wote wa Wizara ya Maji na RUWASA, pamoja na Mamlaka kuhakikisha maeneo yote ambayo yanatoa vyanzo vya maji lazima wawe wanufaika namba moja.

**SPIKA:** ahsante sana. Baada ya muuliza swali hasa watu walisimama hapa, ee tuanze na Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Serikali imeweza kutoa fedha nyingi sana za walipa kodi masikini kwenda kwenye miradi ya maji, lakini uhalisia ni kwamba miradi mingi sana haitoi maji kwa ukamilifu au mingine haitoi maji kabisa. Ningependa kujua, ni lini Serikali itafanya ukaguzi kwenye miradi yote nchi nzima ambayo haitoi maji ili sasa iweze kutubainishia bayana ni miradi ipi

kwa fedha kiasi gani zimewekezwa na haitoi maji kwa wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Maji tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli fedha nyingi zimeelekezwa katika miradi ya maji na ndiyo maana tatizo la maji linaendelea kupungua. Namna ambavyo tatizo lilikuwa huko awali ni tofauti na sasa hivi, na tayari sisi Wizara tunafanya kazi kwa makusudi kabisa usiku na mchana ili kuhakikisha kuona kwamba miradi yote ambayo haitoi maji itatoa maji. Tayari miradi ambayo ilikuwa ya muda mrefu haikuweza kutoa maji. Baadhi tayari inatoa maji na tayari watendaji wetu wanaendelea kufanya kazi. Tutahakikisha miradi yote ambayo maji hayatoki maji yatatoka bombani.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Keisha.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Serikali ilikuwa na nia njema sana ya sisi kuhamia Dodoma, na Dodoma sasa imekuwa ni sehemu ambayo ina mrundikano wa watu na maji pia yamekuwa hayatoshelezi. Je, ni lini Serikali itatekeleza ile adhma yake ya kuleta mradi wa Ziwa Victoria mpaka hapa Dodoma ili tuweze kupata maji hapa Dodoma?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** hilo swali muhimu sana. Mheshimiwa Waziri wa Maji, Maji Dodoma, *priority* namba moja.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana. Kubwa ni kwamba tulishafanya kikao mimi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dodoma na ukiwa kama mwenyekiti. Juzi Mheshimiwa Rais alitoa

maelekezo, na ameenda mbali zaidi ya kusema ukizingua, tutazinguana.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama Waziri wa Maji na timu yangu tumeshajipanga na tumeshafanya stadi tunahangaika kutafuta fedha...

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi la Halmashauri ya Rungwe linafanana sana na tatizo la Halmashauri ya Rorya ambayo kwa 2015/ 2020, Serikali ilitupa zaidi ya bilioni 7.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji zaidi ya miradi 12, lakini mpaka sasa ninavyozungumza hakuna mradi ambao umetekelezwa kwa kiwango cha 100% na wakandarasi wameshalipwa fedha na hawapo *site*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alifanya ziara mwezi wa kumi na mbili na akatoa maelekezo kwamba wakandarasi hao wakamatwe lakini mpaka leo ninavyozungumza hakuna mkandarasi aliyekamatwa badala yake kuna fedha inatoka kuja kukamilisha miradi ambayo kuna wakandarasi wamekula fedha.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni, je, lini Serikali sasa itaona umuhimu wa kuleta wakaguzi kwenye Halmashauri ile ili kujiridhisha ile fedha bilioni 7.9 kwa miaka ile mitano imetumika vipi na yule ambaye kweli ametumia hizo fedha pasipo kutimiza wajibu wake achukuliwe hatua zinazo stahiki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Kiswahili kweli kimeimarika, maana yake fikiria hicho ni Kiswahili cha Mbunge wa Rorya, safi kabisa, maana kile Kiswahili chenyewe hapa tungetafutana hapa. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Maji au Naibu kadri mlivyojipanga. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Winfred Mahundi, majibu tafadhali (*kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Chege kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilitoa fedha nyingi sana kwa Halmashauri ya Rorya, na swali lake anahitaji kujua lini wakaguzi watapelekwa kuona namna gani wale ambao walikula fedha wanashuhulikiwa. Sisi kama Wizara tayari tumeunda timu yetu ambayo itazunguka majimbo yote kuona kwamba miradi ambayo fedha ilitoka na wakandarasi wakafanya janja janja basi wanakwenda kushughulikiwa na kama kuna mtumishi yeyote wa Serikali aliweza kujihusisha pamoja na hawa wakandarasi na yeye sheria itafuata mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nipende kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi karibuni watafika Rorya na wote ambao wanastahili kutumikia sheria basi sheria itafuata mkondo wake.

**SPIKA:** Swali la mwisho, Mheshimiwa Kunti Majala, tafadhali.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya mimi kuuliza swali la nyongeza kwenye Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chemba ni kati ya wilaya ambazo zinachangamoto kubwa sana ya maji. Nilitaka kujua tu Serikali, ni lini itawapatia maji wananchi wa vijiji; Chandama, Changamka, Babayo, Maziwa pamoja na Ovada?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kunti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa Wilaya ya Chemba pia taasisi yetu ambayo iko pale inaendelea kufanya jitihada kuona vijiji hivi ulivyovitaja vinapata maji mapema iwezekanavyo. Naomba mtupe muda tuweze kufanya kazi, siku si nyingi kabla ya mwaka huu wa fedha tayari tutapunguza idadi ya vijiji ambavyo havina maji kwa Chemba.

**SPIKA:** Ahsante Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kamishna Fakharia Shomar Khamis, uliza swali lako.

Na. 37

**Hitaji la Soko la Matunda Ndani na Nje ya Nchi**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta soko la uhakika la matunda ndani na nje ya nchi pamoja na kuanzisha viwanda vya kusindika matunda ili kufanya kilimo cha matunda kuwa chenye tija?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa utafutaji masoko ya ndani na nje kwa mazao na bidhaa mbalimbali, ikiwemo masoko ya matunda ni jukumu endelevu. Utekelezaji wa jukumu hilo huhusisha taasisi zetu kama *TanTrade*, Balozi za Tanzania nje ya nchi, Bodi za mazao, Soko la Bidhaa za Mazao na sekta binafsi. Lengo la kutumia balozi zetu nje ni kupata taarifa za kina kuhusu mahitaji ya masoko ya mazao na bidhaa za Tanzania katika nchi husika.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali katika kutafuta masoko unahusisha uhamasishaji wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kupitia taasisi zetu za uwekezaji *TIC, EPZA,* Balozi zetu nje pamoja na Serikali ngazi za Wilaya na Mikoa. Uhamasishaji huo unaenda sambamba na kutoa vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi kupitia sheria za uwekezaji pamoja na zile za Uendelezaji Maeneo Maalum ya Uwekezaji yaani *EPZ* na *SEZ*. Aidha, Serikali kupitia Taasisi za *SIDO, NDC* na *EPZA* inaendelea kutoa ushauri wa namna ya kuanzisha viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya aina mbalimbali ikiwemo vya kusindika matunda na kuvilea ili viweze kukua na kuweza kuwa soko kwa matunda yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Juhudi za Serikali ni kuhamasisha uanzishaji wa viwanda na ambapo juhudi hizo zimezaa matunda ambapo kwa sasa kuna viwanda viwili vikubwa vya kusindika matunda katika Wilaya ya Bagamoyo ikiwa ni vya *Elven Agri Co. Ltd* na *Sayona Fruits Co. Ltd* vyenye uwezo wa kusindika tani 28 za matunda kwa siku na kuajiri jumla ya wafanyakazi 755.

Mheshimiwa Spika, viwanda hivyo hutoa soko la uhakika la matunda kwa wakulima mbalimbali hapa nchini. Aidha, ili kuwa na uhakika wa malighafi za kutosha kwa mwaka mzima, tunashauri Mheshimiwa Mbunge kuendelea kushirikiana na Serikali kuhamasisha uzalishaji wa aina mbalimbali za matunda yatakayotumika katika viwanda hivyo ili viwanda hivyo viweze kupata malighafi za uhakika kwa kipindi kirefu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fakharia, ee maswali mengi ya nyongeza hapa.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza sina budi kuishukuru Wizara kwa jawabu zuri lenye mantiki ambalo linaeleweka na linalofahamika. Itakuwa ni hasa Watanzania wengi watalifurahia jawabu hilo kutokana na maelezo yake aliyojipanga.

Mheshimiwa Spika, lakini nina maswala mawili ya nyongeza. Kwa kweli matunda kama mananasi, matikiti, machungwa, embe n.k huwa yanazaliwa kwa wingi na yanakosa soko na yanaharibika mitaani. Je? Serikali inawaambia nini wananchi wa mikoa hiyo wanaozalisha matunda kwa wingi mbinu ya kunusuru matunda hayo ili yaweze kukaa kwa muda mrefu? *(makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa tunazungumza Tanzania ya viwanda na ninakubaliana na maelezo yako, lakini ningeiomba Serikali ikawahamasisha wazawa wa Tanzania wa kila mkoa wakaweza kuanzisha viwanda ili kila mkoa ukawa na viwanda vya kusindika au cha kufanya juhudi yoyote ili mikoa inayozalisha matunda kwa wingi iweze kuyanusuru matunda yao na iweze kufanikiwa na wanachokilima kiwape faida yao? Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe majibu.

**NAIBU WAZIRI VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunajua changamoto ya upotevu wa mazao yaani *(post harass losses)* kwa ujumla wake na hasa katika msimu ambao kunakuwa na mavuno mengi, kwa maana ya matunda mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango Madhubuti, kwanza wa kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo ambavyo Waheshimiwa Wabunge kila mmoja maeneo yake anaweza kuwa na viwanda hivyo ambavyo vinaweza kuchakata mazao haya au matunda hayo kwa muda ambao yanakuwa yamezalishwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, lakini pili kupitia SIDO tuna teknolojia na viwanda vidogo vidogo vingi ambavyo

vinachakata mazao ya matunda lakini pia teknolojia ya kukausha ili kuyatunza matunda hayo yasiweze kuharibika, yaweze kutunzwa ili yasiweze kupotea kabla ya kutumika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo nashukuru kwa ushauri wa Mheshimiwa Mbunge; kwamba Serikali tunaendelea kuhamasisha kweli uanzishaji wa viwanda lakini pia na teknolojia nyingine ikiwemo kuwa na vyumba maalum *cold rooms* ambazo ni *facility* za kutunza matunda kabla ya kuuza yaweze kukaa kwa muda mrefu ili angalau yaweze kudumu yasiharibike haraka.

Mheshimiwa Spika, tunachukua ushauri wake lakini tunaendelea kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo, lakini pia kupitia masharika yetu tuna teknolojia mbalimbali ambazo tunawakaribisha Waheshimiwa Wabunge kupitia SIDO na taasisi zetu nyingine waweze kupata teknolojia hizi ili ziweze kuwasaidia katika kutunza matunda ili yasiweze kupotea wakati wa mavuno mengi.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Mbunge wa Liwale, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Ni kwamba, Serikali yetu sasa hivi imeingia kwenye mfumo wa Serikali ya viwanda na uhamasishaji huu umekuwa mkubwa sana. Katika Wilaya ya Liwale viko viwanda vidogo vidogo kazi yake ni kusindika korosho, lakini wananchi wale wanashindwa kupata mali ghafi kwa sababu ya kuwa na mitaji midogo. Tunafahamu kwamba korosho, zinazalishwa, zinauzwa kwenye minada; na kwa sababu wale wawekezaji ni wadogo wadogo hawawezi kuingia kwenye mnada matokeo yake anapoingia kwa wananchi kwenda kununua korosho anaoneka wananunua kangomba.

Mheshimiwa Spika, je, sasa Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wale wadogo wadogo kupata mali ghafi hii ya korosho ili vile vikundi vyao vya kubangua korosho viweze kubangua kwa msimu mzima au kwa mwaka mzima?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la mwisho kwa siku ya leo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kigahe tafadhali.

**NAIBU WAZIRI VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kutoka Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli usindikaji wa zao la korosho angalau sasa unaimarika kwa sababu sasa tumehamasisha uanzishaji na kufufua viwanda vingi vya kusindika korosho.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaweka utaratibu maalum baada ya kuona changamoto hiyo inayowapata wazalishaji au wabanguaji wa korosho wa viwanda vya ndani kutokana na ile changamoto ya kuweza kutokununua kwenye minada.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo ni kwamba wale wote wenye viwanda vya kuchakata au kubangua korosho ambao wanazalisha kwanza kabla ya kufungua msimu wa mnada huwa tunawapa kipaumbele wao kwanza, wanunue waweze kutosheleza mahitaji yao halafu zile korosho zinazobaki ndizo zitaingizwa kwenye mnada wa jumla. Lengo ni hilohilo kuwalinda, kulinda viwanda vyetu vya ndani ili viweze kupata *raw material* au malighafi ya kutosha kabla ya kuingia kwenye ile *competition* ya mnada mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Liwale kwamba hilo tutalichukulia kwa umakini sana kuhakikisha viwanda vyetu vya ndani vinapata malighafi za kutosha ili waweze kuzalisha kadri ya uweze ambao viwanda hivyo vimesimikwa.

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, na leo tuna mambo mengi mazito yanakuja mbele, naomba nichukue nafasi hii kuwatambulisha wageni tulionao Bungeni, Viongozi Waandamizi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu Emmanuel Mpawe Tutuba, Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya

Fedha, Makofi Waheshimiwa Wabunge kwa Katibu Mkuu Mpya wa Wizara ya Fedha. (Makofi)

Ahsante sana, tunakukaribisha sana Bungen, muda wako mwingi sana utafanya kazi na Waheshimiwa Wabunge hawa hasa kipindi hiki cha Bajeti na wakati mwingine wowote tunakuhakikishia kukupa kila aina ya ushirikiano wewe na timu yako yote tunamatazamio makubwa kwamba utalisaidia Taifa hili, ahsante sana.

Manaibu Katibu Wakuu wako watatu, yuko Naibu Katibu Mkuu Ndugu Adolf Chasifu Ndunguru, karibu sana, yuko Katibu Mkuu Amina Hamis Shaaban, ahsante Amina, yuko Naibu Katibu Mkuu Khatib Malimi Kazungu. Karibu sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Maafisa kumi kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wakiongozwa na *CAG* mwenyewe Ndugu Charles Kichele, karibu sana *CAG*, Naibu *CAG* na maafisa wako wote mliofuatana na tunashukuru kwamba Taarifa za Kazi za Mwaka 2019/2020 zilizo nyingi zimewasilishwa hapa tayari leo. *(Makofi)*

Kwa niaba ya Bunge hili ningependa tuwapongezeni sana kwa kazi nzuri mnayoendelea kufanya na mnafanya kwa wakati na kwa haraka tunaendelea kuwategemeeni sana katika siku zijazo katika kazi yetu muhimu sana. Niwahakikishie ushirikiano wa Bunge kupitia kamati zetu mbalimbali na hata Bunge zima na kwamba taarifa zenu tunazithamini sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

wageni Waheshimiwa Wabunge, wageni25 ambao ni wanawake wajasiliamali kutoka Mkoa wa Simiyu wakiongozwa na Madam Rahel Haima, Rahel Haima na timu yako, ahsanteni sana. Hawa ni wamama wajasiliamali kutoka kule Simiyu wamekuja kuangalia namna ya ujasiliamali unavyoendelea katika Mji Mkuu wa Tanzania Dodoma na wanatembelea maeneo mbalimbali pia watapata nafasi ya kumtembelea Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mizengo Pinda na kuona shughuli zake za kilimo. *(Makofi)*

Katika mizunguko yao hiyo wamependa pia kufika Bungeni na kuona shughuli zinazoendelea. Nafikiri mnaona jinsi ambavyo wamama katika masuala ya ujasiliamali wanavyozidi kujipanga kisawasawa. Nawapongezeni sana, sana, tunawatakia kila la kheri na bahati nzuri mmekuja siku ambayo hata Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha yupo naye anaona. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kutoka Mfuko wa Wanyama Pori Duniani, *World Wildlife Fund* wakiongozwa na Dkt. Severin Kalonga pia wameambatana na Mabalozi wawili wa Uhifadhi wa Mazingira ambao ni wasanii wa muziki wa kizazi kipya. *WWF!* karibuni sana, karibuni sana Dodoma, karibuni sana wanamazingira wenzangu, mbarikiwe sana. *(Makofi)*

Lakini wapo hawa Mabalozi ambao ningependa kuwatambulisha kipeke yake, yupo Benard Paul Mnyang'anga, yeye anaitwa Ben Paul! Karibu sana Ben Paul. Lakini pia yuko Mwasiti Almas, karibuni sana, sana muendeleze juhudi hizi za masuala yanayohusiana na Hifadhi ya Mazingira, kwasababu kwa kweli kama kuna eneo moja wapo ambalo linapaswa kutazamwa kipekee katika nchi yetu ni eneo hili la hifadhi ya mazingira. Kwasababu maeneo mengi yameharibika mno. *(Makofi)*

Hata maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge mnalalamikia barabara! Barabara, panahitajika daraja mahali pengi ni kutokana na uharibifu wa mazingira ambao unasababisha makorongo, kuharibika kwa barabara, maji yanakimbia hovyo, barabara ndio zimekuwa mfereji wa maji kupita, kwa hiyo, gharama za matengenezo ya barabara zinakuwa kubwa sana lakini ni kwasababu ya uharibifu wa mazingira. Nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mnafahamu Waheshimiwa tunaendelea na Bunge *Sports Club*, wale wa mazoezi kila siku kupitia michezo mbalimbali, niwatangazieni kwamba siku ya Jumatatu tutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa Bunge *Sports Club*.

Jumatatu ijayo, kwa hiyo, naomba kuanzia leo mpaka mwisho iwe Jumamosi tuchukue fomu kwa Katibu wetu Ndugu Kizingiti wale ambao tungependa kuwa viongozi, kwa nafasi mbalimbali za *Bunge Sport Club*. Kwanza tupate Makepteni ikiwezekana na wasaidizi wao kwa kila mchezo, Kepteni wa *Netball, wa Football, wa Volleyball,* wa mchezo wa kuvuta Kamba*,* wa *Basketball* tuwapate hao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wale wenye *interest* mtajaza fomu. Na siku hiyo ya Jumatatu basi wachezaji wa hiyo michezo watatuchagulia viongozi wao. Lakini pia tutampata mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*, Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* na wale wajumbe watano wanaoingia kwenye Kamati ya Uongozi, katika wale wajumbe watano ni lazima wanawake wasipungue wawili. Wanaweza kuwa zaidi ya hapo lakini wasipungue wawili. Kwa hiyo, fomu zitapatikana kwa Ndugu Kizingiti kuanzia kesho, hata kuanzia leo mpaka Jumamosi.

Wako Wageni Watano wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango ambao ni watoto wake. Naomba niwatambulishe, wasimame mmoja mmoja, Joshua Mwigulu, Karibu sana Joshua, yuko Isack Mwigulu Nchemba, Isack karibu sana. Halafu yupo Gracious, karibu sana , Gracious, oooh, *you are gracious,* yupo Nazareth Jonas, na yupo Veronica Jackson, karibuni sana, karibuni sana. Hawa ni Watoto watano wa Mheshimiwa Waziri, naweka msisitizo! Wale ambao ana taarifa zao. *(Makofi/Kicheko)*

Maana mwalimu wangu alinifundisha zamani hizo kwamba wenye uhakika wa idadi ya Watoto ni wanawake, akikwambia nina watoto wawili ana maanisha wawili, akikwambia na mmoja ana maanisha mmoja, akikwambia nina kumi kwakweli ni kumi lakini wanaume ukijigamba nina Watoto wawili, wee bwana weee! Kuna siku utaitwa ofisi ya Spika huko, unakuta mwanao huko sasa sijiu tunafanyaje hapo. Ahsante, ahsante yote mema, karibu sana wanangu, karibuni sana. *(Kicheko)*

Katibu Sasa!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2021/2022 – 2025/2026**

**SPIKA:** Ahsante sana, moja kwa moja sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ili atuwasilishie sasa ule Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, karibu sana. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mungu kwa kutujalia uzima na afya na kutuwezesha kukutana tena kwa ajili ya kupokea na kujadili kwa mara ya pili na kuidhinisha mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yaani 2021/2022 – 2025/2026 kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni ya 113 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee na kwa masikitiko makubwa napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, Chama Cha Mapinduzi na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Msiba huu umekuwa pigo na umeleta majonzi kwa Taifa letu kutokana na uongozi wake mahiri, uchapa kazi, uzalendo uliotukuka wa kulitumikia Taifa letu. Mwenyezi Mungu ampumzishe mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kutoa pole kwa Taifa kwa kuondokewa na Viongozi wetu wakuu nikianza na Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Balozi Mhandisi John Kijazi

aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Aidha, nimpongeza Makamu Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania. Wote tuwaombee afya njema na Mungu awape nguvu mpya ili waendelee kulitumia Taifa letu na kipekee kuiendeleza kauli mbiu ya kazi iendelee.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumpongeza Balozi Hussein Katanga na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kushika nafasi hizo muhimu katika uongozi wa nchi yetu. Na kipekee, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muunganzo wa Tanzania kwa kuonesha Imani yake kwangu na kuniteua kuwa Waziri wa Fedha na Mipango na uteuzi wa Makamu wa Rais na uteuzi wangu, umeonesha Mheshimiwa Rais ana Imani kubwa sana na wana Yanga. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walishangilia)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, wanasema nirudie. Inaonesha uteuzi wa Mheshimiwa Makamu Rais na uteuzi wa Waziri wa Fedha unaonesha Mheshimiwa Rais ana imani kubwa sana na wana Yanga. Hasa ukizingatia historia ya ukombozi wa Taifa hili. *(Makofi/ Vigelegele)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha una nusu saa tu ya kuwasilisha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Eng. Hamad Yusufu Masauni, Mbunge na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walionipa katika maandalizi

ya Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa ya Miaka Mitano Mwaka 2021/2022 – 2025/2026 wakiongozwa na Katibu Mkuu mpya Ndugu yetu Emmanuel Tutuba.

Mheshimiwa Spika, pia nitoe pongezi, shukrani za dhati kwa Wizara, Taasisi, Idara za Serikali, Sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo, Asasi zisizo za Kiserikali na Wadau mbalimbali waliotoa maoni na michango katika kukamilisha Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, CCM, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, CCM, kwa maoni yao wakati wa majadiliano ya vikao vya Kamati. Aidha, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti yaliyoletwa katika vikao vya mwezi Januari na Machi, 2021 pamoja na mjadala wa Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililojadili mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano kwa muda wa siku tano, kuanzia tarehe 02 Februari, 2021 yamezingatiwa katika uandaaji wa mapendekezo wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, Serikali imezingatia kikamilifu maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge katika Taarifa ninayoiwasilisha. Majibu ya hoja zilizoibuka wakati wa Kamati ya Bunge ya Kudumu pamoja na Bunge lako Tukufu yamewekwa kwenye Kiambatanisho Na.1.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano yameandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo yaani 2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi mwaka 2020 – 2025, Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa 2011/2012 – 2025/2026, matokeo ya tathmini huru ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa

Miaka Mitano, Sera na Mikakati mbalimbali ya kisekta, Dira ya Afrika ya Mashariki 2050, Dira ya Jumuia ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika 2050, Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika na Mpango wa Maendeleo Endelevu 2030.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano una dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Mpango huu, una maeneo makuu matano ya kipaumbele ambayo ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara na kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kimegawanyika katika Sura Nane. Niombe nitumie fursa hii kuomba Taarifa yangu yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge. Sura ya Kwanza ni utanguliza ambao unaelezea chimbuko na historia ya Dira ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Maendeleo kwa ujumla. Sura ya Pili, inahusu mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa 2016/2017 – 2020/2021 ambayo yana msingi wa maandalizi wa Mpango wa Tatu ambao unaendeleza mafanikio yaliyopatikana na kutatua changamoto zilizokabili utekelezaji wa Mpango wa Pili.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Tatu, imejikita katika masuala ya Maendeleo ya Sekta Binafsi ikiwa ni msukumo wa kujenga sekta binafsi na kushirikiana katika utekelezaji wa Mpango utakaoendelea.

Sura ya Nne, inaelezea dhana ya kujenga uchumi shindani, maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu. Sura ya Tano, inaainisha hatua mahsusi za kuchukuliwa katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango. Sura ya Sita, inahusu ugharamiaji na utekelezaji na Mpango. Sura ya Saba, inaainisha mpangilio wa utekelezaji wa Mpango na Sura ya Nane, inaainisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha mpango huu unatekelezwa kikamilifu, Serikali inaendelea na maandalizi ya mikakati ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ikijumuisha mikakati ya utekelezaji, mikakati ya ugharamiaji na mkakati wa ufuatiliaji na tathmini ya Mpango.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini na utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano uliopita, viashiria vya kiuchumi kwa ujumla, tathmini ya utekelezaji ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano inaonesha kuwa katika kipindi cha miaka Minne ya utekelezaji wa Mpango, pato la Taifa lilikuwa kwa wastani wa asilimia 6.9, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 4.1 kwa mwaka ikiwa ni ndani ya lengo la kutozidi asilimia 5. Akiba ya fedha za kigeni ilijitosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.9 ikiwa ni zaidi ya lengo la miezi minne.

Mheshimiwa Spika, na nakisi ya Bajeti ikiwa ndani ya lengo la kutozidi asilimia 3 kwa kipindi chote. Katika kipindi kipindi hicho, deni la Serikali lilikuwa himilivu katika muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Vilevile, pato la wastani la kila mtu liliongezeka kutoka shilingi 2,225,099 sawa na dola za Kimarekani 1,022 kwa mwaka 2016 hadi shilingi 2,577,967 sawa na dola za Kimarekani 1,080 kwa mwaka 2019. Kielelezo kikuu cha mafanikio ya Utelekezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa ni Tanzania kufanikiwa kuingia katika kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati cha chini mwezi Julai, 2020.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda, utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano, ulijikita katika kujenga viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini hususan kilimo, madini na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji

wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika uzalishaji viwandani, mafanikio ni kujengwa kwa jumla ya viwanda 8,477 kati ya mwaka 2015 – 2019 ambapo viwanda vikubwa ni 201, vya kati ni 460, vidogo ni 3,406 na vidogo sana ni 4,410. Ujenzi wa viwanda hivyo umeongeza idadi ya viwanda nchini kutoka viwanda 52,633 mwaka 2015 hadi viwanda 61,110 mwaka 2019. Viwanda hivyo, vimechangia ongezeko la uzalishaji wa bidhaa mbalimbali katika soko la ndani na la nje ikijumuisha bidhaa za ngozi, nguo, ujenzi (nondo, mabati, saruji, misumari, marumaru pamoja na rangi), plastiki, zana za kilimo pamoja na vinywaji.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji huo umeleta mafanikio yafuatayo: kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Viwanda katika pato la Taifa kutoka asilimia 7.9 mwaka 2015 hadi asilimia 8.5 mwaka 2019. Kwa upande wa kilimo, mafanikio yaliyopatikana ni baadhi ya shughuli zilizotekelezwa, pamoja na kujengwa na kuboreshwa kwa miundombinu ya umwagiliaji, ambayo imeongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 461,376 mwaka 2015 hadi hekta 694,715 mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 36,614 mwaka 2015 hadi tani 76,726 kwa mwaka 2020. Mafanikio mengine ni kukamilika kwa ujenzi wa maabara ya mbegu katika makao makuu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo Morogoro na kuanzishwa kwa soko la bidhaa la pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kujenga kiwanda kipya cha *Kilimanjaro International Leather Industries*, kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhamilishaji cha *NAIC*, kujengwa kwa viwanda vipya vya kimkakati vya nyama. Pamoja na kujengwa kwa kiwanda cha maziwa cha *Galaxy Food and Beverage Company Ltd.* na kujengwa kwa kiwanda cha kuzalisha

chanjo, pamoja na kuendelea kuboresha huduma za malisho ya mifugo na majosho.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji huu, umewezesha mafanikio yafuatayo: kuongezeka kwa viwanda vya kusindika nyama nchini kutoka 25 mwaka 2015/2016 hadi viwanda 32 mwaka 2019/2020; viwanda vya kusindika maziwa kutoka 82 mwaka 2015/2016 hadi viwanda 99 kwa mwaka 2019/2020; na kuongezeka kwa usambazaji wa mitamba katika mashamba ya Serikali kutoka mitamba 11,449 mwaka 2015/2016 hadi mitamba 18,255 kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa shughuli za uvuvi kupitia utekelezaji wa Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015, Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni za Uvuzi za mwaka 2009, pamoja na kutungwa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 5 ya Mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na kupambana na uvuvi haramu kupitia doria na ukaguzi mbalimbali. Hatua hizi zimefanikisha kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki katika maji ya asili kutoka tani 362,645 mwaka 2015/2016 hadi tani 497,567 kwa mwaka 2019/2020. Vile vile, kumetokea mafanikio ya kuongezeka kwa usindikaji wa minofu ya samaki aina ya sangara kutoka tani 23,000.58 mwaka 2015/2016 hadi tani 27,596.27 kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini, kupitia na kutunga sheria, sera na mikataba ya madini ambapo imewezesha kuundwa kwa kampuni ya ubia ya *Twiga Minerals Cooperation* ambapo imetoa gawio la shilingi bilioni 100. Hiyo ni moja ya mafanikio ambayo yamepatikana katika utekelezaji wa Mpango uliopita.

Mheshimiwa Spika, mengine ni pamoja na kuanzishwa kwa kampuni ya *Tembo Nickel Cooperation Ltd.;* kujengwa kwa masoko 39 ya madini na vituo 41 vya kuuzia madini; kukamilika kwa ujenzi wa vituo vinne vya umahiri katika

maeneo ya Bariadi, Musoma, Bukoba na Handeni; kuendelea na ujenzi wa vituo vya Songea, Mpanda na Chunya; kujenga ukuta wenye mzingo wa kilometa 24 wa Mererani Mkoani Manyara; na kukamilisha ujenzi wa vituo vitatu vya mfano vya uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo, ambavyo viko katika maeneo ya Geita, Itumbi, Chunya pamoja na Katente iliyoko Bukombe.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zimechangia kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini kutoka Dola za Kimarekani bilioni 1.91 sawa na shilingi trilioni 4.46 za mwaka 2015/2016 hadi Dola za Kimarekani bilioni 2.9 sawa na shilingi trilioni 6.77 mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maliasili na utalii, mafanikio yaliyoonekana ni kuongezeka idadi ya watalii na mapato, kupitia mradi wa kujenga uwezo katika Hifadhi ya Taifa, kudhibiti ujangili kwa asilimia 90 na kubadilishwa na kupandishwa hadhi kwa mapori ya akiba ya Nyerere, Burigi, Kigosi, Ugalla, Ibandakyerwa na Rumanyika kuwa Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, mengine ni kuendelea kutangazwa kwa vivutio vya utalii katika nchi mbalimbali hapa duniani. Hatua hizi zimechangia kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia hapa nchini kutoka watalii 1,137,182 mwaka 2015 hadi watalii 1,527,230 mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ufungamanishaji wa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Ujenzi wa miundombinu na upatikanaji wa huduma za afya, maji, elimu umeongeza kasi ya ufungamanishaji wa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuendelea kutoa huduma za kupandikiza uroto *(born marrow transplant)* na

kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za dharura na ukarabati wa jengo la *X-Ray* katika Hospitali ya Rufaa ya Dodoma; kukamilika kwa asilimia 98.2 ya ujenzi wa Hospitali ya Uhuru iliyopo hapa Dodoma; kununuliwa kwa mashine za *digital X-Ray* na *Ultra-sound*, vifaa vya maabara na mashine za kiuchunguzi wa Kifua Kikuu na vimelea *(BACTAC 960)* pamoja na *Blood Culture Machine* katika Hospitali ya Rufaa ya magonjwa ya Kifua Kikuu, Kibong'oto na ununuzi wa mashine za *Rectum Scan* kwa ajili ya Hospitali ya *Ocean Road*.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kujenga na kuboresha miundombinu ikijumuisha jengo la huduma za upasuaji la jiolojia na jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje, maabara na jengo la mama na mtoto katika Hospitali za Rufaa za Mara, Geita, Songwe, Katavi, Sekoutoure kule Mwanza na Hospitali za Rufaa za Kanda ya Kusini Mtwara na nyanda za juu za Kusini Mbeya na Hospitali ya Kanda ya Kaskazini, *KCMC* na Hospitali ya Kanda ya Ziwa Burigi Geita.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zimechangia kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 62 mwaka 2015/2016 hadi miaka 66 mwaka 2019/2020; kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka wastani wa vifo 67 kwa vizazi 1,000 mwaka 2014/2015 hadi wastani wa vifo 50.3 mwaka 2019/2020; kupungua kwa vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua, kutoka vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/2016 hadi vifo 321 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuongezeka kwa watoto waliozaliwa kwa kuhudumiwa na wahudumu wa afya wenye ujuzi kutoka asilimia 51 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 80 mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu, mafanikio yaliyopatikana ni ujenzi wa miundombinu muhimu katika shule 3,904.

**MHE. CONCHESTA M. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. CONCHESTA M. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, kinachosomwa hakipo katika *tablets* zetu. Tunaomba kusudi tuweze kufuatilia.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri endelea, hilo nitalitolea maelezo muda mfupi sana ujao. Ahsante Mheshimiwa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa upande wa elimu, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ujenzi wa miundombinu muhimu katika shule 3,904 ambapo shule za msingi ni 3,021na Sekondari ni shule 883; ujenzi wa mabweni 547; nyumba za walimu 101 na majengo ya utawala 25 na maktaba 43; kukamilika kwa ujenzi wa maboma 2,815 katika shule za msingi 2,133 na kuendelea kugharamia elimu ya msingi bila ada ambapo shilingi trilioni 1.24 zimetolewa; kukarabatiwa kwa shule kongwe 84 kati ya 89; na kuboreshwa kwa miundombinu ya vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi na kutolewa kwa mikopo ya elimu ya juu ambapo jumla ya shilingi trilioni 2.29 zimetumika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji, kukamilika kwa miradi 1,845 ya maji iliyotekelezwa mijini na vijijini, ni moja ya maendeleo na mafanikio yaliyojitokeza katika utekelezaji wa mpango uliopita. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa na hatua zilizofikiwa ni pamoja na kukamilika kwa miradi ya maji katika miji ya Geita, Njombe, Songwe; kuendelea kwa ujenzi wa mradi wa maji katika Mji wa Kigoma asilimia 90; kukamilika na kuzinduliwa kwa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria kwenda katika Miji ya Isaka, Tinde, Kagongwa, Tabora, Igunga, Uyui na Nzega; na kukamilika kwa asilimia 76 ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kukamilika kwa asilimia 62 ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Arusha na kuendelea na ujenzi wa mradi wa maji wa Same, Mwanga, Korogwe ambapo utekelezaji wake umeshafikia asilimia 65.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utawala bora, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliyoko Dodoma, Mahakama Kuu mbili katika mikoa ya Mara na Kigoma; ukarabati wa Mahakama Kuu tatu katika mikoa ya Mbeya, Tanga pamoja na Rukwa, Mahakama za Hakimu Mkazi tano, katika mikoa ya Pwani, Geita, Simiyu, Manyara na Njombe na Mahakama za Wilaya 15, Mahakama za Mwanzo 18; na kuanzishwa kwa ofisi ya Mwendesha Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ajira, jumla ya ajira 12,777,126 zimezalishwa, ambapo ajira za moja kwa moja ni 11,891,772 na ajira zisizo za moja kwa moja ni 881,354. Aidha, jumla ya vijana 65,008 katika kipindi cha mwaka 2017 - 2020 wamepatiwa mafunzo ya ujuzi na ustadi na kazi, ikiwemo mafunzo ya uanagenzi katika fani za ujenzi, useremala, umeme wa majumbani na viwandani na umeme wa jua na ufundi wa magari pamoja na ufundi bomba na utengenezaji wa vifaa vya *aluminium*, pamoja na uchomeleaji na uungaji wa vyuma. Maeneo mengine ni pamoja na kilimo na ufugaji, ushonaji, uchongaji vipuri, uchapaji nyaraka, pamoja na *TEHAMA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kulinda ajira za wazawa kwa kuhakikisha kuwa wageni wanaokuja kufanya kazi hapa nchini wanakidhi vigezo vilivyoainishwa katika Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Na. 1 ya Mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika eneo la kutengeneza mazingira wezeshi ya uwekezaji na uendelezaji wa biashara; kwa upande wa nishati ya umeme, kuendelea na ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa maji wa Mwalimu Julius Nyerere Megawati 2,115

ambapo kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 30.1 na kiasi cha Shilingi Trilioni 1.97 kimetumika katika kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi mingine ni kukamilika kwa mradi wa Kinyerezi I, Megawati 150, pamoja na II Megawati 240; mradi wa njia za kusafirisha umeme *KV-220* kutoka Makambako hadi Songea; ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupooza umeme na njia za kusafirisha umeme katika miradi ya njia kuu ya kusafirisha umeme wa msongo wa *KV 220* Bulyanhulu, Geita; kukamilika kwa asilimia 73.3 ya utekelezaji wa mradi wa kufua umeme Rusumo Megawati 80 na kukamilika kwa asilimia 86 kwa ujenzi wa njia za kusafirisha umeme *KV 400* Singida, Arusha, Namanga. Mafanikio mengine ni kuendelea kwa utekelezaji wa mradi wa Kinyerezi I na *extension* Megawati 185.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine kwa upande wa reli, ni Serikali kuendelea na ujenzi wa reli ya kati ya kiwango cha *standard gauge* ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro umeshakamilika kwa asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano, yaani 2021/2022 – 2025/2026; misingi iliyozingatiwa katika kuandaa mpango huu, ni pamoja na kuendelea kuwepo kwa amani na usalama, umoja na utulivu wa ndani ya nchi na nchi jirani, kuhimili athari za majanga ya asili kama vile mafuriko pamoja na magonjwa ya milipuko, ushiriki mpana wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi, hali nzuri ya hewa itakayowezesha uzalishaji wa chakula cha ziada na kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, shabaha ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano, ni pamoja na kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa mwaka kuongezeka kutoka 6% mwaka 2021 na kufikia wastani wa asilimia 8.0 ifikapo mwaka 2026. Mapato ya ndani, ikijumuisha mapato

ya Halmashauri kuongezeka kutoka asilimia 15.9 ya pato la Taifa mwaka 2021/2022 hadi asilimia 16.8 mwaka 2025/2026. Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ya wastani wa 3% hadi 5% katika kipindi cha muda wa kati. Akiba ya fedha za kigeni kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje usiopungua miaka minne na sekta binafsi kuzalisha ajira mpya zipatazo milioni nane katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Juni, 2026.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, yana maeneo makuu matano ya kipaumbele. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, kuchochea uchumi shindani na shirikishi. Eneo hili linajumuisha miradi ambayo itajikita katika kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kikanda na Kimataifa; kuchochea utulivu wa viashiria vya uchumi jumla; kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuchochea uvumbuzi na uhalishaji wa teknolojia kutoka nje na kuendeleza miundombinu na huduma za reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini na angani, TEHAMA, nishati, bandari na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa viwandani na utoaji huduma. Eneo hili linajumuisha miradi ya viwanda inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi pamoja na madini na kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, ni kukuza uwekezaji na biashara. Eneo hili linajumuisha *program* zitakazoimarisha masoko ya ndani na kutumia fursa za masoko ya kikanda na Kimataifa katika kukuza biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa eneo la nne, kuchochea maendeleo ya watu; eneo hili linajumuisha utekelezaji wa miradi ambayo inajikita katika kuboresha maisha ya watu ikiwemo elimu na mafunzo kwa ujumla, afya

na ustawi wa jamii, kinga ya jamii, huduma ya maji pamoja na usafi wa mazingira, mipango miji, nyumba na maendeleo ya makazi na athari dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa eneo la tano ambalo ni kuendeleza rasilimaliwatu; eneo hili linajumuisha programu za mikakati inayolenga kuendeleza maarifa na ujuzi wa rasilimaliwatu hapa nchini kuanzia ngazi za elimu ya awali hadi elimu ya juu ikiwemo kuwawezesha vijana kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, vile vile mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa yatajumuisha utekelezaji wa miradi ya kielelezo. Miradi hiyo ni ile iliyo mikuu ambayo nimetoka kuitaja katika hotuba hii inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango na umuhimu wa Sekta Binafsi, Mpango huu umeipa Sekta Binafsi uzito mkubwa. Mpango huu unalenga kujenga mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kukua, lakini pia Mpango huu unalenga kuishirikisha Sekta Binafsi katika ugharamiaji na utekelezaji wa Mpango ukitilia mkazo maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa katika hotuba zake za hivi karibuni katika matukio ya Kitaifa aliyoyafanya ambayo yanalenga kujenga imani ya Sekta Binafsi katika ujenzi wa uchumi wa kisasa wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mgawanyo wa majukumu ya utekelezaji wa Mpango, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zitawajibika katika kutafsiri mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika mipango yao ya kila mwaka na kuwasilisha taarifa za utekelezaji Wizara ya Fedha na Mipango.

Aidha, Baraza la Taifa la Biashara litaratibu na kusimamia ushiriki wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Mpango. Vile vile, washirika wa maendeleo watahamasishwa kushiriki katika utekelezaji wa mpango kupitia vikao rasmi vya ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali itaweka mfumo thabiti wa ufuatiliaji na tathmini ambao ni msingi mkuu wa usimamizi wa utendaji. Lengo la Serikali ni kuhakikisha mapato yanatumika kwa ufanisi na hatimaye miradi kuwa na thamani halisi ya fedha, uwajibikaji na uwazi katika hatua zote za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yatawezesha nchi kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo ni maisha bora na mazuri kwa kila Mtanzania, amani, utulivu na umoja utawala na uongozi bora, jamii iliyo elimika na inayopenda kujifunza na uchumi wenye uwezo wa ushindani. Aidha, Mpango huu unaweka msingi wa maandalizi ya dira mpya ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako lipokee na kujadili Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yaani 2021/2022 hadi 2025/2026.

## HOTUBA YA MHE. DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA (MB.), WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2021/2022 – 2025/2026 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na kuweza kukutana tena kwa ajili ya kupokea na kujadili kwa mara ya pili na kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 kwa mujibu wa ibara ya 63 (3) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kanuni ya 113 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**2. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee na kwa masikito makubwa napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge Wote, Chama cha Mapinduzi pamoja na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Msiba huu umekuwa pigo na umeleta majonzi kwa Taifa letu kutokana na uongozi wake mahiri, uchapakazi na uzalengo uliotukuka kwa Taifa. Mwenyezi Mungu ampumzishe mahali pema peponi, Amina. Vile vile, napenda kutoa pole kwa Taifa kwa kuondokewa na Viongozi Wakuu, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, na Balozi Mhandisi John Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema paponi.

**3. Mheshimiwa Spika,** kwa dhati naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mak. Aidha, ninampongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, napenda kumpongeza Balozi Hussein Katanga na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kushika nafasi hizo muhimu katika uongozi wa nchi yetu. Kipekee nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha imani yake kwangu na kuniteuwa kuwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**4. Mheshimiwa Spika,** napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni (Mb), na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bw. Emmauel Mpawe Tutuba kwa ushirikiano walionipa katika maandalizi ya kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Aidha, ninawashukuru sana Wizara, Taasisi, Idara za Serikali, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo, Asasi Zisizo za

Kiserekali na wadau mbalimbali waliotoa maoni na michango yao katika kukamilisha Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26.

**5. Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini (CCM) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi (CCM) kwa maoni yao wakati wa majadiliano ya vikao vya kamati. Aidha, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti yaliyotelewa katika vikao vya mwezi Januari na Machi 2021 pamoja na mjadala wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipojadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 kwa muda wa siku tano (5) kuanzia tarehe 02 Februari, 2021 yamezingatiwa katika uandaaji wa Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26.

**6. Mheshimiwa Spika,** Serikali imezingatia kikamilifu maoni na ushauri wa Kamati na Bunge katika taarifa niliyowasilisha. Majibu ya hoja zilizoibuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yameambatishwa **(Kiambatisho I)**.

**7. Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 yameandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025; Mpango Elekezi wa Muda Mrefu 2011/12 – 2025/26; Matokeo ya Tathmini Huru ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21; Sera na Mikakati mbalimbali ya Kisekta; Dira ya Afrika Mashariki 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika 2050; Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu, 2030.

**8. Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 una dhima ya

**Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu**. Mpango huu una maeneo makuu matano (5) ya kipaumbele ambayo ni: (i) kuchochea uchumi shindani na shirikishi; (ii) kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; (iii) kukuza uwekezaji na biashara; (iv) kuchochea maendeleo ya watu; na (v) kuendeleza rasilimali watu.

**9. Mheshimiwa Spika,** Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kimegawanyika katika sura nane (8): Sura ya kwanza ni Utangulizi ambao unaelezea chimbuko na historia ya Dira ya Maendeleo 2025 na Mipango ya Maendeleo; Sura ya Pili inahusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa 2016/17 – 2020/21 ambayo yanajenga msingi wa maandalizi ya Mpango wa Tatu ambao unaendeleza mafanikio yaliyopatikana na kutatua changamoto zilizokabili utekelezaji wa Mpango wa Pili; Sura ya Tatu imejikita katika masuala ya maendeleo ya sekta binafsi ikiwa na msukumo wa kuijenga Sekta Binafsi na kuishirikisha katika utekelezaji wa mpango; Sura ya Nne inaelezea dhana ya kujenga uchumi shindani, maendeleo ya viwanda na maendeleo ya watu; Sura ya Tano inaainisha hatua mahususi za kuchukuliwa katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango; Sura ya Sita inahusu ugharamiaji wa utekelezaji wa Mpango; Sura ya Saba inaanisha mpangilio wa utekelezaji wa Mpango; na Sura ya Nane inaainisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango.

**10. Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha Mpango huu unatekelezwa kikamilifu, Serikali inaendelea na maandalizi ya Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ikijumuisha Mkakati wa Utekelezaji, Mkakati wa Ugharamiaji na Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango.

## 2.0 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2016/17 – 2020/21

### 2.1 Viashiria vya Uchumi Jumla

**11. Mheshimiwa Spika,** Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 –

2020/21 inaonesha kuwa, katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango (2016/17 – 2019/20): Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.9; mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 4.1 kwa mwaka ikiwa ni ndani ya lengo la kutozidi asilimia 5; akiba ya fedha za kigeni ilitosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.9 ikiwa ni zaidi ya lengo la miezi minne (4); na nakisi ya bajeti ilikuwa ndani ya lengo la kutozidi asilimia 3 kwa kipindi chote. Katika kipindi hicho, deni la Serikali lilikuwa himilivu katika muda mfupi, wa kati na mrefu. Vile vile, Pato la Wastani la Kila Mtu liliongezeka kutoka shilingi 2,225,099 (sawa na dola za Marekani 1,022) mwaka 2016 hadi shilingi 2,577,967 (sawa na dola za Marekani 1,080) mwaka 2019. Kielelezo kikuu cha mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa ni Tanzania kufanikiwa kuingia katika kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati cha chini mwezi Julai 2020.

**12. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi trilioni 107 ambapo shilingi trilioni 59 ni kutoka sekta ya umma na shilingi trilioni 48 kutoka Sekta Binafsi. Katika miaka minne ya utekelezaji wa mpango huo, sekta ya umma imetumia jumla ya shilingi trilioni 34.9, sawa na asilimia 76.5 ya lengo la miaka minne la shilingi trilioni 45. Aidha, sekta binafsi imetumia jumla ya shilingi trilioni 32.6 sawa na asilimia 85 ya lengo la miaka minne la shilingi trilioni 38.4

### 2.2 Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

**13. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 ulijikita katika kujenga viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini hususan za kilimo, madini na gesi asilia. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni kama ifuatavyo:

(i) **Uzalishaji Viwandani:** kujengwa kwa jumla ya viwanda vipya 8,477 kati ya mwaka 2015 – 2019 ambapo viwanda vikubwa ni 201, vya kati 460, vidogo 3,406 na vidogo sana 4,410. Ujenzi wa viwanda hivyo umeongeza idadi ya viwanda nchini kutoka 52,633 mwaka 2015 hadi viwanda 61,110 mwaka 2019. Viwanda hivyo vimechangia ongezeko la uzalishaji wa bidhaa mbalimbali katika soko la ndani na la nje ikijumuisha bidhaa za ngozi, nguo, ujenzi (nondo, mabati, saruji, misumari, marumaru na rangi), plastiki, zana za kilimo na vinywaji.

Uwekezaji huo umeleta mafanikio yafuatayo: Kuongezeka kwa mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kutoka asilimia 7.9 mwaka 2015 hadi asilimia 8.5 mwaka 2019; kukua kwa sekta ya uzalishaji viwandani kwa wastani wa asilimia 8.3; kuzalishwa kwa fursa za ajira kutoka ajira 254,786 mwaka 2015 hadi ajira 482,601 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 47.2; na kuchangia katika mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi kutoka asilimia 13.8 mwaka 2016/17 hadi asilimia 14.2 mwaka 2019/20. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 45.3 kimetumika kuchochea miradi ya uzalishaji viwandani;

(ii) **Kilimo:** Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kujengwa na kuboreshwa kwa miundombinu ya umwagiliaji ambayo imeongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 461,376 mwaka 2015 hadi hekta 694,715 mwaka 2020; kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 36,614 mwaka 2015 hadi tani 76,726 mwaka 2020; kukamilika kwa ujenzi wa maabara ya mbegu katika makao makuu ya Wakala wa Mbegu za Kilimo – Morogoro; na kuanzishwa kwa soko la bidhaa (Tanzania Mercantile Exchange – TMX).

Hatua hizi zimechangia kupatikana kwa mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kuongezeka kwa utoshelevu wa chakula kufikia asilimia 118 mwaka 2019/20; kupungua kwa mfumuko wa bei za chakula kufikia wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2020 kutoka asilimia 8.6 mwaka 2015; na kupungua kwa Umaskini wa Chakula kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011/

12 hadi asilimia asilimia 8.0 mwaka 2017/18. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 188.9 kimetumika kuendeleza sekta ya kilimo;

(iii) **Mifugo:** kujenga kiwanda kipya cha Kilimanjaro International Leather Industries Co Ltd; kuimarisha kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha NAIC (Arusha); kujengwa kwa viwanda vipya vya kimkakati vya nyama vya Tanchoice (Pwani), Elia Food Oversees Limited (Arusha) na Binjiang Company Limited (Shinyanga); kujengwa kwa kiwanda cha maziwa cha Galaxy Food and Beverage Company Limited (Arusha); kujengwa kwa kiwanda cha kuzalisha chanjo cha Hester Bioscience Africa Limited (Pwani); na kuendelea kuboresha huduma za malisho ya mifugo na majosho.

Utekelezaji huu umewezesha mafanikio yafuatayo: kuongezeka kwa viwanda vya kusindika nyama nchini kutoka 25 mwaka 2015/16 hadi viwanda 32 mwaka 2019/20 na viwanda vya kusindika maziwa kutoka 82 mwaka 2015/16 hadi 99 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa usambazaji wa mitamba katika mashamba ya Serikali kutoka mitamba 11,449 mwaka 2015/16 hadi mitamba 18,255 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa maeneo ya malisho ya mifugo kutoka hekta milioni 1.4 mwaka 2015/16 hadi hekta milioni 2.85 mwaka 2019/20; na kuongezeka kwa ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na zao la ngozi kutoka shilingi bilioni 1.73 mwaka 2015/16 hadi shilingi bilioni 9.1 mwaka 2019/20. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 5.66 kimetumika kutekeleza miradi na programu za sekta ya mifugo;

(iv) **Uvuvi:** Kuimarisha usimamizi wa shughuli za uvuvi kupitia utekelezaji wa Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015, Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009; kutungwa kwa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 5 ya mwaka 2020; na kupambana na uvuvi haramu kupitia doria na kaguzi mbalimbali. Hatua hizi zilifanikisha: Kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki katika maji ya asili kutoka tani 362,645 mwaka 2015/16 hadi tani 497,567 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa usindikaji wa minofu ya

samaki aina ya Sangara kutoka tani 23,000.58 mwaka 2015/16 hadi tani 27,596.27 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa huduma za usafirishaji wa mazao ya uvuvi kwenda masoko ya Ulaya ambapo katika mwaka 2019/20, jumla ya tani 777.750 za mabondo zilisafirishwa; kuongezeka kwa mauzo ya samaki na mazao ya uvuvi nje ya nchi kutoka shilingi bilioni 379.25 mwaka 2015/16 hadi shilingi bilioni 506.24 mwaka 2019/20; na kuanza maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi (Mbegani) na ununuzi wa meli nne (4) za uvuvi. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, jumla ya shilingi bilioni 33.5 zimetumika kwa ajili ya kuendeleza sekta ya uvuvi;

(v) **Madini:** kupitia na kutunga sheria, sera na mikataba ya madini ambapo imewezesha kuundwa kwa kampuni ya ubia ya Twiga Minerals Corporation ambapo imetoa gawio la shilingi bilioni 100; kuanzishwa kwa kampuni ya Tembo Nickel Corporation Limited; kujengwa kwa masoko 39 ya madini na vituo 41 vya kuuzia madini; kukamilika kwa ujenzi wa vituo vinne (4) vya umahiri katika maeneo ya Bariadi, Musoma, Bukoba na Handeni na kuendelea na ujenzi wa vituo vya Songea, Mpanda na Chunya; kujenga ukuta wenye mzingo wa kilomita 24 wa Mirerani mkoani Manyara; na kukamilisha ujenzi wa vituo vitatu (3) vya mfano vya uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika maeneo ya Lwamgasa (Geita), Katente (Bukombe) na Itumbi (Chunya).

Hatua hizi zimechangia kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini kutoka dola za Marekani bilioni 1.91 (sawa na shilingi trilioni 4.46 mwaka 2015/16 hadi dola za Marekani bilioni 2.9 (sawa na shilingi trilioni 6.77) mwaka 2019/20; na kuongezeka kwa maduhuli kutoka shilingi bilioni 196 mwaka 2015/16 hadi kufikia shilingi bilioni 528.3 mwaka 2019/20. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, jumla ya shilingi bilioni 83.4 zimetumika kugharamia miradi mbalimbali ya madini;

(vi) **Maliasili na Utalii:** kuongeza idadi ya watalii na mapato kupitia Mradi wa Kujenga Uwezo katika Hifadhi za Taifa;

kudhibiti ujangili kwa asilimia 90; kubadilishwa na kupandishwa hadhi kwa mapori ya akiba ya Nyerere, Burigi, Kigosi, Ugala, Ibandakyerwa na Rumanyika kuwa Hifadhi za Taifa; na kuendelea kutangazwa kwa vivutio vya utalii katika nchi mbalimbali duniani.

Hatua hizi zimechangia kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini kutoka watalii 1,137,182 mwaka 2015 hadi 1,527,230 mwaka 2019; kuongezeka kwa wastani wa idadi ya siku zinazotumiwa na watalii kukaa nchini kufikia siku 13 mwaka 2019 kutoka siku 10 mwaka 2015; nakuongezeka kwa mapato yatokanayo na utalii kutoka dola za Marekani bilioni 1.9 (sawa na shilingi bilioni 4,436.7) mwaka 2015 hadi dola za Marekani bilioni 2.6 (sawa na shilingi bilioni 6,071.3) mwaka 2019. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, jumla ya shilingi bilioni 269.7 zimetumika kuboresha na kuendeleza sekta ya Maliasili na Utalii.

### 2.3 Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu

**14. Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa miundombinu na upatikanaji wa huduma za afya, maji na elimu, umeongeza kasi ya ufungamanishaji wa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

(i) **Afya:** Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuendelea kutoa huduma za kupandikiza uloto (bone marrow transplant); kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za dharura na ukarabati wa jengo la X-ray katika Hospitali ya Rufaa Dodoma; kukamilika kwa asilimia 98.2 ya ujenzi wa Hospitali ya Uhuru – Dodoma; kununuliwa kwa mashine za digital X-ray na ultrasound, vifaa vya maabara na mashine za uchunguzi wa kifua kikuu kwa kuotesha vimelea BACTEC 960 (Mycobacteria Growth Indicator Tube - MGIT) na Blood culture machine katika Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu – Kibong'oto; ununuzi wa mashine ya Positron Emmission Tomography (PET Scan) kwa ajili ya Hospitali ya Ocean Road; kujenga na kuboresha miundombinu

ikijumuisha: jengo la huduma za upasuaji; radiolojia; jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje; maabara; na jengo la mama na mtoto katika hospitali za rufaa za Mara, Geita, Songwe, Katavi, Sekou Toure (Mwanza), na hospitali za rufaa za kanda ya kusini Mtwara na kanda ya nyanda za juu kusini Mbeya na Hospitali ya Kanda ya Kaskazini (KCMC) na Hospitali ya Kanda ya Ziwa ya Burigi (Geita).

Vile vile, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya sekta ya afya ambayo imefikia hatua mbalimbali ikiwemo: kufikia asilimia 98 ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa Mwananyamala; kukamilika na kuanza kutumika kwa jengo la wagonjwa wa nje na kufikia asilimia 73 ya ujenzi wa jengo la maabara katika Hospitali ya Rufaa Njombe; na ujenzi wa jengo la ghorofa moja la huduma za upasuaji, radiolojia na maabara na kufikia asilimia 50 ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa Simiyu. Aidha, mafanikio mengine ni pamoja na: ununuzi wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; na kuongezeka kwa idadi ya zahanati kutoka 4,922 mwaka 2015 hadi 6,120 mwaka 2020, vituo vya afya kutoka 535 mwaka 2015 hadi kufikia vituo 710 mwaka 2020 na Hospitali za Halmashauri za Wilaya kutoka 77 mwaka 2015 hadi 179 mwaka 2020.

Hatua hizi zimechangia: Kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 62 mwaka 2015/16 hadi miaka 66 mwaka 2019/20; kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kutoka wastani wa vifo 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2014/15 hadi wastani wa vifo 50.3 mwaka 2019/20; kupungua kwa vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua kutoka vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16 hadi vifo 321 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019/20; na kuongezeka kwa watoto wanaozaliwa kwa kuhudumiwa na wahudumu wa afya wenye ujuzi kutoka asilimia 51 mwaka 2015/16 hadi asilimia 80 mwaka 2019/20. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 736.67 kimetumika katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za afya;

(ii) **Elimu:** Ujenzi wa miundombinu muhimu katika shule 3,904 (Msingi 3,021 na Sekondari 883), mabweni 547, nyumba za walimu 101, majengo ya utawala 25 na maktaba 43; kukamilika kwa ujenzi wa maboma 2,815 katika shule za msingi 2,133; kuendelea kugharamia elimu msingi bila ada ambapo shilingi trilioni 1.24 zilitolewa; kukarabatiwa kwa shule kongwe 84 kati ya 89; kuboreshwa kwa miundombinu ya vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi (Folk Development Colleges - FDC); na kutolewa kwa mikopo ya elimu ya juu ya jumla ya shilingi trilioni 2.29.

Hatua hizi zimechangia: Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi kutoka asilimia 93.3 mwaka 2015 hadi asilimia 110.6 mwaka 2020; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na mafunzo ya ufundi stadi kutoka 196,091 mwaka 2015/16 hadi 320,143 mwaka 2019/20 na elimu ya ufundi kutoka 117,067 mwaka 2015/16 hadi 151,379 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu nchini kutoka 65,064 mwaka 2015/16 hadi kufikia 87,813 mwaka 2019/20; na kuongezeka kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka wanafunzi 125,126 mwaka 2015 hadi kufikia 132,392 mwaka 2020. Aidha, kiwango cha ufaulu wa mitihani ya Darasa la Saba kimeongezeka kutoka asilimia 67 mwaka 2015 hadi asilimia 81.5 mwaka 2019 na Sekondari (Kidato cha nne) kutoka asilimia 68 mwaka 2015 hadi asilimia 80.7 mwaka 2019. Vile vile, wanafunzi waliohitimu elimu ya juu walifikia 60,940 mwaka 2019/20, elimu ya mafunzo stadi 90,849 mwaka 2018/19 na elimu ya ufundi 86,547 mwaka 2019/20. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi trilioni 3.19 kimetumika kuboresha miundombinu na huduma za sekta ya elimu;

(iii) **Maji:** Kukamilika kwa miradi 1,845 ya maji iliyotekelezwa mijini na vijijini. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa na hatua zilizofikiwa ni: kukamilika kwa miradi ya maji katika miji ya Geita, Njombe na Songwe na kuendelea kwa ujenzi wa mradi wa maji katika mji wa Kigoma (asilimia 90); kukamilika na kuzinduliwa kwa Mradi mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Isaka, Tinde, Kagongwa, Tabora,

Igunga, Uyui na Nzega; kukamilika kwa asilimia 76 ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Mwanza; kukamilika kwa asilimia 62 ya ujenzi wa mradi wa maji katika Jiji la Arusha; na kuendelea na ujenzi wa mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 65. Aidha, katika eneo linalohudumiwa na DAWASA (mikoa ya Dar es Salaam na Pwani) utekelezaji wa miradi umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na umehusisha maeneo ya Kibamba hadi Kisarawe, Mlandizi hadi Chalinze, Kisarawe-PuguUkonga, Mbezi Luis, Kiluvya, Tegeta, Wazo, Madale, Mivumoni, Mabwepande na Bagamoyo (maeneo ya Vikawe, Zinga, Mapinga na Kerege).

Kwa ujumla miradi yote iliyotekelezwa imewezesha wananchi zaidi ya milioni 25 kupata huduma ya maji ambapo wastani wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama imeongezeka kutoka asilimia 74 mwaka 2015 hadi asilimia 84 mwaka 2020 kwa mijini na kutoka asilimia 47 mwaka 2015 hadi asilimia 70.1 mwaka 2020 kwa vijijini. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi trilioni 2.03 kimetumika kuboresha huduma ya maji vijijini na mijini;

(iv) **Utawala Bora:** kukamilika kwa ujenzi wa ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi - Dodoma; Mahakama Kuu mbili (2) katika mikoa ya Mara na Kigoma na ukarabati wa Mahakama Kuu tatu (3) katika mikoa ya Mbeya, Tanga na Rukwa; Mahakama za Hakimu Mkazi tano (5) katika mikoa ya Pwani, Geita, Simiyu, Manyara na Njombe; Mahakama za Wilaya 15; Mahakama za Mwanzo 18; na kuanzishwa kwa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Hatua hizi zimechangia kuongezeka kwa idadi ya kesi za rushwa zilizotolewa maamuzi kutoka asilimia 10.4 mwaka 2015/16 hadi asilimia 82.0 mwaka 2019/20; kupungua kwa mlundikano wa mashauri katika mahakama ya Tanzania kutoka asilimia 13 ya mashauri yaliyokuwepo mahakamani mwaka 2015 hadi asilimia tano (5) mwaka 2019; na kuongezeka kwa upatikanaji wa haki karibu na wananchi; uwiano wa halmashauri zilizobandika bajeti kwenye mbao

za matangazo za umma ulifikia asilimia 86 ya lengo la halmashauri zote; kufanikisha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 bila kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambapo kiasi cha shilingi bilioni 268.5 kilitumika; na kuhamishia makao makuu ya Serikali Dodoma. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 530.8 kilitumika kutekeleza miradi hii; na

(v) **Ajira:** Jumla ya ajira 12,773,126 zimezalishwa, ambapo ajira za moja kwa moja ni 11,891,772 na ajira zisizo za moja kwa moja ni 881,354. Aidha, jumla ya vijana 65,008 katika kipindi cha mwaka 2017 hadi 2020 wamepatiwa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi ikiwemo mafunzo ya uanagenzi katika fani za ujenzi, useremala, umeme wa majumbani na viwandani, umeme wa jua, ufundi magari, ufundi bomba, utengenezaji wa vifaa vya aluminium, uchomeleaji na uungaji vyuma, kilimo na ufugaji, ushonaji, uchorongaji vipuli, uchapaji nyaraka na TEHAMA. Serikali imeendelea kulinda ajira za wazawa kwa kuhakikisha kuwa wageni wanaokuja kufanya kazi nchini wanakidhi vigezo vilivyoainishwa katika Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Na. 1 ya mwaka 2015.

## 2.4 Mazingira Wezeshi kwa Uwekezaji na Uendeshaji Biashara

**15. Mheshimiwa Spika,** baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili ni kama ifuatavyo:

(i) **Nishati ya Umeme:** Kuendelea na ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere MW 2,115 ambapo kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 30.1. Kiasi cha shilingi trilioni 1.97 kimetumika kutekeleza mradi huu.

Hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi mingine ni: Kukamilika kwa miradi ya Kinyerezi I MW 150 na II MW 240, mradi wa njia ya kusafirisha umeme kV 220 kutoka Makambako hadi Songea, ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme na njia za kusafirisha umeme katika Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 Bulyanhulu – Geita; kukamilika kwa asilimia 73.3 ya utekelezaji wa mradi wa Kufua Umeme - Rusumo MW 80; kukamilika kwa

asilimia 86 kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kV 400 Singida – Arusha – Namanga; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Kinyerezi I Extension MW 185 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 84; kukamilika kwa usanifu wa miradi ya Kakono MW 87 na Malagarasi MW 45; kuendelea na kuhuisha upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya Kufua Umeme wa Maji ya Ruhudji MW 358 na Rumakali MW 222; na kukamilika kwa upembuzi yakinifu na kuendelea na uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Rufiji – Chalinze – Dodoma na Chalinze – Kinyerezi.

Miradi iliyokamilika imechangia kuongezeka kwa uzalishaji wa nishati ya umeme kufikia MW 1,602.3 mwaka 2019/20 kutoka MW 1,308 mwaka 2015/16; kupungua kwa kiwango cha upotevu wa umeme kutoka asilimia 19.0 mwaka 2015/16 hadi asilimia 16.4 mwaka 2019/20; na kuunganishwa umeme kwa jumla ya vijiji 10,018 kati ya vijiji 12,317 hadi Januari 2020, sawa na asilimia 81.3. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi trilioni 2.98 kimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme;

(ii) **Ujenzi wa Barabara na Madaraja Makubwa:** Kujengwa kwa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami wenye urefu wa kilomita 3,537 (barabara kuu na za mikoa kilomita 2,209 na barabara za halmashauri kilomita 1,328) na hivyo kufanya mtandao wa barabara uliojengwa kwa kiwango cha lami hadi mwaka 2019/20 kufikia kilomita 13,044 ambapo kilomita 10,939 ni barabara kuu na kilomita 2,105 ni barabara za mikoa. Vile vile, kukamilika kwa ujenzi wa madaraja 13 katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili. Kiasi cha shilingi trilioni 8.8 kimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara na madaraja makubwa katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo.

(iii) **Reli:** Serikali inaendelea na ujenzi wa Reli ya Kati ya kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railways – SGR) ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) umefikia asilimia 90 na kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) umefikia asilimia 52.2; kusainiwa kwa

mkataba wa ujenzi wa kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) wenye thamani ya shilingi trilioni 3.07 na kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya Makutupora – Tabora (km 294) na Tabora – Isaka (km 133). Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi trilioni 4.04 kimetumika kutekeleza mradi.

Aidha, ukarabati wa miundombinu ya reli ya kati kutoka Dar es Salaam - Isaka (km 970) sehemu ya Dar es Salaam - Kilosa (km 283) na Kilosa – Isaka (km 687) umekamilika. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 728.3 kimetumika kukarabati miundombinu ya reli ya kati.

Shughuli nyingine zilizofanyika ni pamoja na: kukarabati na kurejesha huduma za reli ya Tanga hadi Arusha (km 439); na kurejesha huduma ya kusafirisha shehena za mizigo kwa njia ya reli kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Uganda.

(iv) **Bandari:** Katika **Bandari ya Dar es Salaam** shughuli zilizofanyika ni: Kuboreshwa kwa gati namba 1 – 5; kukamilika kwa ujenzi wa gati la kupakia na kushushia magari (RoRo); na kuendelea na uboreshaji wa gati Na. 6 hadi 7. Hatua hizi zimechangia kupungua kwa idadi ya siku za meli kukaa bandarini kutoka siku saba (7) hadi siku tano (5) na kuongezeka kwa shehena ya mizigo iliyohudumiwa kutoka tani milioni 15.4 hadi tani milioni 19.52. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 253.7 kimetumika kutekeleza mradi huu.

Katika **Bandari ya Mtwara,** ujenzi wa gati jipya lenye urefu wa mita 300 na yadi ya kuhudumia makasha umekamilika. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 88.6 kimetumika kutekeleza mradi huu.

Mafanikio yaliyopatikana katika **Bandari ya Tanga** ni uongezaji wa kina cha lango la kuingia meli kutoka mita nne (4) hadi mita 13 na kuweka vifaa vya kuongezea meli; na kukamilika kwa ujenzi wa gati mbili (2) kwenye kina kirefu.

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 86.9 kimetumika kutekeleza mradi huu.

**(i) Kuboresha Usafiri wa Abiria na Mizigo katika Maziwa Makuu: Ziwa Victoria na Tanganyika**: Kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili (2) za New Butiama Hapa Kazi Tu na New Victoria Hapa Kazi Tu; kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa kazi Tu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 35; na kukamilika kwa ujenzi wa Chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza chenye uwezo wa kubeba meli yenye uzito wa kuanzia tani 1 hadi 4,000, kikiwa na reli na mfumo unaowezesha kupandisha meli zaidi ya moja kulingana na ukubwa. Shughuli nyingine zilizokamilika ni: ukarabati wa meli za MV. Clarias na ML. Wimbi; Ujenzi wa magati ya Lushamba, Ntama, Nyamirembe, Magarine na Gati la majahazi Mwigobero; na ununuzi wa vifaa vya kuhudumia mizigo na meli.

Katika **Ziwa Tanganyika**, mikataba kwa ajili ya Ujenzi wa Meli Mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 imesainiwa pamoja na ukarabati wa meli ya MV Liemba; na ukarabati wa meli ya MT. Sangara. Katika katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 148.0 kimetumika kuboresha na kuendeleza hali ya usafiri katika Ziwa Victoria na Tanganyika.

**Ziwa Nyasa:** Kukamilika kwa ujenzi wa matishari mawili (2) yenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja; na kukamilika na kuanza kufanya kazi kwa meli moja mpya ya MV Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 17.5 kimetumika kuboresha na kuendeleza hali ya usafiri na usafirishaji katika Ziwa Nyasa;

(v) **Viwanja vya Ndege na Rada:** Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa jengo la tatu la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere – JNIA chenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka; na kuendelea na ujenzi wa viwanja vya

Geita (asilimia 98), Songea (asilimia 95) na Mtwara (asilimia 53.2). Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 411.2 kimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya viwanja vya ndege.

Kununuliwa kwa rada nne (4) za kuongoza ndege za kiraia na kufungwa katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Kilimanjaro, Songwe na Mwanza na hivyo kuongeza kiwango cha usalama wa abiria na mizigo katika viwanja vya ndani. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 79.8 kimetumika kuimarisha usafiri wa anga nchini;

(vi) **Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL):** Baadhi ya mafanikio ni pamoja na kununuliwa kwa ndege mpya 11 kutoka ndege moja (1) iliyokuwepo mwaka 2015 na kuifanya ATCL kuwa na jumla ya ndege 12; na kuimarishwa kwa Shirika la Ndege Tanzania. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi trilioni 1.27 kimetumika kutekeleza mradi;

(vii) **Mawasiliano na Uchumi wa Kidigitali:** Ujenzi wa mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unaendelea ambapo awamu ya tatu ya ujenzi imekamilika; Mradi wa mfumo wa Anuani za Makazi na Postikodi unaendelea kutekelezwa; na ufungaji wa nguzo zenye majina ya barabara umefanyika katika halmashauri 12 za majiji ya Dodoma, Mwanza na Tanga.

Uwekezaji huu umechangia kuongezeka kwa idadi ya laini za simu kutoka milioni 39 hadi milioni 48.6; idadi ya watumiaji wa mitandao ya simu kuongezeka kutoka milioni 9 hadi milioni 27 na kupungua kwa gharama za kupiga simu za mkononi kutoka shilingi 274 kwa dakika kwa mwaka 2015 hadi shilingi 70 kwa dakika mwaka 2020. Aidha, huduma za mawasiliano kwa njia ya simu za viganjani zimeenda sanjari na ongezeko la huduma jumuishi za fedha (financial inclusion), na biashara mtandao (e-commerce). Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 874 kimetumika kutekeleza miradi hii; na

(viii) **Serikali Mtandao na Mifumo ya Kielektroniki:** Huduma za Serikali Mtandao zimeimarishwa kwa kuongeza kiwango cha ubora wa huduma zinazotolewa na Serikali kwa wadau mbalimbali ambapo mifumo ya Serikali mtandao imeongezewa mawanda.

Hatua hizi zimechangia mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za miamala, hususan utunzaji wa kumbukumbu za wateja utoaji wa ankara, kupunguza matumizi ya shajala kurahisisha malipo ya ada, tozo na kodi. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo, kiasi cha shilingi bilioni 1.4 kimetumika kuboresha Serikali Mtandao na mifumo ya kielektroniki.

**16. Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: Uharibifu wa miundombinu uliosababishwa na mafuriko; kupungua kwa shughuli za kibiashara duniani kulikotokana na athari za COVID-19; na ukwepaji kodi kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu hususan kupitia njia za magendo, uhamishaji wa faida (transfer pricing) kwa kampuni zenye mtandao wa kimataifa na kutokutoa na kudai stakabadhi za kielektroniki (EFD receipt) wakati mauzo yanapofanyika.

**17. Mheshimiwa Spika,** Hatua zilizochukuliwa katika kukabiliana na changamoto hizo ni pamoja na: kukarabati miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko pamoja na kuimarisha ukaguzi wake; kuendelea kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa biashara duniani ili kutumia fursa zilizotokana na athari za COVID-19 kwa manufaa mapana ya nchi pamoja na kuchukua hatua za kisera na kiutawala kurejesha biashara zilizoathirika; na kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa mapato ili kudhibiti ukwepaji kodi pamoja na kuendelea kuhamasisha umma juu ya matumizi ya stakabadhi za kielektroniki.

## 3.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2021/22 – 2025/26

**18. Mheshimiwa Spika,** misingi iliyozingatiwa ni pamoja na: Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama, umoja, utulivu wa ndani na nchi jirani; Kuhimili athari za majanga ya asili kama vile mafuriko na magonjwa ya mlipuko; Ushiriki mpana wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi; Hali nzuri ya hewa itakayowezesha uzalishaji wa chakula cha ziada; na Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya kimataifa**.**

**19. Mheshimiwa Spika,** Shabaha za Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ni pamoja na:

(i) Kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa mwaka kuongezeka kutoka asilimia 6.0 mwaka 2021 na kufikia wastani wa asilimia 8.0 ifikapo mwaka 2026;

(ii) Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri kuongezeka kutoka asilimia 15.9 ya Pato la Taifa mwaka 2021/22 hadi asilimia 16.8 mwaka 2025/26;

(iii) Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika kipindi cha muda wa kati;

(iv) Akiba ya fedha za kigeni kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne; na

(v) Sekta binafsi kuzalisha ajira mpya zipatazo milioni nane kati ya Julai 2021 na Juni 2026.

**20. Mheshimiwa Spika,** kama nilivyosema awali, Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yana maeneo makuu matano (5) ya kipaumbele. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

(i) **Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi**: Eneo hili linajumuisha miradi ambayo itajikita katika: kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kikanda na kimataifa; kuchochea utulivu wa viashiria vya uchumi jumla; kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuchochea uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje; na kuendeleza miundombinu na huduma za reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini na angani, TEHAMA, nishati, bandari na viwanja vya ndege;

(ii) **Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma:** Eneo hili linajumuisha miradi ya viwanda inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na madini pamoja na kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana nchini. Aidha, eneo hili linajumuisha pia miradi na programu inayolenga kuboresha huduma za utalii, fedha na bima;

(iii) **Kukuza Uwekezaji na Biashara:** Eneo hili linajumuisha programu zitakazoimarisha masoko ya ndani na kutumia fursa za masoko ya kikanda na kimataifa katika kukuza biashara. Aidha, masoko yanayolengwa ni yale yatakayotoa fursa kwa bidhaa zinazozalishwa nchini, ikiwemo bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu;

(iv) **Kuchochea Maendeleo ya Watu:** Eneo hili linajumuisha utekelezaji wa miradi ambayo inajikita katika kuboresha maisha ya watu ikiwemo: elimu na mafunzo kwa ujumla; afya na ustawi wa jamii; kinga ya jamii; huduma za maji na usafi wa mazingira; mipango miji, nyumba na maendeleo ya makazi; na athari dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi; na

(v) **Kuendeleza Rasilimali Watu:** Eneo hili linajumuisha programu na mikakati inayolenga kuendeleza maarifa na ujuzi wa rasimali watu nchini, kuanzia ngazi za elimu ya awali hadi elimu ya juu ikiwemo kuwawezesha vijana kujiajiri. Vile vile, eneo hili linajumuisha hatua za kuboresha viwango vya utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na ujuzi adimu kwa lengo la kuongeza tija na ushindani wa

wananchi katika kutumia rasimali zilizopo nchini ili kuleta maendeleo.

**21. Mheshimiwa Spika,** vile vile, Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 yatajumuisha utekelezaji wa miradi ya kielelezo. Miradi hiyo ni: Mradi wa Kufua Umeme wa Maji - Julius Nyerere MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge); Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga ikijumuisha ujenzi wa reli ya kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway – SGR) kutoka Mtwara hadi Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga; Bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Mradi wa Kuchakata Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji - Ruhudji MW 358; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji - Rumakali MW 222; Uchimbaji wa madini ya Nickel; Ujenzi wa Madaraja Makubwa na Barabara za Juu za Daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza), Tanzanite (Dar es Salaam) na Interchange ya Kamata (Dar es Salaam); Bandari ya Uvuvi (Mbegani) na Ununuzi wa Meli za Uvuvi; Kiwanda cha Sukari Mkulazi; Utafutaji wa mafuta katika vitalu vya Eyasi Wembere na Mnazi Bay North; Mradi wa Magadi Soda – Engaruka; Kuongeza Rasilimali Watu yenye Ujuzi Adimu na Maalum (Ujuzi wa Kati na Wabobezi) kwa Maendeleo ya Viwanda na Ustawi wa Jamii; na Kanda Maalum za Kiuchumi.

**22. Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua mchango na umuhimu wa sekta binafsi, Mpango huu umeipa sekta binafsi uzito mkubwa. Mpango unalenga kujenga mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kukua lakini pia Mpango unalenga kushirikisha sekta binafsi katika ugharamiaji na utekelezaji wa Mpango.

**23. Mheshimiwa Spika,** Mpango unakadiriwa kugharimu jumla ya shilingi trilioni 114.8, zikijumuisha mchango wa sekta binafsi wa shilingi trilioni 40.6 na sekta ya umma shilingi trilioni 74.2 kutoka vyanzo vya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, misaada na mikopo. Aidha, vyanzo mbalimbali bunifu vinavyoweza kutumika katika kugharamia shughuli za

maendeleo vimeanishwa vikiwemo Ugharamiaji wa Pamoja (joint venture), Hati Fungani za Mashirika, Mitaji Binafsi (private equity) na Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi.

**24. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mgawanyo wa majukumu ya utekelezaji wa Mpango, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zitawajabika kutafsiri Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika mipango yao ya kila mwaka na kuwasilisha taarifa za utekelezaji Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, Baraza la Taifa la Biashara litaratibu na kusimamia ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango. Vile vile, Washirika wa Maendeleo watahamasishwa kushiriki katika utekelezaji wa Mpango kupitia vikao rasmi vya ushirikiano.

**25. Mheshimiwa Spika,** ili kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali itaweka mfumo thabiti wa Ufuatiliaji na Tathmini ambao ni msingi mkuu wa usimamizi wa utendaji. Lengo la Serikali ni kuhakikisha mapato yanatumika kwa ufanisi na hatimae miradi kuwa na thamani halisi ya fedha, uwajibikaji na uwazi katika hatua zote za maendeleo.

## 4.0 HITIMISHO

**26. Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 yatawezesha nchi kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo ni: maisha bora na mazuri; amani, utulivu na umoja; utawala na uongozi bora; jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza; na uchumi wenye uwezo wa ushindani. Aidha, Mpango huu unaweka msingi wa maandalizi ya Dira mpya ya Maendeleo ya Taifa letu.

**27. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naomba sasa Bunge lako lipokee na kujadili Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26.

**28. Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Muwe mnakaa karibu karibu mnapokuwa mnafuata kwenye mtiririko.

Waheshimiwa Wabunge, uchaguzi wa Bunge *Sports Club,* siku ya Jumatatu utasimamiwa na Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge mchana saa saba. Ukumbi wa Msekwa Jumatatu. Niseme hapa hapa, Wajumbe wa *PAC, LAAC* na *PIC,* leo saa saba mchana tukutane pale Msekwa na pia Naibu Spika awepo na Mheshimiwa *Chief Whip,* saa saba pale Msekwa tutaomba tukutane pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, tafadhali.

**MHE. SILLO D. BARAN - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni Taarifa ya Kamati ya Bunge la Bajeti Kuhusu Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa kwa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/ 2026.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 113(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026) uliobeba dhima ya "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu".

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ninayoisoma ni muhtasari wa taarifa nzima ya Kamati yangu. Hivyo naomba taarifa nzima iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani, yenye kurasa 29.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Tatu ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, pia ni wa mwisho katika Mpango Elekezi wa Muda Mrefu 2011/2012 – 2025/2026. Utaratibu huu wa kuandaa mipango ya muda wa kati ulilenga kuelekeza upya juhudi za kufikia malengo ya dira kwa kuweka mkazo katika ukuaji wa uchumi sanjari na kupunguza umaskini na kuchochea maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu umelenga kuweka mazingira mahsusi na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana tangu Dira ilipozinduliwa ili kufikia malengo ya dira yaliyokusudiwa. Kwa msingi huo, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano utawezesha nchi kutumia fursa za kijiografia na rasilimali zilizopo nchini kwa ajili ya uzalishaji na ukuaji wa uchumi utakaonufaisha wananchi wengi kuendana na malengo ya dira ya kuwa na maisha yenye ubora wa juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kujumuisha kwa kiasi kikubwa maoni ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati yaliyotolewa katika Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Mbili Mwezi Februari, 2021 wakati Serikali ilipowasilisha kwa mara ya kwanza Mapendekezo ya Mpango huu Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kuuboresha. Hivyo, taarifa hii ninayotoa inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu pamoja na kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026) ambao utaenda kutekelezwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa mwaka mmoja mmoja kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2016/2017 - 2020/2021). Kuhusu mwenendo wa uchumi jumla. Mwenendo wa hali ya uchumi ni kama ulivyowasilishwa kwenye taarifa yangu Sehemu ya Pili.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Sekta zilizopewa kipaumbele kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021). Naomba taarifa

ya Utekelezaji wa Sekta zilizopewa Kipaumbele kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) iiingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyo katika Sehemu ya Pili.

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bajeti Kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026). Kamati ya Bajeti imepitia na kuchambua Mpango wa Tatu wa Maendeleo wenye dhima ya *"Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."* Maeneo yaliyochambuliwa kwa kina ni misingi ya Mpango, matarajio ya ukuaji wa uchumi, viashiria vya sekta mbalimbali na matarajio, miradi ya kimkakati, ugharamiaji wa Mpango, tathmini na ufuatiliaji wa Mpango pamoja na vihatarishi vinavyoweza kusababisha malengo ya Mpango yasifikiwe. Aidha, Kamati ilifanya ulinganifu wa matarajio na hali ilivyo sasa ili kuona endapo malengo tuliyojiwekea yanaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata wasaa wa kujiridhisha endapo Mpango wa Tatu wa Maendeleo umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Muda Mrefu wa Maendeleo yaani *Long Term Perspective Plan,* Mipango na mikakati mingine ambayo Serikali imejiwekea pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020. Kamati imejiridhisha kwa kiwango kikubwa kwamba mipango mikakati husika imezingatiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mapendekezo ya Mpango wa Tatu ili kufanikisha azma ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati na sio wa kipato cha kati cha chini, Kamati imependa kuwasilisha uchambuzi wake kwenye maeneo mahsusi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja ni kwenye Malengo Mahsusi ya Mpango wa Tatu. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa umeainisha malengo mahsusi ya Mpango ambayo Serikali inatarajia kuyatekeleza. Kamati inaona kuna umuhimu wa malengo haya kwenda sanjari na hatua stahiki

zitakazochukuliwa ili kuyafikia. Kama tunavyofahamu, kutajwa na kuorodheshwa kwa malengo haya ni suala moja na kuanishwa kwa hatua stahiki za utekelezaji ni suala jingine. Ni muhimu hatua stahiki za utekelezaji wa malengo ya mpango zikaainishwa na kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kati ya malengo tajwa kuna yale ambayo ni mtambuka na yale ambayo ni ya kisekta. Ni rai ya Kamati kuwa, malengo ya kisekta yajulikane na yaonekane katika mipango ya sekta husika na kujua masuala ambayo yanapaswa kutekelezwa. Aidha, ikiwa malengo husika yatahitaji rasilimali fedha basi kuwepo na fungu la kufanikisha hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu (SATU). Mafanikio ya Mpango huu na kufikiwa kwa Dira ya Maendeleo iliyokusudiwa kwa kiasi kikubwa kunategemea matumizi ya SATU. Aidha, ni ukweli usipopingika kuwa, katika nyanja hii hasa ya sayansi na teknolojia tupo nyuma kama nchi. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali ichukue hatua za makusudi katika kuwekeza kwenye matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kufanikisha utekelezaji wa Mpango.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fursa mbalimbali za ugharamiaji wa mpango. Kati ya vyanzo vya ugharamiaji wa Mpango wa Tatu vilivyoainishwa ni pamoja na kutumia hatifungani za Halmashauri. Aidha, Serikali imekuwa na uzito kidogo katika kulitekeleza hili, kwani ni suala ambalo limekuwepo kwenye mipango kwa miaka mingi bila kutekelezwa. Hivyo basi, Kamati inaisisitiza Serikali kuanza kutumia kwa chanzo hiki na ikamilishe kwa haraka uundaji wa sera, sheria na mifumo ili chanzo hiki kianze kutumika.

Mheshimiwa Spika, kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Pamoja na kwamba Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umejielekeza katika kuhamasisha viwanda, kuzalisha kupitia malighafi za ndani. Serikali ione pia umuhimu wa kuvilinda hasa vile viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa kutumia

malighafi zinazotoka nje ambazo hazipatikani ndani. Serikali ivisaidie viwanda hivyo kuwa shindani kwa kuhakikisha kuwa mazingira ni wezeshi hasa kwa upande wa kodi zinazotozwa kwenye malighafi hizo. Hatua hii sio tu itawezesha viwanda kuwa shindani lakini pia Serikali itapata kodi stahiki. Lengo likiwa ni kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa nchini pamoja na kuongeza uuzaji wa bidhaa shindani nje ya nchi. Kamati inaona kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa viwanda hivi vya ndani vinalindwa na kulelewa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa miundombinu. Ili nchi iweze kunufaika na fursa ya kijiografia, uwepo wa miundombinu ni suala la msingi la kuzingatiwa. Pamoja na mikakati ya ujenzi na ukarabati ya miundombinu iliyoanishwa kwenye Mpango, Kamati inaisisitizia Serikali kuhakikisha kuwa miuondombinu hiyo inajengwa katika maeneo ya kimkakati ili Taifa linufaike na fursa na nafasi yake kijiografia ya kuzungukwa na kuhudumia soko la nchi sita zisizo na bandari.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Pamoja chini ya *TIC.* Kati ya maboresho yanayoenda kufanyika katika Kituo hiki cha Pamoja *(One Stop Centre-OSC)* chini ya *TIC* ni kuongeza idadi ya taasisi zinazofanya kazi kwa pamoja kufikia idadi ya taasisi 11. Aidha, pamoja na hatua hii nzuri masuala ya wawekezaji yanaweza yasifanikiwe na Kituo kushindwa kufanya kazi iliyokusudiwa ikiwa kama kutaendelea kutokuwepo kwa wafanya maamuzi wa papo kwa hapo. Hivyo, suala la kuongeza idadi ya taasisi liende sanjari na kupeleka wataalam wanaoweza kufanya maamuzi ya bila kurudi au kusubiria maelekezo kutoka makao makuu ambayo ni dhahiri kuwa yatachukua muda.

Mheshimiwa Spika, wakandarasi wa ndani; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa umekiri wakandarasi wa ndani kukosa fursa katika Sekta ya Ujenzi na hivyo miradi mingi ya ujenzi kutekelezwa na makampuni ya nje. Pamoja na hatua na mikakati mizuri iliyowekwa na Serikali ya kutoa kipaumbele kwa kampuni za ndani na mafunzo, Serikali pia

ione umuhimu wa kuyasaidia makampuni haya kifedha kwa sababu nayo ni changamoto kubwa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuweka mipango mizuri ya kusaidia makampuni ya ndani kuweza kuwa shindani, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mitaji, utoaji wa vivutio vya kikodi kwenye mitambo inayotumika na vifaa vya ujenzi. Matumizi ya wakandarasi wa ndani badala ya wakandarasi wa nje yatainufaisha nchi kiuchumi kwa kuwezesha fedha kubaki nchini na kuchochea uwekezaji, uzalishaji na kuongeza mzunguko wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ingependa kuona hatua za haraka zinachukuliwa katika kurasimisha na kuimarisha Mfuko wa Kusaidia Wakandarasi ambao tunaamini utaleta mageuzi makubwa kwa wakandarasi wa ndani katika Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa Mpango; kwa kuwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa unaenda kutekeleza pamoja na masuala mengine, maendeleo ya watu wenye vipato na viwango vya maisha tofauti, itakuwa ni busara basi Mpango huu na mipango mingine ya mwaka mmoja kuwa na Toleo la Wananchi *(publication)* ambao ndio walengwa. Hatua hii inalenga kuwaweka wananchi karibu na kujua masuala ambayo Serikali yao pendwa inataka kuwatekelezea, lakini vile vile ni nini kinachohitajika kutoka kwao. Hii itakuwa ni hatua kubwa kwa upande wa ushirikishwaji wa wananchi wake ambao wataenda kuunga mkono juhudi za Serikali na hivyo kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Pia Serikali iweke mazingira bora yatakayowezesha wananchi kuchangia katika kutekeleza baadhi ya miradi katika maeneo yao kwa mfano ujenzi wa madarasa, shule, vituo vya huduma za afya. Aidha, elimu ya mara kwa mara kutolewa na upatikanaji rahisi wa nakala za Toleo hilo ni jambo la muhimu.

Mheshimiwa Spika, ushindani wa masoko ya kikanda na kidunia; kilimo nchini kwa asilimia kubwa kinafanywa na watu binafsi ambao ni wananchi wa kawaida na ndio sekta ambayo asilimia 65 ya watu wanapata kipato. Aidha, Kamati

imebaini kwamba suala la utafutaji wa masoko nje ya nchi kwa mazao ya Kilimo halijatambuliwa wala kupewa umuhimu unaostahili katika Mpango.

Mheshimiwa Spika, kama kweli Serikali ina nia ya kuisaidia sekta hii pamoja na maendeleo ya watu wake, basi ichukue suala la utafutaji wa masoko nje ya nchi kwa manufaa ya watu wake. Serikali iainishe Mkakati wa kutafuta masoko ya mazao ya kilimo nje ya nchi kwa kuingia mikataba na wanunuzi au nchi, ili ziweze kununua mazao yetu. Aidha, moja ya jukumu la Ofisi zetu za Balozi nje ya nchi liwe ni kuongeza kasi ya utafutaji wa masoko ya mazao ya kilimo nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na kuwepo na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TanTrade)*, Mamlaka hii imekuwa inalalamikiwa kwa kutokuwa msaada kwa wakulima. Mamlaka hii imekuwa ikichukua sampuli za mazao kupeleka kwenye maonesho nje ya nchi bila ya jitihada hizo kuleta matunda. Hivyo, Kamati inaomba suala la kusaidia utafutaji wa masoko nje lipewe kipaumbele kwa sababu litahamasisha kuongezeka kwa shughuli za kilimo. Serikali iweze kusaidiana na Balozi zetu katika suala hili na vilevile ione umuhimu wa kuiangalia upya mamlaka hii na kuisaidia pale inapobidi ili iweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kujenga uchumi shindani na viwanda; Kamati imefanya uchambuzi wa viashiria vinavyoweza kutupeleka kuwa na viwanda na uchumi shindani na kubaini changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, moja ni nishati ya umeme; Taifa letu linakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa nishati ya umeme ya uhakika. Hivi sasa kiasi cha umeme kinachozalishwa nchini ni *megawatt* 1,602.3 ambapo matarajio ni kufikiwa *megawatt* 4,915 ifikapo 2025/2026. Ni wazi kwamba lazima juhudi za makusudi zifanyike ili kukamilisha miradi iliyopo na mingine ambayo iko kwenye mchakato ili kufikia azma ya kuwa na uchumi shindani. Juhudi za kuunganisha umeme kupitia Mradi wa *REA* lazima ziende

sambamba na uzalishaji wake vinginevyo miundombinu ya usambazaji itakuwepo bila umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini; Tanzania ni sehemu ya dunia na hivyo ni wazi kwamba kinachoamriwa duniani kama kigezo cha kupima wepesi wa ufanyaji biashara na uwekezaji kinatumiwa na wawekezaji wote duniani. Katika Mpango wa Pili, Taifa lilijiwekea lengo la kuwa ndani ya nchi 100 zenye mazingira mazuri ya uwekezaji na ufanyaji biashara, ambapo hadi kufikia mwaka 2020 Taifa letu lilikuwa katika nafasi ya 141 kati ya nchi 190. Aidha, lengo ni kuwa nchi ya 95 ifikapo mwaka 2026. Kamati imejiridhisha kama hakutakuwa na mabadiliko katika utekelezaji wa *Blue Print* ni wazi kwamba lengo hilo halitafikiwa. Lazima Serikali ifanye uamuzi thabiti wa kuunganisha Taasisi zote zinazohusiana na masuala ya uwekezaji na ufanyaji biashara na kubadili Sera, Sheria na Kanuni ambazo zimekuwa vikwazo kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, niongelee Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kwanza, kilimo cha mazao; pamoja na kwamba Sekta ya Kilimo inachangia asilimia 26 ya pato la Taifa na inatoa ajira kwa Watanzania zaidi ya asilimia 65, lakini sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo ambazo hazijapata utatuzi. Moja ni kilimo kwa kiasi kikubwa ni cha kujikimu, gharama kubwa ya pembejeo za kilimo, kilimo cha kutegemea mvua, upotevu wa mazao baada ya kuvuna *(post-harvest loss),* pamoja na kukosekana kwa masoko ya uhakika ya mazao ya kilimo. Changamoto hizi kwa Mpango wa Kwanza na wa Pili zilikuwepo na zimeendelea hadi kwenye Mapendekeo ya Mpango huu wa Tatu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweza kufanya yafuatayo ili kukwamua Sekta hii. Kuweka vivutio maalum kwa viwanda vya uzalishaji wa mbolea na pembejeo mbalimbali za kilimo, Kuwa na mkakati maalum wa kujenga maghala na vihenge ili kupunguza upotevu baada ya mavuno, kuongeza kiwango cha uvunaji kwa eka ili kuondoa kilimo cha kujikimu, kuanzisha na kuendeleza skimu za umwagiliaji ili kupunguza utegemezi wa mvua na kutafuta masoko ya

uhakika ya ndani na nje ili kuhakisha wakulima wanapata wanachostahili.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo ndio msingi wa uchumi wa viwanda kwa sababu ndio sekta zalishi ya malighafi ambazo zinatumika viwandani. Kilimo si tu kina tija katika uchumi wa nchi, lakini pia kina mchango mkubwa sana katika kuamua hatma ya maisha ya kila siku na maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja. Hivyo, bado Kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi kwenye sekta hii kwa sababu ya umuhimu wake katika uchumi wa viwanda na kuondoa umaskini. *(Makofi)*

Mhesimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na mwitikio mkubwa wa wananchi katika kuzalisha mazao hasa mazao ya biashara na matunda. Baada ya miaka michache ijayo kutakuwa na ongezeko kubwa la mazao kama korosho, parachichi, karanga pori, michikichi na kadhalika. Ni vyema Serikali ikaanza mapema kuweka mikakati ya kupata masoko ya mazao haya pamoja na kuhakikisha kunajengwa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao haya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo juu, Kamati inashauri yafuatayo yafanyike katika sekta ya kilimo:-

(i) Serikali itatue changamoto ya urasimu ikiwemo uwepo wa Bodi nyingi za Mazao na kusababisha Bodi hizo kuwa mzigo kwa Serikali na kwa wakulima. Serikali ilete Bungeni Muswada wa Sheria ili kufuta baadhi ya Bodi na kuanzisha taasisi chache zitakazosimamia mazao yote.

(ii) Serikali iingie mikataba na nchi nyingine ili waweze kununua baadhi ya mazao yetu yanayozalishwa kwa wingi. Kwa mfano korosho, mahindi, mbaazi, soya, matunda, mboga, nyama, samaki na maua.

(iii) Serikali ifanye ukarabati wa haraka wa machinjio za kisasa zilizopo nchi nzima na kupata ithibati kwa nyama inayozalishwa nchini ili kuwezesha kuuza nyama yetu moja

kwa moja katika masoko ya Ulaya, Asia na Uarabuni badala la kutegemea kupitia nchi jirani.

(iv) Serikali ikamilishe haraka mchakato na kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi pamoja na Viwanda vya Samaki.

(v) Serikali iboreshe utaratibu wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani na uhusishe mazao yote ya biashara ili kurahisisha mazao hayo kuuzwa katika soko la mazao.

Mheshimiwa Spika, Uvuvi. Imekuwa ni kilio cha siku nyingi cha Bunge lako kuhusiana na rasilimali zilizopo Bahari Kuu kutolinufaisha Taifa letu kama ilivyo kwa mataifa mengine. Ikumbukwe kwamba, uliunda Kamati Maalumu kushughulikia suala hili na ikatoa mapendekezo ambayo utekelezaji wake unaenda kwa mwendo usiyoridhisha. Kamati inaishauri Serikali kwanza kuharakisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kama miundombinu muhimu ya kuweza kunufaika na Uvuvi wa Bahari Kuu. Pili, kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni ambazo ni kikwazo kwa wawekezaji kuja nchini na kufanya uvuvi katika Bahari Kuu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwenda kupitia upya Taarifa ya Kamati Teule ya Spika kuhusu Uvuvi wa Bahari Kuu ili itekeleze mapendekezo yaliyotolewa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Mifugo. Tanzania pamoja na kuwa ni nchi ya Tatu Barani Afrika kwa wingi wa mifugo, ambapo inakadiriwa kuwa na ng’ombe milioni 32.2, mbuzi milioni 20 na kondoo milioni 5.5 sekta hii inakabiliwa na changamoto za ng’ombe kuwa na uzito wa chini wa wastani wa kilo 75 kati ya kiwango kinachokubalika cha kilo 135. Aidha, kwa upande wa ngozi ni asilimia 10 tu ya ngozi inayozalishwa ndiyo inafaa kwa matumizi ya viwandani.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine inayoikabili sekta hii ni pamoja miundombinu ya malisho inayosababisha migogoro ya mara kwa mara ya wakulima na wafugaji na ufugaji wa kuhamahama. Vilevile, soko la maziwa yanayozalishwa ndani linakabiliwa na changamoto kubwa hasa za kikodi na kusababisha maziwa yanayozalishwa ndani

kuwa ghali kuliko yanayoingizwa kutoka nje ya nchi. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kutatua changamoto hizi haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Watu. Katika kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, Kamati ilijielekeza katika Sekta za Elimu, Afya na Maji.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Elimu. Kamati baada ya uchambuzi wake imegundua Sekta ya Elimu inakabiliwa na changamoto kuu tatu, ambazo ni kukosekana kwa miundombinu muhimu ya kujifunza na kufundishia, mitaala kupitwa na wakati na kuzalisha wataalamu ambao hawakidhi mahitaji ya soko na uhaba wa walimu katika ngazi zote za Elimu. Changamoto zote hizi, utatuzi wake unahitaji rasilimali fedha na rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwanza kutatua suala la mitaala ili tuwe na wataalamu wanaokidhi mahitaji ya soko na pili ni kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia. Pamoja na juhudi nzuri zinazofanywa na Serikali katika Sera ya Elimu ya Msingi Bila Ada bado jitihada kubwa zinahitajika ili sera hii ilete tija iliyokusudiwa kama vile upatikanaji wa walimu wa kutosha, kuongeza miundombinu muhimu kama madarasa, matundu ya vyoo na nyumba za walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya. Katika kipindi cha miaka mitano 2015/2016 hadi mwaka 2020/2021, Serikali imeweza kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya kutoka vituo 7,014 hadi vituo 8,783 sawa na ongezeko la vituo 1,669. Hata hivyo, katika sekta hii bado kuna changamoto ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na wahudumu wa afya. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali pamoja na kasi nzuri ya ujenzi, iende sambamba na upatikanaji wa vitendea kazi muhimu na wahudumu wa afya ili majengo yatumike kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji. Kamati imebaini kwamba yawezekana kabisa changamoto ya maji haichukuliwi kwa uzito wake kutokana na takwimu ambazo

hazionyeshi uhalisia. Kulingana na takwimu za Serikali upatikanaji wa maji vijijini ni asilimia 70.1 na mijini ni asilimia 80. Takwimu hizi zinaonyesha kwamba tatizo la maji limeshughulikiwa kwa kiasi kikubwa jambo ambalo ni tofauti na uhalisia. Sababu za msingi zikiwa ni vyanzo kukauka, uharibifu wa miundombinu, miradi kukamilika lakini haitoi maji. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ili kutambua ukubwa wa tatizo na kisha kuandaa mkakati maalumu wa kutatua changamoto ya maji ambayo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Kielelezo. Kamati imefanya uchambuzi wa Miradi ya Kimkakati na kubaini kuwa Miradi ya Kielelezo imeongezeka kutoka miradi 9 iliyokuwa kwenye Mpango wa Pili hadi kufikia miradi 17 katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo. Pia, Kamati imebaini kwamba Miradi ya Kielelezo iliyokuwa kwenye Mpango wa Kwanza na wa Pili, ambayo bado haijatekelezwa na ina manufaa makubwa, utekelezaji wake umekuwa sio wa kuridhisha mathalani Mradi wa Mchuchuma na Liganga, Magadi Soda Engaruka na *Kurasini Logistic Centre*. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali badala ya kuendelea kuongeza Miradi ya Kielelezo wakati kuna miradi muhimu bado haijakamilishwa, ni vyema kuwa na Miradi michache ya Kielelezo yenye manufaa makubwa ambayo inaweza kutekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Maeneo Wezeshi ya Maendeleo ya Viwanda (Kilimo, Ardhi, Mifugo na Uvuvi). Uzoefu unaonyesha kuwa nchi nyingi duniani zimepiga hatua za uchumi wa viwanda baada ya kupiga hatua katika mapinduzi ya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ikiwa ni pamoja na kulinda uzalishaji wa viwanda vya ndani. Kamati inaona ni muhimu Serikali ikasimamia ipasavyo miradi iliyoainishwa kwenye sekta hizi kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi za viwanda pamoja na kulinda viwanda vya ndani na hivyo kupata fursa ya kukuza uchumi wetu na ushindani wa kikanda na kimataifa kupitia sekta husika.

Mheshimiwa Spika, Ugharamiaji wa Mpango. Mpango wa Tatu unatarajiwa kutumia jumla ya shilingi trilioni 114.9 kati ya fedha hizo Serikali, itachangia jumla ya shilingi trilioni 74.2

na Sekta Binafsi itachangia jumla ya shilingi trilioni 40.6. Uchambuzi wa Kamati umebaini masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mchango wa Serikali. Mpango huu katika utekelezaji wake Serikali itatoa asilimia 64.6 na Sekta Binafsi itachangia asilimia 35.3 ya rasilimali fedha zinazohitajika. Hivyo ni wazi kwamba mapato yote ya Serikali ya kodi, yasiyo ya kodi na ya Halmashauri yanatarajiwa kukua ili kutimiza lengo hili. Ili lengo hilo litimie, Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kurahisisha uendeshaji wa biashara na utozaji wa kodi ili kuvutia sekta isiyo rasmi kuwa rasmi.

(ii) Kuwekeza zaidi kwenye Mashirika ya Umma ambayo yanaweza kuleta faida ndani ya muda mfupi, mfano Shirika la *TTCL*.

(iii) Kuhakikisha kwamba, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* inafanya kazi kwa weledi na ufanisi ili kuendeleza biashara na si kuua au kuzuia ukuaji wa biashara kwa kutoza kodi kandamizi na kupanua wigo wa ukusanyaji.

Mheshimiwa Spika, endapo haya hayatafanyika itakuwa ni vigumu kufikia lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, Sekta Binafsi. Katika utekelezaji wa Mpango wa Pili Sekta Binafsi ilitarajiwa kuchangia jumla ya shilingi bilioni 48. Hadi kufikia mwaka 2020, Sekta Binafsi ilikuwa imechangia takribani shilingi bilioni 32.6. Hatua hii inaonyesha kwamba endapo Sekta Binafsi ikishirikishwa kikamilifu ina uwezo mkubwa wa kuchangia kikamilifu katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu. Changamoto kubwa inayoikabili Sekta Binafsi ni kutoaminiana na Serikali kwa sababu kumekuwa na maamuzi ambayo hayatabiriki juu ya uwekezaji wao na hivyo kusababisha uwekezaji mdogo.

Kamati inaishauri Serikali kuimarisha uwezo wa kusimamia mikataba ili Sekta Binafsi iweze kutabiri maamuzi ya Serikali na kuwekeza kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Miradi kwa Njia ya Ubia *(PPP).* Ni zaidi ya miaka 10 sasa tangu tuwe na Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Pamoja na kufanya mabadiliko mbalimbali katika sheria hiyo bado hatujaweza kuvutia na kutekeleza miradi kwa njia hii. Utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia ni njia mojawapo ya kupunguza ugharamiaji wa miradi kwa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo ni utayari wa Serikali na watendaji wake katika kutumia na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ubia. Watendaji wengi wana mtazamo wa kutekeleza kwa kutumia Bajeti ya Serikali na hivyo kutokuwekeza nguvu kwenye kuandika maandiko ya miradi ambayo inaweza kutekelezwa kwa njia ya ubia. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mtazamo huu usio na tija unabadilishwa kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa miradi kwa ubia.

Mheshimiwa Spika, Tathmini na Ufuatiliaji. Moja ya changamoto kubwa ambayo Kamati imebaini, pamoja na uwepo wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini katika Mpango wa Pili na sasa huu wa Tatu, ni kukosekana kwa Sera na Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji wa Mpango. Mfano unaonekana katika utekelezaji wa Mpango wa Pili, ambapo Serikali ilitakiwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango kila mwaka, baada ya miaka miwili na miaka minne ili itumike kupanga Mpango wa Tatu. Kamati inaishauri Serikali kuleta Sera na Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji ili kubainisha majukumu ya kila mdau katika kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango. Aidha, lisipofanyika hili tutarajie kuona utakelezaji hafifu wa Mpango huu wa Tatu tunaoupitisha sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Ujumla. Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura. Kwa mujibu wa Kifungu cha 35 cha Sheria ya Bajeti kinataka Serikali kuanzisha Mfuko wa Dharura yaani *“Contingency Fund”.* Pamoja na uwepo wa takwa hilo kisheria, bado Serikali haijaanzisha mfuko huo na badala yake imekuwa ikitenga fedha za dharura kupitia Fungu 21 - Hazina. Uwepo wa Mfuko huu utasaidia Serikali katika kutekeleza

Mpango wake wa mwaka mmoja na mitano kwa sababu pindi panapotokea majanga au matukio ambayo hayakukusudiwa mfuko huu utatumika kikamilifu tofauti na ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Serikali imefanya jitihada kubwa sana kuboresha huduma za Afya nchini jambo ambalo ni la kupongeza sana. Hata hivyo, changamoto kubwa iliyoko mbele yetu ni namna gani wananchi wanapata huduma hizo kwa bei nafuu, kwa ubora na kwa haraka. Suluhisho la jambo hili ni kuwa na Sheria ya Bima kwa wote *"Universal Coverage Health Insurance"*. Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuleta Muswada wa Sheria hiyo mbele ya Bunge lako Tukufu ili iendane sambamba na utekelezaji wa Mpango huu wa Tatu kwa sababu hivi sasa ni asilimia 20 tu ya Watanzania wako kwenye Mifuko ya Bima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Zao la Korosho. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutambua faida kubwa inayoweza kupatikana na mazao yatokanayo na korosho ni vema Serikali ikaweka katika Mpango wake wa Tatu wa Miaka Mitano unaokuja mikakati ya moja kwa moja itakayowezesha zao la korosho kuongezewa thamani na kutumia mazao yake katika kutengeneza bidhaa nyingine ili kuwaongezea kipato wakulima na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo. Pamoja na kutambua dhamira nzuri ya Serikali ya kuhakikisha tunapata manufaa makubwa kwenye uwekezaji katika Bandari zetu, Bandari ya Bagamoyo kwa muktadha huu, ni vema Serikali ikaongeza kasi ya mazungumzo na wawekezaji ili bandari hii ianze kujengwa kwani manufaa yake ni makubwa kwa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge, Naibu Spika, kwa miongozo ambayo kwa pamoja mmekuwa mkitupatia. Vilevile

napenda kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai na timu yake kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, kipekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Mbunge, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu Fedha na Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara na wataalamu wote ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Mathew Kileo, Makatibu wa Kamati Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala, Maombi Kakozi na Wilfred Akasi pamoja na Msaidizi wa Kamati Editruda Kilapilo kwa miongozo yao na ushauri wa kitalaam hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama walivyoorodheshwa kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2021/22-2025/26) - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

### 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 113 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) uliobeba dhima ya *“Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”.*

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Tatu ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, pia ni wa mwisho katika Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (Long-Term Perspective Plan - LTPP) 2011/12 – 2025/26. Utaratibu huu wa kuandaa mipango ya muda wa kati ulilenga kuelekeza upya juhudi za kufikia malengo ya Dira kwa kuweka mkazo katika ukuaji wa uchumi sanjari na kupunguza umaskini na kuchochea maendeleo ya watu.

**Mheshimiwa Spika**, Mpango huu umelenga kuweka mazingira mahsusi na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana tangu Dira ilipozinduliwa ili kufikia malengo ya Dira yaliyokusudiwa. Kwa msingi huo, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano utawezesha nchi kutumia fursa za kijiografia na rasilimali zilizopo nchini kwa ajili ya uzalishaji na ukuaji wa uchumi utakaonufaisha wananchi wengi kuendana na malengo ya Dira ya kuwa na maisha yenye ubora wa juu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kujumuisha kwa kiasi kikubwa maoni ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati yaliyotolewa katika Mkutano wa Pili wa Bunge la 12 Mwezi Februari, 2021 wakati Serikali ilipowasilisha kwa mara ya kwanza Mapendekezo ya Mpango huu Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kuuboresha. Hivyo, taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako tukufu pamoja na kutoa Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) ambao utaenda kutekelezwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa Mwaka mmoja mmoja kwa kipindi cha miaka mitano (5).

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/17-2020/21)

### 2.1. Mwenendo wa Uchumi jumla.

**Mheshimiwa Spika,** Ukuaji wa pato la Taifa ni mojawapo wa vigezo vya kupima uwezo wa nchi kukua kiuchumi na kuondoa umaskini. Katika kipindi cha miaka 4 (2016-2019)

ukuaji wa Pato la Taifa umeendelea kuwa imara, ambapo Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa **asilimia 6.9.** Sekta zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji huu ni pamoja na ukuaji katika sekta ya ujenzi (**asilimia 14.4**), uzalishaji viwandani (**asilimia 8.3**), usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (**asilimia 8.2**), shughuli za uchimbaji madini na mawe (**asilimia 8.0**); na habari na mawasiliano (**asilimia 6.2**). Aidha, Ukuaji wa sekta ya kilimo bado upo chini ya **asilimia 4** kwa kipindi chote hicho licha ya kuwa ndio sekta inayoongoza katika kuchangia Pato la Taifa kiasi cha wastani wa **asilimia 27**.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa iliyopo ni kuona Mpango huu wa Tatu unajumuisha sekta ya kilimo, viwanda na biashara katika ukuaji ambazo zinahusisha idadi kubwa ya watu. Hatua hii itasaidia kuweza kufika na kupita lengo la ukuaji wa uchumi wa zaidi ya **asilimia 8** kama ilivyoainishwa katika malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kiwango ambacho kingesaidia kukuza uchumi kupunguza umaskini nchini kwa kasi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mfumuko wa bei umeendelea kuwa kwenye kiwango cha chini na kubaki katika wigo wa tarakimu moja **asilimia 4.4** katika kipindi cha miaka minne 4 (2016-2019) na hivyo kufikia malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa kiwango cha kutokuzidi **asilimia 5** ya Mfumuko wa Bei. Ni matumaini ya Kamati kuwa katika Mpango huu wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa, Serikali itaendelea kudhibiti mwenendo wa ukuaji wa mfumuko wa bei kwa utekelezaji thabiti wa sera za fedha na kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) umeonyesha ufanisi mkubwa katika kudumisha uhimilivu wa uchumi jumla na hivyo kusaidiaTanzania kuwa miongoni mwa nchi za kipato cha kati cha chini mapema zaidi kabla ya kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Hatua hii ilitokana na kuongezeka kwa pato la mtu (GNI) kutoka **shilingi**

**2,452,406 (sawa na dola za Marekani 1,020)** mwaka 2018 hadi **shilingi 2,577,967** (sawa na **dola za Marekani 1,080**) mwaka 2019, kiasi hicho ni juu ya kiasi kilichowekwa na Benki ya Dunia cha **dola za Marekani 1,036** ili nchi iweze kufikia hadhi ya kipato cha kati cha chini (Lower-middle income status).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha miaka minne thamani ya shilingi imeendelea kuimarika dhidi ya sarafu kubwa kutokana na kuimarika kwa urari wa biashara kati yetu na washirika wetu wa kibiashara. Takwimu zinaonyesha kuwa, mwaka 2016/17 kiwango cha kubadilisha dola moja ya Kimarekani ilikuwa ni **Shilingi 2,230.1** na mwishoni mwa mwaka 2019/20 kiwango cha kubadilisha dola moja ya marekani kilikuwa **Shilingi 2,295.5**. Utulivu huu umepelekea uwepo wa fedha za kigeni za kutosha na hivyo kukidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha **miezi 5.6** (Desemba, 2020). Hivyo, ni matumaini ya Kamati kuwa shabaha na malengo ya Mpango huu wa Tatu yatasaidia kuendelea kuimarisha sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Deni la Taifa limeendelea kukua na kufikia **shilingi trilioni 59 (Desemba 2020)** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 54.8** kipindi kama hicho mwaka 2019 ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 7.6.** Kati ya kiasi hicho deni la ndani lilifikia **shilingi trilioni 16.2** na deni la nje **shilingi trilioni 42.8.** Ongezeko la deni limetokana na Ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Hata hivyo, Kamati inatoa angalizo kwamba mikopo yote ielekezwe katika kukamilisha miradi ya maendeleo hasa ile ya kimkakati iliyoanzishwa ili ikamilike kwa wakati badala ya kuanza miradi mipya. Aidha, katika Mpango huu wa Tatu, Serikali iendelee kufanya tathmini ya Viashiria vyote vya uhimilivu wa deni kuona kama vinaendelea kukidhi chini ya viwango vya ukomo vilivyokubalika kimataifa ili Deni la taifa liendelee kuwa himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu kwa viashiria vyote muhimu

## 2.2. Utekelezaji wa Sekta zilizopewa Kipaumbele kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21)

### 2.2.1. Sekta ya Miundombinu

#### a) Barabara

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imepata mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu ya barabara nchini, ambapo katika kipindi cha miaka mitano barabara za lami zenye urefu wa **km 3,537.0** na barabara za mzunguko za kuepusha na kupunguza msongamano wa magari mijini, zenye urefu wa **km 82.6** zimejengwa. Aidha, hadi kufikia Juni 2020, **km 1,298.44** za barabara za lami zilikuwa katika matengenezo na barabara kuu zenye urefu wa **km 300.9** zilikarabatiwa pamoja na madaraja makubwa 12 yalikamilika ujenzi wake. Hii ni hatua kubwa na inastahili pongezi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo ya kuridhisha ni dhahiri bado kuna changamoto kubwa ya barabara nchini hasa kwa kutambua kuwa nchi yetu ina urefu wa mtandao wa barabara (vijijini, wilaya, mikoa na barabara kuu) unaokadiriwa kufikia **km 143,279** na hadi sasa tumeweza kujenga barabara zetu kwa kiwango cha lami takribani **km 15,000** tu tangu tupate uhuru. Hii ni chini ya **asilimia 10.5** ya mtandao wote wa barabara tulionao. Maeneo mengi bado hayafikiki kwa urahisi hasa kipindi cha masika kutokana na ubovu wa barabara au kutokuwa na barabara kabisa. Ubovu wa barabara umepelekea kuongezeka kwa gharama za maisha katika maeneo hayo inayosababishwa na gharama za usafirishaji kuwa kubwa, na pia wakulima kushindwa kusafirisha mazao yao kwa urahisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kwa sasa, kuendelea kutoa kipaumbele kwa barabara ambazo zinaunganisha maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya biashara na chakula. Ukamilishaji wa barabara hizo utawezesha mazao hayo kusafirishwa kwa urahisi, na pia kuvutia wawekezaji kujenga viwanda katika maeneo hayo

ambayo kiuhalisia yana malighafi nyingi na hivyo kurahisha uchukuzi wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kufanya hivyo, tutafungua fursa za kiuchumi na biashara haraka zaidi katika maeneo hayo na kuleta matokeo makubwa kwa nchi nzima. Vile vile, Serikali ione umuhimu wa kufanikisha ujenzi wa barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani ili kukuza biashara baina yetu na majirani zetu, ambao kwa kiasi kikubwa wanategemea sana bidhaa kutoka kwetu hasa chakula.

**b) Reli**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya reli nchini, kwa kuanza ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge), kukarabati Reli ya Kati yenye kiwango cha Meter Gauge, kukarabati karakana, kununua mabehewa na vifaa vingine. Hatua hizi zimetuwezesha kuendelea kusafirisha mizigo na abiria katika Reli ya Kati (Dar es salaam hadi Mwanza) na Dar es salaam – Tanga – Kilimanjaro – Arusha na hivyo kuiingizia mapato Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio haya yaliyopatikana katika uboreshaji wa miundombinu ya reli, Kamati haijaona Serikali ikizungumzia kwa kina Reli ya TAZARA ingawa Kamati ilitoa maoni yake ilipowasilisha taarifa yake kuhusu Mapendekezo ya Mpango huu mwezi Februari, 2021. Reli hii ambayo nayo ni ya kiwango cha kimataifa *(standard gauge)* bado ina umuhimu mkubwa sana wa kiuchumi na inaweza kutumiwa vizuri na nchi za Malawi, Zambia, Msumbiji, na DRC. Hivyo, Kamati ingependa kuishauri tena Serikali mambo yafuatayo: -

i. Serikali ikamilishe haraka mapitio ya Mkataba na Sheria inayosimamia Reli ya TAZARA ili kutatua changamoto zilizopo na kuiwezesha Tanzania kuisimamia na kuiendesha reli hiyo pamoja na miundombinu yake kwa upande wa Tanzania;

ii. Serikali itatue haraka changamoto za kimenejimenti zinazoikabili TAZARA; na

iii. Serikali ione uwezekano wa kuiunganisha Reli ya TAZARA na reli nyingine ili kuwa na mtandao mmoja wa Reli nchi nzima.

## c) Usafiri wa Anga

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza Serikali kwa juhudi zake za kuboresha miundombinu ya usafiri wa anga kwa kukarabati viwanja vya ndege, kujenga viwanja vipya katika maeneo mbalimbali nchini, kununua na kufunga rada nne (4) za kuongozea ndege za kiraia katika Viwanja vya ndege vya JNIA, KIA, Songwe na Mwanza, kuimarisha Shirika la ATCL kwa kununua ndege 8, kuendelea na mchakato wa kununua ndege nyingine 3, ambapo kati ya hizo ndege moja itakuwa ni ndege ya kubeba mizigo. Maendeleo ya sekta ya anga yataiwezesha nchi yetu kupiga hatua zaidi katika sekta ya utalii pamoja na usafirishaji wa bidhaa zetu hasa zile za kilimo (Matunda, mbogamboga na maua).

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia changamoto ya kushuka kwa idadi ya watalii wanaokuja nchini, Kamati inaishauri ATCL kuongeza safari zake za ndani ili kujiongezea miruko na hivyo kupunguza hasara kwa kusimamisha ndege. Aidha, ATCL itumie fursa ya kusafirisha mizigo hasa matunda, mbogamboga, maua na samaki kutoka hapa nchini kwenda nchi za nje badala ya kuachia ndege za nchi jirani kutumika.

## d) Bandari

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika miundombinu ya bandari nchini. Maboresho makubwa yamefanywa katika Bandari ya Dar es salaam, Mtwara na Tanga, zilizopo Bahari ya Hindi, lakini pia imeboresha bandari zilizopo Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Baada ya maboresho haya, sasa ni vema Bandari hizi zikapewa vifaa vyote muhimu vitakavyoongeza ufanisi katika utendaji kazi. Vifaa hivyo ni pamoja na *Scanners, Cranes, Rollers* pamoja na kujenga miundombinu ya reli bandarini.

**e) Sekta ya Viwanda na Biashara**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mazingira bora yaliyowezesha kuanzisha viwanda nchini. Mafanikio haya lazima yalindwe na kuendelezwa kwa juhudi kubwa. Ili kulinda viwanda vyetu na kulinda mafanikio yaliyopatikana, ni vema Serikali ikaja na mkakati mahsusi wa kulinda viwanda na bidhaa zetu za ndani. Hili linaweza kufanikiwa kwa kupunguza uingizaji wa bidhaa ambazo hazina umuhimu mkubwa na badala yake kuhamasisha bidhaa ambazo zinazalishwa au zinaweza kuzalishwa kiurahisi nchini na kuzuia uingizaji wa bidhaa zisizo na ubora. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha haraka iwezekanavyo mchakato wa kuleta Bungeni Sheria ya Kuwezesha Biashara (Business Facilitation Act) pamoja na Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Biashara (Trade Remedes Act) ili zianze kutumika Julai 1, 2021.

**f) Sekta ya Ardhi na Mazingira**

**Mheshimiwa Spika,** Karibu asilimia sabini (70%) ya watu wa Tanzania wanaishi maeneo ya vijijini wakitegemea kilimo na maliasili katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Kutokana na utegemezi mkubwa wa shughuli hizi, kumepelekea kuanza kuwa na uharibifu mkubwa wa ardhi na vyanzo vya maji, uharibifu wa misitu (*Deforestation*) na uharibifu wa uoto wa asili. Endapo hakutakuwa na hatua madhubuti ya kulinda mazingira yetu, maisha ya watu hawa karibu asilimia 70 yatakuwa hatarini.

**Mheshimiwa Spika,** ili kulinda mazingira yetu Kamati inaishauri Serikari yafuatayo;

i. Serikali iwezeshe uwepo wa Mfuko wa Mazingira wenye Vyanzo vya Mapato vya uhakika kwa kufanya mabadiliko ya Sheria iliyoanzisha Mfuko huu;

ii. Serikali iweke mkakati wa kuwepo na programu za upandaji miti nchi nzima kila mwaka; na

iii. Serikali iongeze usimamizi na ulinzi katika vyanzo vya maji na misitu.

## g) Maendeleo ya Rasilimali watu na huduma za jamii

### i. Afya

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua kubwa ya kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya nchini kwa kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali nyingi katika maeneo yote nchini, kuongeza idadi ya watoa huduma za afya pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio ya kuridhisha yaliyopatikana katika Sekta ya Afya, Kamati ingependa kutoa maoni yafuatayo;

i. Serikali ikamilishe ujenzi wa Maboma ya Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali na kupeleka watumishi, dawa na vifaa tiba vya kutosha;

ii. Serikali itoe fedha inazopaswa kutoa kwa MSD ili Taasisi hii iweze kusambaza dawa na vifaa tiba vya kutosha nchini pamoja na kuiwezesha kusambaza dawa na vifaa tiba katika nchi za SADC kwa lengo la kujiongezea mapato;

iii. Serikali iweke mkakati mahsusi wa kukabiliana na milipuko ya Ugonjwa wa Virusi vya Korona (Covid-19), pamoja na kuendelea kupambana na magonjwa mengine hasa Malaria na Kansa, ambayo yanachangia sana katika idadi ya vifo nchini; na

iv. Serikali iongeze kiwango cha dawa inachonunua kwenye Kiwanda cha *Biotech Products Limited* kwa ajili ya kuua viluwiluwi ambao wanapokomaa hugeuka kuwa mbu wanaoeneza vijidudu vya ugonjwa wa malaria pamoja na magonjwa mengine kama dengue, zika, matende, homa ya manjano (yellow fever), chikungunya na homa ya bonde la ufa (rift valley fever).

**ii. Elimu**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio makubwa ambayo Serikali imeyafikia katika kuboresha elimu nchini, wakati umefika kwa nchi yetu kuona umuhimu wa kupitia upya mitaala pamoja na muundo wa elimu (*education structure)* kuweza kufanya maboresho yatakayoweza wahitimu kuwa na ujuzi na maarifa yanayohitajika kwenye soko la ajira, yatakayo wawezesha kujiajiri au kufanya kazi kwenye sekta muhimu kiuchumi kama viwanda, TEHAMA, sayansi na teknolojia, nishati na madini. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini hii haraka, ili tunapoanza kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo tuanze tukijielekeza katika mtazamo mpya unaofungamanisha elimu na maendeleo ya viwanda na uchumi shindani.

## 3.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2021/22-2025/26)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti imepitia na kuchambua Mpango wa Tatu wa Maendeleo wenye Dhima ya ***"Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."*** Maeneo yaliyochambuliwa kwa kina ni misingi ya mpango, matarajio ya ukuaji wa uchumi, viashiria vya sekta mbalimbali na matarajio, miradi ya kimkakati, ugharamiaji wa Mpango, tathmini na ufatiliaji wa Mpango pamoja na vihatarishi vinavyoweza kusababisha malengo ya Mpango yasifikiwe. Aidha, Kamati ilifanya ulinganifu wa matarajio na hali ilivyo sasa ili kuona endapo malengo tuliyojiwekea yanaweza kufikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipata wasaa wa kujiridhisha endapo Mpango wa Maendeleo wa Tatu umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Muda Mrefu wa Maendeleo yaani *Long Term Perspective Plan,* Mipango na mikakati mingine ambayo Serikali imejiwekea pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020. Kamati imejiridhisha kwa kiwango kikubwa kwamba mipango mikakati husika imezingatiwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mapendekezo ya Mpango wa Tatu ili kufanikisha azma ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati, na sio wa kipato cha kati cha chini, Kamati imependa kuwasilisha uchambuzi wake kwenye maeneo mahsusi yafuatayo:-

### 3.1. Malengo Mahsusi ya Mpango wa Tatu

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa umeainisha malengo mahsusi ya Mpango ambayo Serikali inatarajia kuyatekeleza. Kamati inaona kuna umuhimu wa malengo haya kwenda sanjari na hatua stahiki zitakazochukuliwa ili kuyafikia. Kama tunavyofahamu, kutajwa na kuorodheshwa kwa malengo haya ni suala moja, na kuanishwa kwa hatua stahiki za utekelezaji ni suala lingine. Ni muhimu hatua stahiki za utekelezaji wa malengo ya mpango zikaainishwa na kutekelezwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya malengo tajwa kuna yale ambayo ni mtambuka na yale ambayo ni ya kisekta. Ni rai ya Kamati kuwa, malengo ya kisekta yajulikane na yaonekane katika mipango ya sekta husika na kujua masuala ambayo yanapaswa kutekelezwa. Aidha, ikiwa malengo husika yatahitaji rasilimali fedha basi kuwepo na fungu la kufanikisha hilo.

### 3.2. Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (SATU)

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Mpango huu na kufikiwa kwa Dira ya Maendeleo iliyokusudiwa kwa kiasi kikubwa kunategemea matumizi ya SATU. Aidha, ni ukweli usipopingika kuwa, katika nyanja hii hasa ya sayansi na teknolojia tupo nyuma kama nchi. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali ichukue hatua za makusudi katika kuwekeza kwenye matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kufanikisha utekelezaji wa Mpango.

### 3.3. Matumizi ya fursa mbalimbali za ugharamiaji wa Mpango

**Mheshimiwa Spika,** kati ya vyanzo vya ugharamiaji wa Mpango wa Tatu vilivyoainishwa ni pamoja na kutumia

hatifungani za Halmashauri. Aidha, Serikali imekuwa na uzito kidogo katika kulitekeleza hili, kwani ni suala ambalo limekuwepo kwenye mipango kwa miaka mingi bila kutekelezwa. Hivyo basi, Kamati inaisisitizia Serikali kuanza kutumia kwa chanzo hiki na ikamilishe kwa haraka uundaji wa sera, sheria na mifumo ili chanzo hiki kianze kutumika.

### 3.4. Kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umejielekeza katika kuhamasisha viwanda kuzalisha kupitia malighafi za ndani. Serikali ione pia umuhimu wa kuvilinda hasa vile viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa kutumia malighafi zinazotoka nje ambazo hazipatikani ndani. Serikali ivisaidie viwanda hivyo kuwa shindani kwa kuhakikisha kuwa mazingira ni wezeshi hasa kwa upande wa kodi zinazotozwa kwenye malighafi hizo. Hatua hii sio tu itawezesha viwanda kuwa shindani lakini pia Serikali itapata kodi stahiki. Lengo likiwa ni kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa nchini pamoja na kuongeza uuzaji wa bidhaa shindani nje ya nchi. Kamati inaona kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa viwanda hivi vya ndani vinalindwa na kulelewa.

### 3.5. Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu

**Mheshimiwa Spika**, ili nchi iweze kunufaika na fursa ya kijiografia, uwepo wa miundombinu ni suala la msingi la kuzingatiwa. Pamoja na mikakati ya ujenzi na ukarabati ya miundombinu iliyoanishwa kwenye Mpango, Kamati inaisisitizia Serikali kuhakikisha kuwa miuondombinu hiyo inajengwa katika maeneo ya kimkakati ili Taifa linufaike na fursa na nafasi yake kijiografia ya kuzungukwa na kuhudumia soko la nchi sita (6) zisizo na bandari.

### 3.6. Kituo cha pamoja chini ya TIC

**Mheshimiwa Spika,** kati ya maboresho yanayoenda kufanyika katika Kituo hiki cha pamoja (One Stop Centre-OSC) chini ya TIC ni kuongeza idadi ya taasisi zinazofanya kazi kwa pamoja kufikia idadi ya taasisi 11. Aidha, pamoja na hatua hii nzuri

masuala ya wawekezaji yanaweza yasifanikiwe na Kituo kushindwa kufanya kazi iliyokusudiwa ikiwa kama kutaendelea kutokuwepo kwa wafanya maamuzi wa papo kwa hapo. Hivyo, suala la kuongeza idadi ya taasisi liende sanjari na kupeleka wataalamu wanaoweza kufanya maamuzi ya bila kurudi au kusubiria maelekezo kutoka makao makuu ambayo ni dhahiri kuwa yatachukua muda.

### 3.7. Wakandarasi wa Ndani

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa umekiri wakandarasi wa ndani kukosa fursa katika sekta ya ujenzi na hivyo miradi mingi ya ujenzi kutekelezwa na makampuni ya nje. Pamoja na hatua na mikakati mizuri iliyowekwa na Serikali ya kutoa kipaumbele kwa kampuni za ndani na mafunzo, Serikali pia ione umuhimu wa kuyasaidia makampuni haya kifedha kwa sababu nayo ni changamoto kubwa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuweka mipango mizuri ya kusaidia makampuni ya ndani kuweza kuwa shindani, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mitaji, utoaji wa vivutio vya kikodi kwenye mitambo inayotumika na vifaa vya ujenzi. Matumizi ya wakandarasi wa ndani badala ya wakandarasi wa nje yatainufaisha nchi kiuchumi kwa kuwezesha fedha kubaki nchini na kuchochea uwekezaji, uzalishaji na kuongeza mzunguko wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamati ingependa kuona hatua za haraka zinachukuliwa katika kurasimisha na kuimarisha Mfuko wa Kusaidia Wakandarasi ambao tunaamini utaleta mageuzi makubwa kwa wakandarasi wa ndani katika sekta ya ujenzi.

### 3.8. Usambazaji wa Mpango

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa unaenda kutekeleza pamoja na masuala mengine maendeleo ya watu wenye vipato na viwango vya maisha tofauti, itakuwa ni busara basi Mpango huu na mipango ile ya mwaka mmoja kuwa na Toleo la Wananchi (publication) ambao ndio walengwa. Hatua hii inalenga kuwaweka wananchi karibu na kujua masuala ambayo Serikali yao pendwa inataka kuwatekelezea lakini

vile vile ni nini kinachohitajika kutoka kwao. Hii itakuwa ni hatua kubwa kwa upande wa ushirikishwaji wa wananchi wake ambao wataenda kuunga mkono juhudi za Serikali na hivyo kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Serikali iweke mazingira bora yatakayowezesha wananchi kuchangia katika kutekeleza baadhi ya miradi katika maeneo yao kwa mfano ujenzi wa madaraja, shule, vituo vya huduma za afya. Aidha, elimu ya mara kwa mara kutolewa na upatikanaji rahisi wa nakala za Toleo hilo ni jambo la muhimu.

### 3.9. Ushindani wa Masoko ya Kikanda na Dunia

**Mheshimiwa Spika,** Kilimo nchini kwa asilimia kubwa kinafanywa na watu binafsi ambao ni wananchi wa kawaida na ndio sekta ambayo **asilimia 65** ya watu wanapata kipato. Aidha, Kamati imebaini kwamba suala la utafutaji wa masoko nje ya nchi kwa mazao ya Kilimo halijatambuliwa wala kupewa umuhimu unaostahili katika Mpango.

**Mheshimiwa Spika**, kama kweli Serikali inania ya kuisaidia sekta hii pamoja na maendeleo ya watu wake, basi ichukue suala la utafutaji wa masoko nje ya nchi kwa manufaa ya watu wake. Serikali iainishe Mkakati wa kutafuta masoko ya mazao ya Kilimo nje ya nchi kwa kuingia mikataba na wanunuzi au nchi, ili ziweze kununua mazao yetu. Aidha, moja ya jukumu la Ofisi zetu za ubalozi nje ya nchi liwe ni kuongeza kasi ya utafutaji wa masoko ya mazao ya Kilimo nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, pamoja na kuwepo na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Mamlaka hii imekuwa inalalamikiwa kwa kutokuwa msaada kwa wakulima. Mamlaka hii imekuwa ikichukua sampuli za mazao kupeleka kwenye maonesho nje ya nchi bila ya jitihada hizo kuleta matunda. Hivyo, Kamati inaomba suala la kusaidia utafutaji wa masoko nje lipewe kipaumbele kwa sababu litahamasisha kuongezeka kwa shughuli za kilimo. Serikali iweze kusaidiana na balozi zetu katika suala hili na vilevile ione umuhimu wa kuiangalia upya Mamlaka hii na kuisaidia pale inapobidi ili iweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

### 3.10. Kujenga uchumi Shindani na Viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa viashiria vinavyoweza kutupeleka kuwa na viwanda na uchumi shindani na kubaini changamoto zifuatazo:-

#### 3.10.1. Nishati ya Umeme

**Mheshimiwa Spika,** Taifa letu linakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa nishati ya umeme ya uhakika. Hivi sasa kiasi cha umeme kinachozalishwa nchini ni **Mw 1,602.3** ambapo matarajio ni kufika **Mw 4,915** ifikapo 2025/26. Ni wazi kwamba lazima juhudi za makusudi zifanyike ili kukamilisha miradi iliyopo na mingine ambayo iko kwenye mchakato ili kufikia azma ya kuwa na uchumi shindani. Juhudi za kuunganisha umeme kupitia mradi wa REA lazima ziende sambamba na uzalishaji wake vinginevyo miundombinu ya usambazaji itakuwepo bila umeme wa uhakika.

#### 3.10.2. Mazingira ya Ufanyaji Biashara na Uwekezaji nchini

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni sehemu ya Dunia na hivyo ni wazi kwamba kinachoamriwa Duniani kama kigezo cha kupima Wepesi wa Ufanyaji Biashara na Uwekezaji kinatumiwa na Wawekezaji wote Duniani. Katika Mpango wa Pili, Taifa lilijiwekea lengo la kuwa ndani ya nchi 100 zenye mazingira mazuri ya Uwekezaji na Ufanyaji Biashara, ambapo hadi kufikia mwaka 2020 Taifa letu lilikuwa katika nafasi ya 141 kati ya nchi 190. Aidha, lengo ni kuwa nchi ya 95 ifikapo mwaka 2026. Kamati imejiridhisha kama hakutakuwa na mabadiliko katika utekelezaji wa *Blue Print* ni wazi kwamba lengo hili halitafikiwa. Lazima Serikali ifanye uamuzi thabiti wa kuunganisha Taasisi zote zinazohusiana na masuala ya uwekezaji na ufanyaji biashara na kubadili Sera, Sheria na Kanuni ambazo zimekuwa vikwazo kwa wawekezaji.

#### 3.10.3. Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

**a) Kilimo cha Mazao**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba Sekta ya Kilimo inachangia **asilimia 26** ya Pato la Taifa na inatoa ajira kwa Watanzania zaidi ya **asilimia 65**, Sekta hii inakabiliwa na

changamoto zifuatazo ambazo hazijapata utatuzi. Moja ni Kilimo kwa kiasi kikubwa ni cha kujikimu, gharama kubwa ya pembejeo za kilimo, kilimo cha kutegemea mvua, upotevu wa mazao baada ya kuvuna *"post-harvest loss",* pamoja na kukosekana kwa masoko ya uhakika ya mazao ya kilimo. Changamoto hizi kwa Mpango wa Kwanza na Pili zilikuwepo na zimeendelea hadi kwenye mapendekeo ya Mpango huu wa Tatu.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inaweza kufanya yafuatayo ili kukwamua Sekta hii. Kuweka vivutio maalumu kwa viwanda vya uzalishaji wa mbolea na pembejeo mbalimbali za Kilimo, Kuwa na mkakati maalumu wa kujenga maghala na vihenge ili kupunguza upotevu baada ya mavuno, kuongeza kiwango cha uvunaji kwa eka ili kuondoa kilimo cha kujikimu, kuanzisha na kuendeleza skimu za umwagiliaji ili kupunguza utegemezi wa mvua na kutafuta masoko ya uhakika ya ndani na nje ili kuhakisha wakulima wanapata wanachostahili.

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Kilimo ndio msingi wa uchumi wa Viwanda kwa sababu ndio sekta zalishi ya malighafi ambazo zinatumika viwandani. Kilimo si tu kina tija katika Uchumi wa Nchi lakini pia kina mchango mkubwa sana katika kuamua hatma ya maisha ya kila siku na maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja. Hivyo, bado Kamati inaishauri Serikali kuwekeza zaidi kwenye sekta hii kwa sababu ya umuhimu wake katika uchumi wa viwanda na kuondoa umasikini.

**Mhesimiwa Spika,** hivi karibuni kumekuwa na mwitikio mkubwa wa wananchi katika kuzalisha mazao hasa mazao ya biashara na matunda. Baada ya miaka michache ijayo kutakuwa na ongezeko kubwa la mazao kama korosho, parachichi, karanga pori (macadamia nuts), michikichi, n.k. Ni vema Serikali ikaanza mapema kuweka mikakati ya kupata masoko ya mazao haya pamoja na kuhakikisha kunajengwa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao haya.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maelezo ya hapo juu Kamati inashauri yafuatayo yafanyike katika sekta ya kilimo: -

i. Serikali itatue changamoto ya urasimu ikiwemo uwepo wa Bodi nyingi za Mazao na kupelekea Bodi hizo kuwa mzigo kwa Serikali na kwa wakulima. Serikali ilete Bungeni Muswada wa Sheria ili kufuta baadhi ya Bodi na kuanzisha Taasisi chache zitakazosimamia mazao yote;

ii. Serikali iingie mikataba na nchi nyingine ili waweze kununua baadhi ya mazao yetu yanayozalishwa kwa wingi. Kwa mfano Korosho, mahindi, Mbaazi, Soya, matunda, mboga, nyama, samaki na maua;

iii. Serikali ifanyie ukarabati wa haraka wa machinjio (arbortour) za kisasa zilizopo nchi nzima na kupata ithibati (hati ya ubora) kwa nyama inayozalishwa nchini ili kuwezesha kuuza nyama yetu moja kwa moja katika masoko ya Ulaya, Asia na Uarabuni badala la kutegemea kupitia nchi jirani;

iv. Serikali ikamilishe haraka mchakato na kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi pamoja na Viwanda vya samaki; na

v. Serikali iboreshe utaratibu wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani na uhusishe mazao yote ya biashara ili kurahisisha mazao hayo kuuzwa katika soko la mazao (TMX).

**b) Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika**, imekuwa ni kilio cha siku nyingi cha Bunge lako kuhusiana na rasilimali zilizopo Bahari Kuu kutolinufaisha Taifa letu kama ilivyo kwa mataifa mengine. Ikumbukwe kwamba, uliunda Kamati maalumu kushughulikia suala hili na ikatoa mapendekezo ambayo utekelezaji wake unaenda kwa mwendo isiyoridhisha. Kamati inaishauri Serikali **kwanza** kuharakisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kama miundombinu muhimu ya kuweza kunufaika na Uvuvi wa Bahari Kuu. **Pili,** kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni ambazo ni kikwazo kwa wawekezaji kuja nchini na kufanya uvuvi katika Bahari Kuu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwenda kupitia upya Taarifa ya Kamati Teule ya Spika kuhusu Uvuvi wa Bahari Kuu ili itekeleze mapendekezo yaliyotolewa kikamilifu.

**c) Mifugo**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania pamoja na kuwa ni nchi ya Tatu Barani Afrika kwa wingi wa mifugo, ambapo inakadiriwa kuwa na Ng'ombe **milioni 32.2,** Mbuzi **milioni 20** na Kondoo **Milioni 5.5.** Sekta hii inakabiliwa na changamoto za ng'ombe kuwa na uzito wa chini wa wastani wa kg 75 kati ya kiwango kinachokubalika cha kg 135. Aidha, kwa upande wa ngozi ni **asilimia 10** tu ya ngozi inayozalishwa ndio inafaa kwa matumizi ya viwandani. Changamoto nyingine inayoikabili sekta hii ni pamoja miundombinu ya malisho inayosababisha migogoro ya mara kwa mara ya wakulima na wafugaji na ufugaji wa kuhamahama. Vilevile, soko la maziwa yanayozalishwa ndani linakabiliwa na changamoto kubwa hasa za kikodi na kusababisha maziwa yanayozalishwa ndani kuwa ghali kuliko yanayoingizwa kutoka nje ya nchi. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kutatua changamoto hizi haraka iwezekanavyo.

### 3.11. Maendeleo ya Watu

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, Kamati ilijielekeza katika Sekta za Elimu, Afya na Maji.

#### 3.11.1. Sekta ya Elimu

**Mheshimiwa Spika,** Kamati baada ya uchambuzi wake imegundua Sekta ya Elimu inakabiliwa na changamoto kuu tatu, ambazo ni kukosekana kwa miundombinu muhimu ya kujifunza na kufundishia, mitaala kupitwa na wakati na kuzalisha wataalamu ambao hawakidhi mahitaji ya soko na uhaba wa waalimu katika ngazi zote za Elimu. Changamoto zote hizi, utatuzi wake unahitaji rasilimali fedha na rasilimali watu. Kamati inaishauri Serikali **kwanza** kutatua suala la mitaala ili tuwe na wataalamu wanaokidhi mahitaji ya soko na **pili** ni kuboresha miundombinu ya kujifunza na kufundishia. Pamoja na juhudi nzuri zilizofanywa na Serikali katika sera ya elimumsingi bila ada bado jitihada kubwa zinahitajika ili sera hii ilete tija iliyokusudiwa kama vile upatikanaji wa walimu wa kutosha, kuongeza miundombinu muhimu kama madarasa, matundu ya vyoo na nyumba za walimu.

### 3.11.2. Sekta ya Afya.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha miaka mitano 2015/16 hadi mwaka 2020/21, Serikali imeweza kuongeza vituo vya kutolea huduma za Afya kutoka **vituo 7,014** hadi **vituo 8,783** sawa na ongezeko la **vituo 1,669**. Hata hivyo, katika sekta hii bado kuna changamoto ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na wahudumu wa afya. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali pamoja na kasi nzuri ya ujenzi, iende sambamba na upatikanaji wa vitendea kazi muhimu na wahudumu wa afya ili majengo yatumike kikamilifu.

### 3.11.3. Sekta ya Maji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba yawezekana kabisa changamoto ya maji haichukuliwi kwa uzito wake kutokana na takwimu ambazo hazionyeshi uhalisia. Kulingana na takwimu za Serikali upatikanaji wa maji vijijini ni **asilimia 70.1** na mijini ni **asilimia 80.** Takwimu hizi zinaonyesha kwamba tatizo la maji limeshughulikiwa kwa kiasi kikubwa jambo ambalo ni tofauti na uhalisia. Sababu za msingi zikiwa ni vyanzo kukauka, uharibifu wa miundombinu, miradi kukamilika lakini haitoi maji. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ili kutambua ukubwa wa tatizo na kisha kuandaa mkakati maalumu wa kutatua changamoto ya maji ambayo ni kubwa sana.

### 3.12. Miradi ya Kielelezo (Flagship Projects).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa Miradi ya Kimkakati na kubaini kuwa Miradi ya kielelezo imeongezeka kutoka **miradi 9** iliyokuwa kwenye Mpango wa Pili hadi kufikia **miradi 17** katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo. Pia, Kamati imebaini kwamba miradi ya kielelezo iliyokuwa kwenye Mpango wa Kwanza na wa Pili, ambayo bado haijatekelezwa na ina manufaa makubwa, utekelezaji wake umekuwa sio wakuridhisha mathalani mradi wa Mchuchuma na Liganga, Magadi Soda Engaruka na Kurasini Logistic Centre. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali badala ya kuendelea kuongeza miradi ya kielelezo wakati kuna miradi muhimu bado haijakamilishwa, ni vyema kuwa na miradi michache ya kielelezo yenye manufaa makubwa ambayo inaweza kutekelezwa kikamilifu.

### 3.13. Maeneo Wezeshi ya Maendeleo ya Viwanda (Kilimo, Ardhi, Mifugo na Uvuvi)

**Mheshimiwa Spika**, uzoefu unaonyesha kuwa nchi nyingi duniani zimepiga hatua za uchumi wa viwanda baada ya kupiga hatua katika mapinduzi ya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ikiwa pamoja na kulinda uzalishaji wa viwanda vya ndani. Kamati inaona ni muhimu Serikali ikasimamia ipasavyo miradi iliyoainishwa kwenye sekta hizi kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi za viwanda pamoja na kulinda viwanda vya ndani na hivyo kupata fursa ya kukuza uchumi wetu (Pato la Taifa) na ushindani wa kikanda na kimataifa kupitia sekta husika.

### 3.14. Ugharamiaji wa Mpango

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Tatu unatarajiwa kutumia jumla ya **shilingi trilioni 114.9** kati ya fedha hizo Serikali itachangia juma ya **shilingi trilioni 74.2** na Sekta Binafsi itachangia jumla ya **shilingi trilioni 40.6.** Uchambuzi wa Kamati umebaini masuala yafuatayo:-

#### 3.14.1. Mchango wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Mpango huu katika utekelezaji wake Serikali itatoa **asilimia 64.6** na Sekta Binafsi itachangia **asilimia 35.3** ya rasilimali fedha zinazohitajika. Hivyo ni wazi kwamba mapato yote ya Serikali ya kodi, yasiyo ya kodi na ya Halmashauri yanatarajiwa kukua ili kutimiza lengo hilo. Ili lengo hilo litimie, Kamati inashauri Serikali kutekeleza yafuatayo. **Kwanza**, kurahisisha uendeshaji wa biashara na utozaji wa kodi ili kuvutia sekta isiyo rasmi kuwa rasmi. **Pili**, kuwekeza zaidi kwenye Mashirika ya Umma ambayo yanaweza kuleta faida ndani ya muda mfupi, mfano Shirika la TTCL. **Tatu** ni kuhakikisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inafanya kazi kwa weledi na ufanisi ili kuendeleza biashara na si kuua au kuziua ukuaji wa biashara kwa kutoza kodi kandamizi na kupanua wigo wa ukusanyaji. Endapo haya hayatafanyika itakuwa ni vigumu kufikia lengo hilo.

#### 3.14.2. Sekta Binafsi

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Mpango wa Pili Sekta Binafsi ilitarajiwa kuchangia jumla ya **Shilingi bilioni 48**.

Hadi kufikia mwaka 2020, Sekta Binafsi ilikuwa imechangia takribani **shilingi bilioni 32.6**. Hatua hii inaonyesha kwamba endapo Sekta Binafsi ikishirikishwa kikamilifu ina uwezo mkubwa wa kuchangia kikamilifu katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu. Changamoto kubwa inayoikabili Sekta Binafsi ni kutoaminiana na Serikali kwa sababu kumekuwa na maamuzi ambayo hayatabiliki juu ya uwekezaji wao na hivyo kusababisha uwekezaji mdogo. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha uwezo wa kusimamia mikataba ili sekta binafsi iweze kutabiri maamuzi ya Serikali na kuwekeza kikamilifu.

### 3.14.3. Utekelezaji wa Miradi kwa Njia ya Ubia (PPP)

**Mheshimiwa Spika,** ni zaidi ya miaka 10 sasa tangu tuwe na Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Pamoja na kufanya mabadiliko mbalimbali katika Sheria hiyo bado hatujaweza kuvutia na kutekeleza miradi kwa njia hii**.** Utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia ni njia mojawapo ya kupunguza ugharamiaji wa miradi kwa Bajeti ya Serikali. Changamoto iliyopo ni utayari wa Serikali na watendaji wake katika kutumia na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ubia. Watendaji wengi wana mtazamo wa kutekeleza kwa kutumia Bajeti ya Serikali na hivyo kutokuwekeza nguvu kwenye kuandika maandiko ya miradi ambayo inaweza kutekelezwa kwa njia ya ubia. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mtazamo huu usio na tija unabadilishwa kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa miradi kwa ubia.

## 3.15. Tathmini na Ufuatiliaji

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto kubwa ambayo Kamati imebaini, pamoja na uwepo wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini katika Mpango wa Pili na sasa huu wa Tatu, ni kukosekana kwa Sera na Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji wa Mpango. Mfano unaonekana katika utekelezaji wa Mpango wa Pili, ambapo Serikali ilitakiwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango kila mwaka, baada ya miaka miwili na miaka minne ili itumike kupanga Mpango wa Tatu. Kamati inaishauri Serikali kuleta Sera na Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji ili kubainisha majukumu ya kila mdau katika kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango. Aidha,

lisipofanyika hili tutarajie kuona utakelezaji hafifu wa Mpango huu wa Tatu tutakaoupitisha.

## 4.0. KUKUZA USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI KWENYE MAENDELEO YA KIUCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Tatu umetambua sekta binafsi kama nguzo muhimu katika kufikia azma ya kujenga uchumi shindani na wa viwanda kwa maendeleo ya watu. Mpango umetoa uzito wa kipekee kwa sekta binafsi ambapo Serikali imefanya uchambuzi wa kina wa changamoto na vikwanzo vinavyoikabili sekta binafsi pamoja na kuweka mikakati ya kuboresha sekta hii na kuoanisha ushiriki wake katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu.

**Mheshimiwa Spika,** ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itaenda kutatua na kuzifanyia kazi changamoto hizo kama Mpango wa Tatu ulivyoziainisha. Kushindwa kutekeleza hili, itakuwa ni kufeli kwa utekelezaji wa Mpango wa Tatu na hivyo kutofikiwa kwa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Aidha, muda sasa ufike wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kufanya kazi iliyoianzisha katika ngazi zote ili kuweza kushughulikia masuala ya sekta binafsi. Vilevile, asasi mwamvuli zinashauriwa kusimamia vema taasisi inazoziwakilisha na kuwa na msimamo mmoja na kuwa na ushirikiano.

## 5.0. MAONI YA UJUMLA

### 5.1. Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 35 cha Sheria ya Bajeti kinataka Serikali kuanzisha Mfuko wa Dharura yaani *"contingency fund".* Pamoja na uwepo wa takwa hilo kisheria, bado Serikali haijaanzisha Mfuko huo na badala yake imekuwa ikitenga fedha za dharura kupitia **Fungu 21 - Hazina**. Uwepo wa Mfuko huu utasaidia Serikali katika kutekeleza Mpango wake wa mwaka mmoja na mitano kwa sababu pindi yatakapokuwa yanatokea majanga au matukio ambayo hayakukusudiwa Mfuko huu utatumika kikamilifu tofauti na ilivyo hivi sasa.

### 5.2. Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya jitihada kubwa sana kuboresha huduma za Afya nchini jambo ambalo ni la kupongeza sana. Hata hivyo, changamoto kubwa iliyoko mbele yetu ni namna gani wananchi wanapata huduma hizo kwa bei nafuu, kwa ubora na kwa haraka. Suluhisho la jambo hili ni kuwa na Sheria ya Bima kwa wote *"Universal Coverage Health Insurance"*. Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuleta Muswada wa Sheria hiyo mbele ya Bunge lako tukufu ili iendane sambamba na utekelezaji wa Mpango huu wa Tatu kwa sababu hivi sasa ni **asilimia 20** tu ya watanzania wako kwenye Mifuko ya Bima.

### 5.3. Kilimo cha Zabibu na Mbaazi

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iongeze katika Mapendekezo ya Mpango wa Tatu, Mradi wa kuboresha zao la Zabibu na mnyororo wa thamani (*Value Chain*) yake. Aidha, kilimo cha mbaazi nacho kihamasishwe hasa ukizingatia uwepo wa uhitaji wa zao hili katika soko la dunia.

### 5.4. Zao la Korosho

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutambua faida kubwa inayoweza kupatikana na mazao yatokanayo na Korosho (Cashew nuts products and by products), ni vema Serikali ikaweka katika Mpango wake wa Tatu wa Miaka Mitano unaokuja mikakati ya moja kwa moja itakayowezesha zao la korosho kuongezewa thamani na kutumia mazao yake katika kutengeneza bidhaa nyingine ili kuwaongezea kipato wakulima na Taifa kwa ujumla.

### 5.5. Kuhamasisha Matumizi ya Bidhaa za Ndani

**Mheshimiwa Spika,** Serikali itoe Waraka utakaozitaka Ofisi na Taasisi za Umma kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini kabla ya kutumia bidhaa za nje. Kwa mfano Taasisi zetu za Polisi, Jeshi la Wananchi, Idara ya Uhamiaji, Magereza kutumia bidhaa za ngozi (viatu, mikanda, mabegi n.k) vinazozalishwa

katika kiwanda cha ngozi cha Karanga, kinachomilikiwa na Magereza.

**5.6. Ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kutambua dhamira nzuri ya Serikali ya kuhakikisha tunapata manufaa makubwa kwenye uwekezaji katika Bandari zetu, Bandari ya Bagamoyo kwa muktadha huu, ni vema Serikali ikaongeza kasi ya mazungumzo na wawekezaji ili Bandari hii ianze kujengwa kwani manufaa yake ni makubwa kwa uchumi wa Taifa letu.

**5.7. Ujenzi wa Bandari Kavu**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ione uwezekano wa kujenga Bandari kavu katika Mikoa ya Mbeya, Kigoma, Mwanza na Shinyanga (Isaka) ili mizigo ya nchi jirani (On Transit Cargo) itakayosafirisha na Reli zetu ipokelewe na kupakiwa huko badala ya kuwalazimu kuja Dar es salaam.

**6.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kumshukuru Mhe. Tulia Ackson, Mb, Naibu Spika kwa miongozo ambayo kwa pamoja mmekuwa mkitupatia. Vilevile napenda kumshukuru Ndg. Stephen Kagaigai na timu yake kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, kipekee napenda kumshukuru, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb, Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu Fedha na Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara na wataalamu wote ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mpango huu.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa naomba kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Mathew Kileo, Makatibu wa Kamati Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala, Maombi Kakozi na Wilfred Akasi pamoja na Msaidizi wa

Kamati Editruda Kilapilo kwa miongozo yao na ushauri wa kiutalaam hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |
| 7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb | Mjumbe |
| 8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb | Mjumbe |
| 9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb | Mjumbe |
| 10. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb | Mjumbe |
| 11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb | Mjumbe |
| 12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb | Mjumbe |
| 13. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb | Mjumbe |
| 14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb | Mjumbe |
| 15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb | Mjumbe |
| 16. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb | Mjumbe |
| 17. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb | Mjumbe |
| 18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb | Mjumbe |
| 19. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb | Mjumbe |
| 20. Mhe. Halima James Mdee, Mb | Mjumbe |
| 21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb | Mjumbe |
| 22. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja**.**

Sillo Daniel Baran, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**
08 Aprili, 2021

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na niwapongeze sana Wajumbe wote wa Kamati hya Bajeti na Kamati ya Uongozi, wamefanya kazi *overtime* hata wakati wa likizo ya Pasaka wao wamefanya kazi kwa saa nyingi sana. Nawapongezeni sana na tunawashukuru sana. Wangelegeza leo tusingeweza kuwa na ripoti hapa, lakini kwa kweli wametufanyia kazi nzuri sana, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Taarifa karibu zote ambazo zilitolewa leo asubuhi tayari ziko kwenye *iPad zetu.* Taarifa zote zile za *CAG* na nyingine zote zilizowekwa Mezani leo asubuhi naziona hapa, lakini pia hotuba hii iliyomaliza kusomwa, Mpango wa Maendeleo wa Taifa pia umo humu. Kama bado, bado vitu viwili vitatu vidogo tu na wanaendelea kufanyia kazi Waheshimiwa. Kama mtagundua bado kuna kitu hakimo niandikie tu ili tuweze kuhakikisha kwamba kila kitu unacho kwenye *iPad* yako.

Kama nilivyosema, tunashukuru sana maoni ya Kamati ya Bajeti, naamini yatasaidia sana katika kuboresha Mpango wetu huu wa Miaka Mitano. Mpango wa Miaka Mitano ni mahali pa kujitathmini kwamba tulikuwa tunafanya utekelezaji wa mipango, sasa tunaenda katika *focus* mpya ya miaka mitano. Kwa hiyo, ni vizuri sana Waheshimiwa Wabunge tukajaribu kuangalia ni maeneo gani tunahitaji kuyapa kipaumbele, kuyatilia mkazo katika miaka mitano ijayo ambayo tunaamini kabisa yataimarisha uchumi wetu na watu wetu kwa kiwango kikubwa zaidi.

Tusiogope katika kuchangia, mawazo yako ni mawazo yako, wewe toa mawazo yako. Huu ni uwanja wa kupokea mawazo na kwa pamoja tutaangalia na wenzetu Serikalini wataangalia yanaweza kuwa mawazo yanayoweza kusaidia sana Serikali na nchi yetu.

Kwa hiyo, nawatia moyo sana kuchangia; tuna siku tatu tu, usije ukataka kuchangia Jumatatu ijayo nafasi itakuwa dakika tano au dakika tatu, lakini leo hapa una dakika kumi za kuchangia na kesho pia dakika kumi, kwa hiyo, tutapokea mawazo. Tusisubiri wenzetu Serikali wakikosea

ndiyo tuwe mafundi wa kulaumu, lakini wakati wa Mpango ni wakati wa kujenga, wakati wa kuweka fikra zetu sawasawa mbele iwe ndiyo kiongozi chetu. Mpango ndiyo kiongozi chetu kwa miaka mitano inayokuja.

Baada ya maelezo hayo, kwa kweli sasa tunaingia kwenye uchangiaji wenyewe na tunawaomba sana Wizara ya Fedha na Mipango muyasikilize, muyatilie maanani. Kwa mfano Ripoti ya *CAG* inaonesha kwa mwaka 2019/2020 peke yake tumepata hasara *ATCL* ya *60 billion.* Je, tukiendelea kuagiza ndege mpya itasaidia? Au tu-*stop* kidogo kwa sasa tushughulike na hizi zilizoko na kadhalika, mawazo kama hayo ni muhimu sana kipindi kama hiki.

Kwa upande wa reli yetu, je, ni lazima mabehewa Serikali inunue? Tumeshajenga miundombinu ya reli, hivi lazima mabehewa yote ya abiria yawe nayo ni ya Shirika la Reli la Taifa? Ni lazima mabehewa yote ya mizigo Serikali ndiyo inunue?

Niliwahi kuwa Russia ambako kile kipisi cha treni, labda kina behewa kumi, kumi na tano, ni watu binafsi wamewekeza kama vile ambavyo Serikali imejenga barabara, lakini mabasi yanayopita ni ya watu binafsi si lazima mabasi yawe ya Serikali. Reli ni kama barabara ni lazima kila behewa pale liwe la Serikali? Wananchi wanaweza kuunda kampuni mbalimbali wakawekeza. Watu hawana namna ya kuwekeza kwa uhakika mpaka Wabunge tunanunua pikipiki, bodaboda, eeeh, kwa pamoja mnanunua vibehewa viwili, vitatu na Watanzania wengine, hizo ndizo biashara za kufanya. Kama kila kitu Serikali inafanya sasa watu wengine wafanye nini sasa, eeh? *(Makofi)*

Serikali ikishaweka muundombinu ule mkubwa lazima kuangalia na watu binafsi kwenye *SGR,* ndiyo *PPP* yenyewe hiyo sasa nao kwenye sekta zipi wanaweza wakashiriki. Badala yake tutategemea makampuni yatoke nje yaje yaweke mabehewa, hiyo itakuwa ni *okay* wakati hii mali ni yetu wenyewe. Mawazo tu, tunachozungumzia ni mawazo lipi linawezekana, lipi haliwezekani na kadhalika. *(Makofi)*

Basi, atakayetuanzishia mjadala wetu ni Mheshimiwa Josephat Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza na wengine wajiandae. Yeyote aliyeleta jina basi asitoke nje; Mheshimiwa Kandege, tafadhali.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa kuwa mchangiaji wa kwanza kwa siku ya leo. Nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na sisi sote Wabunge ambao tumepata fursa ya kuwepo leo mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Bajeti. Kwa hiyo, nimepata fursa ya kutosha katika kuchangia mawazo ambayo yameboresha Mpango. Hata hivyo, naomba niendelee kujazia katika baadhi ya maeneo ambayo naamini Serikali itakuwa tayari kuendelea kuya-*accommodate* ili Mpango wetu uwe ni ambao utaleta tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nina kila sababu ya kuipongeza Serikali yetu, imefanya kazi kubwa na nzuri sana katika suala zima la miundombinu. Hata hivyo, tunapofanya kazi nzuri tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba kasi ileile tuliyokuwanayo ya kujenga miundombinu inaendelea na inaendelezwa kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nina kila sababu ya kuipongeza Serikali yetu imefanya kazi kubwa nzuri sana katika suala zima la Miundombinu; lakini tunapofanya kazi nzuri kuna wajibu wa kuhakikisha kwamba kasi ile ile tuliyokuwa nayo ya kujenga miundombinu inaendelea na inaendelezwa kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, tumeweza kuunganisha karibu mikao yote Tanzania, imebaki Mikoa michache, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba kasi ya kuunganisha miundombinu kwa maana ya barabara inaenea katika Mikoa yote, maeneo ambayo yamebaki na twende kuunganisha Wilaya zote.

Mheshimiwa Spika, iko haja ya kwenda kutazama barabara za kimkakati na hasa zile barabara ambazo zinaunganisha nchi yetu na nchi Jirani. Kwa mfano barabara iliyoko katika Jimbo langu la Kalambo kutoka Matai kwenda Katesha Boda ni miongoni mwa Barabara muhimu sana, ni vizuri Serikali ikatilia maanani ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ambayo inaunganisha nchi yetu na nchi ya *Mozambique* iko Ruvuma kule maarufu kwa jina la Likuyufusi Mkenda, ni vizuri kabisa Serikali ikahakikisha katika mpango barabara hii ikawekwa ili fursa ya kiuchumi kama nchi tuweze kuipata kwa majirani zetu wa *Mozambique*.

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi kwenye suala la barabara kazi nzuri ambayo inafanywa na Serikali katika ujenzi wa Reli yetu, tena ya *Standard Gage,* ni kazi ya kutiliwa mfano ya kupigiwa mfano, ni kazi ambayo imeanzwa, si vizuri tukaishia katika maeneo hayo; ni vizuri sasa tukaanza kufikiria *networking* kwa Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tunayo Reli ya kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka Zambia Kapiri Mposhi, lakini reli ile imejengwa kwa kiwango cha *Standard Gauge.*

Mheshimiwa Spika, tutumie fursa ya ujenzi ambao tumeianza kwenda mpaka Mwanza na Kigoma. Tutumie fursa ya Reli ya *TAZARA.* Kwanza tuondoe makandokando yaliyopo katika uendeshaji, kwa maana ya *Management,* lakini ni vizuri pia tukaendelea kuongea na wenzetu wa Zambia. Sisi tuna eneo kubwa, na hili eneo ambalo tunalo sasa tuanze kutazama uwezekano wa kuanzisha vipande vingine kutoka Tunduma pale kwenda mpaka Kasanga *Port* ili tuweze kutumia fursa ya kuunganisha na *DRC* kwa ajili ya mizigo yetu; wanahitaji sana mizigo kutoka kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Lakini kama hiyo haitoshi, hata ukitazama kuna hii habari ya Mtwara *Corridor* suala limeongelewa muda mrefu sana. Ifike mahali katika mpango wetu tujue kwamba tunataka *network* kwa nchi yetu ili kusiwe

na sehemu hata moja katika nchi hii ambayo inakuwa *disadvantage.* Ni vizuri na ni wakati muafaka kwa Serikali kuhakikisha kwamba eneo hilo nalo reli inajengwa ili tuweze kutumia fursa ya kuunganisha na *Lake* Nyasa pale.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna mradi wetu ambao umeongelewa muda mrefu kuhusu Liganga na Mchuchuma tukiwa na uhakika wa usafiri wa uhakika kwenda kufika kule hakika nchi yetu tutakuwa tumefungua kila eneo, ni vizuri Mheshimiwa Waziri ukatilia maanani masuala haya ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusiana na suala zima la Afya. Naipongeza Serikali imefanya kazi nzuri sana katika kujenga vituo vya afya vingi vya kutosha. Sasa tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba sasa wataalamu na vifaa vinakuwepo vya kutosha ili hicho ambacho kimekusudiwa kiweze kutoa matunda kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na wewe ni shuhuda, umekuwa ukilisema mara nyingi kwamba tusipokuwa na Bima kwa watanzania hawa hakika juu ya Mwananchi kupata matibabu kuanzia Januari mpaka Disemba itakuwa kwenye mashaka.

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa wa kuja na mpango na ukamilike haraka juu ya *universal health coverage* kwa watanzania hawa, ndio namna ambayo itatuhakikishia afya kwa watu wetu bila kujali kwamba mtu ana kipato au hana. Kwa sababu katika hali ya kawaida ugonjwa hauna muda, kwamba mtu atajiandaa na kuwa fedha ambayo ameitenga kwamba nikiugua nitakwenda kuitumia hii. *Window* pekee ambayo itatusaidia ni *universal health coverage* kwa Watanzania, tuanze sasa. Mheshimiwa Waziri wa Afya unasikia, ndicho kipimo chako katika kuhakikisha kwamba Watanzania wote watakukumbuka kwa kazi nzuri ambayo utakuwa umewafanyia kwa kuwaanzishia mfuko na ukamilike.

Mheshimiwa Spika, alianza Waziri aliyetangulia na eneo alilofika sasa ni wajibu wako kuhakikisha kwa maana wewe unaenda kumalizia kipande ambacho kilianzishwa na mwenzako.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichangie kuhusiana na suala zima upande wa Kilimo. Safari hii tumepata *wake-up call,* kwamba uhitaji wa mafuta ya kula ni jambo ambalo halibishaniwi, kila mtu atahitaji mafuta ya kula kinachotofautia ni kiasi gani na wingi ndicho mtu atatumia lakini hakuna mtu ambaye atasema hata tumia mafuta ya kula. Na sisi kama Taifa tumekuwa tukitumia fedha nyingi sana za kigeni kuagiza mafuta kutoka nje ambayo wakati mwingine hatuna hata uhakika na juu ya ubora wake.

Mheshimiwa Spika, nilishawahi kulisema hata siku moja hapa; kama kuna mambo ambayo enzi zile yalifanywa vizuri na *the so called SIDO* ilikuwa ni pamoja na uanzishwaji wa viwanda kwa ajili ya kukamua mafuta ya alizeti na mafuta ya karanga. Hivyo viwanda na mawazo hayo ni wakati muafaka kwa kutoa hamasa kwa watu wetu kuhakikisha kwamba mbegu zilizo bora ambazo zitakuwa zinatoa mafuta ya kutosha (*extraction rate)* iliyo nzuri ebu tuhimize kila kaya; kama ambavyo ilitokea kipindi Fulani. Kwamba ilikuwa kila familia ijitosheleze katika chakula. Sasa ifike pahali ambapo hamasa itolewe kila familia walau kila mwananchi akawa na hata nusu heka akalima alizeti, ama karanga, kulingana na hali ya mahali Fulani. Ifike pahali ambapo tujitosheleze kwa mafuta ambayo tunazalisha sisi wenyewe. Kwanza tuna uhakika na ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilishawahi kusema siku nyingine hapa, hivi ile *super G* ambayo tulikuwa tunaiona imeenda wapi? Nini ambacho kilitokea *Tanbond* imeenda wapi? Nini ambacho kimetokea? Yale mafuta ambayo tunayapata kutokana na mbegu za pamba yameenda wapi? Nini kimetokea? Kama Taifa tuna kila sababu ya kujifanyia tathmini sehemu ambazo tumekosea turudi katika mstari ili wananchi wetu wawe na uhakika wa mafuta yaliyo bora, lakini pia ni chanzo kizuri cha mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe, kwa ujumla wake kazi ambayo imefanyika ni nzuri. Ni wajibu wetu sisi Watanzania tukahakikisha kwamba tunakuwa na *spirit* ya kupenda kufanya kazi; na ubunifu tukiupata kwa mtu tuulee, si kwamba inakuwa kama vile anafanya mtu kwa ajili ya manufaa ya Taifa lakini hatumuungi mkono kwasababu kama vile hatunufaiki wote.

Mheshimiwa spika, nakushukuru na Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana sana sana Mheshimiwa Josephat Kandege, hakika umetuanzishia vizuri tunakupongeza sana. Nilikwisha mtaja Mheshimiwa Oran Manase Njeza na atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi ya kuchangia Mpango wetu wa Tatu wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali. Kama ulivyosema mwenyewe, huu mpango unatupa fursa ya tathmini lakini vile vile inakuangalia tunaenda vipi mbele ya safari yetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tathmini ya tulikotoka tumefanya vizuri kiuchumi, kutoka uchumi wa chini kwenda uchumi wa chini kati nafikiri ni hatua nzuri sana. Lakini ukiangalia vile vile kwenye miundombinu tumefanya vizuri na maeneo mengi tumefanya vizuri sana. Kwa hiyo napenda sana kumshukuru na kumpongeza Mheshimwa Rais, Serikali yake nzima, Mheshimiwa Waziri wa Mipango kwa kutuletea hii taarifa nzuri sana ambayo kwakweli ukiangalia inatupa matumaini makubwa sisi kama Taifa, na ukiangalia dhima nzima ya huu mpango ni kujenga uchumi shindani, lakini vile vile inaenda pamoja na viwanda na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, kwakweli uzito wa hiyo dhima ni mkubwa mno. Lakini nilikuwa najaribu kuangalia, sisi kama Taifa pamoja na hii dhima, je, tunasimama wapi?

Mheshimiwa Spika, hii dhima nguzo kubwa ziko kwenye uimara wa uchumi; uchumi wetu je, ni imara au si imara? Kama tathmini tuliyoifanya tumetoka uchumi wa chini sasa hivi tupo kwenye uchumi wa kati ina maana uchumi wetu ni imara. Vile vile nguzo yake ingine ni miundombinu, je, tuna misingi mizuri ya miundombinu? Ndiyo, tumeanza vizuri tumejijenga vizuri katika miundombinu na tunakwenda vizuri, nakadharika, nakadhalika.

Mheshimiwa Spika, ukianza na hii hatua ya kwanza tu ya uchumi. Nina imani ya kwamba kuna maboresho machache sana ambayo tunaweza kuyafanya katika nchi yetu. Tunategemea sana kilimo, kilimo ndiyo nguzo ndicho kinachoajiri asilimia kubwa ya Watanzania. Watu wengi tunafikiri masoko hayapo, masoko yapo, na masoko ya Tanzania ya mazao yetu naweza kusema kwa kiasi fulani ni ya upendeleo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia zao la kahawa, hasa *arabica,* kwenye Soko la Dunia la *New York* bei yetu ya kahawa inaongezewa senti thelathini mpaka hamsini kutegemea na bei shindani ya *New York* hiyo ina maana kuwa wakulima wetu wangepata bei nzuri sana ya Kahawa kutokana na upendeleo tulionao kwenye Soko la Dunia.hata hivyo hali siyo hivyo, kuna matatizo tuliyonayo ambayo usimamizi wa masoko haya ambayo yapo inaelekea kuna mahali hatufanyi vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia huu mpango wa tatu tungeangalia hizi fursa zilizopo, tufanye namna gani haya masoko yaliyopo yaende vizuri. Kama tumeongezewa bei ya *arabic*a kwa senti thelathini mpaka arobaini kwa kila *lb, lb* 2.2 ndio sawa na kilo moja, kama tumeongezewa hizo kwanini hatufanyi vizuri?

Mheshmiwa Spika, kwenye mahindi Mwenyezi Mungu ametupa ardhi nzuri, lakini nayo uzalishaji wetu si wa ushindani kwasababu uzalishaji wa Tanzania kwa mahindi ukilinganisha na majirani zetu kwakweli hatufanyi vizuri.

Mheshimiwa Spika, soko la nje la majirani zetu, ukiangalia nchi zinazotuzunguka, hasa Zambia wanaweza kuuza kwa faida mahindi yao kwa kilo kwa shilingi 300, lakini kwa sisi tunaozalisha Tanzania ukiuza kwa shilingi 500 kwa kilo ni hasara; ni kwanini? Kwasababu bei ya mbolea kwa hapa kwetu si Rafiki, na hiyo inasababisha kwa kiasi kikubwa na utendaji ambao sio mzuri katika miundombinu.

Mheshimiwa Spika, usafirishaji unachukua kiasi kikubwa sana cha bei ya pembejeo. Kwa hiyo tukiweze kuboresha miundombinu, tukaboresha vile vile na wenzetu wa Barandari ambao walikuwa wanaendelea na maboresho nafikiri kwa kiasi kwa kiasi kikubwa tunaweza kuwa na ushindani. Huwezi wenzetu wa Zambia wakauza Mahindi yao kwa faida kwa shilingi 300 na sisi tukauza bila faida kwa shilingi 500, hiyo haileti ile dhama nzima ya Uchumi wa ushindani. Ina maana sisi hatutakuwa washindani kwa hiyo hata ukitafuta soko, soko ambalo utauza kwa bei ambayo ni ya hasara hilo soko litakuwa baya. Kwa hiyo tuanze kwanza na kuboresha kilimo cha tija.(Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Miundombinu, mwenzangu amezungumzia kuhusu *TAZARA.* sasa ni kwanini ukiangalia *TAZARA* kwenye mpango haizungumziwi kama mradi ambao ni *quick win?* Reli ya *TARAZA* ipo pale na ni *Standard Gauge* lakini bidhaa nyingi zinazokwenda nje ya nchi asilimia zaidi ya 70 zinatumia barabara yetu ya *TANZAM* na hawatumii *TAZARA.* Mimi mwenyewe nimejaribu kuulizia usafirishaji kwa kupitia *TAZARA* ni takriban mara mbili ya usafirishaji kwa gari. Sasa unashangaa, tungetegemea reli iwe rahisi kuliko barabara; hasa ni kwa nini usafirishaji kwa reli hapa kwetu umekuwa ni tatizo na bei ya juu? Ina maana hapa tunatatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba, ninaomba sana tuangalie tunapoboresha *SGR* tuangalie ni namna gani tunaweze kuiunganisha *SGR* na mtandao wa Reli za kwetu za Afrika Mashariki pamoja na nchi za *SADC,* ikowemo kuunganisha *TAZARA* pamoja na *SGR.* Kama alivyosema mtangulizi wangu, kuna kumuhimu wa kuunganisha Reli ya

*TAZARA* na *Port* ya Kasanga kutokea Tunduma, lakini vile vile kuanzia Mbeya kwenda Ziwa Nyasa, ili uwe na muunganiko mzuri sasa na wa Reli ya Mtwara mpaka Mbamba *Bay,* na hapo sasa kutakuwa na mzunguko mzuri wa reli yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uzalishaji wa viwanda na fursa za pesa za kigeni. Tuna Madini mengi hapa nchini wawekezaji wapo, lakini ukiritimba tulionao wakati mwingine unasababisha wawekezaji wanakosa imani na kuwekeza hapa kwetu. Nimezungumzia mara nyingi kuhusu madini ya *Niobium.* Madini ya *niobium* ni madini ambayo ni adimu. Kiwanda ambacho kinategemewa kuwekeze hapa nchini kwetu kitakuwa ni cha nne duniani, na hiki kiwanda kitatumia rasilimali zetu na madini yaliyoko Tanzania na kitatuletea mapato kwa kila mwaka zaidi ya Dola 200 na Serikali itapata Dola zaidi ya milioni 20 kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Ukiangalia *direct investment* ni zaidi ya Dola milioni 200 vile vile. Sasa, ni ka nini tusichukue fursa kama hizo kama hao watu wapo tayari nao kwenda pamoja na sheria tulizonazo nchini kwetu?

Mheshimiwa Spika, nafikiri tukiweza kuyaboresha haya na yakawepo kwenye mpango wetu, tukawa na mazingira ambayo ni rafiki tukapunguza gharama, hayo tutakwenda vizuri sana. Lakini kwenye miundombinu, hata ukiangalia *TARURA* sasa hivi barabara ziko hoi. Kwenye Wilaya ya Mbeya Jimbo la Mbeya Vijijini barabara zetu takriban kilometa 1000 zote zina hali mbaya. Lakini unaangalia, wakati mwingine ni utendaji wa watendaji wetu. Kwenye Bajeti ya mwaka huu tu bado miezi miwili ametumia asilimia 20, wananchi hawaweze kusafirisha mazao yao.

Mheshimiwa Spika, sasa tusipoboresha hata kilichopo nina imani kuwa hatuweze kufanya vizuri. Hivyo ninaiomba Serikali kupitia *TARURA* iboreshe Miundombinu ya barabara zetu, lakini barabara zetu ambazo zina fursa za kwenda mipakani kama kutuunganisha sisi na Zambia, sisi na Malawi nazo zipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningeomba Barabara kama hii ya Mbalizi kwenda Shigamba ambayo inakwenda mpaka Isongole karibu na mpaka na Malawi iwe kwenye kipaumbele cha mpango wetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana niendelee tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri, na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Oran Manase Njeza, nilishakutaja Mheshimiwa Nusrat na utafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwanza kwasababu ni mara yangu ya kwanza tangu tumepata janga kubwa la Taifa kuzungumza hapa nitoe pole kwa Watanzania wote kwa msiba mkubwa tulioupata wa kuondokewa na Mheshimiwa Rais, lakini pia nitoe pole kwa Mheshimiwa Rais mteule Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuondokewa na Mheshimiwa Rais ambaye yeye alikuwa msaidizi wake wa kwanza na wa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Rais mteule Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mwanamke wa kwanza Afrika Mashariki kwa kuwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Philip Mpango kwa kuteuliwa kwa mujibu wa Katiba kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania, lakini pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kuwa pamoja na nchi yetu kutokana na kipindi ambacho tumepitia cha mpito na mambo magumu ambayo tumepitia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie na nitachangia kwenye Sekta za uzalishaji na nitajikita katika sekta ya kilimo, kwasababu Kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu na tunajua tumekuwa tukitumia kauli hiyo tangu tunasoma; lakini pia *practicability* yaani utekelezaji wa maendeleo ya Taifa tunategemea sana kilimo

kwasababu kama tunazungumza Tanzania ya Viwanda na kama mwelekeo wa Serikali maana yake hatuwezi kuzungumza viwanda bila kilimo.

Mheshimiwa Spika, na kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamekuwa wana *champion* hoja ya kilimo, kwabababu utakumbuka hata mzungumzaji aliyepita amezungumza pia kilimo, na ninajua Waheshimiwa Wabunge wengi sisi kama nchi wengi tunajua tunalima kwa namna tofauti tofauti, lakini pia tunajua umuhimu; wake, kama ambavyo Mwenyekiti wa Kamati ametoka kuzungumza. Kwamba tunahitaji malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu kwasababu tunategemea malighafi za ndani sasa hauwezi kuzungumza malighafi za ndani bila kuzungumza kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa pekee sana kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* na mambo ambayo amechambua kwenye ripoti yake, ukiangalia mpango wa kwanza na wa pili kwasababu tunazungumza Mpango wa Tatu lakini wakati tuko sasa hivi lazima tukumbuke tulikotoka kwa hiyo, kwenye suala zima la kilimo kuna mambo kadhaa ambayo *CAG* katika ukaguzi wake ameyaona.

Mheshimiwa Spika, mathalani nitayazungumzia hayo huwezi kuzungumza kilimo bila kuzungumza mbegu, sasa kama Taifa tulikubaliana kwamba tutakuwa na mashamba tisa ya kuzalisha mbegu lakini ukweli ni kwamba kwa mujibu wa ripoti ya CAG mpaka sasa ni shamba moja tu ambalo linafanyakazi mwaka mzima lakini mashamba mengine nane yanategemea msimu wa mvua kwa hiyo yako kwa mujibu wa msimu. Sasa hatuwezi tukazungumza kwamba tunataka tufanye kilimo kiwe sekta ambayo ni *stable* wakati hatuzungumzi tunapataje mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji mashamba yote tisa ambayo yametengwa kwaajili ya kuzalisha mbegu nchini yafanye kazi yote mwaka mzima bila kusubiri msimu wa mvua kwasababu ripoti ya CAG inasema tunategemea shamba moja ambalo linafanyakazi mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye nchi ambayo asilimia kubwa tuna *water bodies* tuna maji kwa asilimia kubwa sana kwenye nchi yetu ardhi ya Tanzania hatuwezi tukawa tunategemea mvua watu wanatushangaa kwasababu kuna vitu tu haviko sawa kwenye *scheme* za umwagiliaji kwasababu ili uweze kufanya uzalishaji kwa kutumia umwagiliaji lazima utengeneze *scheme* za umwagiliaji zifanye kazi ili uweze kufanya kilimo *especially* cha kuzalisha mbegu kwasababu mashamba tisa kama nchi ni mashamba machache sana ambayo tunaweza tukatengeneza utaratibu mzuri na tukayahudumia mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kama nchi ripoti ya *CAG* inatuambia ni 39% tu ya pembejeo za kilimo zimegawiwa yaani ugavi kwenye pembejeo za kilimo ni 39% tu. Sasa unategemea Taifa lizalishe malighafi kwaajili ya viwanda vyake kwa Tanzania ya viwanda halafu unafanya ugavi wa pembejeo za kilimo kwa 39% tu. Kuna jambo Wizara na Waheshimiwa Wabunge kuna jambo lazima tukubaliane kwamba kama tumeamua kwamba tunatengeneza Tanzania ya viwanda ni lazima tukubaliane suala zima la kilimo ndiyo msingi na ni lazima wote ikiwezekana tuzungumze kuhusu kilimo. Kwasababu ndiyo tutapata malighafi kwaajili ya viwanda vyetu lakini ndiyo sehemu ambayo itatusaidia sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwasababu sasa hivi mwenyekiti wa kamati amezungumza kwamba sasa hivi tunalima kilimo cha kujikimu yaani watu wanalima sana ni kwaajili ya kuendeleza maisha kwamba wapate chakula waishi lakini kwa ardhi ukubwa wa ardhi ambao tunao kwenye Taifa letu lakini *water bodies* ambazo tunazo kwenye Taifa letu, *resourcefully* ya wasomi na watu ambao wana *profession* za mambo ya *agriculture* Taifa letu limebarikiwa sana tunatakiwa tutoke huku tuende sehemu nyingine zaidi kwenye kuboresha kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa ripoti ya *CAG* inatuambia ni 1% tu ya wakulima wamepatiwa mafunzo na mbinu bora za kilimo sasa asilimia moja tu wamepatiwa

mafunzo ya mbinu bora za kilimo. Kuna jambo hapa haliko sawa, na hii ni kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* na wapo maana yake watu wanaelewa nini tunachokizungumza. Bahati nzuri nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Naibu Waziri pale kwasababu mara nyingi ndiyo tumekuwa tunamuuliza hata yeye maswali na yeye anajibu na anafuatilia Mheshimiwa Hussein Bashe. Kwa hiyo, kwasababu lengo letu ni kujenga na hii nchi ni ya kwetu maana yake hakuna mtu atatoka huku aje kutuambia tunajengaje nchi yetu hapa ni sehemu ambayo ni lazima tuweke nguvu Mheshimiwa Waziri yupo na Mheshimiwa Naibu Waziri pia yupo na Mheshimiwa Naibu Waziri pia yupo tuangalie tunafanyaje kwenye suala zima la kilimo na kimsingi mimi ni wa Singida kwetu tunalima alizeti, na tunalima kweli kweli alizeti kwa hiyo, ni *declare interest* kwamba mimi pia ni mkulima Pamoja na kwamba tunalima kwa simu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye upande wa pili nitoe mapendekezo labda nini kifanyike kwaajili ya kuhakikisha kwamba pengine utekelezaji wetu wa mipango ukiangalia mpango wa kwanza na mpango wa pili ni lazima tukubali kwamba kuna sehemu inawezekana haiko sawa ndiyo maana unakuta tunapanga bajeti za sekta za uzalishaji halafu hazitekelezwi kama tunavyopanga kama Bunge linavyopanga.

Mheshimiwa Spika, labda nitoe mapendekezo yafuatayo, pendekezo langu la kwanza napendekeza kuwe kuna sheria maalum kwasababu ni miaka 10 imepita mpango wa kwanza na Mpango wa Pili tunajadili Mpango wa Tatu *phase* ya mwisho ya miaka mitano ili itimie 15 tunaianza. Kwa hiyo, na nikiangalia hata nikisoma *documentation* na nini na Waheshimiwa Wabunge ambao ni wazoefu nyinyi mtalizungumza hili vizuri hatuna sheria mpaka sasa hivi ya kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama tunakaa tunajadili na tumekuwa tunajadili kuhusu mpango sisi wengine tumekuja juzi siyo wenyeji sana lakini kama tunapanga vitu ambavyo hatuvitungii sheria ya utekelezaji maana yake baadaye

tunashindwa kujibana yaani tunashindwa kwamba tutabanana wapi kwasababu kama kutafanyika bajeti *reallocation* hakuna sheria ya kutu-*guide* kwamba sasa tumepanga mpango huu tunatumia sheria gani kusimamia utekelezaji wa mipango hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nishauri uletwe muswada wa sheria Bungeni tutunge sheria ya kusimamia utekelezaji wa mipango tunayoipanga kama Wabunge, kwasababu sisi ni watu wazima tuna akili zetu na kuna watu ni wasomi sana hapa na kuna watu wana mawazo mazuri sana lakini hatuna sheria ya kutu-*guide* kwamba sasa tunatekelezaje mipango tuliyojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili naweza kushauri ni kwamba sisi kama Wabunge sasa hivi tuko kwenye Bunge la Bajeti tunapanga bajeti na kuna bajeti ambazo tunajua kabisa kwamba Bunge hili ndiyo linatoa muelekeo wa Taifa kwenye masuala la bajeti. Lakini kama tunapanga bajeti za miradi ya maendeleo halafu hazitekelezwi katika kiwango ambacho Bunge limepanga maana yake ni kama vile kuna kukosekana nguvu kwa upande mmoja. Kwa hiyo, nishauri tunapokaa kama bunge tukapanga bajeti zinazokwenda kwenye miradi ya maendeleo tunaomba bajeti zitekelezwe kadri ambavyo Bunge hili limepanga kwasababu hiki ni chombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki ni chombo ambacho kinakaa na tunatumia fedha na tunatumia muda kupanga kwa hiyo hatuwezekani tukiwa tunapanga halafu bajeti hazitekelezwi kama ilivyo na kimsingi sheria ndiyo itatusaidia kwasababu hata bajeti *reallocation* haitakuwa sana kwasababu kama sheria itatulazimisha kwamba kusifanyike bajeti *reallocation especially* kwenye miradi mikubwa ya maendeleo ambayo tutajiwekea kufanya kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia jambo la mwisho naweza kushauri kuwe na uwajibikaji na kimsingi watu wanajitahidi katika kufanya wajibu wao lakini kwenye masuala la fedha kuwe kuna uwajibikaji endapo tunapanga tunapangiana

*program* za kufanya na *project* za kufanya basi watu kuwe kuna uwajibikaji mkubwa kwenye masuala ya fedha ili kuwe kuna *accountability* kuwe kuna *patriotism* ule uzalendo mtu anauona kwamba sasa mimi hili ni jukumu langu kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwasasa nimechangia hapo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat Hanje ni ni hotuba yako ya ngapi Bungeni? Mheshimiwa Nusrat ni hotuba yako ya ngapi Bungeni? Ya tatu *okey* ya pili nashukuru sana nimeuliza hivyo kwasababu makusudi kwamba sasa hivi Bunge letu lina Wabunge walio wengi Bungeni na Wabunge toka Kambi ya walio wachache.

Sasa *terminology* hii ndiyo rasmi duniani kuliko ile ya neno upinzani na kadhalika na mtaona faida ya hili ni kwamba hata kama mko wachache mnawaza namna gani ya Taifa letu liende mbele badala ya kuwaza kupinga ili kukwamisha ili mambo yasiende ili wewe uonekane wa maana, na lazima tutoke huko mnaona jinsi ambavyo hata uchangiaji mzuri kabisa Mheshimiwa Nusrat nakushukuru sana. *(Makofi)*

Kumbe na wewe unatoka Singida unalima alizeti hongera sana na sisi wakulima wa alizeti jamani sisi mbegu tu Wizara ya Kilimo mbegu ya alizeti, mbegu ya mahindi ukizunguka mashambani huko sasa hivi vi mahindi vimekauka yaani havifai mbegu na hiyo mbegu kidogo inayokuwepo ni *very expensive*, na mbegu nyingi *fake* utanunua utapanda mahekari haioti hata punje ni hasara kweli kwa wakulima. *(Makofi)*

Eneo la mbegu hili tukikaa nalo vizuri hatuwezi kuagiza mafuta ya kula kutoka nje hatuna sababu kwanza ni hatari sana kwa Taifa letu mnaagizaje mafuta kutoka kwa Jirani hayafai. Wanaotuuzia mafuta kina Singapore hawana hata eka moja ya kulima alizeti tunaagizaje mafuta kwao hawa.

Mheshiniwa Ali Hassan King na atafatiwa na Mheshimiwa Twaha Mpembenwe na Mheshimiwa Felister Njau ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia neema hii ya uhai siku ya leo tukapata fursa ya kuchangia katika katika Mpango wa Taifa letu ambao utakuwa ni chachu ya maendeleo na kuweka sawa hali za Maisha za wananchi.

Mheshimiwa Spika, nianze na dhana au dhima ya mpango huu ni kuwa na uchumi shindani lakini pia kuangalia na maendeleo ya watu na maana ya kuwa na uchumi shindani maana yake tunawashindani na kwa kuwa tunawashindani kwa maana hiyo tuna watu ambao pia tunawashindania kwamba hawa wawe wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa tukiangalia kwenye maana hiyo Taifa letu sasa kwa kuwa tuna ushindani na uchumi wetu uwe shindani siye tuwe juu tunapaswa kuwa na miundombinu mizuri na kuondosha vikwazo ili hao tunaoshindana nao sasa sisi tuibuke kuwa *champion*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika sekta ya usafirishaji tunajua tunaanza kuanzia bandarini tunashukuru tumejenga bandari zetu vizuri tumeimarisha lakini kama tunahisi tunavikwazo hivi vikwazo ndivyo vya kupambana navyo ili tuondoshe. Kwasababu katika eneo la bandari majirani zetu wa Kenya ndiyo tunashindana nao kwa bandari ya Mombasa, Msumbiji tunashindana nao kwa bandari yao ya Beirra lakini Durban pia tunashindana nao na hakuna bandari nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo kama mnataka kujenga uchumi shindani katika sekta ya usafirishaji ina maana kwamba sisi tuwe na bandari bora lakini pia tuwe na mambo mazuri ambayo yataondosha vikwazo watu waweze kuraghibika kupita katika bandari zetu wapiti kwenye mabarabara yetu wapite katika *railway* zetu wapite na maeneo mengine ili ule usafirishaji uende vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tutizame wateja wetu hawa tunaowasafirishia wako wapi na wapi na sasa hivi katika usafiri wa barabara ukiangalia tunaweka maeneo ambayo ya mizani. Pengine linaweza likasababisha pengine sisi ku-*slow down* watu wakatukimbia wakaenda katika maeneo mengine. Kwa hiyo, tufikirie tuwe na hikma ya kutizama katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ni kodi ambazo zinahusiana na usafirishaji tukiweza kuondosha kikwazo hicho kwa hiyo, tutaweza kujenga huo uchumi shindani lakini pia tutapata kuwagharamia watu wetu katika maendeleo yao hilo ni moja.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili niende katika sura inayozungumzia ugharamiaji wa mpango tumesema mpango wetu utagharamiwa kwa trilioni 114 tukaweka Serikali itachangia trilioni 74 na sekta binafsi tukasema itachangia trilioni 40.6. Sasa nije katika upande wa Serikali, Serikali tumesema kwamba tutakuwa tuna mapato ya ndani ambayo ni trilioni 62 katika kuchangia mapato ya ndani sasa mapato haya ya ndani yanachangiwa na mapato ya kodi sasa hapa kwenye mapato ya kodi ambayo yanachangia 65% mapato ya kodi tunaweza tukaja tuka tukaona kwamba kumbe tuna vikwazo kwenye mapato haya ya kodi.

Mheshimiwa Spika, vikwazo vyenyewe ni vipi zipo kesi kule *TRA* katika Bodi na katika Baraza ambazo zina fedha trilioni lakini kesi zile zimesimama hazijaendeshwa au nyingine zimekaa zimedunda ina maana pale pana mapato ya ndani ya kodi lakini tunayakosa, tukiboresha tukienda kwa wakati tukawa na ufanisi katika mashauri haya ya kodi ina maana kwamba tutaongeza mapato ya kodi na tunaweza kufika vizuri katika mpango wetu huu katika utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ripoti ya *CAG* ya mwaka 2018/2019 ambayo tuliijadili hapa Bungeni imeelezea kesi ambazo zimekwama kwasababu Bodi haitimizi *quorum* au hilo Baraza halitimizi *quorum* na halitimizi *quorum* kuna mtu ana mamlaka ya uteuzi? Hakuteua huyo mtu hao wajumbe hajawateua.

Sasa tukiondosha hivi vikwazo ina maana kwamba hizi fedha tuna uwezo wa kuzipata na tukagharamia miradi yetu wka kupitia mapato ya kodi. Kwa hiyo, Serikali tusikilize katika hili kuna nafasi zinahitaji uteuzi kesi haziendi kwa hiyo kama tutafanya hivyo tutaongeza mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, pia kuna fedha ambazo zipo katika kesi, kesi ambayo anayeshitakiwa anatakiwa alipe 1/3 yake fedha zile zikikwama 1/3 ya yule mtu imekaa pale imeganda hawezi kujiendeleza kuajiri wala kufanya jambo jingine. Lakini 2/3 ya Serikali ambayo kama Serikali itashinda ina maana kwamba pia itakuwa imekosekana kwa hiyo, tunaomba Serikali hili ikalifanyie kazi ili katika kugharamia mpango wetu tuende vizuri.

Mheshimiwa Spika, jingine katika sekta binafsi ambayo inagharamia trilioni 40 mpango uliopita sekta binafsi tulilipa trilioni 48 lakini ikafanya vizuri mpaka kufikia miaka minne katika mpango uliopita sekta binafsi ilikuwa tayari washatumia trilioni 32 kati ya trilioni 48. Kwa maana hiyo ukiweka *average* kwamba kila mwaka sekta binafsi ina uwezo wa kuchangia trilioni 8. Kwa maana hiyo ndani ya mwaka huu sekta binafsi itakuwa tayari inakamilisha trilioni 40 ingawaje zile 8 kwamba zitakuwa hazikuweza kupatikana.

Sasa safari hii tumeweka *blue print*, tunaondosha vikwazo lakini bado sekta binafsi tuliweka hii trilioni 40 ina maana hapa ni lazima kuna jambo la kufanya kwa sekta binafsi pamoja na kutumia uwezo huo ambao tumeondosha ina maana ilikuwa sekta binafsi hapa ni lazima tuzidi kwasababu tayari watu watakuwa washashawishika katika kuendelea kutu-*support* katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali izidi kushirikiana na sekta binafsi ili ugharamiaji wa sekta binafsi ukiongezeka itakuwa vizuri kwasababu Serikali haijaipata ki-*percentage* sekta binafsi. Sekta binafsi ki-*percentage* iko juu kuliko Serikali, kwahiyo hilo ilikuwa nalo pia nilikuwa naomba tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, jingine ni jambo muhimu sana ambalo kamati ya bajeti imeshauri tuwe na sera ya *monitoring and evaluation* tuwe na sera hiyo tusipokuwa na sera hiyo ina maana hata sisi hapa Wabunge tutakuja kujadili mwezi wa tano lakini bila kuletewa ripoti ya utekelezaji ambayo ipo sahihi. Kwa mfano kama tukiwa na *monitoring* tu peke yake tutajua *base line* tutajua kwamba hapa tunaanza kutokea ngapi kwenda ngapi. Tuna *set target* zetu tutapata kupima *target* zetu *whether* tumeshindwa katika kupata input tutajua kwamba tatizo ilikuwa ni *input* na *input* hizo zimeshindikana na kitu gani tunaweza tukabadilisha msimamo katikati kabla ya kufika miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spka, lakini tukisubiri miaka mitano ina maana kwamba tutakuja kupima matokeo makubwa tutashindwa kujikosoa katikati na ndiyo maana mfano tuna miradi hiyo ambayo imetajwa na kamati hapa miradi ya Mchuchuma Liganga Magadi soda kule Engaluka kwasababu haiwezi kufanyiwa hivyo kwasababu kila mwaka inapita vilevile na mpaka sasa hivi ukiuliza utaambiwa kwamba iko katika hatua ya kulipiwa fidia mradi wa miaka 20 uko katika hatua ya kulipiwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ingelikuwa kunafanyika *monitoring* wapi tunakwamba tungeweza kutatua vikwazo na sisi Wabunge tungeweza kushauri. Niseme hayo ingawaje na wengine watayasema haya haya kwasababu mtemewa mate na wengi hurowa tunapenda ushauri wetu huo uchukuliwe nashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan King kwa mchango wako mzuri sana Mheshimiwa Twaha Mpembenwe atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Njau.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji katika mpango huu. Lakini awali ya yote kwanza naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Wabunge wenzangu ambao wameteuliwa katika *portfolio* mbalimbali nataka niwaahidi

tu kwamba sisi tutaendelea kuwapa ushirikiano katika nafasi zao walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama hivyo haitoshi vile vile nilikuwa naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Fedha kwa uwasilishaji wake mzuri ambao ameweza kuuwasilisha katika suala zima la mpango huu.

Mheshimiwa Spika, lakini kama hivyo vilevile haitoshi nimshukuru mwenyekiti wetu wa kamati ya bajeti kwa vile vile kuweza kuwasilisha na kuweza kutoa maoni mazuri zaidi kuhusiana na suala la mpango huu.

Mheshimiwa Spika, kubwa kuliko lote nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu mama yetu mama Samia Suluhu Hassan ameanza vizuri sana kwa kuweza kuwatia matumaini watanzania ambao walikuwa tayari wameshapoteza matumaini na walikuwa na vilio ndani ya nafsi zao. Lakini mama ameanza vizuri sana na naomba tu nipite katika kauli yake niseme wale ambao wanakusudia kumzingua mama basi tutakwenda kuzinguana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba ni nichangie mpango huu katika maeneo mawili tu. Eneo la kwanza ni suala zima la *tax base* na eneo la pili ni suala zima la *performance of the projects* hizi kubwa kubwa ambazo tunaendelea nazo sisi kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kuchangia kwenye *tax base* kuongeza wigo wa *tax base* nilikuwa naomba kidogo nitoe ushauri hapa kwa Serikali. Hizi *tough decision* kuzichukua wakati mwingine kuzichukua zinakuwa ni ngumu lakini *they are wealth taken* mimi nilikuwa naomba niishauri Serikali tuangalie uwezekano wa ku-*reduce cooperate tax rate* tukifanya hivyo tafsiri yake ni nini tutakwenda kutengeneza kitu kinachoitwa *multiply effects* tunapo *reduce cooperate tax rate* tunawa-*encourage cooperate citizen* siyo tu wale kutoka nje lakini hata hawa wa *local investors* wale wenye mitaji iliyokuwa iko ndani sasa watatoka na watakwenda ku-invest maeneo tofauti.

Mheshimiwa Spika, sasa tunakwenda kutengeneza *multiply effect* kwa kufanya hivyo. Tafsiri yake pana ni kwamba anapokuja mtu aka-*invest,* mndengereko kama mimi nikawa na hela yangu ya mkopo nikachukuwa, nikaenda ku-*invest* kwenye kiwanda, ni kwamba nitaajiri watu. Ninavyoajiri watu, kinachofuata maana yake ni kwamba tunakwenda kuongeza wigo wa *tax;* na wale watu wanaokwenda kuajiriwa pale, tuta-*improve their standard of living.*

Mheshimiwa Spika, *hii ni very basic economics* ya *form four* sijui *form five* na nafikiri Mheshimiwa Waziri *you know better than this. We have to reduce the corporate tax rate,* lazima tucheze na *fiscal policy* ili sasa tuweze kuwa-*encourage investors* waje waweze ku-*invest.* Mama yetu alisema hii katika hotuba zake katika mambo aliyokuwa anazungumza, kwamba lazima tutumie fursa mbalimbali ili kuhakikisha kwamba hatuwakumbizi wawekezaji, tunawavuta ili tuendelee kuwa nao. Kwa kufanya hivyo, tafsiri yake ni kwamba lazima tuchukue *tough decision*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna nchi ambazo zimeweza kufanya hivyo. Marekani katika miaka ya nyuma huko waliweza ku-*reduce tax corporate rate* na athari yake ni kwamba, kukawa na viwanda vingi, wawekezaji wakawa wengi waka-*increase* vilevile *rate employment.* Tukifanya hivyo, ile *corporate tax base* tunaiongeza.

Mheshimiwa Spika, wale watu ambao tunawakamua; nakumbuka kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja; mwanangu mmoja kutoka Mtama aliwahi kuzungumza kwamba ng'ombe tunamkamua mpaka inafikia hatua sasa hakuna cha kumkamua. Tafsiri yake ni kwamba *we do have to expect* kwamba hawa *larger tax payer* ndio watakuwa wao tu peke yao wanaweza waka- *finance* hizi fedha ambazo tunaenda kuzikusanya kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kimaendeleo ndani ya nchi.

Nilikuwa naomba nishauri katika eneo hilo. Enep la pili katika suala lazima la kungoze hii *tax base…*

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha, mwanao anakuangalia.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, mwanangu ananiangalia!

**SPIKA:** Mh! Endelea Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Sawa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, vile vile katika suala la kuongeza hii *tax base* nilikuwa naomba niishauri Serikali tuongeze wigo, tumefanya vizuri sana katika suala zima la *electronic stamp,* tumefanya vizuri sana kule kwenye *wine* katika mambo ya *spirit* tumefanya vizuri sana kwa sababu tumeweza ku-*increase* ile *collection.* Kwa mfano tumeweza ku-*increase domestic collection 74.4 percent* katika *quarter* ya kwanza ya 2020.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, *Value Added Tax* ilikuwa imeongozeka *22.8 percent,* vile vile tumeweza ku-*increase* suala nzima la makusanyo ya *soft drinks* kwenye asilimia 11.7. Hapa tumefanya vizuri. Sasa ni muhimu vile vile Serikali tukaongeza ile *electronic stamp* katika *point of production* kwenye maeneo mengine. Kwa mfano katika sekta nzima ya uzalishaji wa *cement,* kule bado hatujakugusa.

Mheshimiwa Spika, watu wengi sana wanatumia *cement* na *action* ambayo inafanyika kule, *we can not control it*. Katika maeneo mazima ya mambo ya nondo, mabati, *we cannot control it.* Kwa hiyo, ili sasa ili tuweze *ku-extend* ile *tax base,* mambo ya namna hii lazima tuweze kuyashungulikia. Tumefanya vizuri, lakini naomba kuishauri Serikali tuendelee kuweka msisitizo katika maeneo hayo mengine ili sasa tusije tu tukawabana wale *larger tax payers* peke yao. Wanatukimbia, wanaondoka.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mama yetu wakati anahutubia Taifa, watu wengi sana waliweza kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais. Wakati nikiwa hapa, Wandengereko wenzangu kutoka Kibiti walikuwa wanapiga

simu na kutuma *message* kedekede wakisema kwamba sasa jembe limekuja na tunakwenda kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni lazima tuangalie, hii *tax burden* tuweze kui- *balance.* Tukifanya hivyo, nafikiri tutafanya vizuri sana, *collections* zetu za ndani zinaweza zikaongezeka.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo nilikuwa naomba niichangie ni katika suala la zima la *PPP.* Mimi ni mgeni hapa Bungeni, lakini *I know for sure,* kwa kupitia *paper works* nilijua kuna Sheria ya *PPP* ililetwa hapa na ikaja mwaka 2018 kufanyiwa *some amendments.* Nilikuwa naomba niishauri tena Serikali, kama kuna upungufu katika sheria ile, basi iletwe tena tuweze kuishungulikia, kwa sababu miradi mikubwa mikubwa hii ni lazima tuifanye kwa kupitia *PPP.* Tukifanya hivyo, tafsiri yake ni kwamba haka kasungura kadogo, fedha zetu hizi za ndani tunazozikusanya zinaweza zikaenda kutusaidia ili kuweza kuendeleza huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, mfano katika Sekta za Afya na katika mambo mengine fedha hizi zinaweza kutumika. Kwa hiyo, miradi mikubwa mikubwa hii ili tuweze kuiendeleza vizuri zaidi, basi ile *idea* ya *PPP* tuilete tena hapa kama ile sheria ina upungufu. Kwa sababu tunapozungumzia *PPP,* tunazungumzia mifano tunayo pale ndiyo, tumejenga mabweni, lakini tuzungumzie *substantial,* ile miradi mikubwa mikubwa kama Serikali. Tunakwenda kutengeneza pale mradi wa Mwalimu Nyerere. *If not,* twendeni kwenye *PPP*. Najua tunatumia fedha zetu za ndani, ni suala la busara zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama hivyo haitoshi, siyo vibaya vile vile, tukiona kwamba mazingira siyo rafiki *and of course it has to be so,* twendeni tukatumie *PPP* ili sasa kwa namna moja ama nyingine, miradi hii iende sambamba na iweze kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, uliweza kutoa hapa maelezo kidogo kwamba mabehewa siyo lazima tu yashughulikiwe na watu wengine, sisi wengine tuliwahi kupata bahati kukaa

kwa Wandengereko nchi za nje huko, tuliona. Ukienda pale *UK* utakuta zile *British* reli zinazokuwa zinazunguka, siyo zote zinakuwa *controlled na British Government.* Unaweza ukakuta kwamba kuna tajiri tu mmoja anashughulikia eneo fulani, tajiri mwingine anashughulikia eneo fulani lakini mambo yanakwenda.

Mheshimiwa Spika, when you *talk about infrastructure in UK it is superb,* ipo namba moja. Sisi twendeni tukaige mambo haya, wakati ndiyo huu. Mama tunaye, Mheshimiwa Samia anatupa sana uwezo sisi Watendaji. Ameweza kutupa fursa kusema kwamba tumieni vipaji mlivyonavyo ili tuweze ku-*extend tax base* tuweze kuongeza maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana nichangie katika haya maeneo mawili. Hata hivyo, katika suala hili la *tax base* nitakwenda kwa Mheshimiwa Waziri kwa wakati maalum kumpa takwimu ambazo ni *research* ambayo nimeweza kuifanya kwenye *Commercial City* pale Dar es Salaam. *If you look at the number from 2015 to date, the number of corporate citizen* ambazo tayari zimeshafungwa *they are so many.*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *amount of tax* tunazo-*collect* zina-*increase* katika *decreasing rate,* iko pale Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri akiniruhusu, mimi nitakwenda, nitamfuata, nitampa *research* ambayo tulikuwa tumeifanya. Sasa ni lazima tuchukue maamuzi magumu ili tuweze kusonga mbele na tuweze kum-*support* mama yetu katika kuweza kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Twaha Mpembenwe kwa mchango wako mzuri, tunakushukuru sana. Mheshimiwa Felista Njau atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na Mheshimiwa Elibariki Kingu ajiandae.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nakushukuru kwa ajili ya kunipa nafasi hii. Pia nitoe pole kwa Watanzania wote kwa msiba mkubwa uliotufika. Kimsingi nimesimama mbele yako niweze kuchangia kidogo, lakini niweke msisitizo; naingia moja kwa moja kwenye Sekta ya Kilimo. Natamani kila mtu akisimama aweze kuona upana na ukubwa wa sekta hii ili tuweze kuweka nguvu inayohusika katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme sekta ya kilimo inaweza kuchukua asilimia 56.5 ya ajira zote za Watanzania. Nikienda kwenye asilimia; nakwenda kwenye asilimia 20 ya mauzo yote ya nje. Unaona hapa kidogo kuna ufinyu, kwa sababu sekta hii haijachukuliwa kwa uzito wake. Ikichukuliwa kwa uzito wake, hatutalia ajali za boda boda barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Nairobi wameweza kutenga *SACCOSS* maalum, wakakusanya vijana katika makundi na wanatengeneza mfumo wa kununua daladala kule wanaziita matatuu ili waweze kuwekeza. Sisi tuna ardhi kubwa ambayo ina rutuba, tuna maji. Kwa mfumo wa umwagiliaji, kama hatuna ile miundombinu, lakini tuangalie hizi mvua zinazonyesha, tunalia mafuriko; haya maji yanayotokana na mvua tungeweza kuweka pale miundombinu ya umwagiliaji tukavuna yale maji yakatusaidia kwenye kumwagilia, tusingelia leo mambo ya mafuta, tungewekeza kwenye alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa hawa vijana wanaokufa kwa boda boda hawajapata *Plan B* za ajira. Wakipata *Plan B* hatutalia vifo hivi, kwa sababu kila kijana anafikiria ajira ni boda boda. Pia tungeweza kuwapa elimu, wakaweza kuwekeza kwenye kilimo ambao ni asilimia kubwa sana, hawa vijana wangetoka na wangekwenda kusimama na utaona uchumi unakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuomba, kuna benki ambazo zinatoa mikopo kwa wakulima, benki hizi hazijaona vijana. Vijana hawawezi kuwekeza kule kwa sababu wanaonekana hawana thamani fulani hivi. Labda wawekwe kwenye vikundi

ili waweze kwenda kwenye benki hizi waweze kukopeshwa au waundiwe *SACCOSS* zao maalum waweze kukopa maana hawana dhamana, ndiyo maana hawakopesheki.

Mheshimiwa Spika, kijana wa Tanzania hata akienda mahali anaonekana muhuni tu, lakini ni Mtanzania ambaye kimsingi tukimpa mbinu, tukampa elimu, tukawekeza kwenye kilimo, hawa vijana wasingelia leo. Kingine, akina mama wengi wanalima kwa jembe la mkono, hawalimi kilimo chenye tija. Hata wakilima hiki kilimo chenye tija, hawajui zao ambalo wanaweza kulima liweze kwenda nje. Tuwekeze kwenye tafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwekeza kwenye tafiti, tukalima kilimo chenye tija, tutamkomboa mkulima mdogo na mkubwa na wote tutasimama. Niweze kusema hili suala kwa sababu tuna akina mama wengi wanalima kila siku ni kilio. Analima anaambiwa tu kwa maneno, kwa nadharia kwamba kilimo kitakukomboa, lakini haoni ukombozi wa kilimo hiki.

Mheshimiwa Spika, tukienda vijijini tukakusanya akina mama tukawapa elimu, wakalima kilimo ambacho kitakidhi vigezo kule nje, kwa sababu akina mama wengi wanalima, wanaweka mbolea ya chumvi chumvi, wakija kupima wanaona zao hili halifai. Tuwape elimu. Tuna mifugo; tuchukue mbolea za mifugo, tuweke kwa akina mama wale tuwekeze kwenye tafiti, leo kina mama tutawainua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa ninachoweza kusema kwenye sehemu ya pili ni mambo ya demokrasia. Mheshimiwa ameongea juu ya kuimarisha demokrasia, usawa na amani. Kuna watu wenye makovu, wana makovu yaliyopita huko nyuma. Tuna mategemeo; Tanzania, Taifa hili sasa hivi lina mategemeo makubwa na Rais wa sasa, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu. Lina mategemeo makubwa kutokana na kauli zake, wanasema kimjazacho mtu moyoni ndicho kinachotoka kwenye kinywa chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu ameonyesha kunyesha suluhu kwa Watanzania. Kwa hiyo, Watanzania waliokata tamaa wamekuja kivingine. Niwaambie, kuna watu walikuwa wanagugumia, wanalia, wanashika matumbo, leo wanatembea vifua mbele, hata hawajaona kitu, kwa kauli ya kiongozi wetu mkuu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu. Nampongeza lakini tumwombee kama Watanzania mama huyu asimame kwa hizi kauli anazosema azisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi kilichopita, watu walipata makovu. Kuna Watanzania wanaogopa kuja kwenye nchi yao, kuna Watanzania wana kesi za kubambikiwa, za kisiasa zisizoisha, kesi hazina ushahidi zinapigwa tarehe, hatuwezi kuzizungumzia. Mheshimiwa Mama Samia Suluhu amesema kesi zile zifutwe. Niweze kusema jambo moja, kwenye demokrasia wanasema, bila haki kuonekana inatendeka, demokrasia itakuwa inambwela mbwela. Najua kwa kipindi hiki cha mama yetu, demokrasia itakwenda *ku-take place* na haki za watu zinaenda kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mamlaka husika na viongozi ambao wako hapa wenye dhamana waweze kuangalia hii michango ya Wabunge. Wabunge wanachangia kutokana na mambo yanayowakuta huko na wananchi wao, tuweze kuyachukua kwa *u-serious* ili tuyatekeleze *ku-reflect* kule nje ambapo tunapotoka. Vinginevyo tutakuwa tunaimba mapambio na mambo hayachukuliwi, yakibaki pale pale tunaonekana huku tunakuja kula bata, lakini huku tumesimama kwa ajili ya wananchi wetu. Tunaomba yachukuliwe kwa u-*serious* ili yaweze kutekelezwa na wananchi waweze kuona matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Felista Njau. Tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri na hasa ulipomalizia kwenye demokrasia. Mmh! *(Kicheko/Makofi)*

Ni vizuri tu kujua kwamba tumeshavuka Kanaani. Siasa lazima pande zote tujifunze tunapovuka. Siasa za kupanda kwenye majukwaa, unatukana watu mwanzo mwisho, kisa tu unaitwa mpinzani! Hatuwezi kurudi huko! Lazima wote tukubaliane, *this has to end*. Wako huwatukani! Eeeh! Mimi kama binadamu hunitukani! Iko hivyo! Msifikiri kwamba mama atawalegezea kwa hayo, muanze kumtukana tukana na mambo kama hayo, haiwezekani! *(Kicheko/Makofi)*

Tuendeshe siasa za kistaarabu, siasa nzuri, tunasema za kupeleka nchi yetu mbele. Siyo kupingana tu kwa kila jambo, hata liwe zuri namna gani. Kupotosha kila kilichoko na watu wengine wanaonekana kabisa ni mawakala wa watu fulani fulani eeh! Yaani mtu anafika mahali hana hata aibu, yaani yeye ni wakala moja kwa moja dah! Sasa hiyo haiwezekani, kwa sababu kwa maslahi ya nchi yetu lazima tuyalinde, ndiyo maana tuko. *(Kicheko/Makofi)*

Hii nchi yetu wote, lazima tuilinde, tuifanyie kazi, tusonge mbele na aliyeko nje, mimi nafikiri Waziri Mkuu yuko hapa, sijui kama kuna mtu kafukuzwa hapa! Nani anaitwa jina lake? Kila mtu kaondoka kivyake mwenyewe. Wengine wameswaga na watoto; haya watoto nao nani kawafukuza shule? Si mwenyewe tu! Labda umeona huko ni *green pasture,* haya, lakini Tanzania yetu haina historia hizo. Aliyeko wapi, wapi arudi tu, kwani kuna shida gani? Kama una madeni, lipa. Vinginevyo tunakubaliana kabisa, wala hakuna ubaya wowote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Jaqueline Msongozi ndio anayefuata na atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kutoa pole sana kwa familia ya aliyekuwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, ambaye alifariki dunia tarehe

17 ya mwezi wa Tatu. Natoa pole nyingi sana kwa familia, pole nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan; pole sana kwa Waziri wetu Mkuu; viongozi wengine wote na wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Jemedari, mwanamke shupavu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwenyezi Mungu amjalie kila kheri ampe kila namna iwezekanayo ili aweze kusimama imara katika uongozi mzima wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, leo nina mambo matatu tu ya kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo. Nianze na suala nzima la Sekta ya Kilimo. Mara nyingi sana nimekuwa nikisimama hapa ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nazungumzia sana suala la kilimo hasa tunapokwenda kufungamanisha kilimo na masuala mazima ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri shahiri, pasipo shaka yoyote, bila kuimarisha Sekta ya Kilimo hatutaweza kufikia malengo tunayokusudia katika mpango mzima wa kukuza uchumi katika nchi yetu ya Tanzania. Hivyo basi, naomba Serikali yangu sikivu kwamba mpango huu wa kilimo uende sambamba na kuhakikisha kwamba masuala mazima ya mbegu kuelekea katika uwekezaji kwenye kilimo kuwe na mpango Madhubuti, yaanzishwe mashamba ambayo yataweza kuandaa mbegu nzuri ambazo zitauzwa kwenye maeneo mbalimbali kwa bei nafuu ili uwekezaji huu ufanyike na uwe na tija kwa Taifa na pia katika kuinua masuala mazima ya kiuchumi katika nchi yetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo ni lazima pia liambatane na masuala mazima ya masoko. Masoko imekuwa ni tatizo. Uwekezaji ni mkubwa sana unaofanywa na wananchi wakitumia nguvu nyingi na wakati mwingine wananchi wanafanya kazi kwa kutumia mikono yao, hawana

hata zana za kilimo zilizo bora ili kuweza kuwezesha Sekta hii ya Kilimo na uwekezaji wao.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na tatizo la masoko, masoko ni tatizo. Mkulima alime mwenyewe na atafute soko mwenyewe. Naomba sasa Serikali yangu kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara wajipange vizuri kuhakikisha kwamba wanatafuta masoko ili wawekezaji wetu kwenye masuala mazima ya kilimo wafanye uwekezaji wenye tija.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kumekuwa na mikoa ambayo imekuwa ikizalisha sana mazao ya nafaka ambayo kimsingi inasaidia sana katika kuweka uimara na kuhakikisha kwamba tunakuwa na akiba nzuri ya chakula. Unapoitaja mikoa hiyo, huwezi kuacha kuutaja Mkoa wa Ruvuma ambao umeshika nafasi ya kwanza mara nne mfululuzo katika uzalishaji wa mazao ya nafaka, ukifuatiwa na Mkoa wa Songwe, unafuatiwa na Mkoa wa Rukwa na mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, mikoa hii inafanya vizuri sana. Sasa endapo kama mikoa hii inafanya vizuri, itoshe tu leo niongee mbele yako dhidi ya Waziri wa Fedha aweze kutoa tunu kwa mikoa hiyo kwa kupeleka Benki ya Kilimo. Benki ya Kilimo hiyo itafanya uwekezaji maeneo hayo ili waweze kuwakopesha. Pia iende sambamba na mikoa mingine inayolima pamba, Mkoa wa Dodoma unaolima zabibu na maeneo mengine yote ambayo katika nchi yetu yanafanya vizuri waweze kwenda kupelekewa Benki ya Kilimo ili iweze kuwasaidia wananchi katika kuwainua zaidi kwa sababu wananchi bado wanauhitaji, lakini wanapata wapi mitaji ili wawekeze vizuri zaidi kwenye kilimo. Unakuta Benki ya Kilimo ipo pale Dar es Salaam inashangaa shangaa tu, nani anayelima pale Dar es Salaam. Ni vizuri basi Waziri wa Kilimo apeleke Benki hizi kwenye maeneo husika yanayofanya vizuri ili weweze kuwainua kiuchumi na waweze kufanya uwekezaji mzuri katika masuala mazima ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, sasa naenda kwenye suala la barabara; tumekuwa tukizungumza sana kuhusiana na

masuala ya barabara. Lengo ni kuhakikisha kwamba maeneo yote ya nchi yetu ya Tanzania yanafunguliwa na barabara zetu zikiwemo barabara za kawaida ambazo zinasimamiwa na *TARURA*, lakini pia zikiwepo barabara ambazo zinasimamiwa na *TANROADS ili* kuweza kurahisisha uchukuzi na kurahisha uzalishaji ambao utapelekea ukuaji wa kasi wa uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa naomba niende moja kwa moja kwenye suala la *PPP (Public Private Partnership)*. Suala hili na wewe umelidokeza hapo, ni jambo zuri kabisa, Serikali isijilimbikizie miradi mikubwa kuhenyeka nayo, kutabika nayo, badala yake wafungue fursa ili taasisi na mashirika mbalimbali na sekta binafsi zinazoweza kuja kuwekeza basi zije kuwekeza katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Sheria Na. 18 ambayo ilifanyiwa marekebisho katika Bunge lako Tukufu hili mwaka 2010, sheria hii haijamnufaisha mwananchi wa Tanzania, bado sheria hii haijamnufaisha mwanaumma wa Tanzania. Nasema hivi kwa sababu sheria imefanyiwa marekebisho kwamba sekta binafsi sasa ziungane na Serikali ili kuweza kutanua wigo na waweze kuwekeza kwa maslahi ya Watanzania, lakini bado sheria hii haijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, unakumbuka tarehe sita Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amelihutubia Taifa akiwa anaapisha watendaji mbalimbali pale Ikulu, ameeleza Mama samia na ameonesha dhahiri pasipo shaka kwamba anahitaji sekta binafsi zije ziwekeze katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa ni wajibu wa viongozi mbalimbali wanaohusika katika sehemu mbalimbali kuweza kutoa ushirikiano ili wawekezaji hawa waweze kuja na kuwekeza ili sheria hii Na. 18 iliyorekebishwa mwaka 2010 iweze kufanya kazi na kuleta tija kwa Watanzania ambayo itasababisha ukuaji wa uchumi. Wawekezaji hao watalipa kodi, lakini itaongeza ajira na pia itainua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, utengenezaji wa barabara; nakumbuka mwaka 2017 ulinipa fursa ya kwenda Nchi ya China kikazi kwa majukumu ambayo ulitupa sisi kama Wabunge wako, tulikuwa Wabunge 20. Nilijifunza jambo kubwa sana na Mungu akubariki sana wakati mwingine sasa naomba unipe fursa hiyo kwa nchi nyingine, nitakuja na mchango hapa ndani ya Bunge. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo nililiona China mwaka 2017, leo hii ninachangia ndani ya Bunge kwamba niliona kuna barabara ambazo zimetengenezwa kwa mtindo wa *PPP* ambazo zimekuwa zikisaidia sana katika Nchi ya China ambayo miundombinu ya barabara imezagaa kila mahali. Vile vile imekuwa ikisaidia pato la nchi linaendelea kukua na wananchi walioko wanaendelea kunufaika na kurahisha shughuli zao za kuendeleza uchumi.

Mheshimiwa Spika, hukunipeleka bure kule, nimepata hiyo *exposure* na leo nasimama ndani ya Bunge lako Tukufu kuweza kuchangia hilo na kwamba kuona kwa macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwamba....

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Msongozi anasema kwamba fursa ya Waheshimiwa kutembeatembea kidogo ina faida. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Jacqueline malizia dakika zako.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, sasa hili suala la *PPP* kwenye barabara zetu tungeweza kuchukua watu wa *NSSF* wakatengeneza barabara hapa na zikawa zinalipiwa, Serikali inapata mapato yake, *NSSF* watapata mapato yake na pia wananchi watapata ajira na nchi yetu itaendelea kiuchumi. Hali kadhalika tunahangaika hapa kuzungumzia barabara za kufungua baina ya nchi na nchi, kwa mfano kuna barabara yetu ya Likuyufusi - Mkenda ambayo inaungana na Nchi ya Mozambique. Barabara hii ikitengenezwa kwa mtindo wa *PPP* itasaidia sana kurahisisha kufungua uchumi huo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna barabara ambayo ipo Kakonko barabara hiyo ina urefu wa kilimita 40, inatoka Kakonko halafu inakwenda Muhange. Kwa hiyo hii barabara ingeweza kufungua na mahali pale nimekwenda wakati wa kampeni, nimekuta wananchi wa eneo hilo wana soko kubwa sana pale. Kwa hiyo ikiunganishwa hii barabara na wananchi wale wakawa wana zile *movements* za kulipia hiyo barabara, ni wazi kwamba Serikali itaongeza mapato makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la tatu na la mwisho, sasa nizungumzie uwezeshaji wanawake kiuchumi, mama ni mama tu, kwa kweli ukimwezesha mwanamke umewezesha familia na umewezesha jamii kwa nzima kwa ujumla. Wanawake wamekuwa wakiwezeshwa kupitia halmashauri zetu mkopo wa asilimia 10 kwa mgawanyo wa 4, 4, 2. Halmashauri zingine hazina uwezo wa kuwakopesha wanawake hawa wakaweza kufanya uwekezaji wenye tija kwenye maeneo yao. Sasa niiombe Serikali yangu tukufu iweke utaratibu mzuri ambao utasaidia wanawake wengi kukopeshwa wakiwepo wanawake wa Jimbo la Kongwa, kule Kongwa wanawake wale wakiwezeshwa vizuri kwa vyovyote vile hata familia zao zitaimarika zitaboresheka na mambo yatakwenda barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho suala la mifugo,

**SPIKA:** Ahsante, muda umekwisha.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana ubarikiwe. Mheshimiwa Elibariki Kingu, kwa mchana huu atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa nikiri kwamba mwaka 1999 na kuelekea mwaka wa 2000, Taifa letu la Tanzania lilipata msiba wa kuondokewa na Hayati

Baba wa Taifa letu Mwalimu Nyerere. Taifa lilishuka sana na Watanzania waliingiwa na majonzi na wengi wakajiuliza nini itakuwa hatma ya Taifa letu. Hata hivyo, kutokana na uongozi madhubuti na uimara wa chama kilichopo madarakani Chama Cha Mapinduzi, Taifa la Tanzania liliendelea kuwa *stable* na nchi iliendelea kuwa moja na maendeleo ya kiuchumi na kijamii yaliendelea kuonekana katika nchi Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia mwaka huu pia Taifa la Tanzania lilimpoteza Rais wake ambaye alikuwa kipenzi cha Watanzania, Rais ambaye alikuwa mzalendo, shujaa, jasiri, mwenye kuongoza njia, Rais aliyeaminiwa na umma ambaye na kuleta imani kubwa duniani, kifo chake na maombolezo yake yamedhihirisha namna gani Watanzania na dunia kwa ujumla ilikuwa na imani kubwa na rais huyu, lakini Watanzania wengi waliingiwa na hofu wakaona sasa Tanzania itakwenda wapi. Kuonesha umahiri wa chama kilichopo madarakani kwamba ni chama kinachoweza kuwaandaa viongozi, leo tunapozungumza kila nchi, Raisi aliyepo madarakani Mama Samia Suluhu Hassan, kila mmoja anatoa makofi na pongezi kama ilivyokuwa kwa mtangulizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema ni kwamba Chama Cha Mapinduzi ni ngalawa imara inayoweza kuwaandaa viongozi wa kuliongoza Taifa wakati wowote wa shida na raha. CCM ni tanuru la kuandaa viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,, naomba niende kwenye hotuba yangu. Sasa nakwenda kuzungumzia maeneo makubwa mawili hasa katika sekta ya kilimo. Nashukuru namwona kaka yangu Bashe huwa ni Naibu Waziri msikivu sana, mara nyingi Wabunge wanapozungumza huwa ana-*take note* kwa manufaa ya Taifa. Naomba nitoe takwimu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Nchi ya Misri, ambayo kwa asilimia karibu sabini kama sio themanini ni jangwa; nchi ya Israel ni jangwa. Naomba Bunge lako Tukufu lisikilize takwimu zifuatazo: Taifa la Misri katika sekta ya kilimo cha umwagiliaji

licha ya nchi kuwa imezungukwa na mto mkubwa ambao kimsingi chanzo kikubwa cha mto huo kinatoka Tanzania, ukiangalia takwimu zinaonesha Taifa la Egypt moja ya vyanzo vikubwa vinavyofanya nguvu za kiuchumi za Nchi ya *Egypt* ni kilimo cha umwagiliaji. Kama haitoshi takwimu zinaonesha Taifa la Misri limewekeza zaidi ya hekta milioni 3.4 kwenye Sekta ya *irrigation* peke yake.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia takwimu *suitability* ya land ya Misri na Tanzania ni tofauti kama mbingu na ardhi. *Availability* za *resources* kama maji, *manpower* na mengine, ni sawa na mbingu na ardhi, kwa maana ya kwamba Tanzania hiko katika *competitive advantage* ya ku-*invest* kwenye kilimo cha umwagiliaji, lakini angalia takwimu kwa nchi yetu. Namwomba kaka yangu Mheshimiwa Bashe na Mheshimwa Waziri wameaminiwa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Mchango wangu wa kwanza nilipoingia kwenye Bunge hili nilizungumzia habari ya sekta ya *Irrigation, that was my first* mchango kwenye Bunge la Tanzania. Nilitoa mifano na nikatoa ushauri, namna gani Serikali ya Chama Cha Mapinduzi tunaweza tukalipindua Taifa hili likawa Taifa la ku-*export* mazao duniani kote na watu wote tukainua uchumi wa Taifa, kwa Tanzania sasa tunapozungumza eneo ambalo tumelitumia peke yake kwa umwagiliaji ni hekta elfu 19 wakati Egypt *they have 3.4 million* na hawana *suitable land* kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, natoa takwimu hizi huku nikiwa natambua kabisa, Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi, kama kweli wataamua kudhamiria kusaidia kilimo cha nchi hii katika sekta ya umwagiliaji, nakwenda kutoa mfano, nimekuwa Mkuu wa Wilaya ya Igunga kwa miaka takribani minne. *Irrigation scheme* kubwa katikja Mkoa wa Tabora iko Wilaya ya Igunga inaitwa Mwanzugi. *Production* inayofanyika kwa lile shamba dogo, nataka nikuhakikishie, ndio *irrigation* inayolisha mchele wote wa Rwanda, Uganda pamoja na nchi za Burundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizo, nilitoa mchango wangu nikashauri, *suitable land* tunayo ambayo

inafaa kwa *irrigation,* kwa Tanzania tuna *potential* ya 2.1 *million* hekta za *irrigation* katika nchi zetu. Nilitoa mfano tukiamua kuwekeza, Mheshimiwa Bashe kaka yangu na Wizara na wataalam wakaenda pale Igunga peke yake wakaamua kuyatenga yale maji ya Mto Manonga, wakatengeneza mabwawa, *irrigation* peke yake Mkoa wa Tabora tuna uwezo wa kulisha nchi zaidi ya nne kwa chakula na mazao mengine ya kibiashara tunaweza kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi, hili Bunge ndio mahali peke yake ambapo tunaweza kutoa mawazo ya kuisaidia Serikali, inapotengeneza mipango, Taifa hili likapiga hatua. Kama Rais Hayati Magufuli alivyokuwa anasema, Taifa hili sio maskini, nchi hii tunakosa kuwa na mipango mikakati na mambo ya vipaumbele ambavyo vinaweza vika-*turn upside down* maendeleo ya nchi hii. Niiombe sana Wizara ya Kilimo, kama kuna eneo Bashe na watu wako na Wizara wanatakiwa kufanya waende wakawekeze katika kilimo cha umwagiliaji, hicho peke yake kitaleta suluhu ya kuongeza *export* nje ya nchi na kufanya Taifa letu liweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, nimetoa mifano Egypt peke yake ukingalia *statistic* za dunia, fedha wanazoingiza *Egypt* kutokana na kuuza matunda, ulitupa fursa mwaka juzi, tulikwenda *Egypt* na timu ya Taifa, tulikwenda kutembelea miradi. Ile ilikuwa ni fursa ya kimichezo, lakini tulijifunza kitu, tulienda kutembelea *Irrigation* za zabibu, tukatembelea *irrigation* mbalimbali, *Egypt is complete desert.* Hata hivyo, kinachozaliwa nilipoona yale mashamba nikaangalia baraka za nchi yangu Mungu aliyonipa hii Tanzania, *I was so much embarrassed.* Tuna uwezo Tanzania tunakwama wapi? Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye mipango yetu waandike, walete fedha, wasaidie kilimo cha umwagiliaji kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, ulikuja kunizindulia kampeni kwenye jimbo langu, mahali pekee yake ulipokuja kuzindua kampeni pale Mgungila, pale tuna maji ambayo yanapotea

na nakwambia leo tunavyozungumza Mkoa wa Singida, mchele wote karibia asilimia 75 unatoka Mgungila, lakini wale wakulima *they are just doing agriculture on their own skills,* hakuna mipango ya Serikali, bonde kubwa lina...

Mheshimiwa Spika, haya mambo jamani, napata shida sana. (*Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kingu, watu wa kilimo kila wakileta bajeti ni ya kununua *laptop,* kunuua pikipiki, zinatakiwa zielekee huko.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimwa Spika, kabisa kabisa, yaani hili Taifa nawaambia, tukidhamiria kufanya mambo na hakika kwa hii *style* ambayo Serikali yetu ilikuwa inakwenda, nakwambia nchi hii *in next ten years to come* hili Taifa halitasogelewa na nchi yote kwa Afrika kwa sababu kila kitu tunacho. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, jambo la pili, kwa mfano tumechukulia hata ukiangalia katika kilimo amechangia kaka yangu pale, amezungumza habari ya pesa tunazotumia, sasa hivi *potential* iliyopo ya ku-*import* mafuta ya kupika, inakwenda karibia dola *billion* 275, *that is the potential.* Sasa tukiamua kufanya *PPP* aliyokuwa anaisema kaka yangu, tukashirikiana na Serikali, wakafungua *block farming* ambazo huwa tunazungumza na Mheshimiwa Bashe ya alizeti, nasema, fedha tunazozitumia kuagiza mafuta peke yake kwenye kilimo, *block farming* zikiwepo za mfano, sisi Singida tumemwambia Mheshimiwa Bashe, tuko tayari kumpa maeneo ya kutosha ya alizeti kufungua *block farming* ambazo zitakuwa mfano ili Taifa liweze kuzalisha mafuta.

Mheshimiwa Spika, hii nchi tunaweza kufanya mambo makubwa na mazito endapo Serikali itapokea ushauri wa Wabunge na kuacha kuona Wabunge tunaoshauri kama maadui. Maana kuna Mawaziri wengine ukiwashauri, *we have to be honest,* anakuona adui, yaani unaona kabisa Waziri anakuona huyu mtu adui. Kuna Waziri mmoja nilishauri kwa nia njema, Waziri mwenyewe ni Mheshimiwa Mwambe,

nikasema angalieni kuna shida ya masoko ya Watanzania. Mheshimiwa aknijibu *in very arrogant way,* mimi ni Mbunge mwakilishi wa watu, Mawawiri tunapotoa michango tuheshimiane, *we are doing this for interest* ya nchi. Jibu alilonipa; wewe bwana kama nyama yako imekosa soko..., mimi siuzi nyama. Nikizungumza hapa kwa niaba ya wafanyabaishara, nisichukuliwe nimetumwa, wale ni Watanzania na sisi ni sauti yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *I am very sorry* kama nitakuwa nimem-*offend,* lakini *I was so embarrassed,* hilo siyo jibu la Waziri anayetokana na Chama Cha Mapinduzi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, naomba nizungumzie upande wa *marketing*. Upande wa *marketing* natoa mfano mdogo, Taifa la Ethiopia lilifungiwa kupata *market* ya kuuza nyama kwa nchi za kiarabu, *in within three days*, Mawaziri zaidi ya sita walifunga safari kwenda kufungua masoko ya watu wao. Sisi hapa kwetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nimekuona Mheshimiwa Olelekaita, nitakupa nafasi baada ya dakika moja.

Kwanza niseme kwamba uchangiaji utaendelea jioni na bado tuna nafasi ya majina ya Wabunge ambao wangependa kuchangia kwa leo na wale wengine mnaojiandaa kuchangia kesho, mtaendelea kuleta majina jioni ili tuendelee na uchangiaji.

Kufuatia mchango wa Mheshimiwa Kingu, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo na Mheshimiwa Elibariki Kingu

amezungumza jambo muhimu linalomhusu Mheshimiwa Waziri na *specifically* akamtaja Waziri Mwambe hapa hadharani, basi ni vizuri na mimi nipigie mstari kidogo. Ninayo malalamiko kadhaa kuhusu Waziri, Mheshimiwa Mwambe. *(Makofi)*

Nafikiri kwa kuwa ni Mbunge mgeni anadhani ukiwa Waziri wewe ni mtu mkubwa sana hapa Bungeni; haiendi hivyo. Ana majibu ya hovyo sana, hawaheshimu hata Wajumbe wa Kamati yake, wanapata taabu jinsi ya kufanya naye kazi. *(Makofi)*

Sasa kwa kuwa ni mgeni na ndiyo ameanza kazi na bahati nzuri Mheshimiwa Rais akamuamini katika Uwaziri moja kwa moja bila kuwa Mbunge wa kawaida, nafikiri hajajua nafasi ya Wabunge katika Wizara yake na shughuli zake. Anadhani bajeti ya Wizara yake ataipata yeye mwenyewe hapa kwa juhudi za kwake yeye, haiwezekani! Ukimnyanyasa Mbunge mmoja umewanyanyasa Wabunge wote. Ukinyanyasa Kamati moja umenyanyasa Kamati zote. Duniani kote hakuna Waziri anayemjibu ufedhuli Mbunge, haipo hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni vizuri tumuachie Mheshimiwa Waziri Mkuu ili akakae naye kidogo amfunde. Bado mgeni, kwa sasa hivi tumsamehe, bado kidogo taabu. Hata Wabunge wa Mkoa wake wa Mtwara haelewani nao wote, huyu, ni ufedhuli huohuo. Kwa hiyo, ni vizuri kidogo Mheshimiwa Waziri Mkuu ukalifahamu hilo. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Olelekaita umesimama.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 76 ya Kanuni zetu. Kubwa zaidi niseme tu kwamba kuna mpiga kura wangu mmoja leo ametaka

kuja kunitembelea na akazuiwa getini kwa sababu amevaa nguo za Kimasai. Sasa naomba nipate mwongozo wako kuhusu mavazi haya rasmi kabisa ili na Watanzania wengine walioko huko wenye mavazi yao ya asili wafahamu utaratibu wa mavazi kuhusu Bunge lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *I was embarrassed.* Kwa kweli baba yangu ambaye ana miaka karibu themanini na kitu hivi na hajawahi kuvaa nguo nyingine zaidi ya hizo angekuja hapa leo halafu akaambiwa hawezi kuniona kwa sababu hajavaa hilo vazi lingine kwa kweli ni mbaya sana. Naomba unipe mwongozo na ninajua Watanzania wengi wana mavazi ya asili kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tena nilikuwa naangalia Kanuni hapa kuhusu masuala ya mavazi kwa Wabunge, mavazi ya kimila yanatajwa hapa, vazi la mwambao, suti za heshima za kiafrika na nguo za kimasai ni suti vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Naomba kabla hujakaa utupitishe kwenye Kanuni ipi hasa iliyovunjwa.

**MHE. EDWARD K. OLELEKAITA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni Kanuni za kuendesha shughuli za Bunge hapa, hakuna Kanuni *specific* kwa sababu haihusiani na mambo ya ndani hapa. Hata hivyo, kwa kuwa ni suala mahsusi tu la Watanzania wale ambao wametuleta hapa nikasema niombe mwongozo wako ili Watanzania wale waliotuleta hapa wafahamu namna ya kutembelea Bunge lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sote tunajua, kwanza alilolitoa ni wazo zuri sana lakini tumejiwekea Kanuni za kuendesha mambo hapa. Swali ni kwamba wewe mwenyewe hapo ukija umevaa mavazi yale, je, utaruhusiwa kuingia ndani ya Bunge au hautaruhusiwa? Jibu lake ni lipi jamani?

**WABUNGE FULANI:** Huruhusiwi.

**SPIKA:** Basi kama hauruhusiwi na wengine nao hawaruhusiwi. Kama wewe mwenyewe huruhusiwi, je, watu wengine itakuwa taabu. Lengo si kubagua mavazi, hapana, ni kwamba taratibu tulizojiwekea zinasema tu kwa ujumla wake kwamba Mtanzania yeyote anayeingia hapa atavaa mavazi ya heshima na imeyaorodhesha, haimaanishi yale mengine siyo ya heshima.

Kwa hiyo, hii ni changamoto kwetu sote kuziangalia tena Kanuni zetu kuona inakuwaje katika mazingira hayo. Mavazi ya Pwani yameruhusiwa kufuatana na Kanuni zetu, lakini yameruhusiwa yawe kamili, yaani mtu avae kibarakashia, kanzu, koti asije na kanzu tu haina koti na avae makubazi, siyo avae kitu cha kufunga kamba au vinginevyo, maana yake hatakuwa amevaa soksi na kadhalika, yaani mavazi yetu yako namna hiyo. Sasa na vazi la kimila la aina hii kwa mfano ya Kimasai, nalo tulitazame ikiwezekana lakini nalo tulielezee vizuri, linapokuwa kamili linafananaje ili liwe katika utaratibu. Lile vazi basi labda na mkanda wake na je na fimbo ile, maana ili likamilike lazima liwe na fimbo na ile nanihii yake ile, ili tuelewane maana tunataka vazi kamili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa tumelipokea kama changamoto lakini tunaomba radhi kwa ambaye amepata shida hiyo. Muhimu kwa Wabunge wote kwa wapiga kura wetu, kwa sasa waje tu wamevaa haya mavazi ambayo yanakubalika mpaka hapo tutakapoziangalia tena Kanuni zetu kuweza kuona tu-*accommodate* vazi lipi na lipi. Ni *very embarrassing* kweli anavyoeleza, kabisa na mimi naelewa unachozungumza lakini kwa sasa tuendane tu na Kanuni yetu ile ya 160(2)(b) ambayo inazungumzia mavazi kwa Wabunge na ime-*describe* aina ya mavazi.

Kuna wakati fulani Wizara ya Habari walijaribu kutafuta linaloitwa Vazi la Kitanzania, lakini hawakufika mwisho wa zoezi. Ilikuwa ndiyo watushauri kwamba wageni wetu wengi wanaokuja waje na vazi la aina hiyo, labda shati

la kitenge hivi au nini, lakini zoezi hilo halikufika mwisho, Watanzania hawakukubaliana hasa Vazi la Kitanzania. Unajua wenzetu wa Nigeria na Ghana wana mashuka yao yale na nini au nchi nyingine wanavaa kanzu wanaume. Wanawake ndiyo shida, kwenye mavazi ni taabu kwa sababu wao wana mavazi ya aina nyingi sana. Kwa hiyo imekuwa taabu kidogo namna ya kuya-*regulate* lakini watu wetu magetini wanajitahidi, hasa kwenye ufupi, tunasisitiza zaidi nguo iwe ndefu kadri inavyowezekana na isiwe ya kubana kihivyo na hasa *jeans* tunazi-*discourage* sana. Hata mwananchi wako akija amepiga *jeans* hapa hataingia humu ndani. Wageni wangu mimi huwa wanarudishwa hukohuko.

Wakati fulani mama Makinda alipokuwa Spika hapa alikuja binti yake mmoja basi baadaye sana wakamruhusu na haikuwa siku ya Bunge. Sasa nimeingia ofisini kwa Mama Makinda nakuta binti mmoja analia, nikauliza huyu analilia nini? Akaniambia binti yangu huyu walimzuia huko, si unaona kisuruali chake. Sasa yeye binti wa chuo kikuu anajiona yuko sawasawa, lakini hapa ni uwanja tofauti, amekuja na kibanio wakamwambia hiki huingii humu ndani na yeye mama yake Spika, sasa akawa haelewi ni nini hii. Ikabidi tumuelimishe pale, siku nyingine ukija na nguo kama hii hapo getini hukatizi. Ukijua tu unakwenda Bungeni basi utafute mavazi ambayo hayatakuwa na maswali ya kuingia Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala, mjadala ni mzuri, tumeuanzisha vizuri, tupitie Mpango na tusome taarifa ya Kamati ya Bajeti. Nawapongeza sana Kamati ya Bajeti kwa kuona kama mradi wa Bandari ya Bagamoyo nao unaweza akafikiriwa. *(Makofi)*

Mimi nilisema wakati ule kwamba nimewahi kusafiri, ilikuwa safari ya mambo ya Kibunge ili twende katika mambo ya Bunge mtandao. Nilipokwenda kule nikakutana na ile bodi yenyewe, kwa bahati mbaya tu na nilikuwa na Wabunge wenzangu, *they presented a very convincing presentation.* Mkinipa nafasi Waziri wa Fedha nakumbuka, hata zile hoja zote zile viongozi wetu hawawi-*briefed* sawasawa, kunakuwa na watu wanawadanganya viongozi, kabisa. Sasa kiongozi

akishasema mnanyamaza wote maana ameshasema lakini unaona kabisa amekuwa *misled* hapa na hapa. Sasa ni vizuri vitu kama hivi vikakaa vizuri.

Nakumbuka kitu kimoja ambacho wale wazee waliokuwepo kwenye bodi walisema. *China Merchant is a huge company* na ni kampuni ya Serikali siyo kampuni binafsi, ni Shirika la Umma kule na lina uchumi mkubwa mno na wana-*run* bandari kadhaa kule China na duniani. Yule *chief* akasema neno moja, yule mkubwa wao, akasema Tanzania ni marafiki zetu sana na tunafanya mradi huu tukijua kwamba Watanzania ni marafiki zetu sana.

Hata hivyo, sasa hivi tuko katika dunia ya biashara, kwenye bodi hii wazee tunazidi kupungua tumebaki kama watatu, wanne ambao tunaijua Tanzania, wanazidi kuja vijana ambao hawaijui Tanzania, ndiyo maana sisi wazee hii *project* sisi tumeisimamia sana kabla hatuja-*phase out*, sisi tuki-*phase out you will not get this project* kwa sababu sisi ni watu wazima tunaelewa.

Kwa hiyo, kama hao watu wazima bado wapo, tujaribu ku-*take advantage.* Wao wakiondoka hata ufanyeje ule mradi utakuwa umekufa, huwezi kuupata, *it's not easy.* Unapokuwa na fursa ama uitumie hapo vinginevyo ikipotea inakuwa taabu. Kwa hiyo, nashukuru wameliona nalo wamelipendekeza. Ni kulitazama tu, endapo zile hoja bado ni za msingi tuache lakini endapo ni jambo jema tuendelee nalo.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni ya leo.

*(Saa 07.12 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2021/2022 – 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, ninayo majina hapa ya Wabunge walioomba kuchangia, tutaanza na Mheshimiwa Joseph George Kakunda atafatiwa na Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Fedha na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa uwasilishaji wao mzuri leo asubuhi, kwa kweli mbinu waliyotumia kuwasilisha imefanya mpango wetu uweze kueleweka sio kwetu sisi Wabunge bali hata kwa wananchi, kwa hiyo, kwa niaba ya watu wa Sikonge nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na niseme tu kwamba kwa niaba ya watu wa Sikonge nimeupokea Mpango uliowasilishwa leo asubuhi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa mikono miwili na kwa matumaini makubwa. Thatimini ambayo ameitoa hapa ya utekelezaji wa mpango uliopita unatoa matumaini kwamba Mpango huu wa Tatu utakuwa na mafanikio makubwa zaidi na nina sababu mbili za kusema hivyo. Sababu yangu ya kwanza ni kwamba utekelezaji wa mpango uliopita katika maeneo mawili hasa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza, eneo la huduma za jamii, elimu, afya, maji kwa kweli tunahitaji kuipongeza sana Serikali na kuipa heko kubwa kwa mafanikio

makubwa yaliyopatikana kwenye eneo la huduma za jamii. Eneo la pili ambalo limetengezwa vizuri sana ni eneo la miundombinu kwa ajili ya kuhudumia uchumi, eneo la barabara, madaraja makubwa, vivuko, reli, umeme hasa umeme vijijini, maji, viwanja vya ndege na bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo hayo yalionesha mfano mkubwa, safi kabisa na ni mfano wa kuigwa kwa Serikali nyingi katika Bara la Afrika kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma. Maendeleo tuliyoyapata kwenye eneo la miundombinu, kwenye maeneo hayo niliyoyataja yamefanya Tanzania iwe sehemu muhimu, nzuri ambayo inawavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Mazingira ni mazuri, kwa hiyo kutokana na mafanikio ya hivyo nashauri Serikali ni vema tuendelee kusimamia vizuri utekelezaji kwenye maeneo yote hayo ili tuendelee kuwa bora zaidi na hayo ni maeneo ya vipaumbele vya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya *CAG* ya juzi kwa kweli inanifanya niiombe Serikali kupitia Waziri Mkuu na viongozi wote wa Serikali kwenye Wizara mbalimbali naomba sana taarifa ya *CAG* muipitie kwa kina ninyi ndugu zetu mliopo Serikalini ili muweze kuchukua hatua stahiki, sio hatua za kukurupuka hapana, hatua stahiki kwa kila aliyehusika na ubadhirifu ili tunapoenda kwenye kutekeleza mpango mpya tupate mafanikio makubwa kwa niaba ya wananchi wetu na kila mwananchi aweze kufurahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mimi natangaza rasmi kwamba Halmashauri yangu ya Wilaya ya Sikonge ni miongoni mwa Halmashauri ambazo zimepata Hati Chafu, hili mimi binafsi kama Mbunge wa Sikonge nawaambia wananchi wa Sikonge sijalifurahia na niomba mamlaka zinazohusika ziweze kufuatilia ili tusiwe na mambo kama hayo katika siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni na maeneo matano ya kushauri; eneo la kwanza, kwenye viashiria vya Taifa vya Uchumi kuna kitu kinaitwa mfumuko wa bei au *inflation.* Mimi ni mtaalam wa uchumi tena sio mtalaam wa hivi hivi, ni

mbobezi kabisa kwenye eneo hilo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha anafahamu, hii habari ya kukaa tunatamba kama Taifa hapa unajua *inflation* yetu ni 3.5% sio kitu cha kujivunia sana, tunatakiwa kweli kuwa *single digit,* lakini ni *single digit* ambayo inasogelea 10% ili kuweza kuchochea faida za muda mfupi na faida za muda wa kati za wawekezaji na kwenye eneo la biashara, hii kuweka 3.5% na chini ya hapo ni kuufanya uchumi uwe *dormant,* sawa bei hazitabadilika sana, lakini je, uwekezaji? Je, biashara faida kwenye biashara itakuwaje?

Kwa hiyo namshauri Waziri wa Fedha awaambie watalaam wasiwe waoga sana kwenye *inflation* hasa hii *inflation* ambayo iko chini ya 5% sio nzuri sana kwa Taifa ambalo tumeshatengeneza mfumo mzuri wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili; tunapozungumzia viwanda unataja maelfu ya viwanda, kweli na mimi nilikuwa Waziri wa Viwanda wakati fulani, nataja mafanikio, tumeanzisha viwanda 50,000; mimi kwangu binafsi mafanikio ni kwenye eneo la ajira, tume-*create* ajira kiasi kwenye sekta ya viwanda, sio kutaja viwanda 50,000 hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa viashiria muhimu kabisa kwenye dira yetu ya Maendeleo ya Taifa tulisema kwamba ifikapo mwaka 2020 asilimia 40 ya ajira itatoka kwenye eneo la uzalishaji viwandani, kwa hiyo tunapotoa taarifa ya viwanda tulivyoanzisha lazima tuseme tumefikia hatua gani kwenye kufikia lengo la 40% ya ajira kwenye sekta ya viwanda, hilo ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo na ningependa kulishauri maeneo ya utawala bora. Dira ya Maendeleo ya Taifa ina nguzo nne; nguzo ya kwanza huduma za jamii, nguzo ya pili umoja wa kitaifa, amani na usalama, eneo la nguzo ya tatu ni nguzo ya utawala bora halafu nguzo ya nne ni eneo la kukuza uchumi ambapo tunakuta na mambo ya *infrastructure* na nini. Hiyo ni kengele ya kwanza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yote hayo manne lazima eneo la umoja wa kitaifa, eneo la usalama na amani ya nchi lazima tulihudumie vizuri, lakini vilevile eneo la utawala bora lazima nalo tulihudumie vizuri, kwenye eneo la utawala bora kuna *vi-section* kumi ambavyo nilikuwa nafikiria kwamba niwashauri wenzetu waweze kuviangalia na kuviongezea umuhimu katika bajeti na katika kuisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni ukaguzi na urakibu wa polisi. Tunazungumzia hapo utekelezaji wa Sheria Kuu ya Jinai na hii ni muhimu sana katika kulinda mali na usalama wa wananchi. Polisi naamini katika eneo hilo hawana bajeti ya kutosha. Lakini eneo la pili ni Ukaguzi wa, Ukaguzi wa ndio *risk manager* wa fedha tunazopeleka kule kwenye Halmashauri na kwenye Wizara. Kwa hiyo, Ukaguzi wa Ndani unatakiwa upawe kipaumbele cha juu sana. Halafu cha tatu ni Ukaguzi wa Nje naye *CAG* wakati mwingine anakuwa na hela kidogo, eneo la nne, Tume ya Kudumu ya Uchunguzi, eneo la tano, Tume na Sekretariat ya Maadili ya Viongozi, eneo la sita Usalama wa Taifa, hawa watu wa Usalama wa Taifa wakati mwingine wanakuwa na *informers* wengi kuliko hata wao wenyewe ambao wameajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nashauri wale *informers* ambao wana uzoefu wawachukue waajiri ili kusudi Idara ya Usalama wa Taifa iweze kufanya kazi zake vizuri zaidi *in a formalized manner.*

Mheshimiwa Naibu Spika, la saba ni TAKUKURU hata Mheshimiwa Rais juzi aliwaambia TAKUKURU zingatieni sheria iliyoanzishwa TAKUKURU katika kufanya kazi zenu, sasa walikuwa wanaingilia na maeneo mengine ambayo wao hawahusiki. Lazima tuwajengee uwezo, tuwape watumishi wa kutosha ili waendelee kupambana na ufisadi na mambo mengine ya ubadhirifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la nane Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu hii inafahamika. Eneo la tisa vyombo vya kusimamia utoaji wa haki na eneo la mwisho kujenga umahiri wa viongozi kwenye ngazi za chini. Naomba nimalizie

kwamba eneo hili la kujenga umahiri wa viongozi wa ngazi za chini kwa mfano Maafisa Watendaji wa Vijiji na Maafisa Watendaji wa Kata ni la muhimu zaidi kama tunataka tuendelee na vilevile kuwapa fedha *TARURA* nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kuunga mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** ahsante sana, Mheshimiwa Reuben Kwagilwa atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii ili niweze kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga ni taaluma, lakini kwa Taifa letu na kwa Serikali yetu kupanga si tatizo. Mpango huu tulionao ni mzuri sana kuliko mipango mingi sana ya nchi nyingi hapa Afrika, lakini shida tulionao sisi kwenye kupanga ni kutekeleza Mpango tuliouweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitaongelea mengi isipokuwa nataka nijielekeze eneo moja tu, la Mradi Mkubwa tulionao wa *Standard Gauge Railway,* tunayoijenga. *Standard Gauge Railway* tunayoijenga ukijumlisha tu zile njia kilometa zinazojengwa tunatakiwa tujenge kilometa 4,886, hapo naongelea njia tu, siongelei mahala ambapo reli zinapishana. Mpaka sasa tumeshajenga kipande cha Dar es Salaam kuja Morogoro kilometa 300 na tunaendelea na kipande cha Morogoro – Makutupora kilometa 422, lakini vilevile tuko upande ule mwingine wa Isaka na Mwanza kilometa 249.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa aina ya *financing* ya mradi huu tunavyoindesha tukiendelea nayo tutaujenga Mradi huu wa *Standard Gauge* kwa nchi nzima kwa miaka 81, miaka 81. Ikiwa miaka mitano tumejenga kilometa 300 ndio ambazo ziko *above* 90 *then* kilometa 4,886 tutazijenga

kwa miaka 81. Hii katika nchi ambayo inapambana kutafuta maendeleo ni kitu hakikubaliki, ni kitu hakikubaliki. Hivyo vipande nilivyo vitaja ambavyo vinajengwa vimetugharimu takriban trilioni 11. Trilioni 11 ni *Idle Investment* kwa sababu gani, kwa sababu hatutakamilisha leo ili tuanze kutumia mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokishauri Serikali yetu iondekane na habari ya *Traditional Methods* za *ku-finance* miradi hii mikubwa. Kwanza tunajipa *pressure* kama Serikali, ya *ku-finance* mradi huu halafu tunashindwa kupeleka huduma kwa wananchi ambazo ni za kila siku. Kwa hiyo ninachokishauri Wizara ya Fedha waangalie utaratibu wa *ku-finance* mradi huu *Infrastructure Bond.* Wamefanya hivyo nchi za wenzetu, ukienda Benin wamefanya, ukienda Tunisia wamefanya. Hii inatupa ahueni ya kutekeleza mradi huu na kuutekeleza kwa wakati. Tunapoendelea kutekeleza mradi huu hivi kidogo kidogo ni hasara kwa Taifa letu, ni vile tu *hatui-merge* hii hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa faida ya wasiofahamu na Watanzania kwa ujumla, tunatakiwa tuitoe reli itoke Dar es Salaam iende mpaka Tabora kwa kupitia Singida, ikifika Tabora iende Isaka Shinyanga mpaka Mwanza, ikitoka Tabora iende Keeza ili tukahudumie Kigali na Burundi, ikitoka hapo Tabora tuipeleke Kaliua kwa ndugu yangu hapa, iende Uvinza mpaka Kigoma tukaihudumie Kongo na tukitoka Kaliua tuje Mpanda mpaka Katema; hiyo ni Reli ya Kati tunayojenga. Bado kuna kipande cha Tanga, Musoma, Arusha kilometa takriban 1,233; na hapo hapo bado kuna kipande cha Mtwara – Mbambabei kilometa 10,092.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni kitu *serious* sana, hatuwezi tu kuendesha mradi huu kwa kutumia mapato ya ndani tutawaumiza Watanzania na tunajichelewesha wenyewe kupeleka maendeleo ambayo yanahusu huduma za moja kwa moja za wananchi za kila siku kama vile elimu na afya; na ndio maana kwa mwenendo huu wananchi wa Handeni mpaka sasa hatuja pata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa mradi huu kwa pamoja kutatusaidia sana kama Taifa kwanza kuifungua Bandari yetu ili iongeze mzigo unaopita pale. Kwa sasa hivi tunapitisha tani milioni 17 ukilinganisha na wenzetu wakenya wanapitisha pale Mombasa tani milioni 37. Kukamilika kwa pamoja na kwa wakati mmoja kutatusaidia sana kupata mapato kupitia mradi huu, kwa maana TRA wataweza kukusanya lakini vilevile wananchi wetu uchumi wao unataweza kuwa *activated.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jinsi tunavyojenga kwa vipande vipande hivi na kuchukua muda mrefu kuna maeneo ya nchi yetu yatabaki kuwa-*disadvantaged.* Kwa mfano kipande hiki cha Mbambabei – Mtwara kitabaki kuwa ni historia tu ikiwa hatutatekeleza mradi wa Liganga na Mchuchuma, *viability* ya hii reli hapa haipo. Vivyo hivyo kipande kile cha kutoka Tanga kwenda Arusha kwenda Musoma kama hatukuimarisha vile vipaumbele tulivyoweka ukanda ule ikiwemo *soda ash* pale *Lake Natron* hakuna *viability* ya mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo bomba linalotoka Uganda Hoima kuja Chongoleani Tanga. Kwa vyovyote vile mafuta yatakapofika Tanga yatahitaji reli hii hii kuyarudisha yakisha kuwa *refind.* Kwa hiyo Serikali ione umuhimu wa kwenda kukopa kwa kutumia *Infrastructure Bond* ili tutekeleze mradi huu kwa pamoja kwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo na baada ya kushauri hilo ni malizie kwa kusema; limezungumzwa hapa asubuhi kidogo lakini halikukaziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 ambayo *inatu-guide* kuanzia mwanzo tunapotengeneza bajeti mpaka tunapoitisha bajeti hapa Bungeni, lakini sheria tukishapitisha bajeti hapa wenzetu wa Serikali wanapokwenda kutekeleza bejeti hakuna Sheria ya *Monitoring* na *Evaluation.* Kwa maana hiyo tunamuomba hapa Waziri wa Sera Serikali yetu hapa walete Sera. Kwanza wao watunge Sera ya *Monitoring* na *Evaluation* ili wailete

hapa tuitungie sheria. Ndiyo maana ripoti hii ya *CAG* ambayo tunakwenda kuijadili ni aibu ni aibu ni aibu ni aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tusipofika mahala tukatunga sheria hiyo; huwezi; kwa mfano mradi wa bilioni 380 unaotekelezwa, wa maji kule Handeni, unaojengwa kutoa Maji Korogwe kuyaleta Handeni eti ukasimamiwe na Mtendaji wa Kata, usimamiwe na Diwani. Lazima tutunge sheria ikae vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mpango uliopo mezani, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi).*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mheshimiwa Athuman Almas Maige, ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano. Mpango huu wa Tatu wa Miaka Mitano unajengeka toka kwenye Mpango wa Pili wa Miaka Mitano ambao tumeukamilisha utekelezaji wake mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja katika mambo makubwa ambayo yamebebwa na Mpango huu, ni dhana ya kujenga misingi ya uchumi wa viwanda. Na hapa nitaweka mkazo, kujenga msingi wa uchumi wa viwanda. Maana yake nini, tuliamua, kwenye ujenzi huu wa uchumi wa viwanda au ujenzi huu wa msingi wa uchumi wa viwanda uzingatie viwanda vyenye sifa kubwa mbili. Sifa ya kwanza, viwanda vinavyotumia malighali ya ndani. Lakini sifa ya pili, ni viwanda ambavyo vitatoa huduma au vitakuwa na *impact* kwa watu wengi, kwa maana ya *critical mass*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapoongea viwanda vinavyogusa au viwanda ambavyo vitatumia malighafi ya ndani, moja katika eneo muhimu sana ambalo lingetupa malighafi ambayo sio tu yanakwenda kutengeneza viwanda

lakini nayo ni msingi wa viwanda ni chuma ya Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika huu ni karibu ni mwaka wa 20 au zaidi tunaongea kuhusu kwenda kuchimba chuma ya Liganga. Labda niseme mawili au matatu kuhusu hii Chuma ya Liganga. Kwanza inaambatana na uzalishaji wa umeme *megawatts* 600. *Megawatts* 600 ni robo ya umeme wote ambao tulikuwa nao mpaka mwaka 2015. Robo, yaani asilimia 25 sio mchango mdogo kwa uchumi wa Taifa letu. Kwa hiyo, ule mradi sio kitu kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, mradi wa Liganga na Mchuchuma unaenda kuzalisha *iron owl* chuma ngumu, tani milioni moja kwa mwaka. Sio jambo dogo, lakini sasa manufaa ya malighafi ya chuma ni makubwa sana kwa uchumi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chuma ya Liganga ingeweza kuzalisha viwanda vya nondo vya kutosha na vya kumwaga nchi hii, Chuma ya Liganga ingeweza kuzalisha viwanda vya mabati nchi hii, ingeweza kuzalisha viwanda vya baiskeli na vipuri vya magari vya kutosha kwa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jaribu kufikiria ni viwanda vingapi na vya aina ngapi vingeweza kuzaliwa kutokana na uchimbaji wa chuma ya Liganga na Mchuchuma ukiachilia mbali suala zima la ajira kwa watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo nyakati pia tujifunze kwenye mataifa mengine Marekani, waliamua kuchelewesha ujenzi wa reli ili kujenga uwezo wa ndani wa kuchimba chuma yao ili wajenge reli yao kwa kutumia chuma yao. Maana yake ndio soko la kwanza la chuma yao ilikuwa ujenzi wa reli yao. Sisi nasi tuna fursa kubwa kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye eneo hili nimuombe sana Waziri wa Fedha, Ndugu yangu Mheshimiwa

Dkt. Mwigulu Nchemba, arejee kwenye ajenda zetu tangu mwanzo huwezi kujenga uchumi wa viwanda Tanzania kama hutaki kwenda kuchimba chuma ya Liganga. Tutadanganyana, tutapiga kelele hapa, miaka itapita, nyakati zitabadilika na vizazi vijavyo vitatushangaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, tulivyosema tunataka tujenge viwanda ambavyo vitatumia malighafi ya ndani na vina *critical mass* tulisema viwanda ambavyo vita-*absolved* bidhaa na mazao ya wakulima kwa asilimia kubwa. Mambo niliyotarajia niyaone kwenye Mpango wa mwaka 2015/2016 – 2020/2021 moja nilitaka nione viwanda vingi vya kusindika mazao ya kilimo na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ametoa mifano ya viwanda lakini ukivipima kwa mizani, viwanda ambavyo vina *critical mass effect* ni vi chache sana ambavyo vinagusa mazao ya ngozi, vinagusa mazao ya kilimo. Mheshimiwa wa Wiziri wa Fedha ulikuwa kwenye Wizara ya Kilimo, unajua huwezi kukuza kilimo kama hutakuza viwanda vinavyosindika mazao ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nina aamini, wakati huu upele umempata mkunaji na mkunaji ndio Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ulikuwa kwenye sekta ya kilimo sasa upo kwenye Wizara ya Fedha peleka fedha kwenye kilimo, peleka fedha kwenye ku-*facilitate* kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kupata mapinduzi ya viwanda kama hutaki kuwekeza kwenye utafutaji wa masoko ndani na nje ya mipaka yetu ya Tanzania. Leo tunaongelea barabara za mipakani bado hazipitiki hazina lami, soko kubwa la Mazao ya mkoa wa Ruvuma tunategemea Msumbiji lakini tunatumia barabara ya vumbi. Hatuwezi kujenga uchumi kama hatutaki kutengeneza miundombinu ambayo itakuza biashara, itakuza viwanda. Na mimi naamini hii kengele ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo hoja tatu za haraka. Eneo la tatu, uwekezaji kwenye biashara unahitaji *facilitation* na hapa tuna mifano mingi sana leo, tunataka tuingie kwenye soko la Dunia lakini hatujaweka *mechanism* ya kutosha kuwawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kuweza ku-*meet* vigezo kwa maana ya *quality and quantity demands* za soko la nje, hatutaweza! Hatutaweza kufika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilizobaki nitazihifadhi lakini nilitaka niseme tunapotaka kubadilisha uchumi wa nchi yetu pia lazima tuwekeze kwenye diplomasia ya uchumi, lazima tuwe na mazuri na majirani zetu, lazima tuunganishe nguvu zetu za ndani na nje ili tulete mapinduzi ya uchumi kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara atafuatiwa na Mheshimiwa Athuman Almas Maige. Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuruku, kwanza niungane na wenzangu kutoa pole sana kwa Watanzania kwa msiba mkubwa uliotupata wa kuondokewa na aliyekuwa Rais wa Tanzania. Lakini pili, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais na Makamu wake kwa kuapishwa kuwa viongozi wa juu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye sekta ya elimu yenye vipengele vinne. Pamoja na ufundishaji na *outreach universities* pia ina kazi ya kufanya *research.* Azimio la *AU* inaitaka kila nchi itoe asilimia moja ya pato lake kwa mwaka kufadhili utafiti na maendeleo i.e *RMD*. Sasa kwa kufanya hivyo kutawezesha Vyuo Vikuu kufanya *research* na wakati mwingine tumelalamika kwamba havifanyi utafiti lakini inabidi Serikali ichangie asilimia ya pato hilo ili Vyuo Vikuu wafanye *research*. Mfano leo hii, kuna Chuo cha *MUST* wanafanya *action research* ya kutengeneza majokofu kwa

ajili ya kuhifadhi matunda kama walivyosema wenzangu. Matunda tunayo mengi sasa wao wanataka kutengeneza majokofu ili yahifadhi hayo matunda *throughout* na majokofu hayo yawe ya bei nafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali ikitoa mchango, mimi nafikiri kama mikoa Tanga, Tabora na Tunduru wanaweza wakahifadhi matunda *throughout the year* na wakafanya biashara na wananchi wetu wakapata kipato. Hivyo, hilo nimuombe sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Profesa Ndalichako waliangalie hilo, watoe ile asilimia moja ili kuwezesha au ku-*top-up* fedha ambazo zinahitajika kwa ajili ya kufanya *research. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili sasa hivi kuna upungufu mkubwa sana wa ajira, i.e *lecturers* na waendeshaji. Waziri Mheshimiwa Prof. Ndalichako analijua hilo kwamba Serikali ilikuwa na utaratibu zamani Vyuo Vikuu wanawabakiza pale vyuoni wanafunzi waliofanya vizuri sana wanakuwa ma-*TA, Tutorial Assistant*, halafu baadaye wanawajenga na kupeleka kuwasomesha wanakuwa baadaye *Assistant Lecturers* na baadaye wanakuwa *PHd.* Lakini leo hii utaratibu ule haupo, kwa hiyo, ndio maana tunapata shida katika kuwa na namba ya Wahazili wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali, irudishe utaratibu ule wa zamani wahazili wale wabobezi wanaweza kutambua wanafunzi wazuri sana wakawabakiza pale na baadaye wanawakuza na baadaye tunakuwa na Wahazili angalu wakutosha katika vyuo vyetu. Tukiwaacha waondoke, inavyotokea sasa, wale *best performance* wakiondoka wakatoka kipindi kile wanamaliza masomo yao hatuwezi kuwapata tena wanaenda huko nje na wanachukuliwa. Lakini palepale waka-*identify* na wanarusiwa kuwabakiza pale basi tutapungua hilo tatizo la Wahazili katika Vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, agizo la Baraza la Madaktari Afrika Mashariki, linawataka Vyuo Vikuu vyote vyenye

taaluma ya Sayansi na Tiba viwe na hospitali za kufundishia tunaziita *teaching hospitals.* Kwa mfano *UDOM* inatakiwa iwe *teaching hospital*, *MUHAS* iwe na *teaching hospital*, *UDSM* iwe na *teaching hospital* kwasababu wana ile taaluma ya Sayansi na Tiba. Serikali iruhusu hizo *teaching hospitals* wapewe hawa, wapewe na wanaweza kuziendesha wakati mwingine tumekuwa tunawasiwasi hawataweza kuziendesha mbona vyuo wanaweza kuviendesha. Kwa hiyo, na zile *teaching* hospitals kwanza zinaweza kufanya vizuri kabisa na hivyo ndivyo wanavyofanya wenzetu katika nchi nyingine zilizoendelea. Watoto wanatoka wanaenda pale wanakuwa na hospitali yao lakini *at the same time* ile hospitali yao ndio inakuwa kama wanafanya pale *practical's* na mara nyingi ndio zinafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Suala la mikopo wenzangu wengi hapa wamelizungumza, nishauri, kwasababu kumekuwa na malalamiko mengi na Waheshimiwa Wabunge hapa wengi sana wamefuatwa na wanafunzi kuombwa pesa. Taasisi zinaenda wanafunzi wanakuwa kama ombaomba, kama wanafunzi wote hao wanastahili kupata mikopo na tunashindwa kuwapa ile asilimia, tufanye hivi tupunguze asilimia ile ili kila mwanafunzi apate ile mikopo turudi badala ya asilimia 100 wote wapate *flat rate* ya asilimia 70 ili kusiwe na malalamiko, tukiendelea hivi kila siku na namba ya wanafunzi inaongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tufanye hivyo ili angalau wanafunzi wote wapate mikopo na wengi wanaokosa mikopo ni watoto wa maskini. Kwasababu watoto wote wanaokosa mikopo ni watoto wa maskini ndio waliokosa mikopo, kwasababu mtoto kama hapa wa Mheshimiwa Dkt. Ntara lazima nitajipigapiga hapa nitamlipia lakini wa wale wa maskini hawawezi, ndio maana wamekuja hapa Dodoma. Nina mzigo mzito hapa nitamkabidhi, mzigo mzito wanasema mpe Mnyamwezi, nitamkabidhi hayo majina Mheshimiwa Prof. Ndalichako abebane nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo hapo kuna lile suala la penati, watoto tumeshindwa kuwaajiri au ajira hizi tunazijua

hazipo. Mtoto anamaliza Chuo Kikuu ana kaa miaka sita unamwambia akipata ajira alipe penati, hilo mie naomba liondolewe kabisa. Yaani liondolewe, yaani hakuna ku-*discuss* sijui *percentage* nini, hili liondolewe hatuwatendei haki, sasa hivi wanahangaika wanajiajiri wenyewe, hii mikopo hata kidogo wanayopata watoto wote wanafanya *umachinga* badala ya kusoma sasa, hujikita kwenye kusoma, watoto wana vibanda vya chips, watoto wana pikipiki ndio maana unakuta sasa kunakuwa na vurugu tu. Ebu tuwasidie watoto tuwape asilimia inayofanana wote na baadaye wakimaliza mikopo hakuna mambo ya penati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza mambo ya penati, leo hii niwaambie kitu kingine ambacho kinasikitisha. Kuna wanafunzi wa Vyuo Vikuu wanaofanya *biomedical* wanapokwenda kufanya *field* wanadaiwa walipe pesa. Ni jambo linalosikitisha sana, wanaenda kufanya *field* wanaambiwa walipe pesa kwa kutumia vile vifaa wanavyovikuta pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sawasawa na mwanafunzi ambaye anakwenda *teaching practice* anafika pale kwenye shule anaambiwa wewe umekuja kufundisha hapa, enhee! utulipe pesa, anakwenda pale kutoa huduma halafu anaambiwa alipe. Hilo nalo naomba muliangalia Mheshimiwa Waziri wa Elimu pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Afya. Tunahitaji Watoto hawa waende *field* wakafanye kazi, mikopo wamekosa halafu mnamdai tena pesa, hilo naomba mliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. (Makofi)Napenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, Mheshimiwa Waziri nadhani amekusikia hapa, nadhani muangalie vizuri vile vigezo kwasababu kwa kweli kuna watoto ambao wanatoka familia za maskini kabisa na hawapati mikopo. Na ninyi ni mashahidi Wabunge kila wakati wanahangaika na hivyo vikaratasi, mtoto amekosa mkopo!

Mtoto amekosa mkopo. Muangalie namna Watoto wote wanaostahili mkopo wapewe mkopo, hoja ya wote hilo ni suala lingine pengine Wabunge wote wangeondolewa kwenye orodha ya watoto wao kupewa mikopo lakini watoto wa maskini wapewe mikopo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na uchangia lakini tunao wageni hapa, niwalete kwenu wageni waliopo bungeni mchana huu. Tunao wageni 48 wa kwangu ambao ni *Master of Ceremonies* kutoka jukwaa la Kisima cha Maarifa yaani *KCM,* Tanzania wakiongozwa na Ndugu Braiceson Mkena ambaye ni muasisi wa chama hicho na Ndugu Ester Richard Kimweri ambaye ni Mwenyekiti. Karibuni sana, karibuni sana, hawa ni Ma-*MC* jamani wanatoka kwenye maneo yenu huko hata kwangu wapo. Wanaotoka huko wanatuboreshea sherehe zetu, karibuni sana. *(Makofi)*

Naona wamependeza kabisa kuashiria kwamba hiyo ni kazi rasmi jamani iheshimiwe kabisa, kazi ya wasema chochote kwenye sherehe zetu. Karibuni sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mchangiaji wetu anayefuata Mheshimiwa Athuman Almas Maige atafutiwa na Mheshimiwa Hamis Tabasam. Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kuniruhusu nichangie hoja hii ya mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Miaka Mitano ya nchi yetu. Na nitajikita katika maeneo matatu, maji, kilimo, uvuvi na la nne elimu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji tumeiona kwenye taarifa hapa kwenye Mpango mzima kwamba imekamilika mingi lakini mingi bado haijakamilika. Lipo tatizo kubwa, miradi mikubwa imefanywa lakini baadaye inaharibika, hali hii ni kwasababu kubwa moja tu, mradi kwa mfano wa Ziwa Victoria umegharibu karibu shilingi bilioni 617 halafu baadaye umekabidhiwa kwa *CBOs* wa uendeshe.

Hauna fundi, hauna mtaalam yeyote na miradi mingine kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na Chuo cha Ufundi wa Maji pale Dar es Salaam, lakini bahati mbaya chuo kile kimetelekezwa na ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Serikali na Wizara ya Maji, Chuo kile kifufuliwe ili kifanye kazi iliyokusudiwa. Kutengeneza mitambo ya maji, tumeshaacha mambo ya visima sana lakini miradi mikubwa ya maji haiwezi kukabidhiwa kwa watu ambao hawajui ufundi wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani tukajenga shule, tukawakabidhi watu ambao sio walimu, haiwezekani tukajenga zahanati tusiwakabidhi madaktari n.k. Hata barabara tunajenga tunawakabidhi wahandisi kuitengeneza. Miradi mikubwa ya maji iliyokamilika mingi yake haifanyi kazi kwasababu haina wataalam wakuendesha mitambo ile ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kumekuwa na matatizo makubwa sana, tunasema maji yako vijijini asilimia 85 lakini sijui wanapima pimaje kwasababu kuna sehemu nyingine maji hakuna kabisa, hakuna, wanasema asilimia 85 au 75. Nafikiri upimaji wa upatikanaji wa maji wa vijijini na mijini pia uangaliwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la kilimo ambalo nilisema nitaligusia. Tanzania nzima tunalima kilimo cha kudra ya Mwenyezi Mungu, yaani mvua inyeshe na isiponyesha hatupati; ukame ukija hatupati. tuachane na suaLa hilo la kizamani. Duniani kilimo kikubwa kinachokusudiwa kuleta tija ni kilimo cha umwagiliaji. Pale kwetu Tabora kuna mbuga kubwa na maji mengi, mvua ikinyesha tunakazana kujenga madaraja maji yapite. Hatuyazuii yale maji yakawa mabwawa ya kumwagilia, tumekazana kufungua madaraja makubwa maji yapite, yaende wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hapa Dar es Salaam, tunafungua daraja lile la Magomeni pale maji yapite yaende

baharini. Maji yale yangeweza kutumika kwa umwagiliaji mkubwa sana. Kwa hiyo, kilimo hiki cha kudra ya Mwenyezi Mungu hakiwezi kutuvusha. Tunataka kilimo kile ambacho kitaleta tija kwa kupima. Tuna maji haya, ekari hizi tutazalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ya Kilimo sasa ijikite katika umwagiliaji. Mbuga kubwa kubwa zilizopo hapa zimejaa maji, baadaye maji yanakauka na jua, yanapotea wakati tungeweza kuzalishia chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uvuvi. Nchi yetu imezungukwa na mabwawa, maziwa na bahari, lakini hatupati chochote kikubwa kinachoweza kuingizwa kwenye uchumi wa nchi kutokana na samaki. Pia, ufugaji wa Samaki; nimetembea, nimeangalia huko na huko, tunajaribu hapa na pale, lakini pia hata wavuvi wenyewe wanaotakiwa kuvua samaki wanatungiwa sheria ngumu sana, wavue samaki usiku tu, wasivue samaki mchana, wavue samaki kwenye maji machache yenye mita fulani mengi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia liko tatizo la kuwekeza katika uvuvi wa samaki. Tulikuwa na meli na Shirika letu la *TAFICO*, likauzwa na bahati mbaya sana likauzwa kwa watu ambao hawakuwa na tija na nchi yetu hii na hilo Shirika likafa. Wakati linakufa lilikuwa linaingiza mabilioni. Sasa ndilo kiungo peke yake; katika bajeti hii nimeona kwamba kuna meli zinanunuliwa kwa ajili ya kufufua uvuvi. Meli tano zitakuwa Tanzania Bara na nne zitakwenda Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, meli hizi kiungo chake kiwe Shirika la *TAFICO* ambalo lilikuwa na wataalam wazuri, lilikuwa na taaluma na mitambo mizuri, yaani majengo yake. Majengo yameshaoza na kadhalika. Naomba sana Serikali ionyeshe umuhimu wa uvuvi ili tupate hela kutokana na uvuvi unaoitwa uchumi wa bluu. La sivyo, tunakuwa tunasema, wenzetu wanafaidika. Meli kubwa kubwa zinavua tu na kule, zinaondoka nao. Sisi tumekalia; tutauza hili, tutauza hili. Naomba sana ndugu zangu, Waziri wa Uvuvi na Mifugo

ajitahidi sana kuleta tija katika uvuvi ili Serikali ipate mapato ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu. Waziri wa Elimu naona atanichoka maana nimekuwa nasema. Elimu yetu iendane na Sera yetu ya Viwanda na Biashara. Tunataka kukuza viwanda; viwanda haviwezi kuendelea bila kuwa na mafundi. Mtu ananunua mashine mpya analeta hapa nchini, halafu baadaye zinakufa, hakuna mafundi. Zamani tulikuwa tukileta mafundi kutoka nje. Sasa kila mtu anashangaa, shule zote hizi, vyuo vyote hivi, kimetokea nini? Limetokea tatizo dogo tu, tumejenga *gap* kati ya Wahandisi ambao ni *white colors* na wale walioko chini *ma-artisan.* Wanaofanya kazi ni hawa *FTC technicians*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu iandae upya sera itakayowarudisha Mafundi Sanifu au Fundi Sadifu ili waunganishwe na mafundi *Artisan* au Fundi Mchundo na Wahandisi. Sasa hivi nchi hii inazalisha Wahandisi wengi ambao sio Watendaji kazi, ni wafikiriaji, wanataaluma kuliko watendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niko kwenye sekta binafsi na ninaajiri mafundi. Ukichukua mafundi kutoka Chuo Kikuu na Vyuo vingine, wako juu, lazima umpe na Idara maana ni Mkuu wa Idara. Watu gani watafanya kazi viwandani huku chini? Utamtuma nani? Ukimtuma mtu wa chini kabisa, vitu havielewi. *FTC* hapa hawapo. Chuo cha Ufundi *(Technical College)* kilikuwa ni *branch* ya *TFC.* Rudisheni hiyo ndiyo itatupeleka kwenye viwanda. La sivyo, viwanda vitazorota vile vile. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililiakuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua kengele ya kwanza hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya nayasema yananisumbua sana. Sisi huko, waajiri tunapata taabu kuajiri

watoto wanaotoka shuleni hapa Tanzania. Unamweka wapi? Matokeo yake tumekuwa tunafungua kampuni tunaleta maombi ya kuajiri *skilled people* kutoka nje. Wenzetu kule nje wameendeleza *polytechnic* ambayo inasuka watoto wote kuanzia *engineer, FTC* na *artisans.* Sasa hili linatupa taabu sana. Nawaombeni sana, niseme namna gani sijui mnielewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wa Elimu nifikirie. Usifikirie ulikotoka wewe, *form one, form five, form six*, chuo kikuu. Hiyo ni linle moja tu. Kuna line nyingine inaanzia *Technical School*, *Technical Secondary School*, *Technical College,* ina-*produce engineers,* watendaji kazi. Mwifikirie hiyo ambayo ilifutwa, irudishwe tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala lingine muhimu sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia, juzi ameligusa, anasema Kiswahili tunafundisha kama lugha. Mimi nilimwelewa sana. Lugha ya kufundishia iwe Kiswahili, kwa sababu watoto tunafundisha darasa la kwanza mpaka la saba, Kiswahili; halafu tunabadilisha kinakuwa Kiingereza, lakini kuna kitengo fulani cha Walimu wanafundishwa Kiswahili Chuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mchanganyiko wa kufundisha watoto wetu haueleweki. Wanafika vyuoni kule wanaanza kujifunza lugha kwanza Kiingereza ndipo waanze kujifunza masomo. Tunawakata elimu mara mbili; kujifunza lugha na kujifunza taaluma. Tunapoteza muda nusu nusu, kama wamekaa miaka mitano au minne shuleni, walikuwa miaka miwili wanajifunza lugha. Wote duniani hakuna mtu aliyeendelea kwa kutumia lugha ya mwenzake. Lugha ya mama ndiyo inayomfanya mtoto aelewe. Vinginevyo watoto hawaelewi shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshatoa mifano mingi sana hapa kwamba, elimu na lugha ni vitu viwili tofauti. Tunasema, mtoto anaongea Kiingereza kama maji, kasoma sana yule! Hajui hata mbili kuongeza mbili, ila anaongea Kiingereza kama maji. Ni tofauti na mtoto ambaye hajui

chochote katika lugha; anajua kujumlisha hesabu, anajua maarifa. Tutofautishe kati ya maarifa na lugha. Bado naahidi na bado nina nia ya kuleta hoja yangu binafsi Bungeni humu ya kutaka Kiswahili iwe lugha ya kufundishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa Mheshimiwa Maige, wakati unachangia umesema *cocktail,* halafu ukasema mchanganyiko. Sasa kuna wakati mnatuambia tena *cocktail* ni mchapalo, sasa tena wewe mtaalam wa Kiswahili unatuchanganya kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Hamis Tabasam atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na Mheshimiwa Kuchauka ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema naomba nichangie Mpango wa Maendeleo uliowasilishwa kwetu leo na Mheshimiwa Mwingulu Nchemba, Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango wake aliowasilisha leo sijaona mahali ambapo amezungumzia habari ya zao la pamba. Zao la pamba katika nchi hii linalimwa zaidi ya mikoa 14 na pamba hiyo unayoiona ina uwezo wa kuwa na viwanda vitano. Angalia uchumi mkubwa unaotokana na pamba; pamba ikizalishwa vizuri na ikatafutiwa bei, Serikali ikawekeza katika pamba; na Serikali ilivyojitoa katika kuwekeza katika pamba, wakaachiwa mabepari, zao hili litakuwa limekufa. Kwa nini? Limekufa kwa kupata bei ndogo. Mabepari wameshusha bei. Tusiite wawekezaji, kwa sababu kwenye pamba kule kuna mabepari, zao la pamba likawa limekufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaiambia Serikali, katika Mpango wake wa miaka mitano, wanafanyaje kulifufua zao la pamba? Serikali ikiwekeza katika zao hili,

tutapata viwanda vya pamba, viwanda vya nyuzi, viwanda vya nguo, viwanda vya vyakula vya kuku na mifugo na tutapata mafuta. Haya mafuta ambayo leo mnayaagiza kutoka Malaysia na kwingineko, mnalazimisha mafuta, mafuta, yako kwenye pamba. Huko kote, hizi ni kodi utapata Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Bahati nzuri wewe unatoka kwenye Jimbo ambalo pamba inalimwa. Hebu waonee huruma wananchi wa Iramba, Sengerema wakiwemo na wananchi wengine Tanzania nzima. Njoo na mpango wa pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika pamba ninachotaka kueleza, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba utapata kodi, leta sheria tu hapa. Badala ya pamba kutozwa ushuru, njooni na Sheria hapa mchukue hata *VAT* asilimia kumi na pamba muipe bei ya shilingi 2,000/=. Ekari moja ya pamba ina uwezo wa kutoa tani moja ya pamba. Sasa kama kuna mtu anapata shilingi milioni mbili katika pamba na Serikali ikachukua kodi ya asilimia 10, mkachukua shilingi 200,000/= kwa ekari moja, mikoa inayolima 14: Je, utakuwa na shida gani tena ya pesa hapa Mheshimiwa Mwigulu? Hii miradi yako yote itaisha. Treni ya mwendokasi, sijui kuna Bwawa la Nyerere na la wapi, sisi walimaji wa pamba tu tunatosha kutengeneza kodi ya kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, kuna suala la Ziwa Victoria, kule ukianzia juu; Tarime kule, ukaenda moja kwa moja mpaka kule Misheni mwisho kabisa, Kanyigo, kuna wananchi wanaokaa mwambao wa Ziwa, hawajatumikishwa katika kilimo cha *irrigation.* Sisi tukimwagilia, sasa hivi umeme upo, tukopesheni mashine za kumwagilia, wananchi wetu wana uwezo wa kuzalisha kiwango kikubwa cha mazao. Mnataka uchumi gani kama huu uchumi tunauachia wazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwa mfano, kwenye Jimbo langu tu la Sengerema pale, kuna mradi wa maji wa shilingi bilioni 23, unadaiwa deni la umeme la shilingi milioni 300. Umeme unakatwa, mradi wa shilingi bilioni 23 unateswa na shilingi milioni 300. Sasa tunashangaa, hawa ndio

wawekezaji? Ndio Watanzania wanaotaka uchumi wa bluu? Unaandaa mradi wa shilingi bilioni 23 na una deni la shilingi milioni 300, halafu ule mradi unakaa haufanyi kazi, unadaiwa shilingi milioni 300! Ni maajabu makubwa sana katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliangalie sana hili suala katika miradi kama hii. Huu ni mradi mmoja tu wa Sengerema, sijui miradi mingine inayoteswa na vijipesa vidogo kama hivi kwa uwekezaji mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la uvuvi. Kule katika uvuvi tuna matatizo makubwa. Sheria za Uvuvi zilizoko kule katika Ziwa Victoria na hatujui Maziwa mengine huko; leo kuna samaki ambao ni wadogo hawakui. Kuna furu, kuna vimote na samaki wa aina nyingi; barara, hizi ni lugha za kienyeji kule. Wao wanajua hawa samaki hawakui, lakini wanakamatwa nao wale Samaki, nyavu zinachomwa moto. Mlikuwa na Kiwanda cha Nyavu, fufueni kiwanda hicho halafu mtengeneze nyavu zinazotakiwa na Serikali, lakini mkiwaacha waagizaji wakaleta nyavu, matokeo yake mnakwenda kuzichoma moto, mnatengeneza umasikini katika Ziwa Victoria. Liangalieni sana hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyozungumza tunakwenda kufunga mradi. Mgodi wa Buzwagi unafungwa. Sengerema kuna wawekezaji katika Mgodi wa Nyanzaga wameomba kufungua Mgodi wa Nyanzaga; leo ni mwaka wa nne toka mwaka 2017, mnataka wawekezaji gani? Huu mradi unakuja kuzalisha pesa. Uwekezaji wake tu wa kuandaa ule mgodi una shilingi trilioni moja, leo mnataka wawekezaji gani? Kwa sababu tu ule mradi unatakiwa kukua Sengerema watu hawautaki, halafu wanataka kuita wawekezaji. Waje wawekezaji gani wakati wengine mnawakataa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha aangalie katika Mpango wake wa miaka mitano,

tunahitaji Mgodi wa Nyanzaga Sengerema ufunguliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kuna suala kubwa sana hapa tunalozungumzia la utengenezaji wa barabara. Hizi barabara unazoziona zinakwenda kwa wananchi, ambazo zinatengenezwa na *TARURA,* nilifikiria sana kwa nini *TARURA* isirudi ujenzi? Hata hivyo, naangalia kazi waliyonayo watu wa ujenzi; ukiangalia miradi aliyonayo *TANROAD* na bado ukamwongezee tena mradi mwingine wa *TARURA*, sishauri *TARURA* ihame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana Mheshimiwa *TARURA* ibakie mahali pake, lakini kuna pesa ziko hapa. Nilizungumza hapa siku moja nikawaambieni, jamani kuna pesa za *TARURA,* kuna pesa ziko kwenye ukokotoaji wa mafuta, wanakokotoa watu wa *EWURA.* Shilingi 90/= kila siku ya Mungu wanakusanya katika huu ukokotoaji, hizi fedha zinakwenda kutumika vibaya. Shilingi 1,080,000,000/=. Ukichukua pesa hizi Mheshimiwa Mwigulu, kwa mwezi ni shilingi 32,400,000,000/=; kwa mwaka kunakuwa na fedha hapa zaidi ya shilingi bilioni karibu 400 ambazo zinakwenda kwenye hizi tozo ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa walioweka tozo, wote wako kwenye bajeti. Mnakwendaje kuweka kwenye tozo la mafuta? Kule kuna *import duty,* kuna *import levy* pale, kuna *petrol levy* pale; mnakwenda kuweka hivi vitu vingine vya nini? Hii fedha ileteni *TARURA* tutengeneze barabara zetu. Tunazo Halmashauri za Miji. Halmashauri za Miji tunazo 21, Halmashauri za Wilaya tunazo 137, tunazo Manispaa 20 na Majiji sita, kwa nini *TARURA* haongezewi fedha hapa za kufanyia kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwa Mheshimiwa Mwigulu juzi nimepita barabara ya Ndago, nimepita Shelui kuzungukia Ndago, hata yeye hana barabara. Nitashangaa sana kama Mheshimiwa Mwigulu hata wewe hutakubali *TARURA* iongezewe fedha. Hutarudi 2025. Haya maneno nakwambia kabisa, usidhani hatutarudi sisi tu, hata ninyi

Mawaziri mtakomea ndani huko huko. Tengenezeni pale *TARURA,* ipeni pesa za kutosha tutengeneze barabara zetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wewe hapo hutarudi kama barabara hizi hazitatengenezwa. Msidhani kwamba hili ni suala ni la Tabasam pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nafikiri *message* imekwenda. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam huu utabiri wako huu! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Ndiyo. Hili ni hatari! *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam,

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, angalia dakika zangu lakini.

**NAIBU SPIKA:** Subiri kwanza Mheshimiwa Tabasam, subiri kidogo.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu humu ndani ni *Senator* na mimi nataka kwanza kumkaribia kidogo, lakini sasa wewe ni mgeni kabisa, ukitutabiria sisi kutokurudi humu ndani, nahisi hali yako wewe ni mbaya zaidi kuliko ya kwetu. *(Kicheko/Makofi)*

Endelea Mheshimiwa, karibu.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kukwambia, *TARURA* ni janga la Kitaifa. *TARURA,* yaani kama ingekuwa nchi nyingine tungekuwa tuna mjadala wa Kitaifa tufanyeje kuhusu *TARURA*?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuwaambieni jamani, Waheshimiwa Wabunge humu ndani, nimewaelezeni kwamba fedha ziko kwenye mafuta. Nikawaambia kwamba, nilimwambia hapa Mheshimiwa Spika, tukae tujadili hili jambo, kuna fedha kule sisi tuwaonyeshe. Hii Habari ya kuwa tu bei za mafuta zinapanda kila mwezi, bado hatuna manufaa nazo hizi fedha, kodi yetu iko pale pale, hili ni jambo ambalo kwenda kwenye uwekezaji, kama Serikali haiwezi kuagiza mafuta yake, ninachotaka kukuambia Mheshimiwa Mwigulu, utatwanga maji kwenye kinu. Haitawezekana nchi yoyote inayotaka uchumi wake isipoweka fedha kwenye kuagiza mafuta yake. Tegemeeni wafanyabiashara waje wawatengenezee nchi, hili jambo halipo hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo nchi marafiki nyingi, hili suala la mafuta; tunalo eneo letu la *TIPER* pale. Lile eneo amepewa mwekezaji ambapo hakuna hata faida yoyote. Tungeenda kutengeneza matenki tukawa na *reserve* kubwa pale ya lita hata bilioni mbili. Leo mafuta yanakuja kupanda bei katika Soko la Dunia, sisi tunaweza tuka-*stabilize* pale tukabakia salama. Endeleeni kuudharau huu ushauri ninaowapeni, kwa sababu unatolewa na mtu wa Darasa la Saba katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana. Mimi nimewasilisha. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasamu, Kiti kinakulinda, usiwe na wasiwasi. Humu ndani ni kujua kusoma na kuandika. Pia kuna mtu ameniletea hapa kikaratasi, hajaandika jina lake anasema, Waheshimiwa Wabunge wakati mnaendelea na michango, wageni waliotangazwa hapa leo ma-*MC,* kwa sababu mimi nimesema kazi rasmi, kwa hiyo kinaweza kuwa ni kimojawapo ya chanzo kipya cha kodi. *(Kicheko)*

Sijui ni nani ameleta hiki kikaratasi, lakini Waheshimiwa Wabunge tutakapofika huko msiwachaji nyingi, wana kazi ngumu sana hawa. Wana kazi ngumu.

Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Abbas Tarimba ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona na napenda kwanza nimshukuru sana na nimpongeze Waziri wa Fedha na timu yake pamoja na Kamati ya Bajeti kwa namna ambavyo wamewasilisha Mpango huu. Natumaini wote imetufurahisha. Nataka nianze kwa kusema kwamba naunga hoja yake mkono, japokuwa nitakuwa na maoni mawili au matatu ili kuweza kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme hivi kwamba kusema ukweli kwanza tunawapongeza pia Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuweza kutuwekea uchumi wetu kwenye hali ya utulivu. Tunajua kwamba ukuaji umekuwa mzuri sana, hata wakati huu wa *covid,* lakini pia mfumuko wa bei uko chini, uko vizuri, japokuwa namuunga mwenzangu mkono aliyezungumza kwamba pengine asilimia tatu ni ndogo sana, inatunyima fursa fulani ya kuweza kukuza zaidi kwa kuipa Sekta Binafsi na wale wanaouza, nafasi ya kuona faida watakayopata wakiendelea kuzalisha Zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeona kwamba hali ya deni la Taifa ni himilivu. Pili, tunaona pia kwamba thamani ya shilingi yetu iko vizuri na pia tuna *International Reserves* ambazo ni nzuri. Hiyo ina maana kwamba ni *strength* kubwa sana ambayo tunaweza tukaitumia tukafanya *assessment* ya nchi yetu kwa athari ya wawekezaji na hivyo tukaanza kukopa kwa riba ya chini sana. Riba ya asilimia tano au sita unaweza ukapata kwa mfumo huo wa *infrastructure bond* au pia kwa kukopa moja kwa moja kwa *direct placement* ya *bond* yetu kwa wale wanaotaka kuwekeza Tanzania kwa sababu Tanzania imekaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwamba hakuna sababu ya kuchelewesha utekelezaji wa miradi elekezi. Hii miradi tunasema ya vielelezo kama *SGR* na mradi wa umeme wa Mwalimu Nyerere wakati tunaweza

tukakopa, tukahamasisha na tukafanya haraka haraka tukaanza kuona matunda kutokana na miradi hii mikubwa ambayo itatoa chachu katika ukuaji wa Taifa letu. Nataka niseme kwamba tutumie hiyo kama fursa, kama ni *strength* na hiyo *strength* tuweze kuitumia kuweza kufanya mchakato huo wa kuweza kwenda kwenye soko la Kimataifa na kukopa na tusizingatie sana kukopa ndani kwa sababu tukikopa ndani maana yake tunai-*crowd out private sector.* Watu binafsi hawawezi kwenda nje kwa sababu hawajulikani, lakini Serikali inajulikana kwa sababu ni Serikali na Serikali *is as good as gold.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini tukihamasika sisi Serikali tukakopa nje, tukaacha *resources* za ndani zinakopwa zaidi na watu binafsi, kwanza riba zitakuwa chini. Sasa hivi tuliambiwa kwamba riba nashangaa kwamba licha ya vigezo hivi vizuri vya uchumi, riba bado ziko kwenye asilimia 15. Nimekutana na watu wa *BOT* walituambia kwamba kwa sababu tunakopesha Serikali kwa asilimia 15, sio kweli! Serikali inalipa asilimia 15 kwa *bond* ya muda kati ya miaka 15 na 20, lakini Benki zinakopesha mikopo ya mwaka mmoja mpaka miwili sanasana pengine ni michache sana kwa miaka zaidi ya hapo. Sasa wakikopesha kwa asilimia 15 ni kubwa sana ambapo Serikali ikikopa kwa kipindi hicho kifupi riba inakuwa ni kwenye asilimia chini ya 10. Kwa hiyo unaona kwamba kuna uwezekano wa kushusha hizi riba kwa kuwezesha Sekta Binafsi kukopa zaidi na hivyo kuwezesha Sekta Binafsi kuwekeza na tukaona matokeo ya Mpango wetu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kitu kimoja ambacho nimekisikiliza hapa. Tunafanya mambo kimazoea mazoea sana, yaani tatizo la sisi Waafrika pengine ni kwamba tunaanza kuzalisha halafu ndiyo tunatafuta soko. Kumbe uzalishaji unatakiwa uanze sokoni, unatafuta soko liko wapi. Ukishaona soko liko wapi na bei zake zikoje, ndiyo unasema sasa niki-*incur* au nikitumia gharama hizi kuzalisha nitapata faida, lakini mtu anazalisha ndizi heka 20 halafu zimeshaiva, anasema anatafuta soko liko wapi, hamna soko lolote namna

hilo, huwezi kupata na mtu akijua unazo ndizi zinaoza anakupa bei ya chee! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tujifunze kufanya biashara kitofauti kwanza tufanye utafiti tujue kwamba ni kitu gani kinauzika wapi. Tunapoendelea kulima, tunazungumzia mazao haya ya asili siku zote, pamba, kahawa, tumbaku. Hivi tumeshajiuliza ni wapi masoko haya yakoje duniani kwa sasa hivi? Bei za huko mbele za kahawa zinaenda wapi, bei za tumbaku zinadidimia na tunaendelea kusema tumbaku na kadhalika. Ukweli tukifanya tathmini sahihi tukajua kwamba ni kitu gani cha kuzalisha hapa kwetu, sio lazima iwe ni mazao haya tunayoona, tumeona kwamba tulivyowaambia Wachaga kule kwamba hawa jamaa wenzetu wa Kyela wanalima *avocado* halafu wanapata kilo moja shilingi 1,500; kila mtu anatafuta mbegu ya *avocado,* huna haja ya kumtafutia mbolea, anatafuta mwenyewe kwa sababu anajua kwamba ina faida kulima *avocado.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa na taarifa hizo lakini ukweli ni kwamba taarifa hizi hazimfikii mkulima, tunakaa na hizo taarifa, hujui kwamba unaweza sasa badala ya kulima kahawa ukalima *avocado,* kwa nini? Ukiendelea kulima kahawa kwenye ule udongo wa kule kwetu umeshakwisha kabisa kwa sababu umelima kahawa miaka 40 au 50, kwa hiyo hauna tena rutuba na hauna tija. Kwa sababu hauna tija badilisha uzalishe linguine, baada ya muda mwingine unaweza ukarudia tena kahawa na ndiyo mambo ya *crop rotation,* wale wanaojua mambo ya kilimo. Kwa hiyo naweza kusema kwamba pengine kuna haja ya kusema kwamba ni eneo lipi nibadilishe zao lile, kama kule Uchagani kahawa haiendi tena, pengine twende upande wa *avocado* na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine pia unaona kwamba unatumia gharama nyingi kwa sababu ule udongo unatakiwa ufanye *rotation,* uzalishe kitu kingine. Naamini kwamba tunaposema tutafutiane masoko, cha kwanza ni hizo taarifa na hizo taarifa sasa hivi ni kielektroniki, tufungamanishe masoko yetu. Mtu hajui kwamba kama nina

ndizi, Mbeya wananunua namna gani ndizi, Moshi wananunua namna gani, Nairobi wananunua namna gani kwa kutumia hizi *gadgets* zetu za mawasiliano hizi ambazo zinatupa bei kila mahali duniani *virtually* unaweza ukajua kila kitu kinauzwa namna gani. Kwa hiyo watu watajua bei zake na sio lazima ukutanishe mtu *physically,* unaweza ukakutanisha watu kwa mawasiliano haya tuliyonayo na hiyo ni bei nafuu ya kukutanisha watu, ni bei nafuu ya kumpa mtu tija ya kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hivi, mimi nafikiri kwamba katika huu Mpango wetu, suala zima la ushirikishi, kujenga uchumi shirikishi na uchumi shindani. *Issue* iliyopo ni kwamba tutafanyaje vijana hawa wapate ajira na hawawezi kupata ajira bila kujiajiri wenyewe sasa hivi kwa sababu watu ni wengi ambao hawana ajira na hawataki kuingia kwenye kilimo kwa sababu kilimo hakina tija na kwa sababu hawajafundishwa namna ya kulima kwa tija au kwa faida. Kwa hiyo naomba hivi, kwamba pengine umefika muda sasa tujaribu kutengeneza mfumo wa kuwa-*organize* vijana kwenye vikundi na kuwaonesha namna gani ya kutengeneza mashamba yenye tija, kutengeneza viwanda vidogo vidogo vyenye tija na mtu asifikirie kwamba kiwanda ni kiwanda cha Mchuchuma, hapana. Tena sasa hivi hata kuzungumza mambo ya chuma ni kitu tofauti kidogo kwa sababu dunia haiendi kwenye mambo haya, inaenda kwenye *software* zaidi sasa hivi, kwa hiyo Sekta ya Huduma ndiyo itakuja kuwa ni sekta muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Huduma maana yake ni sekta ya kuhudumia viwanda, kwa sababu ukiwa na kiwanda lazima kihudumiwe, *maintenance* na kadhalika. Sasa kama wewe unakimbizana tu hiki unasahau kule, haitawezekana, lazima tuingize fedha, lakini ili vijana waweze kufanya hivyo wanahitaji mtaji, mtaji unatokana na nini? Tunasema tutawapa vimikopo vidogo dogo kwenye halmashauri, haina kitu hiyo! Tuunde ile Mifuko ya Serikali ambayo imetawanyika kila mahali, tuunde *National Credit Guarantee Scheme or Fund* au kuwe na misingi ya kibiashara lakini nafuu ambayo itakuwa imewekwa na Serikali ili watu

wanaotaka mikopo wanajua tunaenda pale ambapo kutakuwa na kitengo cha wakulima, vijana, vinakaa mahali Pamoja. Pia unaweza uka-*leverage* ile *guarantee scheme* ikazalisha maradufu kwa sababu kama *default rate* kwa mkopo, hiyo iliyotoka kwa vijana pengine ni *only ten percent* ina maana kwamba ukiwa na mkopo wa ku-*guarantee* watu 100 unazidisha mara 10, uta-*guarantee* watu mara 10 yaani kiasi cha fedha mara 10. Sasa hivi unatumia kile unam-*guarantee* mtu mmoja ambapo tunaweza tukapeleka kwenye *guarantee fund* tukawapa watu wakaendesha kibiashara, tukaweza kuwezesha watu kupata mikopo kwa wingi na mitaji kwa wingi kwa muda mrefu na muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, mimi ni muumini wa masuala ya kwamba, kilimo cha sasa hivi ni lazima kibadilike na kubadilika kwa kilimo hicho ni lazima tusifanye mambo ya mazoea, tujaribu kuona ni kitu gani kitaoteshwa wapi na wakulima wapewe taarifa za masoko ambayo ni sahihi. Kwa kumalizia niseme hivi, ili tuweze kuongeza lile fungu la kukopesha au kuwezesha watu kupata mitaji, lazima tuunde *National Credit Guarantee Fund or Corporation* ambayo itashughulika na Mifuko yote na ile fedha inakaa mahali pamoja na inatumika kwa faida ya wengi. Hapa nataka kukuhakikishia kwamba inaweza ikawa ni kubwa kuliko Benki zote hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Abbas Tarimba na Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango huu wa Miaka Mitatu wa Taifa letu. Kwanza, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye upande wa miudnombinu. Ni ukweli usiopingika kwamba nchi yetu imeamua kuingia kwenye nchi ya viwanda. Ili tuweze kulifikia lengo hili la kuwa nchi ya viwanda, matarajio yetu makubwa tunategemea kupata

malighafi kutoka mashambani. Vile vile, sera ya nchi yetu sasa hivi tuko kwenye kuunganisha mikoa yetu kwa miundombinu ya barabara za lami. Tumeshamaliza baadhi ya mikoa, lakini bado mikoa mingine haijafikiwa. Ni ukweli vile vile tunahitaji kujenga barabara za kiulinzi, lakini ziko vile vile barabara za kuunganisha za kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshafikiria kwamba ili mazao yetu yaweze kufika kwenye hivyo viwanda tunavyokusudia kuvijenga, ni lazima tuhakikishe kule ambako mazao haya yanazalishwa tumepeleka hizo barabara kuwezesha mazao haya kufika kwenye soko au kwenye viwanda. Kwa mfano, ni ukweli usiopingika zao la korosho kwa Mkoa wa Lindi na Mtwara lina mchango mkubwa sana kwenye pato la Taifa, lakini kwenye Mikoa hiyo hiyo ya Lindi na Mtwara ndiyo mikoa ambayo haifikiki kwa barabara za lami kwenye wilaya zake karibu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi mmoja una miaka zaidi ya mitano sasa wa barabara ya kimkakati wa Kanda ya Kusini, barabara inayotoka Mtwara – Newala – Tandahimba – Masasi - Nachingwea mpaka Liwale. Huu wote unaozungumziwa ni ukanda wa korosho, ndiyo maana mwaka huu tumepata shida sana watu wa korosho kwa sababu mpaka imefika masika korosho bado hazijatoka kwa wakulima kwa sababu hakuna barabara ya kuzifikisha maghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba kama kweli Serikali inadhamiria kufufua viwanda au kwenda kwenye uchumi wa viwanda lazima tuhakikishe tunayo miundombinu rafiki ya ufufuaji wa viwanda, lakini kama barabara zetu zitabaki kuwa hivi zilivyo, tukategemea kwamba mazao ya wakulima yatafika kwenye masoko au yatafika kwenye viwanda, hapa tutakuwa tunachezeana kiakili. Naomba sana, ufufuaji wa viwanda lazima uende sambamba na ujenzi wa miundombinu. Kweli Taifa letu liko kwenye hatua ya kuunganisha mikoa lakini bado naomba tuingie sasa kwenye barabara zinazounganisha wilaya zetu, hata basi barabara zinazounganisha wilaya zetu na mikoa

yetu ili tuone tija ya wakulima. Wakulima wengi wanateseka hawapati pembejeo kwa wakati, hawapati *infrastructure* yoyote, lakini hata pale wanapojitahidi kulima, mazao yao yanaharibikia mashambani, wanashindwa kuyafikisha kwenye masoko. Jambo hili ni lazima Mheshimiwa Mwigulu alipeleke pamoja kuungamanisha miundombinu na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba nizungumzie huko huko kwenye miundombinu. Fedha nyingi za Serikali tunazipeleka kwenye halmashauri, tunakwenda kujenga hospitali kwenye wilaya zetu na vituo vya afya, tunajenga madarasa na mabweni shuleni, lakini hizi fedha tunazipeleka kwenye halmashauri ambako hakuna wataalam. Tulipounda *TARURA* tuliondoa wahandisi wote tukawapeleka *TARURA,* leo kwenye halmashauri zetu hazina wahandisi, hakuna wakadiriaji majengo. Tunapeleka bilioni 1.5 kwa ajili ya kujenga hospitali ya wilaya, kule unakopeleka yuko Mkurugenzi na watendaji wengine, hakuna mhandisi, nini kinatokea?

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotokea ni kwamba, mahali ambapo mkadiriaji wa majengo akikadiria jengo ili kuezeka bati hamsini anaandika bati 200, zinaenda kununuliwa bati 200 zinakuwa pale jengo limeisha, bati zimebaki, fedha zimeisha. Au jengo lingine ambalo lilitakiwa kuezekwa kwa bati 50 ananunua bati 25, fedha zimeisha, jengo halijaezekwa. Huwezi kumchukulia hatua, hana taaluma hiyo, yuko pale, anafanyaje? Mkurugenzi yuko pale, Mhasibu yuko pale lakini hakuna Mkadiriaji Majengo. Unamchukulia hatua gani huyu mtu ambaye hujamuajiri kwa kwa kazi hiyo? Pangekuwa na Mhandisi pale angeweza kuwajibika, lakini hatuna Wahandisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiondoka hapo, tunayo kada ya wakandarasi. Kwa sababu tumeshaamini kwamba ujenzi kwa *force account* ni rahisi zaidi kuliko wakandarasi, sasa tumeua hii kada ya ufundi. Naomba jambo hili basi liende sambamba na mitaala yetu ya elimu, wanaendelea kuzalisha wataalam kule wa ujenzi, wakati huku hawawahitaji kuna faida gani? Wakandarasi peke yao ambao wanabaki

kidogo ambao tunasema tunataka kulea wakandarasi wazawa, waliobaki ni walioko kwenye barabara tu na ni wachache sana, tena hawana hata mitaji na wala hawafikirii kupata mitaji, lakini wale wakandarasi wa majengo hawana kazi tena nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Elimu waondoe hiyo taaluma kwenye vyuo vyetu, hawana kazi! Sisi tumeshaamua kwamba Mwalimu Mkuu ndiyo atasimamia jengo letu, tumeshaamini Mkurugenzi ndiyo atasimamia jengo, tunaamini kwamba *DMO* ndiyo atasimamia jengo letu, hawa wengine hatuwahitaji! Ndiyo maana tangu tumeunda taaluma mpaka leo hii kwenye halmashauri nyingi hatuna Wahandisi, uongo au ukweli? Naomba sana tulifikirie hilo kwamba tunapeleka fedha nyingi halmashauri, lakini hazina wasimamizi na tutawahukumu kweli lakini tunawahukumu isivyo halali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la uwekezaji. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, amelizungumza suala hili la uwekezaji vizuri sana, lakini naomba nitoe tahadhari kwa nyie mliopata mamlaka. Hiki kitu cha uwekezaji kiko *very delicate.* Nimemsikia Mheshimiwa Rais amesema tusiwabughudhi wawekezaji na naunga mkono, tupunguze urasimu kwa wawekezaji lakini tuwe makini. Haiwezekani kazi ambazo Watanzania wanahangaika nazo kila siku wakizitafuta waende wakagawie wawekezaji eti tu kwa sababu tukimkatalia kuajiri ataondoka. Tuwe makini sana hapo. Tusipoangalia ni mwanya mwingine wa kupoteza ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri mimi nimedumu kwenye Sekta Binafsi zaidi ya miaka 30, najua kinachoendelea kule. Wapo watu wana vyeti vya *expert,* wana vibali vya ma-*expert* lakini ni wasimamizi tu wa kupakia mizigo kwenye malori. Wapo watu wana kada ya *expert* kazi yao ni madereva tu wa kuendesha viberenge mle ndani, kupaki paki mizigo kwenye *godown,* lakini ukiangalia cheti chake, huyo ni *expert.* Muda wa miaka miwili ukiisha, anaombewa tena kibali. Tuwe makini kwenye nafasi hiyo, tunahitaji

wawekezaji, tunawahitaji sana na wafungue milango na wawe rafiki wa wawekezaji, lakini kwa umakini mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo niliomba niyachangie kwa leo. Naomba kabla hujanipigia kengele, hayo hayo mawili, matatu yatoshe kwa leo. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka, lakini hoja ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alivyoeleza kuhusu wawekezaji nia haikuwa kusema mwekezaji aje na kila mtu, lakini huwezi kumzuia mwekezaji anayeleta fedha zake hapa akisema anakuja na watu kwa kiwango kile tulichosema sisi kisheria ukamwambia usije kwa sababu ninao Watanzania. Hilo ndilo ambalo alikuwa amelisisitiza sana kwamba lazima tulitazame vizuri; kama anakuja na watu wake wawili aje nao wawili, wapeni vibali kwa sababu anakuja na hela zake na wale ndiyo anaowaamini yeye. *(Makofi)*

Nadhani hoja hiyo ni ya msingi, lakini pia kwa ujumla wake hakuna mwekezaji anakuja na wale wawili halafu atakaanao haohao, tuangalie sisi idadi yetu anawachukua wangapi kule. Maana tusikazane tu kuangalia yeye kaja na wangapi, yeye anaajiri wangapi hapa? Kama ameshaajiri 200 na yeye anao wawili tu, wewe unamnyima wa nini wa kwake hao wawili? Si ndiyo anaowataka yeye na hela yake kaja nayo? Au anataka watano, unamkatalia wa nini watano wakati yeye hela kaleta na Watanzania kachukua zaidi ya hao watano? *(Makofi)*

Nafikiri ni muhimu kuyapima haya yote ili tuweze kusonga mbele. Tusiwazuie hawa watu kuleta hela zao nchini, tunazihitaji, lakini wakati huohuo tusiwafanye wa kwetu labda wakawa na hali mbaya wale ambao wana vigezo sawa, kama amewaajiri hao na wenyewe awalipe sawasawa. Nadhani sheria zetu ziko vizuri na kama kuna changamoto mahali hapa ndiyo mahali pake pa kufanya hayo marekebisho. Nilitaka niseme hilo ili tuwe tumemuelewa vizuri Mheshimiwa Rais na lengo lake kuhusu uwekezaji. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Abbas Tarimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo ajiandae.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ili niweze kuchangia hoja ambayo Yanga mwenzangu ameileta ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa kwa miaka mitano hadi mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja hii na nina sababu kadhaa za kuunga mkono na wakati huohuo kuleta mapendekezo ambayo naamini kabisa kwa namna moja au nyingine yataweza kuboresha Mpango huu ambao leo tunaujadili. Nitaanza na hii dhana ya Serikali Sikivu. Mpango wowote ambao Serikali inaubuni ni lazima isikilize maoni kutoka kwa wachangiaji, hasa kutoka kwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Serikali Sikivi imeoneshwa vizuri sana na Mheshimiwa Rais Samia naamini kwa kusikiliza mchango tuliokuwa tunautoa mwezi wa pili. Tulizungumza kuhusu ufanyaji kazi wa *TRA* na jinsi gani *TRA* inavyotukosesha mapato pale ambapo taratibu za ukusanyaji wa mapato zinavyokuwa sio sahihi. Vilevile tukazungumza suala la baadhi ya biashara kufungwa kutokana na ugumu wa ufanyaji kazi, Mheshimiwa Rais alichukua hatua za haraka sana. Naomba tumpongeze Mheshimiwa Samia kwa kusikiliza, hii ndiyo maana thabiti kabisa unapozungumzia Serikali Sikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeonesha mwelekeo mpya huko nje *business community* imekuwa na imani kubwa sana na Serikali. Nina imani kabisa kutokana na imani ambayo inajengwa sasa wasaidizi wa Mheshimiwa Rais akiwemo ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu Mchemba atasikiliza vizuri hoja zetu ambazo tunazileta uzichuje, zisaidie huu Mpango ili uwe bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala zima la maendeleo, nataka nimuangalie Mheshimiwa Hayati Julius

Nyerere ambaye aliwahi kuzungumza na akatoa kauli ni nini maana ya maendeleo. Hili limekuwa likizungumzwa pia na Waheshimiwa Wabunge katika Mabunge mengi yaliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Nyerere anasema: "Maendeleo hayawezi yakawa maendeleo kama sio *people centred*." Maendeleo lazima yaguse watu ndipo yatakuwa ni maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haina maana vitu sio sehemu ya maendeleo, hapana, vitu ni sehemu ya maendeleo, lakini lazima i-*translate* na ishuke chini kwa mwananchi mmoja-mmoja. Hapo ndipo panapotuletea maelezo ama swali, je, Mpango huu unamgusa vipi mwananchi wa kawaida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani tuangalie hapo kwamba, Mpango huu lazima uwe na vielelezo vinavyopelekea mwananchi wa kawaida kusema naam, Serikali inakuja na mpango ambao utanigusa mimi, yule na mwisho jumuiya nzima ya Watanzania watafaidika na mpango huu. Yote haya ambayo tunayasema yanaelekea katika maeneo mazima ya uhuru wa watu kuweza kufanya biashara zao, kufanya kilimo chao katika nchi yao, kupata mazao ambayo wanaweza wakayapeleka nje wakaenda kuyauza. Hata utawala wa kisheria kwa sababu, kuna wakati tulilalamika sana hapa yale ambayo yanapangwa katika sheria nayo hayatekelezwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwepo na mjadala mkubwa sana, sitaki nirudie huko, mjadala ambao ndugu yangu msemaji wa mwisho alizungumzia wa korosho ule uliumiza watu wengi sana. Turudi katika utawala ule ambao tumejiwekea sheria zetu na zile sheria tuzifuate. Naamini kwa muelekeo ambao umeoneshwa na Mheshimiwa Rais ni dhahiri kabisa haya sasa yanakwenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Serikali imezungumza mambo mengi sana humu ndani, lakini Mpango huu lazima uwe ni unaotekelezeka. Tunataka Serikali

itakavyokuja kufanya majumuisho itueleze ni namna gani imejitayarisha kuhakikisha kwamba inaitumia sekta binafsi ambayo ndiyo itakuwa ni moja kati ya wabia wakubwa katika Mpango huu. Ukiangalia *numbers* zinaonesha shilingi trilioni 40.6 zitatoka katika mchango wa sekta binafsi, lakini hata ule mchango wa Serikali wa shilingi trilioni 74.2 mchango ule utategemea vilevile sekta binafsi, Serikali haifanyi biashara. Ili *74.2 trillion shillings* ziweze kukusanywa lazima *business community* hapa sasa iweze kuangaliwa na kuwa *natured* vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, napenda nione kwamba, mchango wa Serikali katika kuhakikisha kwamba *business community* inalelewa vizuri uweze kuelekeza vizuri zaidi na Mheshimiwa Waziri aje kutuambia maana kuna kitu kimoja mimi kimenitia moyo, lakini kimenisononesha. Tuna watu wazuri sana katika nchi hii katika mawazo mema ya kufanya biashara na hapa nimpongeze Mpinzani wangu Mohamed Dewji ambaye tumesikia ameteuliwa na Rais wa *South Africa* kuwa ni mmoja kati ya watu ambao watamshauri. Sasa kama tuna mtu kama yule ndani ya Tanzania ambaye wenzetu wanamuona, sisi tunawatumiaje watu kama hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndipo sasa naiomba Serikali na napendekeza kwamba ni wakati umefika sasa Serikali ikaunda angalau timu ya wataalamu pamoja na wafanyabiashara mashuhuri, wakiwemo watu kama Mohamed Dewji, watueleze tufanyeje ili tuweze kufanikiwa zaidi katika suala zima la uwekezaji katika nchi yetu. Tuangalie tu, tusemeni kweli, Kamati ya Bajeti inazungumzia kwamba haijaridhika kuona kwamba Tanzania ni nchi ambayo si nyepesi ya kufanya biashara na wakatoa *numbers* wakasema tuko nafasi ya 141. Hata Mpango ule unaomalizika sasa ulikuwa unajitahidi kuifanya Tanzania iwe ndani ya nchi 100 katika wepesi wa kufanya biashara, lakini hatukufika huko. Ni vikwazo gani vilivyosababisha Tanzania isiweze kuingia katika zile nchi 100 zenye wepesi wa kufanya biashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Serikali itakapokuja Mheshimiwa Dkt. Mwigulu atueleze ni vitu gani ambavyo watavifanya kuhakikisha Tanzania inakuwa ni moja kati ya nchi ambazo ni *easy to do business,* ili wawekezaji waweze kuvutika na wakaja. Kwa sababu bila wawekezaji ukweli ni kwamba tutapata maendeleo, lakini yatachelewa na tusingependa kuchelewa. Mkumbuke Rais wetu aliyepita, Hayati Mheshimiwa Magufuli, aliisababisha Tanzania kwa haraka zaidi kuingia katika Uchumi wa Chini wa Kati, miaka mitano kabla. Naamini kabisa Mheshimiwa Suluhu Hassan atatusogeza mbele zaidi ya pale ambapo Mheshimiwa Hayati Magufuli ameacha, kama mipango hii mizuri ambayo imewekwa itaweza kutekelezwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda nizungumzie kuhusu ahadi za viongozi wetu wakuu. Wananchi wana imani sana na Serikali, wana imani sana na viongozi wao wakuu. Leo hii Wabunge tumekuwa tukilalamika sana tunazungumzia barabara za miaka mitatu, minne, mitano ambazo Mheshimiwa Rais alitoa ahadi. Sasa tusiende mahali tukafikia kwamba viongozi wetu wakitoa ahadi wananchi wa kawaida waseme, aah, haya ni kama yale yaliyopita, lazima tuyaangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu nampenda sana, kwa hiyo, napenda nione safari hii tunabadilisha mwelekeo, viongozi wakuu wakitoa ahadi zao wasaidizi wake wawe ni hodari wa kuzipokea na kuzifanyia kazi. Hatutataka tuje tukumbushie miaka mitatu iliyopita. Mheshimiwa Rais kama anayasikia haya nitaomba awape *support* ya kutosha Mawaziri wake katika suala kama hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemaliza na nilisema naunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Miaka Mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza sana kwa maana ya Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mchemba pamoja na ndugu yangu Mheshimiwa Masauni kwa namna walivyoweza kuwasilisha Mpango huu. Karibu yote nakubaliana nayo, lakini yako mambo ambayo nadhani nimeona kama hayajakaa vizuri sana na tunahitaji tuone namna bora zaidi ya kuyaweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, nchi yoyote ile mojawapo ya jukumu lake kubwa kushinda yote ni kuhakikisha kwamba watu wake wanapata ajira. Kwenye suala la ajira ninyi wote ni mashahidi, vijana wengi wanamaliza darasa la saba, kidato cha nne, vyuo vikuu na vyuo mbalimbali vya kati lakini ukija kwenye ajira ni tatizo. Kwa hiyo, lazima Mpango huu tunapoupanga ujielekeze namna gani utaendelea ku-*solve* tatizo la ajira katika nchi yetu ambalo kwa kusema kweli sasa hivi hilo ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia suala la ajira lazima tuangalie kilimo, viwanda, uvuvi na ufugaji. Labda leo mimi nichukulie mfano kwa pale Musoma; pale Musoma ni kwamba vijana wetu wengi hawana ajira kabisa kwa sababu viwanda vimekufa na vingine kwa bahati mbaya sana ninyi wenyewe Serikali ndiyo mnaviuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na kiwanda pale cha *MUTEX* na kilikuwa kinafanya kazi na bahati nzuri mwekezaji wake ni mkubwa ni huyu *Mohamed Enterprise,* lakini tulimnyang'anya kwamba ameshindwa kukiendesha vilivyo, tukasema tunampa mwekezaji mwingine. Mpaka leo hivi tunavyozungumza huu ni mwaka wa pili kile kiwanda kina makufuli, watu wetu hawana ajira na wako mtaani. Mimi niseme tu kwamba itakapofika wakati wa uwasilishaji wa bajeti ya Mheshimiwa Mwigulu, niseme ni mjukuu wangu, lakini nitalia na shilingi yake kama hatakuja na majibu kamili

ni kwa kiasi gani atatusaidia ku-*solve* tatizo la ajira kwa watu wetu wa Musoma, hasa kuhakikisha kwamba kile kiwanda cha *MUTEX* kinafunguliwa lakini sambamba na viwanda vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapozungumza kati ya mambo tunayohitaji kuyaangalia sana katika kuwasaidia watu wetu, nimezungumzia suala la mifugo, kilimo pamoja na uvuvi. Shida yetu kubwa ni kwamba kila leo hizi fedha zinazotengwa na Wizara badala ya kwenda kwenye ukulima zinaenda kwenye kilimo. Fedha zinapoenda kwenye kilimo hizo ndizo zinaishia kwenye zile mnaita *facilitation;* kununua magari, *computer* na kwenye mambo kama hayo. Tunategemea kwenye bajeti ya sasa fedha zielekee kule kwenye ukulima, kwa maana kwamba watu waweze kupata mabwawa ya kutosha kwa ajili ya *irrigation,* lakini waweze kupata pembejeo nzuri na zilizo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii unaingia kwenye duka la pembejeo za kilimo ziko bidhaa *fake* zinauzwa mle, matokeo yake ni kwamba mtu anakuja kunyunyizia vile viuatilifu vyote ni *fake.*

Kwa hiyo, yeye mwenyewe amehangaika halafu anarudi kupata hasara ya pili. Tunapozungumza suala la uvuvi ni kwamba fedha ziende kwa wale wavuvi wenyewe kwa kuhakikisha kwamba walau tunaweka mikakati ya kuona watu wanakuwa na uvuvi endelevu, unaoweza kusaidia watu. Mfano, vijana wetu wa pale Musoma wamesaidiwa vizimba vingapi ili waweze kupata ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unakuta vyakula vya samaki lakini yule mfugaji anaambiwa kwamba labda baada ya miezi sita yule samaki atakuwa amefikisha nusu kilo, matokeo yake anafuga mwaka mzima kutokana na chakula anachowalisha, lakini gramu 500 au nusu kilo wale samaki hawajafikisha. Shida kama hizo ni kwa sababu fedha haziendi kwenye uvuvi badala yake zinaenda tu katika usimamizi ambao hausaidii sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata unapozungumza suala la ufugaji, unakuta badala ya fedha kwenda kwa wafugaji ili wapate majosho, dawa bora, waweze kuwa na unenepeshaji mzuri matokeo yake ni kwamba hata dawa za mifugo nyingi ni *fake.* Haya yote ni baadhi ya mambo ambayo tunahitaji tuyaangalie na tuone kwamba ni kwa kiasi gani tunavyoweza kuwasaidia watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo tunapozungumzia viwanda, yawezekana tukawa tunaangalia tu vile viwanda vikubwa kama *MUTEX, MWATEX* na vinginevyo, lakini naamini kabisa kwamba tukilisaidia Shirika letu la *SIDO* ambalo ndilo linaloshughulika na viwanda vidogovidogo na bahati nzuri Baba wa Taifa aliliweka karibu katika kila mkoa, lingesaidia sana suala hili la viwanda. Kazi kubwa ya *SIDO* inafundisha habari ya usindikaji na *packaging.* Bidhaa nyingi hata tungeenda kwa wenzetu walioendelea kama China viwanda vyao ni vile vidogovidogo ambavyo kazi kubwa ni kusindika na *packaging,* wanaweka ile bidhaa yao katika hali nzuri ya kuvutia. Kwa kufanya hivyo basi ni rahisi watu wetu wakaweza kufanya biashara zao ndogondogo pasipokuwa na shida. Tatizo *SIDO* zetu zote zimekufa. Kumbe *SIDO* ingeweza kutoa mafunzo mbalimbali ambayo yangewasaidia sana watu wetu wa Musoma, lakini na watu wetu wa Tanzania kwa ujumla katika kuendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nadhani hili kwangu ni suala la ushauri, ni hili suala la *TRA.* Kama tunavyofahamu suala la *TRA* ni kweli wakati mwingine wanachukua fedha kwa nguvu na wananyanyasa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Hayati John Pombe Magufuli amelikemea sana suala hili lakini na juzi Mheshimiwa Mama Samia Suluhu naye amekuja amepigilia msumari wa mwisho kwamba kuwe na utaratibu mzuri wa ukusanyaji. Hata hivyo, kumbuka kuna bajeti ambayo tunategemea Waziri atatukusanyia, lengo ni shilingi trilioni mbili. Lengo la shilingi trilioni mbili si fedha ndogo, yaani unahitaji kwenda *extra mile* kuona namna ya kuweza kuzikusanya.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ushauri wangu, ili uweze kuweka *check and balance,* kwa maana ya kwamba wale *TRA* wafanye kazi yao, ushauri wangu ebu imarisha ile *Board of Appeal* iwe *active,* ifanya kazi ipasavyo. Ili *TRA* wanapombana yule mlipa kodi kama anaona ameonewa basi aweze kupata mahala pa kwenda, na majibu ya pale yakitoka haraka maana yake kama anadaiwa basi, maana siamini kama *TRA* anaweza kumuonea mtu halafu ukaenda na kule kwenye *Board of Appeal* na penyewe napo ukaonewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pale huwa kuna kakipengele, kwamba kama unataka kwenda huko kwenye *Board of Appeal* nadhani unapaswa kulipa *one third* ya kile ulichokadiriwa. Sasa, nimekadiriwa bilioni tatu, *one third* ($^{1}/_{3}$) maana yake nilipe *one billion* sina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunadhani kwamba hicho kipengele mkikiondoa hicho ili hata yule ambaye anadhani kwamba ameonewa aweze kusikilizwa katika ile *Board of Appeal,* na itakapokuwa *active* sasa itamsaidia sana katika kuhakikisha kwamba haki inatendeka, unapata kodi yako lakini na huko kwa mlipa kodi anapata haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo atafuatiwa na Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, Mheshimiwa Kunti Majala ajiandae.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia mpango huu wa maendeleo. Naomba nimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango kwa taarifa nzuri ya mpango huu wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitakuwa sijatenda haki kama sitachangia mawili matatu ambayo naona kuna umuhimu wa kuyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ambalo ni muhimu ni kwamba mpango huu wa maendeleo ni makakati wa kuendelea kuwaondoa wananchi wetu katika umaskini. Ni kweli mpango uliopita umeweza kutufikisha katika uchumi wa kati lakini uchumi huu bado umekosa tafsiri chanya katika maisha ya mtu mmoja mmoja, bado umebakia kwenye Takwimu. Kwa hiyo katika utekelezaji wa mpango huo wa maendeleo naomba uende ukatoe tafsiri chanya katika maisha ya mtu mmoja mmoja ili mabadiliko ya uchumi huu tuyaone kwa macho na si kwa takwimu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa kuliko yote mpango huu ni lazima ujikite katika ukuaji wa uchumi mpana na jumuishi wenye kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa na kuwanufaisha watu wengi hasa wanaoishi katika mazingira ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili jitihada za ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, ufufuaji wa bandari na meli kubwa kubwa na ndogo kwa kweli umeweza kuonyesha ni jinsi gani uchumi ambao tunataka uwe unakuwa jumuishi. Lakini reli hii ya mwendo kasi ambayo tunaijenga inaambatana pembezoni mwake na barabara ambayo inatumika kwa ajili ya ujenzi wa reli hii. Barabara hii imeweza kufikia vijiji vingi ambavyo awali kabla ujenzi wa reli hii vilikuwa havifikiki. Vijiji hivi ni muhimu sana katika uzalishaji wa bidhaa za mashambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Waziri wa Fedha na Mipango ashirikiane na Wizara nyingine kama za Ujenzi na Uchukuzi kuona barabara hii inaenda kuwa ya kudumu, kwasababu tukiiacha barabara hii tutakuwa tumepoteza kitu kikubwa na cha thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kutoka hapa Makutopora kwenda Kilosa ni pa fupi sana ukipita kwa barabara hii ya SGR ambapo awali ilikuwa uende mpaka Dumila. Lakini kutoka Kilosa kwenda Morogoro pamekuwa karibu sana kwa kutumia barabara hii, lakini miaka minne ya nyuma ulikuwa huweze kufikia baadhi ya vijiji hata kwa pikipiki

lakini kwasababu za ujenzi wa Reli hii vijiji vyote vinafikika, na unaweza kuona mabadiliko chanya katika maisha ya mtu mmoja mmoja katika vijiji hivi kwasababu ya uwepo wa barabara hizi ambazo lengo lake si kurahisisha usafiri wa wananchi ilikuwa ni ujenzi reli hii. Kwa hiyo tuiangalie barabara hii kwa jicho la kipekee kwa nia ya kubadilisha maisha ya wananchi wetu katika maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia hatuwezi kuepuka kilimo. Kilimo tunasema ni uti wa mgongo kilimo tunazungumzia kwamba ndiyo dhana ambayo inaweza kututoa katika umaskini, na kilimo ndicho kitu ambacho kinaajiri watu wengi kupita kiasi, lakini tuna changamoto ya masoko. Masoko haya ambayo tunayazungumzia mengine yanatokana na uzalishaji ambao hauzingatii mahitaji ya soko, lakini kuna maeneo ambayo kwa Sheria ama kwa taratibu ambazo tuliziweka ni kwamba zinamnyima fursa Mkulima kuwa na soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika Jimbo la Mikumi kilimo cha miwa ndio uti wa mgongo. Katika bonde lile kuna zaidi ya tani laki nne kila mwaka zinaharibikia mashambani kwasababu mnunuzi ni mmoja ambaye ame-*monopolize* soko la Miwa. Miwa hii ambayo inaharibika tunaweza tukai - *convert* kwenda kwenye tani 40 elfu za sukari ambazo ndizo tunazoagiza kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mzalishaji huyu ambaye alikuwa anapaswa kutafuta suluhisho la kudumu la wakulima hawa kuangalia jinsi gani anaenda kununua miwa yao yeye anapewa kibali na Serikali kwa ajili ya kuagiza Sukari ambayo ni rahisi kuingiza kuliko kuzalisha, kwa hiyo tunajikuta kama Serikali tunaumiza wakulima wetu wenyewe badala ya kuwa - *encourage* ama kuwapa *incentive* ya kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka tumkomboe mkulima kikweli kweli basi ni lazima tuhakikishe tunamuwekea mazingira rafiki ya uzalishaji, lakini pia kumuwekea mazingira ya uhakika wa soko. Kama mzalishaji

huyu ameshindwa kununua miwa hii basi tuanze kuangalia utaratibu wa kuwawezesha wananchi kupitia vyama vya Ushirika ama mmoja mmoja kupitia Benki ya Kilimo kuanzisha viwanda vidogo na vya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeishi nchi ya Asia kwa zaidi ya miaka minne, huwezi kukuta viwanda vikubwa vya sukari. Viwanda ni vidogo vidogo na watu wanashiriki katika kilimo cha miwa lakini uzalishaji wa sukari ya miwa na viazi katika uwezo mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hili, ili tuongeze mnyororo wa thamani na kukuza stadi za uzalishaji wa bidhaa za kilimo basi ni vyema tukajikita katika taasisi zetu za fedha kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wakati kujiingiza kikamilifu katika uzalishaji wa sukari katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kubwa kuliko yote ni uboreshaji wa miundombinu. Tunapozungumzia miundombinu maeneo mengi ya uzalishaji wa kilimo ni mabonde na maeneo haya wakati wa masika hayafikiki. Nchi za Asia zimepata kuendelea kwasababu kwanza walihakikisha barabara zao zote ambazo zinaenda katika maeneo ya uzalishaji zinapitika mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi kama China ambayo tunaweza kuichukulia kama *model* ya maendeleo yetu ni kwamba wenyewe walijikita katika kuhakikisha barabara zote zinapitika kwa changarawe kwasababu uwezo wa Lami hawakuwa nao. Sisi tunaweza tuka - *copy model* hiyo ya maendeleo kwa kuhakikisha kwamba barabara zetu zinaweza zikapitika katika maeneo yote uzalishaji wa kilimo na kuunganisha na barabara kuu. Hilo litapunguza gharama za uzalishaji lakini litafikisha bidhaa masokoni katika bei ambayo inauhalisia na kuongeza ushindani wa bei ya soko na kuongeza tija kwa maisha ya mkulima mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia taasisi zetu za fedha ni lazima zisiseme tu kwamba zinashiriki katika

kumwezesha mkulima bali pia zionekane zikifanya hivyo. Riba yetu bado ni kubwa na riba sio rafiki kwa wakulima wetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dakika sita tu nimeweka *stop watch* hapa

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika hili tunaweze kuangalia ni jinsi gani tunaweza kuweka sera rafiki kwa taasisi zetu za fedha ili kuhakikisha kwamba zinapunguza Riba lakini pia zinamwezesha mkulima mmoja mmoja katika kuongeza tija ya mazao yake pamoja na kuongeza uzalishaji wa bidhaa za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika hili kwakweli hatuwezi kuacha utalii pembeni. Sekta ya utalii ni muhimu mno na ni uti wa mgongo. Kwa Jimbo langu la Mikumi sekta ya utalii imeajiri wengi, lakini tafiti na stadi mbalimbali zinaonyesha kwamba ni asilimia 20 tu ya watalii wanaokuja Tanzania ambao wanarudi tena, kiasi hiki ni kidogo, na hasa ukizingatia kwamba utalii ni moja ya maeneo muhimu katika ukuaji wa uchumi wetu. Kwa hiyo nilikuwa naomba Serikali iangalie ni vitu gani ambayo vinafanya watalii wasirudi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuangalie tena jukumu la Bodi ya Utalii na taasisi zake ambazo zina jukumu la kuhakikisha kwamba mtalii anakuja Tanzania. Wanaboresha huduma zao wanatangaza vivutio vyetu lakini pia wanashirikisha wananchi wetu katika suala zima la sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika hili miundombinu katika mbuga zetu na hifadhi zetu hatuwezi kuliweka kando. Pale Kilosa ama katika Mbuga ya Mikumi kuna geti moja tu la kuingilia mbugani; lakini tunasema tuna reli ya SGR ambayo inakuja mpaka Kilosa. Unaposhuka Kilosa kwa SGR maana yake unaenda kuongeza idadi ya watalii ambao

wangependa kuja Mikumi lakini mtalii huyu angeweze kuja akaingilia katika geti la hapa Tindiga ama Mabwelebwele ama Kilangali ambako ni kilomita 15 kutoka stesheni ya reli ya SGR. Sasa kwa sababu ya kutokuwa na geti pale na kwa kutokuwa na barabara ya kuingilia pale mbugani unamsababisha mtalii huyu atembee kilometa zaidi ya 120 kabla hayakutana na geti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapozungumzia miundombinu ni pamoja na kurahisisha usafiri kwa watalii lakini pia kumpunguzia muda na kuongeza thamani ya fedha zake kwa kulinda muda wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo si kwa umuhimu wake ni suala zima la kwanini tulishindwa katika mipango yetu ya maendeleo huko nyuma. Mipango ya awali ilishindwa kufanikisha malengo yake mengi ilhali Serikali ilikuwa imedhamiria katika ukuzaji wa viwanda kama kipaumbele chake cha miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais imefungua maeneo mengi ambayo yanahitaji mjadala wa kina. Moja ambalo ni kubwa mazingira yetu ya uwekezaji si rafiki kwa sababu hatuangalii Watanzania kama sehemu muhimu ya wawekezaji, lakini pia masharti yetu yakufungua biashara yamekuwa magumu mno. Tuna taasisi nyingi ambazo mfanyabiashara ama Mwekezaji anapaswa kuwasiliana nazo kabla ya kufungua biashara yake; matokeo yake uwekezaji umekuwa ni wa gharama kubwa mno Tanzania ukilinganisha na washindani wetu katika maeneo ya Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika uwekezaji Watanzania wote lazima wapewe kibaumbele bila kujali maeneo yao ya kijiografia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia mpango wa maendeleo haujazungumzia *diaspora*. *Diaspora* ni eneo kubwa na muhimu sana katika uwekezaji wa ndani. Ninaamini kabisa hapo awali tulishindwa kutumia kikamilifu rasilimali

watu hasa ndugu zetu wa *diaspora* ambao wana *skills* lakini pia wana *access* ya mitaji katika maeneo ambayo wapo. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango anapohitimisha hotuba yake atuelezee ama alielezee Bunge lako ni jinsi gani wanaenda kuangalia Watanzania kama *significant players* katika uwekezaji, hasa hawa ndugu zetu za *diaspora*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala atakayechangia kwa dakika tano, Mheshimiwa Kasalali Mageni ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi nami pia nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, kwa *Presentation* nzuri ya Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka mitano lakini pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa *presentation* nzuri pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na timu yake nzima kwa kuliona suala la Bandari ya Bagamoyo ambayo hata Mheshimiwa Spika ameliwekea msisitizo hapa. Labda kwa haraka, nadhani mpango unao maeneo matano makubwa ambayo Waziri ame - *present* hapa lakini kwasababu ya muda mimi nitaongelea mbili tu. Nitaongelea kwenye kuimarisha uwezo wa Viwanda na utoaji wa huduma, lakini pia kukuza uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani mara ya kwanza kabisa niliposiamama wakati nachangia nilisema kwamba nimekuwa katika viwanda kwa takribani miaka 14 nikifanya kazi kama *engineer,* kwa hiyo nina uzoefu mkubwa kidogo katika suala la viwanda; na bahati nzuri nipo kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara kwa hiyo sana naongea kwa

*experience* yangu ambayo ninajua nimeiishi kama kazi lakini pia yale ambayo nimekuwa ninayaona huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila labda tu niweke angalizo. Tunapokuwa tunachangia hapa sio kusema tumetumwa labda na mabosi zetu wa zamani au tunakuja kumsemea mtu yeyote hapa. Tunachangia kwababu tunahakika na tunajua kila ambacho tunakifanya ni sehemu ya *expertism* yetu. Kwasababu ninakumbuka mara ya mwisho hapa kuna mtu aliniambia au hao wafanyabiashara wanawatuma mje kuwasemea, na hawapo humu *by the way* kwa hiyo tupo hapa kwa ajili ya kuwasemea kwababu tunajaribu kuangalia mianya ya kutengeneza kodi, mianya ya kukusanya fedha ili zile fedha ambazo Waziri hapa amewasilisha Trilioni 40 kwa miaka mitano tuweze kuzipata; tutazipata huko kwenye *private sector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani mmemsikia mchangiaji aliyepita Abbas Tarimba. Jana nimeona *we are proud* kwamba kuona Mtanzania sasa anakuwa *recognize* na nchi kubwa ambayo imeendelea kiviwanda kama *South Africa.* Kwa hiyo lazima tujue tunazo hazina hapa, kwa hiyo sasa ni jukumu la Mheshimiwa Waziri kuwaangalia wafanyabiashara wakubwa walioko kwenye nchi hii aweze kuwatumia. Maana najua ameweka mpango wa trilioni 40 kutoka sekta binafsi, anataka atengeneze ajira milioni nane kwa muda wa miaka mitano, mpaka 2026. Hizi ajira milioni nane hataweza kuzipata kama hatatafuta hawa watu wenye viwanda huko nje. Watu kama akina Dewji hawa na wafanyabiashara wengine wakubwa. awatafute akae nao na tuje na hii mipango mikubwa ambayo tunayo hapa, maana tunataka tutengeneze ajira, tunataka tukuze uchumi lakini huu uchumi hatutaweza kukukuza kama wenzetu huko nje hawajui mipango yetu sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha tafuta muda wa kukaa na wafanyabiashara wakubwa na ni sisitizo usikae nao kupitia kwenye taasisi zao zile, kaa nao mmoja mmoja, mtafute

mmoja baada ya mwingine, mwite, mwambie tuna mpango huu, unaweza ukawekeza kwenye nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana niko huku kwetu kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara tunahangaika kutafuta wawekezaji kutoka nje tuwalete hapa, lakini bado wapo wawekezaji wa Kitanzania wakubwa ambao wanaweza wakafanya biashara kutokaea hapa kuliko hata kumtafuta mtu wa nje ukamtumia mfanyabiashara wa Kitanzania aliyekuwepo hapa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hili ambalo ameliona, hasa suala la Kodi maana mimi *last time* tumefanya ziara *EPZA* pale Ubungo niliumia sana, kwamba pale kuna Mtanzania ambaye anafunga kiwanda chake anakipeleka Uganda. Sasa nikawa nafikiria unapofunga kiwanda, leo sasa tunatafuta wawekezaji wa kuja kuwekeza hapa ila Mtanzania ambaye alikuwa ameweka mle ndani, anaondoa anakipeleka kiwanda kwenye nchi Jirani. Maana yake ni nini, *obvious* unapoenda kule watakuuliza kuna nini huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haya mazingira ambayo Rais amesema mwende mkakae na wawekezaji. Ninaomba uyafanyie kazi haraka ili Watanzania ambao ndio watu wa kwanza kuwaleta watu wa nje kuja kuwekeza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina *experience* kidogo, nilikuwa natoa mfano. Ukienda katika nchi ya *Egypt,* kuna sehemu ile ya ukanda wa *Suez* nimetembelea pale, mimi nikaona, yaani lile eneo utafikiri ni kama nchi ya China imehamia pale. Walichokifanya cha kwanza ni kwamba ili uweze kumvutia mwekezaji aje pale lazima uwe na Bandari. Ile Bandari ya *Black Sea* pale ndiyo inayotumika. Wachina wameletwa pale wakapewa eneo, bandari imejengwa wamejenga viwanda vingi sana maeneo yale. Kwa hiyo wanachokifanya wanaleta vitu vyao wanafanya *process* pale Bandari ipo wana-*export* kwenda *Europe*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo badala ya kuchukua mzigo kutoka China uusafirishe kwenda *Europe* kutoka *Egypt* kuushusha mzigo Ulaya inakuwa rahisi Zaidi, ndiyo kazi kubwa wanayoifanya hapa, sasa na sisi kama Kamati ya Bajeti ilivyo-*suggest,* tunayo nafasi kubwa zaidi ya kutumia Bandari ya Bagamoyo, kwasababu lile eneo la Bagamoyo ambayo tayari tulishalitenga na lilishalipiwa fidia takriban bilioni 27 zimewekwa pale. Hatuwezi kusema kwamba tuitelekeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukiweka pale na umwambie mfanya biashara atoke Dar es salaam anatoa mzigo Bandari ya Dar es Salaam anausafirisha mpaka Bagamoyo, aanze kuzalisha pale akimaliza kuzalisha ausafirishe tena kuurudisha Bandari ya Dar es Salaam afanye *export,* huo muda haupo, maana ni *cost* ya *transportation* ya kuja na kurudi, lakini vile vile na *logistic* inakuwa ngumu. Kwa hiyo nishukuru na niomba Waziri wa Fedha pigana unavyoweza bandari ile inyanyuke pale ili sasa fidia zile ambazo tumezifanya na uwekezaji mkubwa tunaotaka kuufanya Bagamoyo uweze kufanyika pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilimo, kwababu tunaongelea viwanda vinavyoweza kuzalisha mazao haya ya kilimo mazao ya mifugo na pia uvuvi na madini. Labda upande wa kilimo Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Waziri wa Viwanda Waziri wa Killimo na hali kadhalika Waziri wa Fedha, mjaribu kutuangalizia njia sahihi ya kufanya. Wakulima wa nchi hii wanahangaika sana. Mimi ninaweza nikatolea wakulima wa upande huu wa Kagera; nilikuwa ninajaribu kufuatilia. Nchi ya *Ecuador* ndio nchi ambayo inaongoza kwa ku-*export banana*, ndizi hizi, 3.3 *billion dollar per year,* ina-*export* ndizi, hiyo ni hela nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika lakini sisi tupo pale, tulihamasishwa ndizi, watu wa Kagera mnaelewa, tumelima ndizi sasa hivi ndizi za mtwishe si zipo kule zimekaa hatuna hata watu wa kuwauzia tena? Maana unalima ndizi, Mkungu ambao hata hauwezi kuunyanyua shilingi 5,000 hatupati mteja tena. Sasa Mtusaidie. Maana nilikuwa ninaangalia

hapa kwa Tanzania tume- *export* kwa mwaka tani 258. Tani 258 ukipiga kwa bei ya tani moja dola 300 katika *World Market* unaongelea dola elfu 75. Yaani mtu ana – *export* ndizi kwa dola 3.3 bilioni wewe hata dola laki moja haifiki, na bado tuna wakulima wanalima ndizi hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Unaongelea nchi kama Egypt, nimekuwa *Egypt.* Ukitoka *Egypt,* kama unatoka *Cairo* unaenda *Alexander* ile njia yote unapotembea imejaa zabibu, imejaa migomba na vitu vingine; nikawa najiuliza hawa watu wanafanyaje hawana maji hawana chochote kile. Wanachofanya zile ndizi wanatumia *Irrigation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unashangaa mtu hana mvua ana *irrigate* ndizi zile, ana *export* ndizi anapeleka Dubai ndilo soko lao kubwa. Sasa mimi hapa nina m vua ya Mungu ndizi zinaozea kule mtusaidie ili sasa tuweze kufanya biashara na tuweze ku-*export* ili ndizi hizi ambazo tunazilima katika kanda hizi ziweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua wako Mbeya wako Kilimanjaro Mzee Mheshimiwa Dkt. Kimei amekuwa anaongea sana suala la ndizi kwa hiyo, haya ni mambo ambayo Serikali ikiingia kati ikaangalia jinsi ya kutusaidia itatutoa hapa tulipo itusogeze mbele maana hatuwezi kuongelea pamba tu hatuwezi kuongelea vitu vingine nadhani mmesikia hapa bei inashuka na kuongezeka. Lakini bado tunazo fursa nyingine za kupeleka matunda huko nje na vitu vingine vikaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado dakika tano suala lingine niongelee suala la Liganga na Mchuchuma Mheshimiwa Waziri nimefika kule kwenye ziara yetu ya Kibunge lile eneo ni pori maana mwanzoni nilikuwa nawaza labda kuna hata majumba kuna hata nini ukifika kule mambo yale yanashangaza lakini umeiweka kwenye mpango humu vipaumbele sita ambavyo inabidi tuende navyo Liganga na Mchuchuma imo humu na mbaya zaidi Serikali tayari imeshaanza kuwekeza fedha nadhani mnajua tunajenga barabara ya zege tusingeweza kujenga barabara ya zege

ya kilomita 50 sasa ya kuruhusu magari yaende kule kwenye ile migodi ile ni pesa nyingi sana ambayo tumeweka pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe nadhani kuna mambo ya kimkataba au mambo mengine ambayo yamekuwepo hapa biashara ni maelewano lazima ifikie *stage* ushuke ukae chini. Nimewahi kutoa mfano siku moja nimekuja kufuatilia biashara nimekuwa nafanyakazi kama *Sales Manager* kwa muda mrefu saa nyingine unaenda mpaka usiku hunywi pombe unakaa na mtu *bar* hapo unatafuta biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna siku nimeenda siku moja mchina mmoja anavuta sigara akipuliza moshi unaniingia puani lakini siwezi kumwambia usipulize maana nimekuja kutafuta biashara. Kwa hiyo, saa nyingine mkubali kushuka chini wafanyabiashara hawa tunapokuwa tunawatafuta kubalini kushuka chini twende tukae chini na hawa wachina, maana unashangaa hivi Mungu huyu aliwaza nini kipindi anakileta hiki kitu kwamba hapa kuna makaa ya mawe na hapa kuna mlima wa chuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu ametuletea kitu cha kufanya sasa niombe hiki kitu tuondoke sasa hivi Mheshimiwa Waziri jaribu kupigana waiteni hawa watu tukae nao chini tuongee kama huu mradi kweli una faida kubwa kama hiyo ni lazima huyu mwekezaji hawezi kuja kushindwa kuwekeza hiki kitu hapa ili tuondoke sasa kwenye hii stori ya Liganga na Mchuchuma ambayo tumeisoma tangu Shule ya Msingi mpaka leo watu tunapata mvi na haijawahi kufanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri hili suala lichukulie *serious* ili sasa itutoe hapa maana matatizo mengine madogo madogo tunayoyasema yatakwisha na yatakwisha kabisa yatamalizika. Maana najua tunawekeza hela nyingi sana kwenye bwana la Mwalimu Nyerere lakini ile ni megawati 2115 hapo unaongelea megawati 650 *almost* 1/3 tu sasa 1/3 tunashindwa kukomboa pale maana ni vitu vingi tutapata chuma tutapata umeme,

tutapata makaa ya mawe vitu vyote vitamalizika pale na bado Serikali itapata pesa ya kuweza kutusaidia kufanya miradi kwa hiyo niombe na hilo uweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia suala la kumalizia niombe viwanda nimekuwa naongea hilo jambo hata kwenye kamati Mheshimiwa Waziri ukijaribu kuangalia wenzetu ningeomba mfanye kitu kimoja kama Serikali na kama Wizara tunazungukwa na nchi tisa hapa ambazo zinatumia Bandari ya Dar es Salaam leo hatuna haja ya kuacha Toyota wana-*assemble* magari Japan halafu Toyota wana *export* magari ambayo yako *assembled* wanayaleta hapa? *Why don't we sit down* na Toyota tujaribu kuangalia Serikali ni mteja mkubwa wa Toyota tuangalie tuongee na Toyota tunavyokuja kutengeneza sehemu hii ya Bagamoyo *special economic zone*, tumuombe Toyota aje aweke hapa akiweka *plant* yake yaku-*assemble* tu maana yake ni kwamba nchi zote Jirani ambazo zinatumia magari ya Toyota tutapata *advantage* magari yanakuwa *assembled* hapa kutoka kwenye bandari yetu wanakuja wanachukua hapa kiwanda kinakuwa cha kwake analeta watu wake lakini tunapata ajira pia na uzoefu wa kuweza kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana nimeona hiyo sehemu nyingi hata Nairobi leo tukiongelea *pump* za KSB Waziri wa Maji yuko hapa nimalizie hiyo dakika moja Waziri wa Maji yuko hapa *pump* za *KSB the needing company* ni Wajerumani wale lakini leo *assembly* inafanyika Nairobi ilikuwa inafanyika South Africa lakini leo *assembly* inafanyika Nairobi wenzetu wamefanya bidii ya kwenda ku-*lob* kule hatimae ikaja hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe *brand* kubwa ambazo wengi wana *export* kwa kutumia bandari ya Dar es Salaam Mheshimiwa Waziri angalia Serikali muangalie kama tunaweza kuonana na hawa watu waje waweke viwanda vyao hapa wafanye *assembly* hapa vitu vitakuwa vinatoka vimekamilika vinaenda kwa wenzetu naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti Majala atachangia dakika tano atafatiwa na Mheshimiwa Kasalali Mageni Mheshimiwa Jane Jerry Mtate ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi kwa dakika hizo tano naomba niseme ya kwangu machache ambayo nitaweza kuyasema. Zaidi ya watanzania 75% wamejiajiri kwenye sekta ya kilimo. Lakini sekta hii ya kilimo ambayo ndiyo imeajiri watanzania walio wengi lakini ndiyo inayochangia uchumi wa pato la Taifa hili, lakini ndilo linalosababisha sisi watanzania tuendelee kuishi, Serikali imekuwa haitoi kipaumbele kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema wenzangu waliotangulia kwenye suala zima la masoko naomba nizungumzie suala zima la upatikanaji wa pembejeo na suala zima la wagani kwenye sekta hii ya kilimo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha sasa alikuwa Waziri wa Kilimo kwenye Serikali ya Awamu ya Tano na alivyokuja akiwa Waziri wa Kilimo aliwatangazia watanzania kuhusiana na suala zima la upatikanaji wa pembejeo na hususan kwenye suala la mbolea akasema mbolea itakuwa kama Coca Cola.

Sasa Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu umerudi huko huko jikoni nikuombe sana suala lile la pembejeo kwenye suala zima la mbolea ile Coca Cola ile tunaitaka safari hii kwenye bajeti hii tuone mbolea inapatikana kwa wakati na yenye tija kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye suala la pembejeo matrekta *power tiller* na vitu mbalimbali ambavyo vinakwenda kumsaidia mkulima huyu wa chini vimekuwa vikipatikana kwa shida sana. Hata hiyo mikopo ya matrekta imekuwa ni changamoto pia watu wanazungushwa kwelikweli lakini ili uweze kupata hata hilo trekta unatakiwa kuwa na hati. Wizara ya Ardhi nayo imekuwa ni changamoto hata kuwapatia tu zile ardhi za kimila wakulima wetu ili waweze kupata hati hizo waweze kwenda kukopa hayo matrekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kujiuliza Serikali ni moja hivi wanashindwaje kuwaamini hawa watanzania kwamba mtu huyu anajulikana anaishi Kijiji fulani ana ekari kadhaa mwenyekiti wa Kijiji yuko pale anamtambua ni kwanini Serikali imekuwa na kigugumizi kuhusiana na suala zima la utoaji wa mikopo ya pembejeo kwa wakulima wetu wadogo huko vijijini na badala yake tumeendelea kuwaacha wanateseka tuna Benki ya Kilimo ambayo inatakiwa kuwasaidia wakulima wa nchi hii haifanyi chochote hakuna mkulima mdogo hata mmoja anaekopeshwa na Benki ya Kilimo tunaambiwa ni Benki ya Kilimo kwenye makaratasi na majina. Ili tuweze kuleta tija kwenye benki hii niombe benki ya kilimo tuirudishe Wizara ya Kilimo ili iweze kuwahudumia wakulima wetu kule chini na hatimae waweze kunufaika na kodi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisemee suala na wagani, bado watanzania tunalima kilimo cha kujisukuma tu cha jana cha leo tunakwenda nacho hivyo hivyo. Wagani ndani ya nchi yetu pia kwenye sekta ya kilimo ni changamoto Wizara inayohusika na kuajiri Wizara ya Utumishi tunaombeni mtuambie shida ni nini inayosababisha kushindwa kuajiri wagani wakutosha kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wagani ni muhimu sana, tunaona hata watu wamoja moja ambao wanajitutumia wenyewe kwa jitihada zao kuweza kulima kilimo cha kuondokana na umasikini, kilimo cha kutoka kwenye mvua ya Mwenyezi Mungu kwenda kwenye kilimo cha kisasa cha umwagiliaji bado wamekuwa wakikosa huduma hii ya ugani kwasababu tu ya Serikali kushindwa kuajiri wagani kwenye maeneo yetu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliombe pia kama kweli tunahitaji tija kwenye sekta ya kilimo na tuweze kujenga na kuimarisha uchumi wa Taifa letu tuhakikishe kwenye bajeti hii inayokuja kwenye sekta ya kilimo twendeni tukaajiri wagani wa kilimo ili wakulima wetu waweze kupata hiyo huduma muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye suala la wagani suala la wagani wako TAMISEMI kwenye kilimo huku hawapo kwa hiyo, pale wanapokwenda kupata changamoto wagani hawa wanashindwa namna ya kuzifikisha mahali husika. Lakini mgani huyu unakuta mgani huyo ni mtendaji wa kata, mgani huyo ni Afisa Mifugo, mgani huyo huyo ndiyo hata yeye anashughulika na masuala ya kilimo kwa hiyo, unamkuta mtu mmoja ana majukumu kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba pia kwenye suala zima la wagani wanaohusiana na kilimo tuwarudishe Wizara ya Kilimo ili waende wakasimamiwe na Wizara yao na waweze kufuatiliwa na tuweze kupata tija kwenye suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie kidogo kwa dakika chache zilizobaki miundombinu tunafahamu vizuri nimalizie tu kidogo dakika moja tunafahamu tuna barabara za kimkakati...

**NAIBU SPIKA:** Nina orodha ndefu hapa Mheshimiwa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja tu *my dear* kidogo tu dakika moja ningekuwa nimeshamaliza tuna barabara za kimkakati tangu Bunge la 10 tuliahidiwa barabara ya kutoka Kilindi kupita Chemba tunaenda kuungana na Singida barabara ile mpaka leo bado hatujaweza kuona nini mkakati wake. Niombe Wizara mtakapokuja kuja kuhitimisha tunaombeni tuione barabara ya kutoka Kilindi inayokwenda kupita Jimboni kwangu Chemba...

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante Mheshimiwa hiyo barabara umeshaitaja, kwa hiyo imeshasikika.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** ...nakwenda kuunganisha na Mkoa wa Singida nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Mageni atafatiwa na Mheshimiwa Jane Jerry Ntate, Mheshimiwa Ndaisaba George Luhoro ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima lakini pia nitumie fursa hii kutoa pole kwa Watanzania na mimi mwenyewe kufuatia kifo cha Rais wetu wa Awamu ya Tano Rais wetu aliyekuwa amejikita kwenye kuhakikisha anatuletea maendeleo ya kweli Watanzania Hayati Dkt John Pombe Magufuli tunamuombea huko aliko apate pumziko jema na sisi tulioko huku tuendelee kuchapa kazi ili kutimiza malengo waliyonayo Watanzania na matumaini waliyonayo na Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan na Makamu wake na Serikali yote na niwakaribishe katika kuchapa kazi sisi tupo tutaungana nao na tutawaunga mkono kuhakikisha kazi ina kwenda ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze katika mpango wa bajeti ambao umewasilishwa leo Bungeni hapa. Ukiangalia Mpango huu unaona yapo matumaini ndiyo maana naanza kwa kuunga mkono lakini yapo mambo ya kuzingatia ambayo nilitaka tuyazungumze kidogo kwenye Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu mambo ya vijijini kwasababu ni moja ya Wabunge wenye Majimbo ya vijijini, huko vijijini asilimia kubwa ya watu ni wakulima na sekta ya kilimo imekuwa ni uti wa mgongo wa Taifa letu lakini sisi kule kijijini ndiyo Maisha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia Bunge lako niiombe Serikali katika sekta ya kilimo mnatakiwa sasa ifike tuanze kuwekeza katika kuboresha sekta hii kuanzia kwenye uzalishaji. Kumekuwa na utaratibu ambao umekuwa ukinishtua nadhani kwenye kikao kilichopita nilisema wakulima wakati tunazalisha mazao yetu Serikali imekuwa

ikikaa kimya ikituangalia inapofika wakati wa kuvuna mazao yetu unaanza kuona vitu vinaitwa *AMCOS* unaanza kuona vitu vinaitwa Stakabadhi Ghalani, unaanza kuona usimamizi ambao si rafiki kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo la Sumve tunalima mazao ya jamii ya kunde hizi choroko na dengu ni mazao ambayo sisi wakulima tunayalima kwa nguvu zetu wenyewe hatujawahi kuona mbegu kutoka Serikalini, hatujawahi kuona dawa kutoka Serikalini, hatujawahi kuona Afisa Ugani kutoka Serikalini lakini inapofika wakati wa kuyauza unaanza kuona kuna watu wanaitwa *AMCOS*, kuna watu wanaitwa Ushirika wanakuja kusimamia mazao ambayo tumeyalima sisi wenyewe kwa nguvu zetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi wanaleta utaratibu wa hovyo utaratibu ambao hautusaidii bei zimeshuka sasa hivi ukienda kwenye maeneo ambayo yanalima hizi choroko na dengu tunakaribia kuanza kuuza choroko soko lake limeporomoka kwa wakulima. Wakulima wameshindwa kabisa kufaidika kwa hiyo, naomba Serikali muwekeze zaidi kwenye uzalishaji kabla hamjaamua kuwekeza kwenye kutupangia namna ya kuuza mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni lazima mliangalie kwa undani hamuwezi kuweka mazao yote kwenye kapu moja zao kama choroko na dengu huwezi kulifananisha na korosho. Dengu sisi na choroko Wasukuma ni zao la chakula na biashara kuna mtu anahitaji kwenda kununua dengu sokoni akapike atumie lakini wewe umemwambia ili aziuze lazima apeleke *AMCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu amezungumza hapa Mheshimiwa Tabasamu kuhusu zao la pamba, ni Mbunge ninayetoka kwenye jimbo la wakulima wa pamba. Wilaya ya Kwimba ni moja ya wilaya ambazo zinazalisha pamba kwa wingi kuliko zote kwenye Mkoa wa Mwanza zao la pamba niwaambie kabisa Serikali mmeshiriki kuliua na mnaendelea kushiriki kupitia namna ambavyo mnasimamia

masoko yake. Wakulima wengi wa Tanzania tunalima hatujui hata kama tunapata faida au hasara huwa tunalima tu lakini ukifanya hesabu asilimia kubwa tunapata hasara. Lakini bado Serikali kwenye kusimamia bei za mazao bado haijaonekana kwamba tuko *serious* kwasababu tunapeleka watu kwenda kusimamia vitu wasivyovijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la pamba asilimia kubwa linasimamiwa na watu wasiolijua na limeingiliwa amesema Mheshimiwa Tabasamu hapa hawa siyo wawekezaji ni mabeberu ni watu ambao wanakwenda kumdidimiza mkulima. Kwa hiyo, ni lazima Serikali muangalie Mheshimiwa Waziri wa Fedha muone namna ambavyo mtalifufua zao la pamba kwasababu tunataka viwanda, viwanda vinatoka wapi kama mazao tunayaua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini huko vijijini kwetu ambako ndiko tunakozalisha mazao haya ya chakula ambayo watu wa mjini wanatumia lakini ndiko nguvu kazi nyingi iko kule, bado tunazo changamoto za miundombinu. Katika mpango wa bajeti nimeona tunazungumza kuhusu miundombinu mikubwa mikubwa kama reli ya kati tunazungumza madaraja lakini pia sisi kule *site* vijijini kuna miundombinu ya kwetu ya kawaida kabisa mabarabara ya vijijini kupitia *TARURA* bado hali vijijini si nzuri barabara za Dar es Salaam zisipopitika utaona watu wamepiga picha zimeonekana kwenye mitandao Serikali imeenda kurekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini barabara za Sumve asilimia kubwa hazipitiki vijijini kuna kata zingine kama Kata ya Mwabomba ikinyesha mvua ikakukuta uko kule kama una pikipiki unaacha unatembea kwa mguu. Kwa hiyo, bado kabisa tunatakiwa tuwekeze pesa kwenye miundombinu ya vijijini ili wakulima wetu waweze kusafiri waweze kusafirisha mazao lakini pia ipo miundombinu ya kimkakati ambayo inawezekana hatujaiona sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ambayo imekuwa ikiongelewa sana tangu mimi nimekuwa chaguzi

zote za Chama cha Mapinduzi za vyama vingi imekuwa ikitajwa barabara yenye urefu wa kilometa 71 inayotokea Hungumarwa kupita Ngudu kwenda mpaka Magu. Barabara hii ni barabara ya kimkakati ambayo imesahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mpango huu pia nimeiona imezungumzwa lakini imezungumzwa katika ile stori ya kutenga pesa na mipango ya baadaye. Lakini imeanza kuzungumzwa niko darasa la tatu. Sasa barabara hizi za kimkakati kwasababu barabara hii ikijengwa kwa kiwango cha lami inapunguza umbali wa mtu anayesafiri kutokea Shinyanga kwenda nchi Jirani ya Kenya au Mkoa wa Mara au Wilaya ya Magu kwa kilometa zaidi ya 83. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ukiijenga unakuwa umeokoa uchumi tunaposema kukuza uchumi barabara za kimkakati ndiyo hizi. Hii ni barabara ambayo inaweza ikafungua mbali na kufungua wilaya ya Kwimba kuongeza mapato kuongeza mzunguko kwasababu Wilaya ya Kwimba ni wilaya pekee ambayo kwenye Mkoa wa Mwanza haijui maana ya lami kwenye Makao Makuu yake kwa hiyo, barabara hii ikipita itafungua uchumi wa Wilaya ya Kwimba. Lakini siyo tu uchumi wa Wilaya ya Kwimba itafungua uchumi wa kanda ya Ziwa na uchumi wa Taifa kwasababu tunahitaji mizigo inayopelekwa nchi jirani ya Kenya iende kwa urahisi zaidi, tunapunguza uhai lakini tunafungua uchumi wa wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika mpango huu wa kiuchumi; Mpango Mkakati wa Maendeleo ambao tumeletewa leo, ni lazima tuangalie pia maeneo ya vijijini. Sisi tunaotoka vijijini, bado tumesahaulika. Hii miundombinu yote tunayoisema inazungumza mambo mengi ya mjini, lakini sisi ambao wakati mwingine hata mawasiliano ya simu siyo mazuri, hatuzungumzwi humu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kupitia Bunge lako, Wizara na Serikali katika Mpango wao huu wahakikishe wanazingatia maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jenejelly Ntate atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro na Mheshimiwa Issa Mchungahela ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami kama wenzangu wote nianze kwa kutoa pole kwa Watanzania wote na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Rais wetu kipenzi, Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii nimpongeze Mheshimiwa Mama Samia Suluhu kuwa mwanamke wa kwanza kuvunja na kuweka historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Nchi kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Mwigulu kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kupewa Wizara nyeti; Wizara ya Fedha na Mipango. Hongera sana. Vile vile nampongeza kwa Mpango ambao ameuwasilisha leo yeye na timu yake yote ya waatalam pamoja na Mwenyekiti wake wa Bajeti. Kwa kweli inatoa matumaini ya Taifa letu, tunaenda wapi kiuchumi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita katika sehemu ya uvuvi na kilimo. Nikianza na uvuvi, Tanzania ni nchi iliyobahatika sana. Tuna maziwa ya kutosha, mito na bahari, lakini bahati hii bado hatujaitumia. Tumeenda na kudra ya Mwenyezi Mungu tu kuvua samaki walio ziwani na baharini; lakini kama tukijikita kwenye vizimba kufuga kitaalam Mheshimiwa Waziri atapata mapato ya kutosha na ugomvi kati ya Serikali na wananchi kwa uvuvi haramu utakuwa umekoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sehemu hii Serikali ijikite kutoa hela za kutosha, Wizara husika ndiyo itafute maeneo na kujenga vizimba. Vizimba hivyo wananchi

wakodishwe kufuga. Nilikuwa napiga mahesabu, lakini mimi sio mtaalamu wa hesabu; ila tukiweka vizimba hivyo kila baada ya miezi sita tunavua Samaki, tena ambao siyo wa kupima na rula, kwa sababu amefikia kiwango kinachotakiwa. Vile vile hapa tutapata kodi, hapa tunawainua akina mama na vijana, watapata ajira kutokea pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi Jirani, Uganda nimetembelea mwenyewe vizimba vya akina mama. Mwanamama anakwambia kwa mwaka ana uwezo wa kutengeneza shilingi milioni 200 au shilingi milioni 15, lakini sisi Tanzania tumekaa tu. Naiomba Serikali, nakuamini Mheshimiwa Mwigulu na Waziri wa Uvuvi, tuchukue hatua, wakati ni sasa. Mwalimu Nyerere aliwahi kusema kwamba tunaukalia uchumi, nasi tumeukalia uchumi kwenye hili la uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wenyewe, ukiamua wewe mwenyewe kutafuta vizimba, kuna idara inaitwa ya Idara ya Mazingira; unaambiwa hapa mazingira hayafai, hapa hayafai, lakini kwa Waganda inafaa vipi? Tunakosea wapi hapa? Sasa sisi tunaiomba Wizara husika, yenyewe ndiyo ishirikiane na Idara ya Mazingira, wote ni Serikali moja, watuambie kwamba maeneo kama haya hamtaharibu mazingira, weka vizimba, fuga Samaki. Mheshimiwa Waziri utapata mapato ya kutosha pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri, kwenye bajeti ijayo Mheshimiwa Waziri tenga ruzuku, tupe akina mama na vijana tukaweke vizimba kule tukutengenezee mapato na tuinue uchumi wa Tanzania. Huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kilimo, toka uhuru mpaka leo bado tuko kwenye kilimo cha jembe, hatujawahi kutoka hapo, lakini tunasema kilimo ndiyo uti wa mgongo, kilimo ndiyo asilimia 70 ya Watanzania tuko pale, kilimo ndiyo kinagusa kila Mtanzania, ndiyo tumekiweka mbali na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri niko kwenye Kamati ya Kilimo. Tumetembelea miradi kama Kilosa, lakini ukiangalia kidogo kwenye sehemu ya umwagiliaji waliyoijenga pale na mazao yanayotoka pale na tumebahatika maziwa na mito ya kutosha, lakini bado hatujaingia kwenye kilimo cha umwangiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kilimo hicho tukiingia, mbegu hakuna. Kilio cha mbegu kimekuwa kikubwa sana. Hakuna mbegu za kutosha, hakuna wataalam wa kutosha, kwa hiyo, kwenye kilimo tunakwama hapo. Ushauri wangu tu, niishauri Serikali sasa ijikite kwenye kilimo cha umwangiliaji, lakini ijikite kabisa kwenye uzalishaji wa mbegu, tena ambazo ni za kiwango kwa kutumia utafiti, tutenge bajeti ya kutosha ya utafiti wa mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuhakikishe tunaajiri Wagani wa kutosha, hawapo. Leo hii kuna Kata nyingine zina vijiji 15 na mgani ni mmoja; lakini kwa sababu yuko TAMISEMI, wanamwambia utakaimu Utendaji wa Kata. Tumeyaona haya. Sasa Ugani anaufanya saa ngapi? Akishaenda kwenye Utendaji wa Kata, kule kuna kusimamia kuuza mashamba na kadhalika, Ugani anaacha, anaomba *recategorization* akawe Mtendaji wa Kata, tunawakosa Wagani namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado hata yule ambaye amejitahidi kulima yeye mwenyewe, masoko hakuna. Kuna kipindi ilitangazwa hapa zikalimwa mbaazi Tanzania kwamba zitaenda India, lakini matokeo zilipelekwa mpaka kwenye vituo vya shule kuwapikia wanafunzi, India hazikuwahi kwenda. Sasa tunakwama wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo na uvuvi, vitu hivi tukivishika, tukaviwekea mkakati kama tulivyoweka kwenye miundombinu ya barabara, Tanzania tutafika mbali. Huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Mchungahela na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Naomba nianze kwa pongezi. Wapo Mawaziri wanne ambao wamegusa maisha ya wananchi wa Jimbo la Ngara na ninapenda nitumie nafasi hii kuweza kuwapongeza. Naomba kumpongeza Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda na Mheshimiwa Hussein Bashe kwa kugusa maisha ya wananchi wa Jimbo la Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipomwomba Mheshimiwa Prof. Mkenda miche ya michikichi ndani ya siku saba, alituma watu wa *TARI,* walifika Ngara na kuotesha vitalu vya miche ya mchikichi. Ahsante sana. Nilipoomba miche ya kahawa, Mheshimiwa Hussein Bashe ndani ya mwezi mmoja amenipatia miche 300,000 na wananchi wangu wa Jimbo la Ngara wameshaipanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *speed* hii ya Wizara ya Kilimo ni *speed* ya *dream-liner* naomba muweze kuindeleza. Vile vile, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dorothy Gwajima pamoja na Mheshimiwa Godwin Mollel kwa kuendelea kuimarisha huduma za afya na hasa kwa kufika kwenye jimbo langu la Ngara na kuhakikisha kwamba changamoto zile za ukosefu wa madawa wamezifanyia kazi na sasa zile simu nilikuwa ninapigiwa kwamba hakuna madawa kabisa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, zimepungua. Ahsanteni sana kwa kuja Ngara, naomba kazi mnayoifanya ya kuboresha huduma za afya muweze kuendelea nayo na mtu yeyote asiwakatishe tamaa, mimi na wananchi wa Jimbo la Ngara nipo pamoja nanyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Maryprisca na Mheshimiwa Aweso kwa kuja Ngara pia kugusa maisha ya wananchi wa Jimbo la Ngara. Walikuja Ngara na wakati Mheshimiwa Maryprisca anafika

pale, alikuja na barua mkononi ambayo ilikuwa na taarifa za kupewa kibali cha kuruhusiwa kujenga mradi wa maji mpya ambao unaenda kutatua matatizo ya maji kwenye Mji wa Ngara Mjini pamoja na viunga vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri hao waliogusa maisha ya wananchi wa Jimbo la Ngara, naomba niseme kwamba Wizara yote itakayotugusa kabla sijaendelea na mchango, nitakuwa nawapongeza hapa hivyo, nikija kuwaomba msaada kutokea Ngara Waheshimiwa Mawaziri, basi ujue kabisa kwamba ukinisikiliza haraka haraka utakula pongezi ndani ya hili Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye eneo la kilimo na ninaomba nichangie kwenye upande wa kilimo cha zao la alizeti. Mahitaji ya mafuta ya kula Tanzania kwa mwaka mmoja tunaitaji *metric* tani 400,000 mpaka 500,000 za mafuta ya kula. Uwezo wa kuzalisha mafuta ya kula kama Taifa ukijumlisha michikichi, alizeti na kadhalika, tunazaliza *metric* tani 200,000 mpaka 250,000 kwa mwaka. Hii inafanya tuweze kuagiza mafuta nje ya nchi kwa kutumia fedha za Kitanzania zenye dhamani ya Dola za Kimarekani milioni 80. Tunatumia fedha hii wakati Watanzania wapo na wana uwezo wa kulima alizeti na hayo mazao mengine tukazalisha mafuta ya kula hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tuko tayari kuzalisha mafuta ya kutosheleza mahitaji ya Taifa. Wapo wakulima wa kutosha, wako wasindikaji wa mafuta ambao kwa Mkoa wa Manyara peke yake, nikitolea mfano, kuna viwanda vya kukamua na kusindika mafuta ya alizeti 234; na kwenye Jimbo la Ngara kipo kiwanda kimoja ambacho ni changu mwenyewe na chenyewe kina uwezo wa kuzalisha mafuta ya kula ya alizeti yanayotosheleza wakazi wa Jimbo la Ngara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, changamoto kubwa inayofanya tushindwe kuzalisha mafuta ya kula ya kutosha, ipo kwenye upatikanaji wa mbegu bora ya kisasa.

Taasisi za utafiti za Tanzania tulizonazo hazijawahi na sijui kama wana mpango wa kuanza uzalishaji wa mbegu bora ya alizeti aina ya *high breed.* Teknolojia wanayoitumia kwa sasa kuzalisha mbegu ya alizeti inaitwa *Open Pollinated Varieties (OPV),* maana yake wanazalisha mbegu yenye daraja la kati ambayo haiwezi kuzalisha mafuta ya kutosha kutosheleza mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, naomba nitumie nafasi hii kuweza kumwomba Waziri wa Fedha kufanya mambo yafuatayo; kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu, mwana wa Nchemba, naomba utusaidie mambo yafuatayo: moja, Wizara yako isaidie kulinda viwanda vya ndani hususani vile vinavyomilikiwa na wasindikaji wadogo, viwanda vya kati na vile vidogo hususani kwa kuzielekeza mamlaka, hasa *TRA* kujitafakari inapokwenda kwenye viwanda hivi na kuviathiri kupitia makusanyo ya kodi kwenye usajili, lakini pia na kodi za ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia zipo mamlaka nyingine zinazoathiri viwanda hivi vidogo vidogo. *NEMC,* hitaji la kufanya *Environment Impact Assessment* ambalo linataka ukiwa na kiwanda uweze kutoa shilingi milioni 10, hiyo una-*depots* benki, umekopa huku kuanzisha kiwanda; hii nayo inatuathiri kwenye viwanda vidogo vidogo. Hivi vitu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango viangaliwe ili athari inayopatikana kutokana na vitu hivyo ipunguzwe ili viwanda hivi viweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ni muhimu, ninaomba Vituo vya Utafiti vya Serikali vya Mbegu viwezeshwe ili vianze kuzalisha mbegu bora za kisasa. Narudia tena kwa msisitizo na herufi kubwa, VITUO VYA UTAFITI VYA SERIKALI VIWEZESHWE KUZALISHA MBEGU BORA ZA ZAO LA ALIZETI ZA KISASA MBEGU ZA *HIGH BREED*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye soko, mbegu la zao la alizeti inanunuliwa shilingi 35,000/=. ukienda Mbeya Vijijini, ni mwananchi gani ana uwezo wa kumudu gharama hii ya mbegu shilingi 35,000/= kwa kilo moja? Hayupo! Ndiyo maana

mimi kule kwenye Jimbo langu la Ngara nimenunua mbegu na nikatoa mikopo nikawagawia wakulima. Ninaomba watu wa kilimo waje wajifunze, tume-*pilot* na inaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ni muhimu sana ninaiomba Wizara ya Fedha iweze kusaidia Pamoja na Wizara ya Kilimo ni utolewaji wa mikopo ya mbegu kwa wakulima. Wakulima wawezeshwe kununua mbegu ili waweze kupanda zao la alizeti kwenye mashamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya kawaida, mwananchi ana shamba lake amelilima, mbegu sokoni inauzwa shilingi 35,000/=, hata kama tukiwezesha kwenye Taasisi zetu za Utafiti, sidhani kama itashuka shilingi 10,000/=. Bila kumwezesha mkulima huyu kwa kumpatia mkopo aweze kununua ile mbegu na kupata nguvu ya kupalilia shamba zima na baadaye kuvuna, hawezi kulima mashamba makubwa kibishara. Hivyo wakulima wawezeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hayo mambo matatu tutakuwa tumepata faida zifuatazo: moja, tutawezesha Watanzania kupata mbegu za kutosha tena mbegu bora za zao la alizeti, ambapo endapo tutawezesha Taasisi zetu za Utafiti kuzalisha; na hii haina chenga chenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatuwezi kutenga fedha za kuwezesha taasisi zetu zizalishe mbegu ya kisasa na badala yake tukawa tunasubiria Mataifa ya nje ambayo yana kampuni zao zinazozalisha mbegu za kisasa, wao ndio waje watuuzie, tena wanatupiga kweli kweli, kilo moja shilingi 35,000/=; bila hivyo tutakuwa hatujawatendea haki wananchi wangu wa Jimbo la Ngara, Shubi pamoja na Wahangaza na Wasukuma wa Nyamagoma pamoja na Wahaya wa Benagu. Tutakuwa hatujawatendea haki wananchi wa Dodoma wanaolima alizeti, Wagogo pamoja na wengine wa Singida, Wanyiramba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, tutapunguza gharama ya kununua mbegu ya zao la alizeti

sokoni iliyopo kwa sasa. Kama tutawekeza kwenye viwanda vyetu vya kuzalisha mbegu, tutawezesha upatikanaji wa chakula cha mifugo cha kutosha. Yale mashudu yanatumika kwa ajili ya kulishia mifugo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia.

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kabisa sekunde tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwekeza hivi kwa kuwezesha taasisi zetu tunaenda kuondoa tatizo la mafuta kwenye nchi yetu ndani ya kipindi cha miaka miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Mchungahela, atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, tutamalizia na Mheshimiwa Ng'wasi Damian Kamani.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Pia nitangulize pongezi zangu kwa watu wote waliopa bahati ya kuchaguliwa kuwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwenye nafasi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nampongeza pia Mheshimiwa Rais, mama yetu kwa kuonyesha njia ya jinsi tutakavyoelekea Tanzania kwa kipindi hiki japo tulikuwa tunashaka kidogo tukifikiria kwamba itakuwaje baada ya kupata msiba mkubwa tulioupata angalau sasa hivi tunaona kidogo kuna hali tunaweza

kuelekea sehemu. Nashukuru kwa hilo na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ametuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, kwanza pia niwapongeze wananchi wangu wa Jimbo la Lulindi kwa kunichagua nawahakikishia kwamba sitawaangusha hata mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuangalia jinsi mwenendo mzima wa huu Mpango ulivyokwenda ni mpango mzuri sana ambao kwa muda mrefu sana tulikuwa tukiusubiri mpango wa namna hii. Kwa kweli hakuna shaka juu ya mpango huu, lakini nafikiri kwa namna moja au nyingine najielekeza katika kuchangia baadhi ya mambo katika mpango huu, hususani katika fursa ambazo kwa namna moja au nyingine tunaweza tukazitumia sisi kama Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa kusini kwa mfano, tuna fursa kubwa sana eneo lote la Mkoa wa Mtwara ni eneo la fursa ambalo tunaweza tukalitumia vizuri sana kujielekeza na kujikita kwenye biashara na nchi takribani tatu au nne. Hiyo ni *advantage* kubwa sana na mfano, ukiangalia kusini kule Mtwara tuna ukaribu kabisa moja kwa moja na Nchi ya *South Afrika* na Nchi ya *Mozambique* lakini pia tuna ukaribu na nchi ya *Comoro,* hali kadhalika tuna ukaribu na nchi ya Madagascar. Hizi nchi kwa namna moja au nyingine kama tutajikita kufanya nazo biashara, kwa sababu kwanza zenyewe zina mapungufu mengi sana ambayo wanayategema sana yanaweza yakasaidiwa na sisi uimara wetu katika kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tunayo bandari kubwa ambayo haina shida, mpaka sasa imetengenezwa kwa kiasi kikubwa kabisa lakini pale ni lango pia ambalo la kuweza kutokea nchi nyingi kwenye bandari hiyo. Kwa sababu kama unavyoangalia ile Bahari ya Hindi imeunganika moja kwa moja katika hizi nchi, lakini sisi tunazalisha vitu vingi hususani mazao ya kilimo ambayo kwa namna moja au nyingine wenzetu kule hawawezi kuzalisha kwa mfano Nchi ya Comoro. Pia tunazalisha mifugo ambayo Nchi ya Comoro

hawawezi kuzalisha, sisi tunaweza kuitumia nafasi hii kwa kuwauzia kwa kiwango kikubwa kabisa tukapata pesa za kutosha. *(Makofi.)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema Bandari ya Mtwara, moja kwa moja kwa makusudio yetu yale ya kuunganisha reli ya *standard gauge* kwenda *Mbamba Bay* lakini kupitia Mchuchuma na Liganga moja kwa moja, hapo tunaona kwa jinsi gani hizi *products* zinazozalishwa kwenye Liganga na Mchuchuma kwa mfano chuma na makaa ya mawe, tuna uwezo wa kuwauzia moja kwa moja nchi hizi ambazo nimeziataja hapa kirahisi kabisa. Kwa namna moja au nyingine pia bandari hii inaweza ikawa ni kiunganishi cha nchi nyingi sana hasa hasa zilizounganikaunganika kwa upande kwa kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naliona kwa sababu Mkoa wa Mtwara unazalisha zao kubwa la korosho ambalo kwa namna moja au nyingine siku zinavyokwenda limekuwa zao linalopendwa kwa matumizi na watu wengi sana inakuwa ni rahisi kwa namna moja au nyingine kuziuza korosho zetu katika nchi hizo ambazo nimezitaja. Kwa hiyo tunaweza kuona jinsi gani Mkoa wa Mtwara unaweza ukawa umetumika kwa namna moja au nyingine ikawa kama mkoa mkakati wakusambaza uchumi wetu, lakini na kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakua kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, naona kwamba, bado hatujachelewa, lakini kuna gesi ambayo Mtwara imekuwa ni kitovu kikubwa sana cha gesi ambayo mpaka sasa hivi haijatumika vya kutosha. Naomba Serikali ifanye jitihada ya kutosha kabisa kuhakikisha gesi Mtwara inatumika. Sijajua tatizo ni nini mpaka sasa hivi ambalo linatukwamisha. Ningeomba Wizara husika ifanye mkakati wa kutosha kabisa kuhakikisha kuona gesi hii inatumika kama vile tumetegemea itumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo la uzalishaji katika masuala ya kilimo, Mkoa wa Mtwara hauko nyuma

pia katika uzalishaji wa mazao mengine ukiachia korosho ambao ni zao maarufu. Mkoa wa Mtwara ni maarufu pia katika kuzalisha ufuta ambao ni kigezo kikubwa kabisa cha kupunguza hili *gap* ya matatizo ya mafuta ya kupikia kama tutaweka nguvu za kutosha kidogo kwenye ufuta, lakini korosho na mazao mengine bila shaka Mtwara itakuwa ni sehemu mojawapo inatusaidia sana kupunguza shida hasa hasa katika suala zima la kupunguza matatizo ya mafuta yanayohitajika katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niweze kuzungumzia suala la miche ya korosho ambayo ilikuwa imelimwa na wajasiriamali wadogo wadogo kwa minajili ya kwamba ilikuwa ikatumike kwenda kuwekezwa katika maeneo mengine ambayo hayalimi hiyo miche. Wawekezaji wale mpaka sasa hivi wamekuwa wakilalamika kwamba hawajalipwa stahiki zao baada ya kuwa wametumia nguvu nyingi sana, lakini pia na kutumia pesa zao katika kuwekeza hiyo miche ambayo namna moja au nyingine ilizalishwa ikaiuzia Serikali kupitia Mamlaka ya Korosho lakini mpaka sasa hivi wananchi wale wanalalamika hawajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kwa jicho la huruma kabisa iwasaidie hawa wawekezaji wadogowadogo kwa sababu wao ni sehemu kubwa kabisa ya maendeleo ya nchi hii kama vile ilivyokuwa wawekezaji wa maeneo mengine, hususani ukizingatia kwamba hawa ni wakulima ambao hutegemea kidogo sana wanachokuwa nacho waweze kukiwekeza sehemu nyingine wajipatie mkate wa siku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna moja ama nyingine hapo ni kama nimchomekea tu maana yake nilijua sitapata nafasi ya kulizungumza hili, nimejaribu kulizungumza kwa mara mbili, mara ya tatu, sijalipatia jibu, naomba japo sio mahali pake hapa, lakini kwa taadhima Waziri husika atuonee huruma watu wa Mtwara, aweze kuwapa wale watu waliowekeza katika ile miche ya korosho wanachostahili angalau waweze kusukuma mbele kidogo maisha yao, japo najua sio mahali pake hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, najaribu kujielekeza pia katika suala zima la gesi kwa ujumla. Gesi kwa namna moja au nyingine imekuwa ni tegemeo kubwa katika eneo la Mtwara, lakini hata kwa Tanzania kwa ujumla, nafikiri itakuwa sehemu ya mojawapo itakayotusaidia kutatua baadhi ya changamoto ndogondogo ambazo kwa namna moja au nyingine tungeweza kushindwa kuzitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naomba nishukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunamalizia na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia katika Mpango huu jioni ya leo. Nianze pia kwa kutoa pole kwa familia ya Dkt. John Pombe Magufuli, Watanzania wote, viongozi wote kwa msiba huu mzito ambao ulitutikisa kama Taifa, lakini pia nizidi kutoa pongezi nyingi niungane na Wabunge wenzangu kwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, kwa *trend* nzuri ambayo ameanza nayo ambayo inatoa matumaini makubwa kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba mchango wangu wa leo nianze kwa kutoa mfano wa mfumo wa familia ya Kisukuma. Wote tunaweza kuwa tunafahamu kwamba sisi Wasukuma tunaishi kwenye familia ambazo ni *extended,* familia yenye watoto wachache sana ni watoto kumi na kuendelea na familia ambayo ina watoto wengi ndio inakuwa familia tajiri Zaidi katika kile kijijini. Hii ni kwa sababu watoto hawa ndio kama *source of labour ndio* watatumika wakienda kuchunga, watagawa vizuri majike yatachungwa vizuri, madume yatachungwa vizuri, ndama zitachungwa vizuri jioni zikarudi zimeshiba. Pia kama wakienda shambani watoto hawa wakiungana kwa pamoja maana yake heka nyingi zitalimwa, lakini pia hata kama mtoto wa familia ile akitaka kuoa anajengewa pale pale pembeni ili aoe na yeye azae waungane wote pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana ya kutoa mfano huu ni nini? Asilimia zaidi ya sitini ya wananchi wa Taifa hili ni vijana, lakini nasukumwa kuamini kwamba Serikali haitaki au haijaona umuhimu wa kutumia wingi huu wa vijana wenye nguvu na ambao wako tayari kutumikia Taifa hili kama ambavyo familia ya Kisukuma inatumia watoto wake wengi ili kujipatia zaidi na kuwa tajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto yetu kubwa sisi ni ukosefu wa ajira, lakini kwa nini kwa wingi wetu huu, bado Serikali yetu inaweza ikatumia pesa nyingi sana kuangiza mafuta ya kula kila mwaka, wakati kwa mwaka tunaweza kutumia pesa hizi, tumeshaambiwa na Mheshimiwa Kingu na wengine kwamba wapo tayari kutupa maeneo, Serikali ikaanzisha kambi, ikaweka miundombinu, vijana wakawekwa pale wakalima alizeti, wakalima michikichi na namna nyingine zote tukapata mafuta ya kutosha tuka-*save* pesa za Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaweza tukaamua kutumia vijana hawa hawa katika kazi nyingine nyingi miradi mingi ya kimkakati, vijana ambo wana ari ya kufanya kazi, kulitumikia Taifa hili kuliingizia kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namna pekee ambayo tunaweza kuweza kufanya hivyo, kwanza kabisa ni kuhakikisha tunakomboa vijana hawa kifikra kwa maana ya kuboresha mfumo wa elimu. Pili, tuwe na *national agenda* au vipaumbele vya Kitaifa ambavyo tutawaonesha vijana hawa kwamba Taifa letu linaelekea huku na Serikali yetu ikafanya juhudi za makusudi za kuhakikisha kwamba zinawezesha vijana hawa kuendana na vipaumbele vya Kitaifa na mwisho tunakomboa Taifa letu kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la elimu, naomba nitoe takwimu chache tu. Mwaka 2014, wanafunzi wapatao 885,000 walimaliza darasa saba, mwaka 2018 walimaliza *form four* lakini walimaliza wanafunzi 425,000 na mwaka huo walipomaliza *form four* wanafunzi 121,251 wakachaguliwa kujiunga na kidato cha sita na vyuo vya

ufundi. Hata hivyo, mwaka 2020 ni wanafunzi 84,212 tu ndio wamemaliza, maana yake wanafunzi 725,645 wako wapi ambao walimaliza darasa mwaka 2014 na mwaka 2020 hawakumaliza kidato cha sita wala vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *VETA* zetu zote nchi nzima *at high capacity* zina uwezo wa ku-*accommodate* watu 150,000 hadi 170,000 tu, wale wengine waliobaki wanakwenda wapi. Pia wote tunakubaliana katika michango yetu Waheshimiwa Wabunge wote tangu mwanzo wa Bunge hili mpaka sasa wame-*hint* kwamba mfumo wetu wa elimu haumwandai kijana kuweza kubaki kwenye jamii na kuitumikia jamii yake kwa kujiajiri mwenyewe, vijana hao wanaobaki wanakwenda wapi? Ndio huku huku tunazidi kuzalisha magenge ya wezi na majambazi, lakini sisi ndio tumezalisha watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya ili niseme nini, ushauri wangu; kuna mifumo mingi ambayo imeanzishwa na Wizara zetu na Serikali yetu ya kuhakikisha kwamba tuna-*remedy* suala hili ikiwa ni pamoja na kuanzisha *program za internship* na *apprenticeship,* kuwapa watu elimu ya vitendo ili wawe tayari kuingia kwenye soko la ajira. Hata hivyo, Serikali yetu kila mwaka imekuwa inatenga pesa nyingi sana kwa ajili ya mifumo hii. Pesa hii hii ambayo ingeweza kutumika kurudi kwenye mifumo yetu ya elimu, tukaboresha mifumo yetu, tukaanza kuwafundisha watu vitu ambavyo ni *relevant* kwa mazingira ya Kitanzania na tuka-*save* pesa nyingi za Serikali zizazotumika kuweka mifumo ya *internship* na *apprenticeship*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi ambayo tumekuwa shuleni tumefundishwa, lakini mpaka leo *applicability* yake hatujaona kwenye maisha ya kawaida. Hii ni kwa sababu mfumo wetu wa elimu umekuwa *static,* kitu ambacho walijifunza watu miaka 20 iliyopita, wanajifunza hawa hawa wa miaka ya leo, lakini dunia inabadilika. Ushauri wangu kwa Serikali na Wizara ya Elimu, suala la elimu liwe suala la kubadilika, liwe *revolving issue,* watu wafundishe vitu ambavyo vinakwenda na muda, kitu alichojifunza jana

kilikuwa *relevant* leo sio *relevant* tena tuache, tuanze kufundisha watu vitu vinavyokwenda na wakati, ikiwa ni pamoja na elimu ya vitendo ambayo itamsaidia kijana, hata akiamua kwamba siendelei mbele naishia darasa la saba, naishia *form four*, naishia *form six* au labda naenda mpaka chou, ana uwezo wa kurudi kwenye jamii, kuitumikia jamii yake akazalisha kujikomboa yeye, familia yake na kujenga uchumi wa nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, nimezungumzia suala la kutengeneza vipaumbele vya Taifa au *National Agendas.* Nitoe tu mfano leo kaka yangu Kingu amezungumzia suala la Misri na namna gani wamebadilisha kutoka jangwa na kuwa wazalishaji wakubwa sana wa vyakula vingine vingi, *land reclamation Egypty* ilikuwa ni *National Agenda* ambayo ilibebwa iwe, isiwe lazima wai-*achieve.* Nchi zetu za Afrika hasa sisi labda Watanzania *National agenda* zinakwenda na uongozi unaoingia, hatuja-*define agenda* zetu sisi kama Taifa labda kwa miaka 20 au 30 kwamba iwe isiwe, inyeshe mvua, liwake jua, sisi tutakwenda na mkondo huu tu mpaka tuhakikishe kwamba tumeufanyia kazi na ume-*bear fruits*.

Mheshimwa Naibu Spika, kwa hiyo kila atakayeingia maana yake ataingia na vipaumbele vyake na vipaumbele hivi ni vyema, lakini labda muda ule ambao tunakuwa tunawapa viongozi wetu ni mfupi. Akiingia mwingine akaingia na lingine maana yake bidii yote, *resources* zote zilizokwishatumika zinaishia pale, tunaanza na vitu vingine, kitu ambacho tunapoteza rasilimali nyingi. Hata hivyo, wananchi wetu watashindwa kuelewa majukumu yao Kitaifa ni yapi, Taifa letu linatoka wapi linaenda wapi, tujikite wapi na tukiwa na vipaumbele hivi itasaidia sasa Serikali nayo kuhakikisha kwamba inachukua *steps* za msingi. *Let say* tumesema sasa hivi ni Serikali ya viwanda na mkondo wetu Kitaifa ni viwanda maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba, Serikali itahakikisha kwenye suala la viwanda inaondoa urasimu wote, inarekebisha au kufuta baadhi ya kodi ili

wavutike na kuingia kule kwenye viwanda. Tukikaa na mkondo huu kwa miaka 20 maana yake viwanda nchi kwetu, *by the time* tunabadilisha kwenda kwenye kipaumbele kingine viwanda vimesimima na nchi yetu kwenye suala hilo imekwishakaa vizuri. Kwa hiyo, naomba Serikali ikae chini, iangalie kwamba vipaumbele vyetu ni vipi na wananchi waambiwe na waambiwe majukumu yao na Serikali iji-*dedicate* kwenye vipaumbele hivyo kuhakikisha inavirahisha kiasi ambacho mwananchi yeyote yule ana uwezo wa kuingia na kufanya kazi katika vipaumbele hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu sisi vijana imekuwa changamoto sana kuingia kwenye hizi biashara kwa sababu bado hakuna urafiki wa kukaribisha mtu anayeanza biashara au anayeanza uwekezaji kwenye nchi yetu. Mtu akiingia mtaji wenyewe ame-*struggle,* amekopa halmashauri, kakopa benki, dhamana inasumbua, lakini akiingia nusu robo tatu yote inatakiwa iende ikalipie leseni, ikalipie kodi na vitu vingine, kwa hiyo tunawakatisha tamaa. Tuki-*define* vipaumbele vyetu, maana yake mtu anajua sasa hivi kuna urahisi wa kwenda huku, wananchi wote wanajua tunaelekea wapi na nini tunafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano kutoka kwenye Nchi ya *Thailand;* ukifika kwenye nchi ile, ukishuka tu *Airport* unaulizwa hii ni mara yako ya kwanza kufika au wewe ni mwenyeji hapa. Ukisema ni mara yako ya kwanza unaanza kupewa vipaumbele; nchi yetu ina hiki, hiki na hiki , kabla hujaondoka tafadhali tembelea hapa na hapa, maana yake ni uzalendo ambao wananchi wa kawaida wamekwishajiwekea kwa kutambua vipaumbele vya nchi yao wapi inakwenda na wanaitangaza kidunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo machache, la mwisho kabisa nimalizie kwa kumshukuru sana Mheshimwa Rais kwa msimamo mzuri alioutoa katika hotuba yake ya mwisho juu zima ya suala ya bando au mitandao. Vijana wengi pamoja na kuwa ajira ni changamoto, wengi tunatumia sana sana mitandao hii kujiajiri. Tunafanya biashara za mitandaoni, lakini hata pia kwenye kusoma,

tunasoma kupitia mitandao, lakini hata kwenye sanaa na michezo, wasanii wetu wanategemea kupitia *you tube* na namna nyingine zingine zote ndio sisi tukaona kazi zao na kuzinunua. Kwa hiyo kidogo changamoto hii ilikuwa inatupeleka kwenye shida kubwa sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na niombe Wizara hii husika basi iliangalie suala hili ili lisije likajirudia tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji kwa siku ya leo, tutaendelea huko baadaye. Niwapongeze na kuwashukuru Wabunge wote waliozungumza siku ya leo, lakini tukumbushane Kanuni ya 175(2), inasema:

"Baada ya Spika kutoa pongezi au pole kwa mhusika au muathirika wa jambo lolote, kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Mbunge yoyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa mhusika au muathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni."

Nadhani hili litakuwa limeeleweka. Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan tunaweza kumpongeza kwa maana ya kazi ambazo zimeshaanza kufanywa kama mbunge aliyepita alivyozungumza na Wabunge wengine, lakini kwa maana ya zile pongezi kuwa rais na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kutangulia mbele za haki alishamaliza Mheshimiwa Spika kwa niaba yetu sisi wote. Ili isije ikanonekana wengine wanaanza hivi wengine wamesahau ama vipi lakini kanuni yetu inatutaka tuheshimu utaratibu huo ambao tumejiwekea wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.03 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 9 Aprili, 2021, Saa tatu Asubuhi)*